**10 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 10 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi Rais, Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 280

### Barabara ya Mkato Kutoka Kigwe B Mpaka Magiri Uyui

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mkato kutoka Kigwe B hadi Magiri Uyui ili kuchepusha magari makubwa kupita Tabora Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara ya mkato kutoka Kigwa B mpaka Magiri - Uyui Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa barabara hiyo inapitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itatenga shilingi milioni 125 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya muda maalum ya kilomita Saba kwa kuziwekea changarawe na kujenga kalavati moja ili iweze kuendelea kupitika muda wote na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea kuifanyia matengenezo na kujengwa kwa kiwango cha lami kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu yaliyotolewa na Serikali yamejielekeza kwenye barabara ndogo iliyokuwepo wakati swali langu lilikuwa ni kutaka barabara kubwa ili malori yasipite mjin,i (barabara ya pete), kwa hiyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali iko tayari kujenga barabara ya pete kutoka Kigwa B kwenda Magiri ili kuepusha magari makubwa yanayokwenda Burundi na Rwanda kupita Mjini na kuharibu barabara za Mjini?

Swali la pili, kwa vile Miji yote inayojengwa sasa ina barabara za pete pamoja na Jiji letu la Dodoma na Mji mdogo wa Nzega. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara za pete kuzunguka Mji wa Tabora?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kadiri ya upatikanaji wa fedha, lakini tayari katika bajeti hii ya 2023/2024 *TARURA* imetenga fedha ya kufanya upembuzi yakinifu kujua gharama jumla itakuwa ni kiasi gani kwa ajili ya ujenzi wa lami wa barabara hii. Hivi ilivyo sasa bado ina uwezo wa kubeba malori na ndiyo maana tunaifanyia *periodic maintenance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu barabara za pete *(ring roads);* Serikali iko tayari kujenga barabara ya pete *(ring road)* katika Mji wa Tabora, tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kuweza kuona tunaanzaje mchakato wa kufanya *feasibility study* ili Mji huu wa Tabora uweze kupata barabara hiyo ya pete.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini.

Na. 281

**Tatizo la wanafunzi kusoma kwa Zamu – Tarime**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kuondoa tatizo la wanafunzi kusoma kwa zamu katika Halmashauri ya Mji Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime imeshatenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ili kuondoa msongamano wa wanafunzi pamoja na kuondoa tatizo la wanafunzi kusoma kwa zamu. Baadhi ya maeneo tayari wananchi wameanza kujenga shule, mfano Kata ya Turwa, Chirya, Kenyamanyori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada hizo za wananchi, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya, hii itasaidia kuongeza madarasa katika shule za msingi na hivyo kuondokana na msangamano wa wanafunzi darasani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule katika Mji wetu wa Tarime inaitwa Bugosi, ina zaidi ya wanafunzi 1,000 lakini ina madarasa Sita na wananchi wamejitahidi sana kujenga lakini jitihada za Serikali kuwatia nguvu inakuwa ni kidogo: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga madarasa ya kutosha katika shule hii? *(Makofi)*

Swali langu la pili, zipo jitihada za wananchi wanazofanya kuhakikisha kwamba wanajenga shule mpya. Kwa mfano katika Kata ya Kenyamanyori kuna Shule zinaitwa Chira, Nyamitembe na shule nyingine ambazo zimejengwa na zimefika katika hatua ya upauaji lakini Serikali haijapeleka fedha kwa ajili ya kumalizia na shule zile zifunguliwe: -

Je, ni lini fedha zitapelekwa ili majengo yale yakamilike na wanafunzi waweze kusoma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kembaki.

Swali lake la kwanza kwenye hule hii ya Bugosi yenye wanafunzi zaidi ya 1,000 na madarasa Sita, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba tunapeleka shilingi bilioni 1.5 katika Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa shule hizi kupunguza msongamano. Kwa hiyo Serikali iko tayari kupeleka fedha na tayari imeshatengewa.

Swali lake la pili, kwenye Kata hii ya Kenyamanyori, nitaa na Mheshimiwa Kembaki tuweze kuangalia upungufu ambao upo katika shule hizi alizozitaja za vijiji vya Kata hii, ili tuone ni namna gani tunaweza tukafanya kuweza kukarabati shule hizi ama kuongeza madarasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Msingi Kizota ambayo iko katika Jiji la Dodoma ni miongoni mwa shule ambazo zina wanafunzi wengi sana na hivyo kusababisha wanafunzi kuingia kwa zamu.

Nini mkakati wa Serikali wa kujenga shule katika eneo la mnada mpya ambapo hakuna shule kabisa kwa sababu watoto wengi wanatokea eneo lile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kujenga shule nyingi kwa wakazi wa kule Kizota kadri ya upatikanaji wa fedha. Tutaangalia katika mradi huu wa *BOOST* ambao Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashuhuda, fedha nyingi sana imetolewa na Serikali hii ya awamu ya Sita kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa shule tuone ni namna gani tunaweza tukafanya kwa ajili ya wakazi wa Kizota wapate shule nyingine na wanafunzi waache kwenda kwa zamu pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Chaurembo kwa niaba.

Na. 282

**Kuwaongezea *TARURA* Bajeti**

**MHE. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO K.n.y. MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawaongezea *TARURA* bajeti ili barabara za ndani ya Jimbo la Kinondoni zijengwe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, Jimbo la Kinondoni lilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 2.38 ambazo zilitekeleza matengenezo ya barabara ya jumla kilometa 26 za lami na changarawe na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya kilometa 0.52. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 32 ya bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 1.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Jimbo la Kinondoni lilitengewa bajeti ya shilingi bilioni 4.87 kwa ajili ya kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara zenye jumla ya kilomita 26.52, ambapo matengenezo ya kawaida ni kilomita 24.32 na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilometa 2.2 ambapo utekelezaji wake unaendelea na umefikia asilimia 70. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 29 ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuiongezea fedha *TARURA* kwa ajili ya kuongeza mtandao wa barabara za

lami katika Jimbo la Kinondoni na maeneo mengine kwa kadri ya upatikani wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara nyingi za Jiji la Dar es Salaam, hasa zile zilizo chini ya *TARURA* huhitaji matengenezo ya mara kwa mara. Je, Serikali haioni ipo haja kwa *TARURA* kuwa na kitengo maalum cha matengenezo badala ya kuwatumia Wakandarasi?

Swali la pili, kwa kuwa Jimbo la Kinondoni linazungukwa na mito midogo midogo ambayo husababisha mafuriko hasa katika Kata za Mwanayamala, Kijitonyama, Tandale, Kigogo na Ndugumbi. Je, Serikali ipo tayari kufanya upembuzi wa kitaalam ili kubaini njia bora za kukabiliana na hali hii ya mafuriko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Tarimba la je, *TARURA* ipo tayari kuanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kuangalia ukarabati wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuanzisha kitengo maalum kunahitaji rasilimali fedha, rasilimali watu na vifaa. Hivyo basi, kwa sasa *TARURA* inaona ni bora kufanya *outsourcing* kwa sekta binafsi. Hii pia inasaidia kutoa ajira kwa Watanzania wengine ambao wanafanya kazi katika sekta binafsi. Vilevile ina-*assure quality control* na kunakuwa kuna *checks and balances* akipewa mtu na *TARURA* wakamkagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, tayari mito ya Jimbo la Kinondoni imetengewa fedha kwenye Mradi wa *DMDP II* ambao utaanza Novemba, mwaka huu 2023. Kwenye *DMDP I* tayari walikuwa wameshatengenezewa Mto Ng'ombe ambayo imezuia mafuriko makubwa sana katika maeneo yanayozunguka barabara hizi na makazi ya watu wa Jimbo la Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wakati Kinondoni wanaomba fedha kwa ajili ya kujengewa lami, Wilaya ya Makete na Mkoa wa Njombe tunaomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za changarawe kwenye barabara ya kutoka Kinyika – Kikondo – Nkenja – Ikuwo, barabara ambazo zimeharibika sana kutokana na mvua nyingi zinazoendelea Jimboni Makete.

Je, Serikali itafanya nini itusaidie tupate fedha hizo kwa sababu barabara hizi ni barabara za uzalishaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwaka wa fedha huu Bunge lako tukufu limeipitishia *TARURA* bajeti ya zaidi ya bilioni 772 tutaangalia barabara hii ya Kinyika – Kikondo katika Jimbo la Makete kule kama nayo imetengewa fedha kwenye bajeti hii. Kama haijatengewa fedha tutaangalia mwaka wa fedha unaofuata tuweze kutenga fedha kwenye bajeti kutengeneza barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wananchi wa Wilaya ya Tanganyika wanapakana na Wilaya ya Nkasi Kusini na upande wa Kaskazini wanapakana na Wilaya ya Uvinza. Maeneo haya kwa wananchi wanaoishi mwambao wa Ziwa hawana njia mbadala tofauti na njia ya majini.

Je, ni lini Serikali wataongeza bajeti kwa upande wa *TARURA* ili tuzifungue hizi njia tuepushe maafa kwa wananchi na mali zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lengo la Serikali kuiongezea *TARURA* fedha. Kama mlivyo mashahidi, mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ya *TARURA* nchi nzima ilikuwa shilingi bilioni 228, lakini baada ya bajeti ya 2021/2022 chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, *TARURA* imeongezewa fedha zaidi ya mara tatu kwenda shilingi bilioni 772. Tutaangalia hizi barabara zinazounganisha Tanganyika, Nkasi na Uvinza ili ziweze kupata fedha na kutengenezwa, kadri ya fedha itakavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, jiandae Mheshimiwa Prof. Mkumbo.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola inatajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ukurasa wa 78, kilometa 11.5, na mpaka sasa Serikali imetenga kilometa 2.2 tu. Ni lini Serikali sasa itatenga fedha za kumalizia kilometa 9.3 ili kutekeleza ahadi iliyoko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ya Msongola ya kilometa 2.2 ambayo ndiyo imetengewa fedha, tayari nilikaa na Mheshimiwa Mbunge, alikuja kulifuatilia na lenyewe na tukakaa na wataalam wa *TARURA* kuhakikisha kwamba tunaona ni namna gani tunapata fedha hii ya kilometa 9.3 iliyosalia kama ambavyo iliahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa kuangalia tunafanya vipi ili fedha hizi ziweze kupatikana na barabara hii iweze kutengenezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkumbo, jiandae Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Suka – Golani ambayo ilianza kujengwa mwaka jana, kilometa nane zimeshajengwa mita 400 lakini imesimama baada ya *flow* ya fedha kushuka.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaahidi hapa kwamba mwaka huu *flow* ya fedha itakuwa nzuri kwa barabara hii ili wananchi wahakikishiwe kwamba barabara inakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, baraba hii ya Suka – Golani kama ambavyo nimeshasema hapa kwenye baadhi ya maswali niliyoulizwa, kwamba *TARURA* imeongezewa fedha sasa na tutaangalia kupitia Meneja wa *TARURA* katika Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ubungo kuona ni namna gani katika bajeti ambayo ameitenga barabara hii itaweza kuendelea kufanyiwa matengenezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Katika Jimbo letu la Kilwa Kaskazini lina mtandao wa barabara za *TARURA* kilometa 528 ambazo zote ni za vumbi. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* itaanza kujenga barabara za lami katika Jimbo la Kilwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ninarudia tena tayari *TARURA* imeongezewa bajeti na Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutaangalia na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilwa kuona katika bajeti ambayo imepitishwa hapa ni kilometa ngapi ya lami ambayo imetengwa ili katika hizi barabara za Kilwa alizotaja Mheshimiwa Ndulane angalau moja ianze kupata lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kigamboni ina mtandao wa barabara za *TARURA* takribani kilometa 1,000, lakini ni kilometa tano tu ambayo ni asilimia 0.5 *percent* ambazo zina kiwango cha lami. Bajeti ya *TARURA* pale ni shilingi bilioni 3.5.

Je, nini mkakati wa *TARURA* kuongeza bajeti ili barabara za Wilaya ya Kigamboni zifanane na barabara nyingine za Jiji la Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* itaendelea kuongeza fedha katika Wilaya ya Kigamboni na Jimbo la Kigamboni kwa Mheshimiwa Ndugulile kadri ya upatikanaji wa fedha. Ni lengo la Serikali hii ya Awamu ya Sita kuhakikisha *TARURA* inakuwa na nguvu ya kutosha kutengeneza barabara nyingi zaidi za lami katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo kule Kigamboni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Akheri inayoanzia Sangisi kwenda Ndoombo ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu

ya Nne kujengwa kwa kiwango cha lami miaka kumi iliyopita. Mwaka jana barabara hiyo imeanza kujengwa: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimalizia mwaka huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Akheri – Sangisi ambayo ameitaja Mheshimiwa Dkt. Pallangyo hapa ambayo tayari imeshaanza kuwekewa lami itaendelea kuwekewa lami kwa sababu ni ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kadri ya upatikanaji wa fedha na tutaendelea kuitengea bajeti kwenye miaka ya fedha ambayo inafuata.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunakwenda Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Sinkamba.

Na. 283

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama yenye hadhi ya Wilaya katika Wilaya ya Kalambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kalambo katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 ambapo taratibu zote za awali za kupitia michoro na makadirio ya gharama vimekamilika. Aidha, hatua ya kupata Mkandarasi wa ujenzi ipo katika hatua za mwisho. Hivyo, tunategemea muda wowote jengo hili litaanza kujengwa na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Mwimbi, Kasanga na Mwazye na Mambwe Nkoswe ni chakavu kwelikweli. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wakati ikiwa inafikiria kujenga Mahakama mpya za Mwanzo?

Swali la pili; kwa kuwa Tarafa ya Mambwe Nkoswe ambayo ni kilometa 150 kwenda Makao Makuu ya Wilaya haina kabisa hata Mahakama ya Mwanzo. Je, Serikali iko tayari kwa uharaka kuhakikisha kwamba tunajengewa Mahakama ya Mwanzo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephat Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha Mahakama imetenga fedha kwa ajili ya kujenga Mahakama katika Kata hii ya Kasanga ambayo ni hitaji la Mheshimiwa Mbunge. Kwa Tarafa ambayo ameitaja katika swali la pili, naomba nimuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mahakama itaendelea kutenga fedha kukamilisha Mahakama za Mwanzo ambazo hazijajengwa katika maeneo ambayo kuna uhitaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita, jiandae Mheshimiwa Aida.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Wilaya ya Kiteto ni ya zamani kidogo na majengo yamechakaa. Kwa jibu la uhakika kabisa, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya kwenye Jimbo la Kiteto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa Mahakama, Mahakama ya Wilaya ya Kiteto itajengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali ilituahidi kujenga Mahakama ya Mwanzo

Tarafa ya Namanyere, ninapenda kujua utaratibu huo umefikia wapi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha wa 2023/2024 kwa bajeti yetu ambayo tumepitisha tunakwenda kujenga Mahakama katika Kata ya Namanyere na katika Wilaya ya Nkasi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Na. 284

**Mafunzo kwa wajasiriamali nchini**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapatia ujuzi na mafunzo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini *(SIDO)*, lenye ofisi katika Mikoa yote nchini hadi kufikia Februari 2023, imeratibu na kutoa mafunzo na ujuzi kwa wajasiriamali wapatao 12,091, ambapo wanaume walikuwa 5,082 sawa na asilimia 42 na wanawake 7,009 sawa na asilimia 58 kupitia kozi 519 katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kutoa mafunzo na ujuzi katika nyanja mbalimbali kwa wajasiriamali nchini. Aidha, Serikali imepanga kuongeza wigo wa kutoa mafunzo ya biashara na ufundi pamoja na ushauri kwa kutumia TEHAMA. Nakushukuru.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni ukweli usiofichika kwamba *SIDO* zetu nyingi zinafanya kazi chini ya kiwango na hiyo ndiyo maana unaona hata idadi ya wanufaika ni wachache. Je, nini mpango wa Serikali wa kuziwezesha *SIDO* hizi ili ziweze kuwanufaisha wajasiriamali wengi zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wajasiriamali wengi wanashindwa kumudu gharama za mafunzo haya. Je, Serikali iko tayari kuweka wazi na kutoa maelekezo kwa *SIDO* zote nchi nzima kutoa mafunzo haya bure na kuweka mwongozo wazi wa namna gani mafunzo haya yanafanyika katika *SIDO* zetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli, niungane na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna changamoto ya bajeti kidogo kwa Shirika letu la *SIDO* lakini sasa ni mpango wa Serikali kuona baada ya kuongeza katika sekta nyingine, ni dhahiri tutakuja kwenye sekta hii ya viwanda ambapo *SIDO* ni wadau muhimu sana kuhakikisha wanaendeleza na kufanya kazi zao kwa weledi wakiwa na bajeti ya kutosha. Kwa hiyo, Serikali imejipanga kuongeza fedha ili waweze kuongezewa *SIDO* waweze kufanya kazi zao zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli tungeweza kutoa bure mafunzo lakini lazima kuna gharama ndogo ambazo wajasiriamali wanatakiwa kuchangia. Hoja kubwa hapa ni kuona namna gani tunawawezesha *SIDO* ili wawe na fedha za kutosha na gharama za wajasiriamali kuchangia kupata mafunzo ziwe chini zaidi au hatimaye yaweze kutolewa bure kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunakwenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Tendega.

Na. 285

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Kata ya Mtwango**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza kujenga Mradi wa Maji katika Vijiji vya Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao vilivyopo Mufindi Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika Kata ya Mtwango, na miradi imekamilika kwenye Vijiji vya Sawala na Mtwango. Kwa sasa miradi inaendelea katika Vijiji vya Rufuna na Kibao ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa Kilometa 21, ujenzi wa matenki mawili yenye jumla ya ujazo wa lita 450,000 na vituo 21 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa kazi hizo utakamilika mwezi Julai, 2023 na wananchi kupata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali, Mbunge wa Mufindi Kusini Mheshimiwa David Kihenzile, amekuwa akipigania sana na akiomba ukarabati wa mradi wa Imayi, yaani Kata za Ihoanza, Malangali na Idunda; na ule wa Vijiji tisa wa Kata za Mbalamaziwa na Itandula, lakini mpaka sasa haujaanza: Je, ni lini Serikali itapeleka fedha? Pamoja na kwamba mmesema fedha zimetengwa, lini Serikali itapeleka fedha mradi huo uweze kufanikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mradi wa watumia maji wa Magubike, Kata ya Nzihi Jimbo la Kalenga umejengwa na wafadhili wa Marekani wanaoitwa *WARIDI,* lakini tayari walishajenga *intake* na *tank* lipo tayari, changamoto ni namna ya usambazaji wa maji kwenda katika vijiji sita pamoja na

vitongoji vyake: Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kupeleka miundombinu hiyo wananchi waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRTI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Victor Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tumejipanga vizuri, mradi huu wa Mbalamaziwa ambao unaenda kuhudumia vijiji tisa, tayari tumeshapata Mkandarasi na tunatarajia bajeti ijayo Mkandarasi huyu aanze kazi kwa sababu kila kitu kimeshakamilika. Mradi wa Malangali ni mradi mkubwa ambao tunatarajia utatumia zaidi ya Shilingi bilioni sita. Dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kumtua Mama ndoo kichwani inaenda kukamilika kwa sababu bajeti ijayo tutahakikisha tunaleta fedha kwa awamu na kwa wakati ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati, na wananchi waweze kunufaika na maji safi na salama ya kitoka bombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la *intake* na tenki kukamilika kwenye Jimbo la Kalenga, tayari tunaendelea na utaratibu kuona kwamba usambazaji wa maji tunakuja kuufanya ndani ya bajeti hii tunayoimalizia, pia kwa bajeti ijayo, tutakuja kuhakikisha maeneo yote ambayo yanapaswa kufikiwa na maji, yanakwenda kufikiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tokea Tanzania imepata uhuru, kuna vijiji mkoani Mara hawajawahi kuyaona maji toka Setikalini: Je, Serikali ina mpango gani kupeleka maji katika Wilaya ya Serengeti na vijiji vyake na

Wilaya nyingine ambazo zinazungukwa na utajiri wa Ziwa Viktoria? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya aliyoyataja katika eneo la Serengeti, tayari tuna miradi ambayo tunatarajia wananchi waweze kunufaika na maji safi bombani. Nasi Wizara ya Maji, toka tumeanza kuhakikisha tunaleta mageuzi ndani ya Wizara hii, maeneo ambayo hayajawahi kupata maji, yanapata maji sasa hivi. Hivyo, wananchi wa Serengeti nao wakae mkao wa kupata maji safi na salama bombani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Suma Ikenda, kwa niaba ya Mheshimiwa Mkundi.

Na. 286

**Mwenyekiti wa Baraza Wilaya ya Rungwe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niamba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za ajira zinaendelea kuchakatwa ili kupata Wenyeviti 57 watakaoweza kukamilisha uhitaji wa Wenyeviti 139 ambayo ni idadi ya Wilaya zote hapa nchini. Kwa sasa tuna Wenyeviti 82 tu ambao wanalazimika kuhudumia Wilaya zisizo na Mabaraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wilaya ya Rungwe inahudumiwa na Mwenyekiti kutoka Wilaya ya Kyela.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa sababu tatizo hili limekuwa kubwa karibu katika Wilaya zote nchini, kuna mlundikano wa kesi nyingi, lakini Wenyeviti hao wa Mabaraza ni wachache sana. Kwa nini Serikali isiwe na mkakati maalum kuhakikisha kwamba mabaraza yote ya ardhi katika Wilaya zetu yanapata Wenyeviti hawa? Swali la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina mlundikano mkubwa wa kesi, ina migogoro mingi inayohusu ardhi: Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi atakayekaa pale kwa ajili ya kuondoa migogoro na kutatua kesi zilizopo zinazohusu masuala ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu

maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia jibu la msingi ambalo nimelitoa, ni kwamba sasa hivi tunaendelea na michakato kama nilivyoeleza, ya kuziba pengo la Wenyeviti 57 ambao utaratibu wake ukikamilika, tutakuwa tumekamilisha Wilaya zote hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ukerewe, kutokana na mlundikano wa kesi, hili tutaliangalia kwa umuhimu wake na tutalifanyia kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Catherine Magige, jiandae Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwaka 2018 Waziri wa Ardhi alitembelea mipaka ya Wilaya ya Monduli - Longido, Monduli - Arumeru, na Monduli - Babati na kuagiza mipaka hii iainishwe: Je, ni lini Serikali itaenda kutembelea mipaka hii na kuibainisha ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima kwa wananchi inayopelekea mapigano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali la msingi lilihusu masuala ya Mabaraza. Kwenye eneo hili la mipaka, tayari tumeshaanza hiyo kazi na katika kipindi cha kama miezi miwili iliyopita, tulikuwa Mkoa wa Arusha ambapo tulitembelea ile mipaka inayotenganisha nchi na nchi. Kwa maana ya migogoro iliyopo kati ya Wilaya na Wilaya, tayari timu

mbalimbali zimeshaundwa na zinakwenda kufanyia kazi haraka sana na Monduli na Arusha zitakuwa ni moja kati ya maeneo ya kupitiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu, lakini ina mwenyekiti mmoja tu wa Baraza la Ardhi. Sasa Serikali ina makakati gani wa kupeleka Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi katika Halmashauri ya Ushetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kama nilivyolieleza katika jibu la msingi, tunaendelea na michakato ya kupata Wenyeviti katika kuziba pengo la karibu Wilaya 57, na tukishafanikisha, Ushetu nayo itapewa umuhimu wa pekee nao katika kufikishiwa Mwenyekiti wa Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, katika maeneo yote hapa nchini ambayo mabaraza hayajafika, Mamlaka za Miji husika, kama kuna majengo ambayo tayari yapo, ambayo tunaweza tukayatumia katika kipindi hiki, basi tuarifiane, na Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yenu mtupe taarifa ili tuweze kuona uharaka wa kuwaleta wenyeviti wetu katika maeneo husika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

Na. 287

## Kumpata Mkandarasi *CCECC* - Ujenzi wa Mradi wa *SGR* kwa Njia ya *Single Source*

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, kwa nini ilitumika njia ya *single source* kumpata Mkandarasi wa *SGR Lot No*. 6 Tabora – Kigoma na kusababisha hasara ya trilioni mbili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi ya Umma imeainisha njia mbalimbali za manunuzi ya mkandarasi zinazoweza kutumiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na njia ya *single source*. Aidha, Manunuzi ya Mkandarasi kwa kipande cha Tabora - Kigoma yalifuata Sheria za Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na Kanuni zake Na. 161 (1) (a) mpaka (c) (*Single source Procurement for works)* ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 na Marekebisho yake ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa hakuna hasara yoyote iliyosababishwa na ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa njia ya reli ya Tabora – Kigoma, bali ununuzi wa mkandarasi ulifuata taratibu zote za manunuzi ikiwemo

majadiliano kwa lengo la kuhakikisha gharama sahihi za mradi zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, makadirio ya gharama za kihandisi *(Engineering Estimates)* yalikuwa dola za Marekani bilioni 3.066 sawa na shilingi trilioni 7.2 ikilinganishwa na gharama halisi za bei ya Mkandarasi *(base price)* baada ya majadiliano ambayo ni dola za Marekani bilioni 2.216 sawa na shilingi trilioni 5.2. Hii ni baada ya majadiliano yaliyookoa dola za Marekani milioni 273,913,703.25 sawa na shilingi bilioni 632.74 kutoka kwenye zabuni ya awali ya dola za Marekani 2,490,124,575.00 sawa na shilingi trilioni 5.8

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa utaratibu wa manunuzi kwa njia ya *Single source* ndiyo uliotumika kumpata Mkandarasi *YAPI MERKEZI* wa Ujenzi wa kipande cha tatu kutoka Makutupora kwenda Tabora, na Kipande cha nne, yaani Tabora - Isaka, ambapo gharama zake ni dola za Marekani bilioni 2.213 sawa na Shilingi za Kitanzania trilioni 5.19, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa nini Wizara na *TRC* waliacha bei ya ushindani ya shilingi bilioni 9.1 kwa kilometa moja ya *standard gauge* na kuamua kumpa kampuni ya *CCECC* kwa shilingi bilioni 12.5 kwa kilomita moja ya *standard gauge* na kuisababishia hasara Serikali ya shilingi trilioni mbili ambayo ni kinyume na matakwa ya *single source* kama alivyoeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kwa nini Serikali isivunje huo mkataba baina ya *TRC* na *CCECC* wa ujenzi wa kipande cha Tabora - Kigoma kwa sababu hata hiyo *Lot III, Lot*

*IV* anayo*i-refer CAG* ameshatuambia kwamba tayari walikiuka utaratibu wa sheria. Kwa nini Serikali isifute huu mkataba wa kinyonyaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya ushindani, bei zilizopo ni tofauti sana na zilizotumika miaka ya 2017 wakati nchi inaanza ujenzi wa *standard gauge*. Kila kitu kimebadilika, hususan katika suala la asilimia zaidi ya 65 ya *SGR,* inatumia chuma. Bei ya Soko la Dunia ya chuma, imeongezeka kwa robo tatu ya gharama yake. Pia mwaka 2017 bei ya mafuta ilikuwa takribani shilingi 1,900, sasa hivi imekwenda mpaka shilingi 3,000 na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo gharama anazolinganisha Mheshimiwa Mpina, ziko tofauti sana na gharama za leo. Hata hivyo, hapa tumesema katika jibu letu la msingi kwamba tumeokoa takribani shilingi bilioni 632.74. Katika nchi za Afrika Mashariki, sisi Tanzania peke yake, kwa gharama ya ushindani, ndiyo tumeweza kuwa na kiwango kidogo zaidi cha kutengeza kilomita moja kwa dola za Kimarekani milioni nne, wakati nchi jirani na hata ukisoma ripoti ya Benki ya Dunia, ni zaidi ya dola za Kimarekani kwa kilomita moja milioni 7.69. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nihakikishie Watanzania na Bunge lako tukufu kwamba hakuna hasara yoyote, zaidi tumeokoa fedha hizi ambazo nimezitamka hapa. *Engineering estimate* zilikuwa dola za Kimarekani bilioni 3.006 sawa na shilingi trilioni 7.2, nasi tumesaini mkataba wa shilingi

trilioni 5.2. Maana yake tumeokoa tena shilingi trilioni mbili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kwa nini mkataba usivujwe? Huu makataba hatuwezi kuuvunja kwa sababu kwanza ni wa gharama nafuu; na pili, ni mkataba na *CCECC*. Ukiangalia *rank* za Makampuni yote duniani, *perfomance* ya kampuni hii, inaonesha kufanya vizuri, ni ya 10 kwa mwaka 2021, na ni ya 11 kwa mwaka 2022. Kwa hiyo, hata kipande kile cha kutoka Isaka - Mwanza ambacho ni kilomeeta 341, wana asilimia zaidi ya 30. Kwa hiyo, wanafanya vizuri na ndiyo maana tuliwapa mkataba huu wa kutoka Tabora kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Taska Mbogo.

Na. 288

**Ujenzi wa barabara ya Mpanda – Karema kwa kiwango cha lami**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mpanda hadi Karema kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya kilometa 10 ya kutoka Mpanda hadi Kagwira na kwa sehemu iliyobaki ya kuanzia Kagwira hadi Karema (kilometa 112) zabuni za kuwapata Makandarasi zilitangazwa tarehe 20 Aprili, 2023 na zimepangwa kufunguliwa tarehe 31 Mei, 2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza napenda kuishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa hii barabara kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa Serikali imewekeza ujenzi wa bandari pale Karema, ujenzi ambao ni mkubwa sana: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba barabara ya kutoka Kagwila kwenda Karema inafanyiwa ukarabati, kwani kwa sasa hivi imeharibika sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kumekuwa na matatizo watu wanapopisha ujenzi wa barabara, Serikali imekuwa na tabia ya kuchelewesha kuwalipa: Je, Serikali imejipanga vipi kuwalipa wananchi watakaopisha ujenzi wa barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami toka Kagwila kwenda Karema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipokee shukurani kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, kwa sababu shukurani hizo ni zake, ndiye anayetoa hizo fedha kujenga hiyo miundombinu. Kwa maswali yake mawili, nakubali kwamba barabara ya Kagwila kwenda Karema kilomita 112 inayoenda kwenye Bandari ya Karema ilikuwa na changamoto, lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Mkoa kupitia Meneja, waliomba fedha za ziadam Shilingi milioni 500 tulishatoa, na wako wanakarabati maeneo yale ambayo yalikuwa hayawezi kupitika hasa maeneo ambayo wanalima mpunga karibu na barabara. Kwa hiyo, kwa sasa tunavyoongea, Mheshimiwa Mbunge barabara ile inapitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia, tayari tumeshakamilisha tathmini na wananchi wote ambao watalipwa kwa mujibu wa sheria zetu kwa barabara ya Kagwila hadi Karema, tayari wameshatambuliwa na tayari wameshajulishwa kila mtu atalipwa kiasi gani. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itawalipa wote watakaopisha barabara kwa mujibu wa sheria, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Barabara ya Nangulukulu - Liwale, inayopita katika majimbo ya Kilwa Kusini, Kilwa Kaskazini na Liwale, imeharibika vibaya kutokana na mvua za hivi karibuni. Nini maelekezo ya Wizara, kuelekeza *TANROADS* Mkoa wa Lindi kufanya marekebisho katika maeneo ya Nangulukulu - Migelegele – Mbate, Naiwanga – Njinjo – Miguluwe mpaka Kimambe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kama tulivyosema huko nyuma na tulikwishatoa maelekezo na ninatoa sasa maelekezo mahususi kwa Meneja wa Mkoa wa Lindi, kuhakikisha kwamba anakwenda maeneo yote ya barabara ya Nangulukulu – Liwale kurekebisha maeneo yote ambayo hayapitiki kwa sasa na kama kutakauwa na changamoto ya kibajeti basi aweze kuwasiliana na *TANROADS* Makao Mkauu kwa msaada zaidi ili kuhakikisha kwamba anarejesha mawailiano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Singida kupitia kwamtoro mpaka Kedashi - Tanga, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na kwa sababu mlituambia tayari imekwishawekwa kwenye mpango wa kujengwa, na imetangazwa katika kilomita 2100. Ni lini sasa mkandarasi atakuja kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia huku mwishoni alichouliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali lako tena.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuuliza tu kwamba ni lini sasa Serikali itamleta mkandarasi aanze kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba barabara hiyo tuna mpango thabiti wa kuijenga kwa kiwango cha lami. Kama tulivyokuwa tunaelezea kwamba nitajengwa kwa mpango wa *EPC+F* na ninaomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira ataisikia tutakapokuwa tunawasilisha bajeti yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimia tunaendelea, Wizara ya Habari na Mawasiliano, Mheshimiwa Laurent Kyombo.

Na. 289

**Kuboresha mtandao wa mawasiliano Misenyi**

**MHE. FROLENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini serikali itaongeza minara au kuboresha mawasiliano katika kata zote 20 za Wilaya ya Misenyi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI,** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frolent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imetekeleza miradi ya mawasiliano iliyokamilika katika kata 10 za Wilaya ya Missenyi. Kufikia mwezi Machi, 2023 tayari ujenzi wa minara 13 imekamilika na inatoa huduma katika teknolojia ya 2G na 3G.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali Serikali imeshapata watoa huduma wa kufikisha huduma za mawasilioano katika Kata za Bugorora, Kasambya, Mutukula na Kakunyu ambapo tayari zimeshapata watoa huduma, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na niipongeze baada ya kipindi cha miaka miwili baada ya ziara ya Naibu Waziri, katika jimbo langu tumekwishapata minara Minne mipya. Pia, nashukuru katika bajeti mpya sasa hiyo minara mipya minne ikienda kujengwa tutaielekeza katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misenyi, kama ilivyo mpakani mwa Nchi ya Uganda imekuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano. Sasa ni lini minara mingine itajengwa katika Kata za Bugandika, Kilimilile, Buyango, Kitobo, Bwanjai na Mabale ili kuweza kufanya wananchi wa maeno hayo waweze kupata mawasiliano mazuri katika jimbo letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, wananchi wa Wilaya ya Misenyi, wamekuwa wakipata mawimbi ya redio ya nchi jirani ya Uganda. Ni lini sasa Serikali itaweka nia ya dhati kuhakikiasha kwamba wananchi wanafaidi mawasiliano ya mawimbi ya *radio* ya nchi yetu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kyombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunafanya *feasibility study* kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano katika Kata ya Bugorora na Kakunyu hapakuwa na minara imejengwa. Lakini kwa sasa tumegundua watoa huduma kwa kutumia uwekezaji wao wamekwisha jenga minara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa minara ambayo tulikuwa tumepanga kupeleka pale sasa tutaihamishia na kupeleka Kata ya Minzilo na tutapeleka katika eneo la Kashenye. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wananchi wa eneo hilo pamoja na maeneo ya Kitobo na Kanyigo wote tutawaweka katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipengele cha pili, eneo la Misenyi lina changamoto ya huduma ya usikivu wa redio. Pia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari ametoa fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo katika eneo la Kyerwa ambapo tukishafunga mtambo wetu pale utaweza kufikisha huduma ya redio katika maeneo ya Misenyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Pfofesa Ndakidemi, jiandae Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Katika bajeti hii tunayomalizia ya 2022/2023 Serikali ilikuwa imepanga kujenga minara ya mawasiliano katika Kata za Urushimbwe, Mabogini na Kibosho Kati. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na ujenzi wa minara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kulikuwa na changamoto hii na Mheshimiwa Mbunge, aliwasilisha changamoto hii mara kwa mara lakini Serikali ilijitahidi sana kutafuta fedha na hatimae Mheshimiwa Rais, ametoa fedha na tunakwenda kuingia mkataba na kampuni ya *Vodacom* na *TIGO* kwa ajili ya Urushimbwe, Mabogini pamoja na eneo la Kibosho kati. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge hili tuna uhakika kwamba kati ya Mwezi wa Sita au wa Saba tayari ujenzi wa mnara huo utaanza rasmi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga minara katika Kata ya Shigala, Nyaruhande na Kijiji cha Kijereshi ili kuboresha mawasiliano kwa sababu kata hizi zinashida kubwa ya mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niwajulishe watanzania, Waheshimiwa Wabunge, tarehe 13 Mei, 2023 tunakwenda kusaini Mkataba wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata 713 ambayo ni wilaya 127 mikoa yote, ambapo ni Vijiji takribani 1407. Watanzania takribani milioni 8.5 wanakwenda kupata huduma ya mawasiliano, ambapo Mheshimiwa Rais, ameidhinisha kiasi cha bilioni 125.9 kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeno hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wahudhurie katika hafla ya utiaji Saini wa mikataba hii ambayo inakwenda kufikisha huduma ya mawasiliano kote Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa  Mwantum Dau.

Na. 290

**Serikali kuongeza gari la polisi Wilaya ya Kusini Unguja**

**MHE. MWATUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza gari lingine la polisi wilaya ya Kusini Unguja kwani gari moja lililopo halikidhi mahitaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwatumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi wilaya ya Kusini Unguja, katika mkoa wa kusini Unguja una magari manne ambayo yote ni mazima na yanatumika kutoa huduma katika eneo hilo. Magari hayo ni *PT* 4807 *Ashok Leyland* ambalo liko kituo cha Polisi Kizimkazi, *PT* 4808 *Ashock Leyland* ambalo liko Kituo cha Polisi Paje, PT 1906 *Toyota Land Cruiser* ambalo lipo Kituo cha Polisi Paje, PT 3860 *Toyota Hilux Double Cabin* ambalo liko kituo cha Polisi cha Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia bajeti yake ya mwaka wa fedha 2022/2023 imetoa kiasi cha fedha shilingi billioni 15 kwa ajili ya Jeshi la Polisi ili kununulia pikipiki pamoja na magari ambayo yamepangwa kugawiwa kwenye mikoa na wilaya zote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dau.

**MHE. MWATUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kujibu maswali yangu yenye kina na ambayo mimi mwenyewe nimeyaelewa. Napenda kumuuliza swali langu hivi, je, ni lini sasa hizo milioni 15 ambazo zimekisiwa kwenda kununuliwa mapikipiki pamoja na hayo magari katika wilaya nyingine pamoja na Mikoa, lini sasa Serikali itapeleka pesa hizo ili zifanyike kununulia magari hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri:

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwatum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 15 sehemu ya fedha hiyo tayari imekwisha tolewa na gari hizo tayari zimekwishaagizwa. Tunatarajia mwezi Agosti, 2023 tuweze kupokea magari hayo utaratibu wa Serikali ambao tunanunua magari hayo kupitia *GPSA*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba sehemu ya fedha hizo tayari zimeshatolewa na sehemu ya magari hayo yamekwishaagizwa na mara yatakapowasili basi tutaanza utaratibu wa kuyagawa katika wilaya kama ambavyo tumepanga.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Shigongo, kwa niaba Mheshimiwa Kiswaga.

Na. 291

**Hitaji la Chuo cha *VETA*- Buchosa**

**MHE. BONIVENTURE D. KISWAGA K.n.y MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga chuo cha *VETA* Wilaya ya Buchosa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika

mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Sengerema eneo lililotengwa kujengwa Chuo cha Ufundi Stadi ni katika Kijiji cha Kayenze Kata ya Nyehunge na tayari kiasi cha shilingi million 45 kimetolewa mwezi Machi, 2023 kwa ajili ya shughuli za awali za ujenzi wa chuo hicho, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURE D. KISWAGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni miezi miwili sasa tangu fedha hizi zitumwe kule Buchosa. Je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi ni lini mkandarasi ataanza kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa milioni 45 ni awamu ya kwanza, je, fedha zilizobaki zitatumwa lini ili kuendelea kutekeleza mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiswaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulipeleka milioni 45 kwa ajili shughuli za awali ambazo zilikuwa kwa ajili ya *due technical survey, topographical* pamoja na ile *ESIAM* na tayari shughuli

hizi zimekwisha fanyika. Mchakato uliokuwa unaendelea ni kwa ajili ya kutafuta mafundi pamoja na wazabuni wa vifaa mbalimbali kwa sababu utaratibu tutakaotumia katika ujenzi ni ule utaratibu wa *force account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaendelea na mchakato huo na hivi sasa mchakato umekamilika, tumekwisha pata mafundi wote kwa ajili ya ujenzi. Lakini vilevile tumepata wazabuni wa kupeleka vifaa eneo hilo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fedha zote kwa ajili ya ujenzi tayari ziko wizarani na kwa awamu ya kwanza tunapeleka jumla ya milioni 300 kwa ajili ya kuandaa misingi ili baadae tuweze kupeleka fedha nyingine kwa ajili ya sehemu ya juu ya majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu nimuondoe wasiwasi hatutatumia mkandarasi na badala yake tutatumia mafundi kwa sababu tunatumia *force account* na fedha sasa hivi tunavyozungumza milioni 300 tayari iko Buchosa ili kuendelea na ujenzi wa misingi ya majengo yote tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso - Waziri wa Maji, ni wageni kutoka Wizara ya Maji; *Engineer* Nadhifa Kemikimba, Katibu Mkuu, *Engineer* Luhemeja Cyrpian, Naibu Katibu Mkuu, *Engineer* Mbogo Mfutakamba, Mwenyekiti Bodi ya Maji ya Kitaifa, Jenerali Davis Mwamunyange, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji *DAWASA* (Mkuu wa Majeshi Mstaafu), Ndugu Victoria Elango, Makamu Mwenyekiti wa Bodi *EWURA, Engineer* Bashir Juma Mrindoko, Mwenyekiti Bodi ya Maji *KASHWASA,* Ndugu Ruth

Koya, Mwenyekiti wa Bodi ya *RUWASA* na Mheshimiwa Balozi Daniel Ole-Njoolay, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Arusha. *(Makofi)*

Wapo pia Profesa Jafari Kideghesho, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Moshi, Ndugu Chavuna Taratibu, Mwenyekiti wa Bodi *DUWASA,* Ndugu Haji Nandule, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Maji, Ndugu Lazaro Msaru, Mwenyekiti wa Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ndugu George Philipo Marmo, Mwakilishi wa Ubalozi wa India, *Engineer* Clement Kivegalo, Mkurugenzi Mkuu *RUWASA, Engineer* Aaron Joseph, Mkurugenzi Mamlaka ya Maji *DUWASA,* Ndugu Kiula Kingu, Mtendaji Mkuu wa *DAWASA* na Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu *EWURA (Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa ahsanteni, ahsanteni.

Yupo pia Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu *EWURA. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mnajua mnachukua muda wenu wa kuchangia. *(Kicheko)*

Halafu pili, mnakataa maelekezo ya kiti. *(Kicheko)*

Dkt. James Andilile, Mkurugenzi Mkuu *EWURA. (Makofi)*

Yupo Ndugu Manoj Bihar Verma, *Deputy High Commissioner* kutoka Ubalozi wa India, Dkt. Adam Karia, Mkuu wa Chuo cha Maji, Ndugu Prosper Bushafwe, Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Maji, Ndugu Hafsa Mtafiwa, Mwenyekiti Bodi ya Bonde ya Wami Ruvu, Ndugu Benardeta Ngulizi, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi Shirika la Maendeleo la Ufaransa *AFD. (Makofi)*

Pia viongozi hao wameambatana na watendaji kutoka Wizara ya Maji ambao ni, wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji ya miji 28, washirika wa maendeleo na menejimenti ya Wizara ya Maji, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni kutoka Mfuko wa Maji wa Taifa, Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Mameneja wa *RUWASA* wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji wa Miradi ya Kitaifa, Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maji, Wakurugenzi wa Mabonde Maji, Wakuu wa Maabara za Ubora wa Maji, Chuo cha Maji na Maafisa wengine wa Wizara na taasisi zake. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambao ni familia yake, Ndugu Fatuma Omary Masanga, mama yake mzazi, karibu sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zainab Abdallah, mke wa Mheshimiwa Waziri, Ndugu Mtanga Aweso, shangazi yake, Ndugu Akida Bohorela, Mwenyekiti Halmashauri Pangani, Ndugu Abdalah Mahamudu Mwenyekiti wa CCM Pangani, Ndugu Hadija Hamidu Aweso dada yake, Ndugu Omary Aweso baba yake mdogo na Ndugu Jumanne Songoro baba yake mdogo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji ambao ni familia yake; Ndugu Winfried Mahundi - baba yake mzazi, Ndugu Veronica Mahundi - mama mdogo, Ndugu Victoria Mbunda - mama mlezi, Ndugu Mouree Balbina Salla - mtoto wake, Ndugu Vailet Kimwage - mtoto wake na Ndugu Julius Mahundi - mdogo wake, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wawili ambao ni Maafisa kutoka Bunge la Zambia, Ndugu Alfred Mulaye, *welcome to the Parliament* na Ndugu Kennedy Bwalya, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wanne wa Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni viongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* kutoka Zanzibar, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni walezi wake alipokuwa anasoma nchini Marekani, *welcome to the Parliament. (Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Fred Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ally Kassinge, ambao ni Viongozi wa *Tanzania Human Resource and Administration Professionals Association* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Nyamagana Jijini Mwanza wakiongozwa na Ndugu Stella Gigaye. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni viongozi wa CCM kutoka Liwale, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa ambaye ni ndugu yake Diwani Mstaafu Kata ya Ulaya, Wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro, Dkt. Matokeo Erasto, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoa wa Tabora, Ndugu Alex Ntonge. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Francis Ndulane ambao ni Mameneja wa *RUWASA* kutoka Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Anatropia Theonest ambao ni Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi Wanawake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Agnesta Kaiza, ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Dkt. Manka Misana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Ole Shangai, ambaye ni mpiga kura wake na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Loliondo, Ndugu Emmanuel Mkwawa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, ambao ni Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Lindi, Ndugu Palina Ninje na Ndugu Petro Lusesa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili kutoka Taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya afya na maendeleo ya jamii ambao ni Ndugu Abdulkarim Nyambi na Ndugu Brayan Kilenzi**,** karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia na kuwakumbusha Wabunge wote kuwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia itaendesha semina kuhusu mapitio ya sera ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014 na mitaala ya elimu ili kuwajengea uelewa kuhusu taarifa na mapitio. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kupata maoni na ushauri wao. Semina hii itafanyika leo siku ya jumatano tarehe 10 Mei, 2023 mara tu baada ya kusitisha bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu kwa mustakabali wa elimu ya nchi.

Nina Dkt. James Andilie ni *CEO* wa *EWURA* na ni mume wake Spika. karibu sana; sasa najua kwa nini haya makofi. *(Makofi/vigelegele)*

Mgeni wa Mheshimiwa Waziri Aweso Ndugu Fatma Mary Masanga, ahaa tayari nilishataja.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**NAIBU SPIKA:** Sasa namuita Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri subiri kwanza. Naomba vilevile kuwatambulisha washiriki wote wa maendeleo, *all developing partners who are here today, thank you very much*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Mheshimiwa Jackson Gidion Kiswaga Mbunge Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maji na Mazingira, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Maji. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupatia uhai afya muda na amani, na kunijalia kusimamia hapa mbele. Napenda

kutoa shukrani zangu za dhati kwa kamati yangu pendwa ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Kiswaga na Makamu wake Ana Lupembe…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba utulivu wale wanaotoka nje mtoke kwa utaratibu unaotakiwa kibunge na wale wanaozungumza jaribuni kupunguza mazungumzo yenu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/2024. Maoni ushasuri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira yamezingatiwa wakati wa maandalizi wa bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi makini na thabiti katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake. Serikali ya Awamu ya Sita katika uongozi wake tumeshuhudia utendaji wenye maono, maridhiano, weledi, uwajibikaji, ujasiri, maarifa na ubunifu wa hali ya juu kwa manufaa mapana ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue fursa hii kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge na Waziri Mkuu kwa mchango wao mkubwa katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuijenga Tanzania kuwa nchi ya uchumi shindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi, na nimshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wanu mahiri wa kuliongoza Bunge

letu Tukufu. Vilevile naomba niwapongeze Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb), na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge na kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye Bunge letu Tukufu katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake mahiri aliyoiwasilisha hapa bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020 - 2025 vilevile nawapongeza mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa ruhusa yako naomba nitoe pongezi za dhati kwa *Dar Young African* kwa kuendelea kuupiga mwingi ndani na nje ya nchi katika kuhakikisha kwamba tunaliwakilisha vyema taifa letu. Na hapa niseme, asiyekubali kushindwa si mshindani. Leo *Dar Young African* wanaenda kuwakilisha taifa letu nataka niseme ukizaa mtoto anafanya vizuri jukumu lako ni kumuombea dua tunawaombea dua sana *Dar Young African*. Lakini kwa namna ya kipekee niipongeze *Simba Sports Club* tumejitahidi sana lakini tujipange zaidi katika ligi ya msimu ujao tuendelee kuupiga mwingi na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenye maeneo makuu matano kama ifuatavyo: -

i. Hali ya sekta ya maji nchini;
ii. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023;

iii. Mafanikio ya miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya maji
iv. Changamoto na hatua zilizochukuliwa na vipaumbele; na
v. Mpango utekelezaji kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Sera na mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 sheria kanuni pamoja na maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sekta ya maji nchini. Napenda kutoa maelekeza kuhusu hali ya sekta ya maji nchini kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji, ubora wa maji na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya rasilimali za maji zilizopo nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126, ambapo juu ya ardhi mita za ujazo bilioni 105 na maji chini ya ardhi mita za ujazo bilioni 21 hivyo kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 2,105 kwa idadi ya watu milioni 59.8 wa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kilichokubalika kimataifa. Kwa hiyo nchi haijaingia kwenye uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba nchi yetu inatarajiwa kufika kiwango cha wastani wa mita za ujazo 1700 kwa kwa mwaka kwa mtu ifikapo mwaka 2030. Aidha takwimu zinaonyesha kwamba mahitaji ya maji nchini kwa sekta mbalimbali kwa mwaka 2022 yalikuwa ni wastani wa mita za ujazo bilioni 62 na yanatarajiwa kufika mita za ujazo bilioni 75 mwaka 2030. Hivyo tunawajibu wa kuendelea

kuongeza msukumo katika utunzaji wa rasilimali za maji, kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji pamoja na kuongeza upatikanaji wa maji ikiwa pamoja na ujenzi wa mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni rasilimali muhimu na maji ni usalama wa taifa. Unapokuwa na maji ya uhakika maana yake una uhakika wa chakula, unapokuwa na maji tosherevu una uhakika wa nishati na unapokuwa na maji toshelevu una uhakika wa uchumi wa taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata vitabu vya dini vimezungumza suala la maji. Ukisoma isaya 12:1-6 imazungumzia pia suala la maji. Nataka niwaombe waheshimiwa Wabunge, suala la ulindaji na utunzaji wa vyanzo vya maji tulione kama mboni ya jicho, tulilinde na kulitunza kuhakikisha kwamba rasilimali hizi zinakuwa nufaishi kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Na kama nilivyozungumza, pamoja kwamba maji ni usalama wa taifa lakini pia uwepo wa maji ni uhakika na usalama wa ndoa za mama zetu katika kuhakikisha wanaendelea kulinda familia za wazee wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ubora wa maji ni kigezo muhimu katika kutoa maamuzi juu ya matumizi mbalimbali ya maji. Hali ya ubora wa maji katika maziwa mito na mabwawa chemchemi na visima inakidhi viwango hivyo na inaweza kuendelezwa na kutumika kwa matumizi mbalimbali ya shughuli za kiuchumi kijamii na mazingira. Aidha wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwekeza katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji ili kuhakikisha maji yanayotumika yanafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini. Hali ya huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwezi Desemba, 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 77 mwezi Desemba, 2022. Kiwango

hicho kimeongeza idadi ya wananchi 3,575,919 wanaopata huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini; hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya mijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 86.5 mwezi Desemba, 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi 2,345,537 wa maeneo ya mijini wanaopata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, haudma ya uondoshaji maji taka kaika maeneo ya mijini imeendelea kuimarika ambapo mtandao wa mabomba ya maji taka umeongezeka. Aidha kwenye miji ambayo haina mtandao wa huduma ya uondoshaji maji taka inatolewa kwa utaratibu wa magari na mabwawa ya kutibu maji taka katika Miji ya Geita, Kahama, Magu, Misungwi, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Bukoba na Lamadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti katika mwaka 2022/2023; upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2022/2023 Fungu Namba 49 Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 709. 36 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 51.46 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 657.89 ni fehda za maendeleo. Hadi mwezi aprili 2023 Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 686.37 sawa na silimia 96.76 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 648.08 ni za kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 38.29 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, asiyeshukuru watu hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru. Bajeti yetu ya Wizara ya Maji kwa miaka iliyopita tulikuwa tukitekeleza kwa asilimia 50 hadi asilimia 55, lakini kwa kipindi cha miaka miwili ya Rais

Samia Suluhu Hassan leo nawasilisha bajeti mbele yako ya asilimia 96, haijawahi kutokea, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi tumepokea malipo ya kandarasi mwezi Machi na mwezi huu wa Aprili zaidi ya bilioni 183. Nataka niwaelekeze watendaji wetu, fedha zilizoingia kwa ajili ya malipo ya wakandarasi ziende zikalipwe haraka ili wakandarasi huko *site* waende kutekeleza kazi nzuri ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. Nataka niwaambie wakandarasi wote popote walipo, pochi la mama limetema hamna kisingizio chochote, nendeni mkafanye kazi na sisi jukumu letu ni kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, programu na maendeleo mbalimbali yaliyotekelezwa katika mwaka 2022 hadi 2023. Wizara imeendelea kutekeleza programu ya maendeleo ya Sekta ya Maji, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi na mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; usimamizi na uendelezaji wa rasilimali unahusisha tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali za maji, kuhifadhi, kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2023, vituo 136 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vimekarabatiwa na vituo sita vimejengwa. Vibali vipya 1,554 vya matumizi ya maji na vibali 630 vya kuchimba visima vya maji vimetolewa. Leseni 105 zimehuishwa na vyanzo vya maji 63 vimewekewa mipaka. Vile vile ujenzi wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati na madogo umekamilika na ujenzi wa mabwawa 40 unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako niwahimize wananchi wote kwa ujumla wanaotaka kutumia maji kutoka katika vyanzo mbalimbali, wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji kutoka Bodi za Maji za Mabonde. Maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji rasilimali za maji yanapatikana ukurusa wa 15 hadi 28 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ubora wa maji; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara yangu kupitia Maabara za Ubora wa Maji imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji nchini. Vile vile Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira.  Jumla ya vyanzo vya maji 1,473 ambavyo ni mito, maziwa, chemichemi na mabwawa vilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa ubora wa vyanzo vya maji nchini na mitandao ya kusambaza maji ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wadau wote kutambua umuhimu wa kupima maji kabla ya kuyatumia kwa matumizi mbalimbali. Maelezo ya kina kuhusu huduma za ubora wa maji yanapatikana ukurasa wa 28 hadi 33 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za usambazaji maji safi na usafi wa mazingira ya vijijini; katika mwaka 2022/2023 Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji *(RUWASA)* ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,029 ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Hadi mwezi Aprili 2023, miradi 586 imekamilika na miradi mingine utekelezaji wake unaendelea. Aidha, katika kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya vyombo 111 vya watoa huduma ya ngazi ya

jamii *CBWSO* zimeundwa na kusajiliwa na hivyo kuwa jumla ya *CBWSOs* 2,515 zilizosajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji imeanzisha Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)* kwa minajimu ili iende ikatatue matatizo mahususi katika maeneo ya vijijini. Nataka nikuhakikishie *RUWASA* tangu kuanzishwa kwake inafanya kazi nzuri na tunapaswa kuwapongeza sana. Kazi ambayo tuliyokuwa nayo kama Wizara na kupitia Taasisi yetu ya *RUWASA* ni kuhakikisha miradi ambayo tunaijenga lazima iwe endelevu. Leo ukiangalia shule kama hakuna Kamati basi kuna Mwalimu na ukiangalia zahanati kama hakuna Daktari, basi kuna Nesi, lakini leo miradi ya maji vijijini inakuwepo Kamati lakini mtaalam hayupo. Hata kama inaharibika koki mradi wa bilioni nne unaharibika, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge sasa hivi katika kila mradi ambao tumeweka Kamati basi tunakuwepo na mtaalam, kwa maana ya mhasibu lakini kwa maana pia na *technician* ili kuhakikisha kama miradi yetu inakuwa endelevu na niseme hapa kupitia jumuiya hizi za watumiaji maji, zimeajiri jumla ya wataalam 5,296 kwa ajili ya uendeshaji. Kwa hiyo, pamoja na ujenzi wa miradi ya maji, lakini miradi ya maji vijijini imeleta fursa kwa vijana katika kuhakikisha wanapata suala zima la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji kupitia *RUWASA* inatekeleza Programu ya Uendelevu ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini - *Program for Result (P4R),* ambapo fedha hizo hutolewa na matokeo ya utendaji. Awali programu hii ilianza kutekelezwa katika mikoa 17, Mikoa ya Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tabora. Awali programu hiyo ilitengewa dola milioni 350. Katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wake, programu

imeonyesha mafanikio yaliyopelekea Benki ya Dunia kuongeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 300 na kufanya kuwa jumla ya dola milioni 650. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)* tuna programu hii inayoitwa *P4R* ambayo tumeianza kwa kupata fedha dola milioni 350. Kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imeifanya leo Benki ya Dunia imeeleza kwamba *RUWASA* ina *lead* katika utekelezaji wa miradi ya maji na tumeongezewa fedha zingine zaidi ya dola milioni 300 na kufikisha dola milioni 650. Miradi hii kwa maana hii programu ya *P4R* tulikuwa tukiitekeleza kwa mikoa 17. Tumepata maelekezo ya Mheshimiwa Rais, sasa mikoa yote nchini isipokuwa Dar es Salaam yote tunakwenda kutelekeza programu hii katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza utolewaji wa fedha unatokana na matokeo ya utendaji ambapo anayefanya vizuri anapata fedha nyingi zaidi. Kwa mfano, Halmashauri ya Nzega ilianza kwa kupewa fedha za awali shilingi bilioni 1.3 mwaka 2020/2021 na mwaka 2022 imeweza kupata shilingi bilioni 10.3 kutokana na utendaji wake mzuri kwa fedha za programu hii. Programu hii itatekelezwa kwa mikoa 25 yote, Mikoa iliyoongezeka ni Njombe, Mbeya, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma, ambapo kwa kila halmashauri Waheshimiwa Wabunge naomba niwaeleze, katika kila halmashauri ya wilaya itapewa shilingi milioni 961 kama fedha za awali. Kwa hiyo, kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge, maendeleo ya Sekta ya Maji yanaanza na mimi, maendeleo ya Sekta ya Maji yanaanza na wewe. Ukisoma Ezra inasoma "inuka hii shughuli inakuhusu na ukaitende kwa moyo mkuu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wasaidizi wa Mheshimiwa Rais tupo pamoja na wewe. Waheshimiwa Wabunge fedha hizi zimepelekwa kwa ajili ya kuleta matokeo chanya katika majimbo yetu. Niwaombe sana kwenda kusimamia na kufuatilia ili kuhakikisha matokeo chanya yanatokea ya kuhakikisha azma ya Rais ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inatimilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini; Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji mbalimbali. Katika mwaka 2022/2023, jumla ya miradi 175 ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2023 miradi 40 imekamilika na miradi 135 inaendelea na ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Mbeya; Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka chanzo cha Mto Kiwila kupeleka katika Jiji la Mbeya kwa gharama ya shilingi bilioni 117. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 hadi lita milioni 184 kwa siku na kuimarisha hali ya huduma ya maji kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95. Upo msemo unaosema "ukipigana vita ugenini nyumbani lazima kuwe na amani".

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana na mimi, Spika wetu akishirikiana na Naibu Spika wanafanya kazi kubwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu letu kama Waziri na Naibu wangu Waziri wa Maji ni kuhakikisha maeneo yao yanakuwa na amani katika kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma; katika mpango wa muda mfupi wa

kuboresha huduma ya maji kwenye Jiji la Dodoma, Serikali inaendelea na utekelezaji wa maji Nzuguni unaogharimu shilingi bilioni tano. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 68.7 hadi lita milioni 76.3 kwa siku na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swawa na Kisasa. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika kwa ajili ya Jiji la Dodoma ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Farkwa na kuyatoa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani. Serikali inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani na baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji safi ambao umekamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Machi 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Usambazaji katika Maeneo ya Mbezi Makabe na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji na Mpera; katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa kipindi chote cha mwaka, Serikali imeanza ujenzi wa Bwawa la Kidunda na mkandarasi yuko eneo la kazi na malipo ya awali shilingi bilioni 49 yamekwishafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji Safi katika Jiji la Mwanza; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Kusafisha na Kutibu Maji katika Eneo la Butimba kwa gharama ya shilingi bilioni 69. Hadi mwezi Aprili

2023 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 71. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023 na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Jiji la Mwanza, Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Bugando, Bucherere, Rwanima, Sahwa, Khumagira, Kishiri na Igoma na utakwenda hadi Magu kwa maana Eneo la Kisesa, Bujora, Nakanyama na Wilaya ya Misumbwi, Usagara, Fela, Bukumbi hadi Nyashishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa pia tumepokea ombi maalum la Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, mama yangu Angeline Mabula kwamba twende tukajenge chanzo kipya cha eneo la Kabangaja. Nataka nimhakikishie sisi Waziri ya Maji hatutokuwa kikwazo kwa wananchi wa Ilemela kuendelea kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mugango, Kiabakari, Butiama; Serikali inatekeleza Mradi wa Maji wa Mugango, Kiabakari, Butiama kwa gharama ya bilioni 70.5. Hadi mwezi Aprili, 2023, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 79 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/2024. Mradi huo utawanufaisha wakazi laki moja waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilometa 12 kutoka bomba kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Simiyu, Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu; Mradi huu unatekelezwa kwenye Wilaya tano za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa gharama ya Shilingi bilioni 444.6. Hadi mwezi Aprili, 2023, kiasi cha Shilingi bilioni 1.97 kimetumika kulipa fidia kwa wananchi wapatao 1,364 kati ya wananchi 1,395 waliofanyiwa uthamini. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi zinaendelea na utekelezaji unatarajiwa kuanza katika mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28; Serikali imeanza utekelezaji wa mradi huo unaogharimu shilingi trilioni 1.48. Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wamepatikana na wameanza maandalizi ya awali maeneo ya ujenzi pamoja na kukamilisha kazi ya usanifu. Miji itakayonufaishwa na mradi huu ni Kilwa Masoko, Nanyumbu, Makonde, Njombe, Makambako, Wang'ing'ombe, Ifakara, Chunya, Rujewa, Singida, Kiomboi, Manyoni, Chamwino, Chemba, Mugumu Serengeti, Tarime, Rorya, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kasulu, Mpanda, Songea, Geita, Chato, Kayanga, Mafinga, Handeni, Korogwe, Muheza na hadi Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapaswa kushukuru kwa kila jambo. Eneo ambalo sisi Wizara ya Maji Bunge lako lilitukalia kooni ni eneo la Miji 28, lakini kwa namna ya kipekee nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais kwa kuukwamua mradi huu. Leo hii nazungumza mbele ya Waheshimiwa Wabunge, nataka niwaambie ukiona giza linatanda ujue kumekucha. Leo wakandarasi ambao wanautekeleza mradi huu wa miji 28, tunao na wameshalipwa *advance payment*. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, huu ni mradi ambao unaenda kutatua matatizo ya maji kwa kiwango kikubwa. Twende tukausimamie kwa pamoja ili kuhakikisha azma ya Rais wetu ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inakwenda kutimilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji katika Miji mingine; miradi mingi inatekelezwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika miji na majiji, mfano Arusha, Tanga, Manispaa za Morogoro, Shinyanga hadi Mtwara Mikindani na Miji ya Tunduma, Tinde mpaka Shelui. Maelezo ya kina kuhusu huduma ya maji safi na usafi wa mazingira mijini inapatikana katika ukurasa wa 41 hadi 56 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maji; katika kipindi cha miaka miwili 2021 hadi 2022 ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa wa wananchi wake, mwenye dhamira njema ya kumtua mama ndoo kichwani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta ya maji. Mafanikio hayo ni pamoja na mageuzi makubwa ya kiutendaji yaliyofanyika kwa watumishi 9,422 waliopo ambao wamechangia mafanikio makubwa ya sekta kutokana na kuwa na ari ya kazi, kujituma, weledi na kubeba maono mema ya Rais wetu ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe tarehe 22 Mwezi wa Nne, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan alihutubia katika Bunge lako Tukufu na alitoa maelekezo mahususi katika Wizara yetu ya Maji. Alisema kwamba yeye ni Mama hataki kusikia akinamama wa nchi wanateseka juu ya adha ya maji. Nataka nikuhakikishie baada ya maelekezo yale, Wizara ya Maji imebadilika sana. Watendaji wa Wizara ya Maji wanafanya kazi kubwa Waheshimiwa Wabunge hapa tuwapongeze sana maaskari wetu wa Wizara yetu ya Maji. Hata maeneo ambayo hayajawahi kuona maji leo yanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda zako Mafia hadi Jibondo wanapata maji kwenye visiwa. Leo ukienda zako Isimani kwa Mheshimiwa Lukuvi hadi eneo la Kijiji cha Malenga Makale ambao hawajawahi kuona maji, leo wanapata huduma ya maji. Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika miaka miwili hii ni kukamilika kwa miradi 1,373 ya usambazaji maji imenayotoa huduma katika vijiji 2,649 na kufikisha jumla ya vijiji 9,737 vinavyopata huduma ya maji nchini. Kukamilika kwa miradi 80 ya usambazaji maji mijini ambayo inatoa huduma kwa wananchi 4,305,801; Kukwamuliwa kwa miradi 157 kati ya miradi 177.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na miradi ambayo miaka ya nyuma ilikuwa imejengwa imekamilika, lakini haitoi maji. Miradi ile ilikuwa inaitwa chechefu, tangu kuundwa kwa *RUWASA* tulibainisha miradi 177, ndani ya muda mfupi miradi 157 tumeweza kuikwamua na wananchi wanaweza kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa mfumo wa takwimu wa miradi kwa maana ya maji *App* na Mfumo wa Usimamizi wa Ankara za Maji yaani *Unified Billing System;* Kuongezeka kwa maabara za ubora wa maji zenye hadhi ya ithibati kutoka maabara moja ya Mwanza iliyokuwepo mwaka 2021 hadi kufikia maabara saba. Maabara hizo ni Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam, lakini pia kuanza kwa ujenzi wa Mabwawa ya Kidundwa na Farkwa na mradi ambao umekwama kwa muda mrefu wa Same Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona kabisa katika Nchi yetu ya Tanzania tuna takribani vijiji 12,318, lakini kwa muda mpaka sasa, tumeweza kuvifikia vijiji 9,737 na tuna vijiji takribani 3,000 ambavyo tunatakiwa tuongeze jitihada za kuhakikisha kwamba wananchi wanapata miradi rasmi ili kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametununulia magari ya uchimbaji visima zaidi ya 25 katika kuhakikisha kila mkoa unapata gari hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ambayo tumeyatoa kwa Wahandisi wa Maji wa Mkoa na Wilaya katika kila Kijiji ambacho wanaweza wakapata maji kwa kuchimba kisima tutakwenda kuchimba kisima, maeneo ambapo tunaona tumechimba kisima hatupati maji tutachimba mabwawa. Kwa mfano, eneo la Kiteto tumefanya jitihada nyingi kuhakikisha kwamba watu wanapata maji kwa uchimbaji wa visima lakini

eneo lile linahitaji mabwawa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kuchimba mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Meatu ambalo tumepata taabu kwa muda mrefu, nataka nimtie moyo ndugu yangu na Mama yangu Mheshimiwa Mbunge wa Meatu, tumejipanga vizuri, mitambo seti tano tumepata tunakwenda kuichakaza Meatu ili kuhakikisha wananchi wa Meatu wanaenda kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanyika kwa marekebisho Namba Nane ya mwaka 2022 na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba 11 ya mwaka 2009 ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maji ilipotoka ni mbali sana. Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maji ilikuwa Wizara ya kero na lawama, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kimfaacho mtu chake. Tumempata Rais wetu Samia Suluhu Hassan lazima tumtumie kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Samia Suluhu Hassan hapatikani kila mahali. Aina ya Rais Samia Suluhu Hassan hawapatikani kila wakati. Naomba tushirikiane nae ili kuhakikisha kwamba dhamira yake njema ya kumtua mwanamama ndoo kichwani inatimilika na kuhakikisha azma ya Chama chetu, Chama cha Mapinduzi itakapofika 2025, asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mjini inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa. Changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya maji ni mahitaji makubwa ya fedha za uwekezaji kwenye miradi mikubwa hasa miradi ya kimkakati, uharibifu wa vyanzo

vya maji unaotokana na uvamizi na uchafuzi na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa zikiwemo kuendelea kufufua, kutafuta fedha, k wa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maji, kushirikiana na wadau katika kutekeleza uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji na kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo na maono ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ni kwenda kutumia rasilimali za maji toshelevu, kwenda kutumia maziwa, kwenda kutumia mito mikubwa ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua matatizo kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu Mwenyezi Mungu ameijalia, leo ukienda Kanda ya Ziwa tuna Ziwa Victoria, ukienda eneo la Kigoma, ukienda eneo la Katavi, ukienda eneo la Rukwa tuna Ziwa Tanganyika. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha tunakwenda kutumia rasilimali toshelevu ili kuhakikisha tunakwenda kutatua changamoto kwa wananchi na kazi hii tumeshaianza. Tumeweza kuyatoa maji ya Ziwa Victoria tumeyapeleka Rorya – Tarime, tunayapeleka yanaenda mpaka Tarime Mjini mpaka Vijijini. Tunao Mradi wa Mugango, Kyabakari, Butiama lakini tumeyapeleka maji Tabora, Igunga, Nzega. Maelekezo ambayo tumeyapata tuyapeleke Kaliua, tuyapeleke Sikonge na mpaka Urambo kwa Mama Sitta, kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma, nataka niwahakikishie Wabunge wa Rukwa na Katavi, dhamira hii njema ambayo

imefanywa na Rais wetu katika maeneo mengine huu ni muda muafaka katika kuhakikisha Ziwa Tanganyika kwa maana ya eneo la Kigoma kwa maeneo ya Rukwa, kwa maeneo ya Katavi tunakwenda kuianza kazi hii na wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, leo miaka ya nyuma Baba wa Taifa alivyokuwa anakwenda kupigana Vita na Idd Amini alisema maneno machache, "Nia tunayo, uwezo tunao na sababu tunayo." Nataka niwaambie Waheshimiwa wa Kigoma na Waheshimiwa Wabunge wa Katavi na Rukwa, sababu na nia tunayo katika kuhakikisha tunaenda kuuanza mradi ule ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu changamoto na hatua za kukabiliana nazo yanapatikana ukurasa wa 73 hadi 75 wa Kitabu cha hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele na mpango wa utekelezaji wa mwaka 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024 Serikali imepanga kuwa na vipaumbele vifuatavyo:-

a) Kukamilisha Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002,
b) Kuimarisha usimamizi na kuendeleza rasilimali za maji,
c) Kuwa na mtandao wa Taifa wa maji kwa maana ya *National Water Grid,*
d) Kuwa na mpango kabambe wa usambazaji maji yaani *water supply master plan,*
e) Kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji,
f) Kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea,

g) Kukabiliana na upotevu wa maji yaani *non-revenue water,*
h) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili kuwa na huduma endelevu ya upatikanaji wa maji,
i) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Miji 28,
j) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya usafi wa mazingira,
k) Kuendelea na ujenzi wa mabwawa madogo yenye ukubwa wa kati na makubwa yakiwemo Kidundwa na Falkwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi,
l) Kuandaa na kutekeleza *program* ya uwekezaji kwenye Sekta ya Maji *(Tanzania Water Investment Program)* katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2030 kwa ajili ya kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Maji,
m) Kuimarisha taasisi za Wizara ya Maji ikiwemo Chuo cha Maji, Mfuko wa Taifa wa Maji na *RUWASA* na
n) Kuimarisha ushirikiano wa ushirikishwaji na wadau wa Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji haiwezi kufanya kazi pekeyake. Wizara ya Maji lazima tushirikiane na wadau kwa maana ya sekta mbalimbali. Upo msemo unaosema, "Jamii ipo tu, ukiishirikisha utafanikiwa, usipoishirikisha utakwama." Nataka nilihakikishie Bunge lako tukufu Wizara ya Maji tutaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge na wadau wote wa maendeleo katika kuhakikisha kwamba sekta ya maji inasonga mbele. Maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na mimi, maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na wewe, maendeleo ya sekta ya maji yanaanza na sisi kwa kushikamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu vipaumbele na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2023/2024 yanapatikana ukurasa wa 76 hadi 82 wa kitabu cha hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Ukimuona kobe juu ya mti ujue amepandishwa. Nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote wanaochangia kufanikisha utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Maji. Michango, maoni na mapendekezo yao yamezingatiwa katika maandalizi ya Bajeti ya Wizara yangu. Kwa mara nyingine napenda kuishukuru Kamati yangu pendwa ya Kudumu ya Maji na Mazingira na Bunge lako Tukufu kwa maoni, ushauri na maelekezo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nayashukuru Mashirika ya Maendeleo na Taasisi za Kimataifa kwa misaada ya kitaalamu na kifedha katika kuiwezesha Sekta ya Maji kutekeleza majukumu yake. Mashirika na taasisi hizo ni pamoja na *World Bank,* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB),* Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(AKFW),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Benki ya Exim ya India, Mfuko wa Maendeleo ya Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OFID),* Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund),* Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD), Foreign Commonwealth,* Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GiZ),* Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), *Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF),* Shirika la Afya Duniani *(WHO),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Maendeleo la Ubelgiji *(ENABEL),* Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kuzishukuru taasisi zote za kidini kwa kuendelea kushirikiana na Sekta ya Maji katika utoaji wa huduma na kuliombea Taifa letu na viongozi wetu. Aidha, nikishukuru Chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa maelekezo na usimamizi katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025. Nataka niwahakikishie mimi Juma Aweso pamoja timu nzima ya Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo

katika kuhakikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka na asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mjini inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninazishukuru taasisi zisizo za kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza sekta ya maji ambazo ni *Global Water Partnership, Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS), OIKOS, TAWASANET, WAMMA, World Vision*, *WWF*, *SNV, WaterAid*, *Water Mission*, *Life Water International,* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Maliasili (*IUCN*) na Mashirika mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kufika haraka, nenda pekeyako lakini ukitaka kufika mbali nenda na wenzako. Ninaomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu wa Wizara ya Maji. Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi Mbunge - Naibu Waziri wa Maji ambaye ameendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu tuliyopewa, akifanya kazi kubwa kuhakikisha sekta ya maji inasonga mbele na wananchi wengi zaidi wanafanikiwa na huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwapongeza Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba *(STK)* wa Wizara ya Maji kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Mhandisi Cyprian John Luhemeja Sankara kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, imani na dhamana waliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa na ninaamini katika utendaji wao tutafanya mageuzi makubwa katika kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee niwashukuru Wenyeviti wangu wa Bodi wote katika taasisi zote kwa usimamizi mzuri na kuleta matokeo chanya katika taasisi zetu zikiwemo mamlaka ya *RUWASA* na maeneo mengine

katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama. Pia niwapongeze na kuwashukuru viongozi wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Watumishi wote wa Wizara ya Maji na taasisi zake, wazabuni hususani Wakandarasi, wataalamu washauri, *suppliers* wote bila kuwasahau Watendaji ambao wamekuwa bora muda wote, Madereva, Ma-*Secretary* na Makatibu Muhtasi ambao wanafanya kazi kubwa katika Wizara yetu ya Maji, wanaopatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na nguvu ya kuwatumikia Watanzania katika sekta ya maji na kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Naomba niishukuru familia yangu na wake zangu wapendwa Kauthari Francis Tarimo na Zainab Abdallah Issa (Mkuu wa Wilaya ya Pangani) pamoja na Wananchi wa Jimbo la Pangani kwa maombi na dua na upendo, ushirikiano, faraja na uvumilivu kuendelea kunilea na kuniamini kutekeleza majukumu yangu. Ninaahidi kuendelea kutumia maarifa yangu yote kwa kujenga Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nimpongeze na kumshukuru sana Mama yangu Mzazi Fatuma Omari Masanga. Mama sina cha kukulipa, Mwenyezi Mungu ndiye atakayekulipa lakini pamoja na familia yangu Baba zangu, Shangazi zangu, ndugu, jamaa na marafiki wote mliokuwepo hapa ndani ya Bunge na nje ya Bunge, kwa ushirikiano mkubwa ambao mnanipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri

wa Maji na mimi namuahidi kufanya kazi kwa nguvu na maarifa ili kufikia malengo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024. Baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwa Bunge lako Tukufu liliidhinishe jumla ya shilingi 756, 205,106,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/2024. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi 60,375,474,000 ambapo shilingi 18,035,561,000 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo *(OC)* na shilingi 42,339,913,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 695,829,632,000 ambapo kati ya fedha hizo ni shilingi 407,064,860,000 ni fedha za ndani na Shilingi 288,764,772,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kusikiliza hotuba hii, pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.maji.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2023/24 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na **Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga (Mb**), iliyochambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2022/23 ninaomba sasa

kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana kwa siku ya leo tukiwa na afya njema. Aidha, kwa unyenyekevu mkubwa ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema na kutupa busara na hekima katika kujadili wasilisho la hotuba yangu pamoja na bajeti nzima ya Serikali kwa nia njema ya kuendeleza nchi yetu na kuboresha ustawi na maendeleo ya wananchi wetu.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee na kwa dhati ya moyo wangu napenda kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa uongozi makini na thabiti katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake wa Serikali ya Awamu ya Sita. **Mheshimiwa Rais** ameonesha uongozi mahiri na uliotukuka kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa mafaniko makubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita tumeshuhudia utendaji wenye maono, maridhiano, weledi, uwajibikaji, ujasiri, maarifa na ubunifu wa hali ya juu kwa manufaa mapana ya Taifa letu. Aidha, **Mheshimiwa Rais** ameendelea kuimarisha mahusiano na mashirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine pamoja na taasisi na jumuiya za kimataifa. Ninamuomba Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu afya njema na amzidishie busara na hekima ili aendelee kutekeleza majukumu yake.

**4. Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri wa Maji. Kwa heshima na imani aliyonipa ninaahidi kuitumikia nafasi hii kwa

uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote kuhakikisha matarajio yake kwangu yanafikiwa na kubwa zaidi ni kuhakikisha huduma ya maji safi, salama na ya kutosha inawafikia wananchi wote.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea wananchi maendeleo, amekuwa akitekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa katika kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele na kupata maendeleo endelevu.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii pia, kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni**, kwa uongozi wake mahiri, ufuatiliaji na kusimamia uwajibikaji serikalini. Sote ni mashahidi wazuri wa namna anavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu akiwa ndani na nje ya Bunge.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira** kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati umetusaidia sana wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu. Napenda kuiahidi Kamati hii kwamba tutaendelea kutoa ushirikiano kwao, kupokea maoni na ushauri wao na kuufanyia kazi ili kuboresha utendaji na mipango ya Sekta ya Maji.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba niwakushukuru **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu**

**(Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa uongozi wenu mahiri wa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Vilevile, naomba niwapongeze **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mb) na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge na kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye Bunge letu Tukufu. Aidha, natoa pongezi kwa wabunge wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatumikia wananchi na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kwenye maeneo yao.

**9. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na watanzania wote kwa msiba uliotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa **Mbunge wa Jimbo la Amani, Mheshimiwa Hassan Mussa** uliotokea tarehe 13 Oktoba, 2022 huko Zanzibar. Mchango wa Mbunge huyo katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu utakumbukwa milele daima. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

**10. Mheshimiwa Spika,** naomba pia nichukue fursa hii, kumpongeza **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa hapa bungeni, hotuba ambayo inatoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba yake imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha mwaka 2022/23 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025). Vilevile, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

**11. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Sera; Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025); Sheria, Kanuni pamoja na maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

**12. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu iliyojikita katika maeneo makuu matano (5) yafuatayo:-

i) Mafanikio ya Miaka Miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita;
ii) Hali ya Sekta ya Maji nchini;
iii) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2022/23;
iv) Changamoto na Hatua zilizochukuliwa; na
v) Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24.

## 2. MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI (2) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MAJI

**13. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka miwili (2021 - 2022) ya Serikali ya Awamu ya Sita mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta ya maji. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

(i) Kukamilika kwa **miradi 1,373** ya usambazaji maji na kuanza kutoa huduma kwa wananchi waishio katika vijiji **2,649** ambako kunafikisha jumla ya **vijiji 9**,**737** vyenye huduma ya maji nchini;
(ii) Kukamilika kwa miradi **80** ya usambaji maji miji na kuanza kutoa huduma kwa wananchi **4,305,801**;
(iii) Kukwamuliwa kwa miradi **157** na kuanza kutoa huduma kati ya miradi **177** ya vijijini iliyokuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa muda mrefu;

(iv) Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi **218** kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO -19 inayohudumia wananchi wapatao milioni **2.09** ambapo miradi **44** imetekelezwa mijini na miradi **174** vijijini;

(v) Kuongezeka kwa maabara za ubora wa maji nchini zenye hadhi ya Ithibati kutoka Maabara moja (1) ya Mwanza iliyokuwepo mwaka 2021 hadi kufikia Maabara Saba (7). Maabara hizo ni maabara za ubora wa maji Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam;

(vi) Kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa maji katika miji 28 yenye thamani ya **Shilingi Trilioni 1.48** baada ya kusainiwa kwa mikataba ya ujenzi mwezi Juni, 2022;

(vii) Kuanza ujenzi wa bwawa la Kidunda linalogharimu **Shilingi Bilioni 329.46** ili kuhakikisha maji yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani;

(viii) Kukamilika kwa ujenzi wa **mabwawa 10** ya ukubwa wa kati ya kuvuna maji ya mvua katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji hususan kipindi cha ukame;

(ix) Kununuliwa na kuanza kutumika kwa **seti 25** za mitambo ya kuchimba visima na **seti tano (5)** za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Mitambo hiyo inarahisisha uchimbaji wa visima na mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini;

(x) Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji ya Tinde na Shelui wenye uwezo wa kunufaisha wananchi wapatao **86,980**;

(xi) Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa choteo la maji kwa ajili ya mji wa Kigoma na kuwezesha wananchi wapatao **215,000** kupata huduma ya uhakika ya maji safi na salama;

(xii) Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa Mradi wa Maji wa Kyaka-Bunazi, Wilaya ya Missenyi-Kagera ambao

umewezesha wananchi wapatao **75,000** kupata huduma ya maji safi na salama;

(xiii) Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa mradi wa kusambaza majisafi katika mji wa Orkesumet wilayani Simanjiro unaonufaisha wananchi wapatao **52,000** pamoja na mifugo;

(xiv) Kuzinduliwa kwa Mpango wa Uhifadhi wa Vidakio vya Maji nchini wa mwaka 2021 hadi 2035 ambapo katika utekelezaji wa Mpango huo, ilizinduliwa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji wa Miti rafiki wa maji kwenye vyanzo vya maji ambapo jumla ya miti rafiki wa maji **2,541,803** imepandwa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji katika Mabonde yote tisa nchini;

(xv) Kufanyika kwa Marekebisho Na.8 ya mwaka 2022 ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini;

(xvi) Kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji nchini ambapo jumla ya vyanzo **150** vimewekewa mipaka ya kuanisha maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji na jumla ya vyanzo vya maji **41** vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu ya hifadhi ya maji hivyo kufikisha jumla ya vyanzo 59 vilivyotangazwa;

(xvii) Chuo cha Maji kilifanikiwa kudahili wanafunzi 2,847 na jumla ya Wahitimu 464 walifuzu mafunzo yao, machapisho ya kisayansi 21 yalitolewa, mabweni matano (5) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 916 yalikarabatiwa, majengo ya madarasa 15 na ofisi 17 yalikarabatiwa na magari matatu (3) yalinunuliwa; na

(xviii) Kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa na Sekta ya Maji. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Pamoja wa Ankara za Maji (*Unified Maji Billing System)* unaofahamika kama '*MAJIIS*', Mfumo Jumuishi unaosaidia kusimamia Shughuli za Taasisi (*Enterprise Resource Management Suite*) na

Mfumo wa Taarifa za Miradi unaopatikana kwa njia ya Simu za Kiganjani unaofahamika kama '*Maji App*'.

**14. Mheshimiwa Spika;** kwa ujumla katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama imeimarika kwa wananchi wa vijijini kutoka wastani wa **asilimia 70.1** mwaka 2020 hadi **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022 na kwa upande wa maeneo ya mijini kutoka wastani wa **asilimia 84** mwaka 2020 hadi wastani wa **asilimia 88** mwezi Desemba, 2022.

## 3. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

**15. Mheshimiwa Spika**, hali ya Sekta ya Maji nchini inajumuisha hali ya rasilimali za maji; ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini. Maelezo kuhusu hali ya Sekta ya Maji ni kama ifuatavyo:-

### 3.1 Hali ya Rasilimali za Maji

**16. Mheshimiwa Spika,** tafiti zilizofanywa na Wizara yangu zinaonesha kuwa rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kila mwaka nchini ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka. Kiasi hicho kinahusisha maji juu ya ardhi **(mita za ujazo bilioni 105)** na maji chini ya ardhi **(mita za ujazo bilioni 21)** kwa mwaka. Upatikanaji huo wa maji unaonesha kuwa kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa **mita za ujazo 2,105** kwa idadi ya watu **milioni 59.8** wa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Kiasi hicho kipo juu ya kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa cha wastani wa mita za ujazo 1,700. Hali hiyo, inaonesha kuwa nchi yetu ipo juu ya kiwango cha uhaba wa maji (*water stress*). Hata hivyo, kutokana na ongezeko la idadi ya watu kiasi cha maji kwa mtu

kwa siku kinatarajiwa kupungua hadi kufikia mita za ujazo 883 ifikapo mwaka 2035.

**17. Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa mahitaji ya maji nchini kwa sekta mbalimbali mwaka 2022 yalikuwa ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 62** na yanatarajiwa kuongezeka na kufikia **mita za ujazo bilioni 80.2** mwaka 2035. Mahitaji hayo yataendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la watu, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali hususan kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi na wanyama pori. Kwa upande mwingine, uharibifu wa mazingira hususan kwenye vyanzo vya maji, uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi na matumizi mabaya ya maji husababisha kupungua au kukauka kwa maji katika vyanzo.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa kihaidrolojia wa Novemba 2021 – Oktoba 2022 wastani wa mvua iliyonyesha ni **milimita 1,023.9** ambapo katika kipindi hicho maeneo ya ukanda wa magharibi yalipata mvua za wastani wa **milimita 700 hadi 1,100**, ukanda wa kaskazini umepata mvua za wastani wa **milimita 950 hadi 1,350**, ukanda wa nyanda za juu kusini ulipata mvua za wastani wa **milimita 1,050 hadi 1,250**, ukanda wa pwani ulipata mvua za wastani wa **milimita 970 hadi 1,220**. Takwimu hizo zinaonesha kwamba maeneo ya ukanda wa kaskazini na nyanda za juu za kusini yalipata mvua nyingi kuliko maeneo mengine ya nchi.

### 3.2 Hali ya Ubora wa Maji

**19. Mheshimiwa Spika**, ubora wa maji ni kigezo muhimu katika kutoa maamuzi juu ya matumizi mbalimbali ya maji kwa lengo la kulinda afya ya jamii na mifumo ya ikolojia. Ubora wa maji katika vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi nchini hutofautiana

kutoka eneo moja hadi jingine kutokana na hali ya miamba ya asili, shughuli za kibinadamu, jiografia ya eneo na mabadiliko ya tabianchi. Hali ya ubora wa maji katika vyanzo vya maji nchini inaonesha vyanzo vingi vinaweza kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali, ingawa kumekuwepo na changamoto ya madini ya *Fluoride* katika mikoa iliyopo katika ukanda wa *Fluoride*; Chumvichumvi katika ukanda wa Pwani; na madini Chuma na Manganese ukanda wa kusini na ukanda wa nyanda za juu kusini.

**20. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia viwango vya ubora wa maji kwa matumizi ya kunywa na kupikia, Ujenzi, Umwagiliaji, Ufugaji wa samaki na Mazingira; ubora wa maji katika vyanzo vya maji, mifumo ya usambazaji maji mijini na vijijini, kwaujumla umeendelea kukidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwekeza katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo ya kisasa ya kuboresha ubora wa maji ili kuhakikisha maji yanayotumika kwa matumizi ya kunywa ni safi na salama.

### 3.3 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

**21. Mheshimiwa Spika,** lengo la Serikali ni kuwapatia wananchi waishio vijijini huduma ya majisafi na salama kufikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025. Katika kutimiza lengo hilo, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwezi Desemba, 2021 hadi kufikia wastani wa **asilimia 77** mwezi Desemba, 2022. Kiwango kilichoongezeka kimetokana na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi **586** yenye vituo **5,748** vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao **4,086,442** kwenye **vijiji**

**1,293**. Hali hiyo, inafanya jumla ya wananchi wa vijijini wanaopata huduma ya maji kuwa 30,209,409.

### 3.4 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**22. Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi waishio mijini imeendelea kuimarika kutokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ya mijini. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 86.5 mwezi Desemba, 2021 hadi wastani wa **asilimia 88** mwezi Desemba, 2022. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi ya maji mjini 40 inayohudumia wakazi 2,345,537 wa maeneo ya mijini.

**23. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika maeneo ya mijini ambayo hutolewa kwa njia ya mfumo wa mabomba na magari ya majitaka. Katika kuboresha huduma utekelezaji wa miradi ya uondoshaji majitaka umeendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Utekelezaji huo, umeongeza mtandao wa majitaka kutoka kilomita 1,385.8 mwezi Aprili 2022 hadi kilomita **1,416.93** mwezi Aprili 2023. Pia, maunganisho yameongezeka kutoka wateja 53,428 mwezi Aprili 2022 hadi wateja **56,923** mwezi Aprili 2023. Aidha, katika miji ya Geita, Kahama, Magu, Misungwi, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Bukoba na Lamadi huduma ya majitaka inatolewa kwa mfumo wa magari na mabwawa ya kutibu majitaka.

## 4. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### 4.1 Upatikanaji wa Fedha

**24. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023, Fungu 49 – Wizara ya Maji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 709,361,607,000** na kati ya fedha hizo **Shilingi 51,462,269,000** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 657,899,338,000** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 686,370,565,613.50** sawa na asilimia **96.76** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 648,076,417,279.05** ni za kutekeleza miradi ya maendeleo na **Shilingi 38,294,148,334.45** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

#### 4.1.1 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Maji - Fungu 49 ilitengewa jumla ya Shilingi **51,462,269,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **34,761,735,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji na Shilingi **16,700,534,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji.

**26.** Hadi mwezi Aprili, 2023 jumla ya **Shilingi 42,344,977,711.37** sawa na asilimia **82.28** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,526,821,578.15** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 10,818,156,133.22** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

#### 4.1.2 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**27. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2022/23, Wizara ya Maji - Fungu 49 ilitengewa

Shilingi 657,899,338,000. Kiasi hicho kinajumuisha Shilingi 407,064,860,000 fedha za ndani na Shilingi 250,834,478,000 fedha za nje.

**28. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 623,753,326,424.64** sawa na asilimia **94.81** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/23. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 374,794,312,195.31** sawa na **asilimia 92.07** ni fedha za ndani na fedha za nje ni Shilingi **248,959,014,229.33** sawa na **asilimia 99.25**.

## 4.2 Utekelezaji wa Programu na Miradi Mbalimbali ya Maendeleo

**29. Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Wizara imeendelea kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Tatu (2022/23 – 2025/26). Hali ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali katika mwaka 2022/23 katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara; masuala mtambuka; na changamoto na hatua za kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:-

### 4.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

#### 4.2.1.1 Usimamizi wa Rasilimali za Maji

**(i) Tathmini na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji (a) Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kufuatilia Mwenendo wa Rasilimali za Maji**

**30. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi na za uhakika za rasilimali za maji, Serikali imeendelea kukarabati na kujenga vituo vya kufuatilia rasilimali za maji nchini. Katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, jumla ya vituo **136** vimekarabatiwa na vituo **sita (6)** vimejengwa na hivyo kuwa na jumla ya mtandao wa vituo **1,265** vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji nchini (**Kiambatisho Na. 1**). Mtandao huo unahusisha vituo **184** vya kufuatilia mwenendo wa mvua; vituo **125** vya kufuatilia hali ya hewa; vituo **314** vya kufuatilia mtiririko wa maji katika mito; vituo **18** vya kufuatilia kina cha maji katika maziwa; vituo **15** vya kufuatilia kina cha maji katika mabwawa; vituo **60** vya kufuatilia kiasi cha mashapo (*sediments*) katika mito; vituo **112** vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi; na vituo **437** vya ubora wa maji.

**(b) Ugawaji wa Rasilimali za Maji, Udhibiti wa Matumizi ya Maji na Utatuzi wa Migogoro**

**31. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na mikakati ya kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali za maji na kudhibiti migogoro inayohusu rasilimali za maji. Mikakati hiyo inatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kutoa elimu kuhusu sheria na kanuni za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji pamoja na kutoa vibali vya matumizi ya maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imetoa vibali vipya **1,554** vya matumizi ya maji katika Bodi za Maji za

Mabonde. Hatua hiyo inafanya kuwa na jumla ya vibali **12,312** vya matumizi ya maji vilivyotolewa nchini. Aidha, katika kudhibiti na kutatua migogoro ya matumizi ya maji, jumla ya **migogoro 34** ya matumizi ya maji ilijitokeza ambapo migogoro **17** imetatuliwa na **17** ipo katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi.

**(c) Utoaji wa vibali vya ujenzi na usajili wa mabwawa**

**32. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji inadhibiti shughuli za ujenzi wa mabwawa ya maji na topesumu kwa lengo la kuhakikisha usalama wa miundombinu hiyo. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imetoa jumla ya **vibali 16** vya ujenzi wa mabwawa ya topesumu na kusajili mabwawa 8 ya topesumu. Vilevile, kibali kimoja (1) cha ujenzi wa bwawa la maji kimetolewa na mabwawa 16 ya maji yaliyokidhi vigezo vya usalama wa mabwawa yamefanyiwa usajili. Aidha, usajili wa wataalamu wa mabwawa kwa ajili ya kutekeleza kazi zinazohusiana na usalama wa mabwawa umeendelea kufanyika ambapo wataalamu watatu (3) wamesajiliwa na kufanya jumla ya wataalamu waliosajiliwa kufikia 32.

**(d) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima**

**33. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchimbaji holela wa visima, Wizara imeendelea kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji kwa makampuni yanayokidhi vigezo. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya **leseni 45** za makampuni ya uchimbaji visima; **leseni 45** za wachimbaji na **leseni 15** za utafiti zimehuishwa. Hatua hizo zinapelekea kuwa na jumla ya **leseni 93** za kampuni za uchimbaji; **leseni 106** za wachimbaji; na leseni **20** za taasisi na makampuni ya utafiti wa maji chini ya ardhi. Vilevile, jumla ya vibali **630** vya kuchimba visima vya maji

katika maeneo mbalimbali nchini vimetolewa na kufanya kuwa na jumla ya **vibali 4,519** vya kuchimba visima.

## (e) Kuhifadhi na Kulinda Vyanzo vya Maji

**34. Mheshimiwa Spika**, Mipango ya Uhifadhi na Utunzaji wa Vidakio nchini kwa kipindi cha 2021 hadi 2035 imeandaliwa ili kudhibiti hali ya uharibifu wa vyanzo vya maji. Utekelezaji wa Mipango hii ni mtambuka na unahusisha sekta zote zinazohusiana na maji. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni yale yaliyobainishwa kwenye tathmini ya Vidakio kuwa yako katika hatari ya kuharibiwa na kupunguza uwezo wake wa kutoa maji kwa ubora na wingi. Aidha, Mipango imebainisha maeneo ya kimkakati ambayo ni pamoja na usimamizi na uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo vya maji, uboreshaji wa maisha ya jamii, kuimarisha uwezo wa kitaasisi, kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi, kuimarisha uwezo wa kifedha na ufuatiliaji na uperembaji. Lengo kuu la Mipango hii ni kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji.

**35. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kutambua, kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji kwa lengo la kuhakikisha vinakuwa endelevu kwa matumizi ya sasa na baadaye. Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma endelevu ya maji, Wizara imeendelea kutambua vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuvihifadhi na kuviendeleza. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya vyanzo vipya **785** vya maji juu ya ardhi vimebainishwa katika Bodi za Maji za Mabonde nchini na hivyo kuwa na jumla ya vyanzo vya maji **2,654** vilivyotambuliwa hadi sasa. Aidha, vyanzo vya maji **63** vimewekewa mipaka kama hatua ya awali ya uhifadhi katika maeneo ya Bodi za Maji za Mabonde na hivyo, kuwa na jumla ya vyanzo vya maji **279** vilivyowekewa mipaka. Vilevile, Serikali imetangaza kwenye Gazeti la Serikali vyanzo vya maji **41** na

hivyo, kuwa na jumla ya vyanzo vya maji **59** vilivyotangazwa na kuwa maeneo tengefu.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha jamii inashirikishwa kwenye usimamizi wa rasilimali za maji na kuongeza ufanisi wa usimamizi katika ngazi ya jamii, Wizara imeendelea kuanzisha na kuzijengea uwezo Jumuiya za Watumia Maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Jumuiya 22 za Watumia Maji zimeundwa na hivyo kuwa na jumla ya Jumuiya za Watumia Maji zilizoundwa kufikia 186. Aidha, kamati za vidakio vya maji (Catchment Water Committees) zilizoundwa hadi sasa ni 11.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji vinatunzwa ipasavyo, Mawaziri wenye dhamana ya maji, mazingira, kilimo, nishati, madini, ardhi, TAMISEMI, maliasili pamoja na mifugo na uvuvi walisaini azimio la pamoja mbele ya **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**. Sambamba na tukio la utiaji saini wa azimio hilo, kampeni ya upandaji wa miti rafiki wa maji katika vyanzo vya maji ilizinduliwa ili kuhamasisha wadau, sekta, taasisi na wananchi kushiriki katika zoezi hilo. Kampeni hiyo imelenga kupanda miti 2,500,000 nchini kote katika mwaka 2022/23. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya miti rafiki wa maji **2,541,803** imepandwa katika vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali ya mabonde nchini. Vilevile, kikao cha kwanza cha timu ya uratibu ya kisekta kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa kazi za Mipango ya uhifadhi kimefanyika.

### (e) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

**38. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji nchini, Serikali imeendelea kusimamia sheria na kanuni za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya **vibali 22** vya kutiririsha majitaka vimetolewa. Idadi hiyo inafikisha jumla ya vibali 184 vya

kutiririsha majitaka vilivyotolewa hadi sasa katika mabonde yote.

**(ii) Majukwaa ya Wadau wa Maji**

**39. Mheshimiwa Spika**, ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi wa rasilimali za maji ni muhimu ili kuhakikisha matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imewezesha kufanyika kwa majukwaa **manne** (**4**) ya wadau katika mabonde matatu (3), na majukwaa **mawili** (**2**) ya kitaifa pamoja na majukwaa **mawili** (**2**) ya vikundi kazi kwa ngazi ya kitaifa. Uendeshaji wa majukwaa hayo umeimarisha mwamko wa wadau katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji.

**(iii) Mfumo wa kutabiri mafuriko na kutoa tahadhari za majanga**

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na maandalizi ya mfumo wa utabiri na kutoa taarifa za awali za kutokea kwa majanga kupitia Mradi wa ***Operational Decision Support System (ODSS) through Enhanced Hydro-Meteorological Services***. Mfumo huo wa Kielektroniki unahusisha mifumo ya utoaji wa taarifa za rasilimali za maji (*Water Resources Management Information System*); ugawaji wa maji (*Water Use Permit Analysis Tool*); mfumo wa utabiri wa mafuriko na tahadhari (*Flood Forecasting and Early Warning System*), Utabiri wa misimu ya maji katika vyanzo vya maji (*Seasonal and Flow Prediction Tool*) na kusaidia uendeshaji wa mabwawa ya maji (*Dam Operational Support Tool)*. Hadi Mwezi Aprili 2023, Wizara imetoa mafunzo yanayohusu mfumo huo kwa wataalamu wa Bodi za Maji za Mabonde yote tisa, Idara ya Rasilimali za Maji na Kitengo cha TEHAMA cha Wizara.

### (iv) Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi

**40. Mheshimiwa Spika**, Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za majishirikishi unahusisha nchi washirika ambazo ni Tanzania, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Sudani, Sudani ya Kusini, Ethiopia, Eritrea, Misri, Malawi, Zambia, Msumbiji, Angola, Botswana, Namibia, na Zimbabwe. Ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za majishirikishi unafanyika kupitia Taasisi za Kikanda na Kimataifa pamoja na Mikataba mbalimbali ya makubaliano. Serikali imeendelea kushirikiana na nchi washirika katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi kama ifuatavyo:-

#### a) Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*)

**41. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile ni ushirikiano baina ya nchi 11 za Bonde la Mto Nile ambazo ni Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Uganda pamoja na Eritrea ambayo ni mtazamaji. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkutano wa mwaka wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Mto Nile ulifanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 19 Agosti, 2022 ambapo Tanzania ilipewa uenyekiti wa Baraza hilo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, Taasisi hiyo inatekeleza Mradi wa *Nile Basin Regional Hydromet System* wenye lengo la kuimarisha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa hali ya rasilimali za maji katika vyanzo. Kwa upande wa Tanzania, ujenzi wa vituo **nane (8)** vya kisasa vya kukusanya takwimu za mtiririko wa maji katika mito mikubwa ya Mara, Kagera, Simiyu na Rusumo iliyopo katika Bonde la Ziwa Victoria umekamilika.

**b) Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe**

**42. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki katika kikao cha tatu cha Kamati Tendaji ya Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kilichofanyika Jijini Mbeya – Tanzania kuanzia tarehe 7 - 11 Desemba, 2022. Madhumuni ya kikao hicho ilikuwa ni kujadili na kuielekeza Sekretarieti kuhusu hali ya utekelezaji wa maelekezo ya Mawaziri kuanzia kikao chao cha mwisho kilichofanyika mwezi Machi, 2022 mjini Lilongwe Malawi. Matokeo ya kikao hicho ni pamoja na kukubaliana kuimarisha Ushirikiano na Usimamizi Jumuishi wa Maliasili katika ngazi za Wilaya.

**c) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*)**

**43. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni moja ya nchi wanachama hai wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na imeendelea kushirikiana na nchi wanachama katika kuleta maendeleo katika jumuiya hiyo. Hadi mwezi Aprili, 2023, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa 41 wa Baraza la Mawaziri wa Maji na Nishati wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika Jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) tarehe 31 Oktoba hadi 4 Novemba, 2022. Moja ya matokeo ya Mkutano huo ni utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa usimamizi wa masuala ya maji chini ya ardhi unaotekelezwa kupitia Taasisi ya SADC *Groundwater Management Institute* ambapo kila nchi inapaswa kupatiwa **Dola za Kimarekani 125,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Tanzania imewasilisha andiko la mradi kwa ajili ya kupitiwa na kamati maalumu ya SADC.

**d) Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria**

**45. Mheshimiwa Spika**, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria imeendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali

ikiwemo Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria. Mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kukarabati na kupanua mtandao wa majitaka wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza kupitia Programu hiyo ulisainiwa tarehe 23 Novemba, 2022. Hatua hiyo imewezesha kupatikana fedha za msaada kiasi cha **Shilingi bilioni 12.7** kutoka Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya mtandao wa majitaka Jijini Mwanza ambao utawezesha kuunganisha wateja wapya takriban **1,600**. Hadi mwezi Aprili 2023, Mhandisi Mshauri ameanza kazi ya usanifu wa mradi huo na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2023.

**46. Mheshimiwa Spika**, Aidha, Wizara imeshiriki katika maadhimisho ya **11** ya Siku ya Mara yaliyofanyika tarehe 15 Septemba, 2022 huko Nakuru, Kenya. Lengo la maadhimisho hayo ni kuendeleza ushrikiano wa nchi wanachama na wadau wengine katika uhifadhi wa mto Mara. Kwa upande wa Tanzania, miti zaidi ya **10,000** imepandwa kando ya Mto Mara; na kwenye vyanzo vingine vinavyoleta maji yake katika Mto huo na uwekaji wa vigingi zaidi ya **80** kuonesha mipaka inayosaidia wananchi kuelewa eneo la mita 60 ya hifadhi ya Mto Mara. Vilevile, elimu kwa jamii imeendelea kutolewa ili kuongeza ushiriki wao katika usimamizi wa rasilimali hii muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa nchi zote mbili.

### e) Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Tanzania (*Tanzania Water Investment Programme* 2023 - 2030)

**47. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Sekta nyingine pamoja na Wadau wa Maendeleo inaandaa Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Tanzania *(Tanzania Water Investment Programme 2023*

- *2030)*. Chimbuko la Programu hiyo ni Umoja wa Afrika kupitia Programu ya Maendeleo ya Miundombinu Afrika *(The Programme for Infrastructure Development in Africa - PIDA)* iliyozinduliwa mwaka 2012 ambayo inatekeleza miradi ya miundombinu katika Sekta za Nishati, Uchukuzi, TEHAMA na Maji. Vilevile, Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali Afrika uliofanyika tarehe 7 Februari, 2021 ulipitisha Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Afrika *(Continental Africa Water Investment Programme - AIP)*. Madhumuni ya Programu hiyo ni kutekeleza Lengo Na. 6 la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa 2015-2030 (*Water and Sanitation for All)* na kutekeleza Agenda ya Umoja wa Afrika (*Agenda 2063: The Africa We Want)* kupitia kutafuta Dola za Kimarekani Bilioni 30 kwa mwaka; pamoja na kuongeza ushawishi wa kisiasa unaolenga kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Maji Afrika.

**48. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Tanzania *(Tanzania Water Investment Programme)* ni ya miaka minane (2023 – 2030) ambayo itahusisha miradi ya uwekezaji inayohusiana na maji yenye thamani ya takriban **Dola za Marekani 20,645,469,954.70.** Kupitia Programu hiyo, Serikali itaongeza wigo wa wadau wa maendeleo na kuongeza bajeti ya ndani kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Maji. Tanzania imepata bahati ya kuwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** pamoja na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete** katika wajumbe wa Jopo la Ngazi ya Juu *(AIP International High-Level Panel on Water Investments for Africa)* linalosimamia Maandalizi ya Programu za Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Barani Afrika.

**f) Mradi wa Kuimarisha Teknolojia za Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Takwimu za Haidrolojia**

**49. Mheshimiwa Spika** Ili kuimarisha huduma za kihaidrolojia nchini, Tanzania kupitia Wizara ya Maji, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na nchi ya Gambia zinaandaa mradi wa Kuimarisha Teknolojia za Ufuatiliaji na Ukusanyaji wa Takwimu za Haidrolojia *(Enhancing Hydromet Services through Regional Monitoring Innovation Hubs in Africa)*. Mradi huo wenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 5** utakaotekelezwa katika kipindi cha 2023-2027. Mradi huo unaandaliwa ikiwa ni sehemu ya majaribio katika kanda za mashariki na magharibi mwa Afrika. Aidha, mradi unatarajia kujenga uwezo wa kitaasisi kupitia kuimarisha ubunifu na matumizi ya teknolojia za haidrolojia na hali ya hewa; kuimarisha usimamizi wa majanga yanayosababishwa na maji na hali ya hewa (*disaster risk reduction and early warning systems*) na kuboresha huduma za hali ya haidrolojia na hali ya hewa nchini.

**g) Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**50. Mheshimiwa Spika**: Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji inachangia katika kupanga, kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya jamii hadi taifa. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imeanza kutekeleza mipango kazi iliyoainishwa katika Mipango Shirikishi iliyokamilika katika Mabonde **saba** (**7**) ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Rufiji, Wami-Ruvu na Bonde la Kati. Aidha, maandalizi ya Mipango Shirikishi katika Bonde la Ziwa Victoria yanaendelea ambapo taarifa ya kati (*Final Interim II Reports*) imewasilishwa na Mtaalam Mshauri. Vilevile, kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 inayoelekeza mipango ya Sekta kufanyiwa Tathmini ya

Kimkakati ya Athari za Kimazingira na Kijamii *(Strategic Environmental and Social Assessment – SESA)*, Wizara imekamilisha tathmini hiyo kwa Mipango ya Mabonde **saba** (**7**) iliyokamilika na kuthibitishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais yenye dhamana na mazingira.

**h) Kujenga Uwezo wa Taasisi zinazosimamia Rasilimali za Maji**

**50. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea kuzijengea uwezo Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji kupitia Awamu ya Pili ya Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji. Kupitia mradi huo, Wizara imeanzisha Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji ili kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Maji kwa kufanya tafiti za kina; ugezi (*callibration*) wa vifaa vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji; na kuongeza utaalam wa watumishi wanaoshughulika na ukusanyaji wa takwimu. Hadi mwezi Aprili 2023, ujenzi wa jengo la kituo hicho umefikia **asilimia 60**. Aidha, kazi zilizotekelezwa na Kituo hicho ni pamoja na kujenga uwezo kwa watalaam wa Wizara Makao Makuu na Bodi za Maji za Mabonde katika maeneo ya kufanya tathmini ya rasilimali za maji na kufanya utafiti wa kijiolojia na kijiofizikia ili kupata maeneo yanayofaa kwa ajili ya kuchimba visima kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji.

**4.2.1.2 Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**(i) Utafutaji wa vyanzo vya maji chini ya ardhi**

**51. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kufanya utafiti wa vyanzo vya maji chini ya ardhi kwa lengo la kutatua changamoto ya uhaba wa upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini. Mathalani katika jiji la Dodoma, Wizara ilifanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya **Nzuguni na Ihumwa** katika wilaya ya Dodoma Mjini na maeneo ya Chamwino, **Fufu na Nyabu** katika Wilaya ya **Chamwino** na vijiji

vya **Seluka na Chipogolo** katika Wilaya ya **Mpwapwa.** Katika maeneo ya Nzuguni, Ihumwa na Chamwino imegundulika kuwa na maji ya kutosha chini ya ardhi ambapo uchimbaji wa visima kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma unaendela. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 uchimbaji wa visima vitatu (3) vya utafiti /majaribio unaendelea katika vijiji vya Fufu, Nyabu, Seluka na Chipogolo.

### (ii) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa

#### (a) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Farkwa

**53. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na mpango wa ujenzi wa mabwawa ya kimkakati likiwemo Bwawa la Farkwa (Dodoma) ambapo **Dola za Marekani milioni 125.3** zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*Africa Development Bank – AfDB*) kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na mtambo wa kusafisha na kutibu maji ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 128,000 kwa siku. Ujenzi wa Bwawa la Farkwa ni mpango wa muda wa kati wa kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma ambao umeongezeka kwa kasi. Hadi mwezi Aprili 2023, Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa bwawa. Aidha, taratibu za kuwapata wataalam washauri watakaofanya mapitio ya usanifu na usimamizi wa ujenzi wa bwawa na chujio; kufanya tathmini ya usalama wa bwawa na utunzaji wa mazingira zinaendelea.

#### (b) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

**54. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu **Shilingi bilioni 329.47**. Mradi huo ni wa kimkakati wenye lengo la kuhakikisha maji yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam

na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ili kukabiliana na changamoto ya ukame ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara na kusababisha upungufu mkubwa wa maji. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji lenye mita za ujazo milioni 190; ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa megawati 20; ujenzi wa njia ya msongo mkubwa wa umeme kutoka Kidunda hadi Chalinze umbali wa kilomita 101; na ujenzi wa barabara ya kiwango cha changarawe yenye urefu wa kilomita 75 kutoka Ngerengere hadi Kidunda. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkandarasi wa ujenzi na Mtaalam Mshauri atakayesimamia ujenzi wa bwawa wamepatikana na Shilingi **bilioni 49.4** ambazo ni fedha za ndani zimetolewa ikiwa ni malipo ya awali ili kuanza ujenzi wa Bwawa hilo.

**(c) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa ya Ukubwa wa Kati na Madogo**

**55. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo katika maeneo mbalimbali nchini hususan katika maeneo kame ili kuondokana na adha ya upungufu wa maji kwa wananchi na mifugo wakati wa kiangazi. Hadi mwezi Aprili 2023, ujenzi wa mabwawa **10** ya ukubwa wa kati ya Paranga, Kambi ya Nyasa, Kelema Kuu, na Haneti yaliyopo Wilaya ya Chemba; Masaka (Iringa); Mtamba (Mpwapwa); Manda (Chamwino); Zebeya (Maswa); Itamboleo (Mbarali) na Bwawa la Muko (Momba) umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mabwawa 27 katika maeneo mbalimbali unaendelea.

### 4.2.2 Huduma za Ubora wa Maji

**56. Mheshimiwa Spika,** huduma za ubora wa maji zinatolewa na Wizara kupitia Maabara 17 za Ubora wa Maji zilizopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Kigoma, Singida, Dodoma, Manyara,

Arusha, Kagera, Mara, Shinyanga na Mwanza. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ilipanga kuimarisha uhakiki na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji 2091, Skimu 4,600 za usambazaji maji mjini na vijijini na mifumo ya uchakataji majitaka 150 kwa kukusanya na kuchunguza sampuli 15,000 za maji na sampuli 2,000 za majitaka; kutoa elimu kuhusu viwango vya ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali; kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji kabla ya manunuzi na wakati wa matumizi; kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji inayohimili mabadiliko ya tabianchi kwa Mamlaka za Maji 34 na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamiii 100; na kuendelea kuimarisha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi, pamoja na kuziwezesha maabara nne (4) kupata ithibati.

**(i) Ubora wa Maji katika Vyanzo**

**57. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na usimamizi wa ubora wa maji kwa kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji kwa ajili ya afya ya ikolojia. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya vyanzo vya maji **1,473** ambavyo ni mito (**240**), Visima (**962**), Maziwa (**27**), Chemichemi (**223**) na mabwawa (**20**) vilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha hali ya ubora wa maji katika vyanzo hivyo inaridhisha na inaendelea kulinda afya ya ikolojia pamoja na uwepo wa changamoto ya uchafuzi wa vyanzo vya maji; madini ya *Fluoride*; Chumvichumvi; Chuma na Manganese katika baadhi ya vyanzo hivyo.

**(ii) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika kutimiza azma ya Serikali ya kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika mifumo ya usambazaji maji mijini na vijijini kwa lengo la kuhakikisha maji

yanayosambazwa kwa jamii yanakidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji ya kunywa. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya **skimu 1,987** za maji vijijini; **skimu 166** za maji mijini; pamoja na vyanzo vya maji **245** vinavyomilikiwa na taasisi na watu binafsi vilifanyiwa uhakiki na ufuatiliaji ambapo jumla ya sampuli za maji **4,461** zimekusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yameonesha kuwa sampuli **3,190** sawa na **asilimia 71.5** zilikidhi viwango na sampuli **1,271** sawa na asilimia **28.5** hazikukidhi viwango vya kitaifa vya ubora wa maji ya kunywa. Aidha, baadhi ya sampuli hazikukidhi viwango vya ubora wa maji kutokana na kuwa na viwango vikubwa vya madini ya Chuma, *Manganese* na Chumvichumvi katika mikoa ya Mtwara na Lindi; pamoja na kiwango kikubwa cha madini ya *Fluoride* katika mikoa ya Arusha, Manyara na Singida. Katika kukabiliana na changamoto hizo, ushauri wa kitaalam ikiwa ni pamoja na kusafisha na kutibu maji ulitolewa kwa wasambazaji wa maji mijini na vijijini.

**59. Mheshimiwa Spika** katika kuhakikisha maji yanayomfikia mtumiaji yanaendelea kuwa safi na salama, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira; na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhusu matumizi ya miongozo mbalimbali ya usimamizi wa ubora wa maji. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Usalama wa Maji Inayohimili Mabadiliko ya Tabianchi; Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Maji ya Kunywa na Uandaaji wa Taarifa; na Mwongozo wa Kitaifa wa Kusafisha na Kutibu Maji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeiwezesha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro kuandaa mpango wa usalama wa maji unaohimili mabadiliko ya tabianchi hivyo kufikisha jumla ya Mamlaka **nane** (**8**) zenye Mipango ya Usalama wa Maji. Vilevile Wizara imetoa mafunzo ya ufuatiliaji wa ubora wa maji kwa Mameneja **108** wa RUWASA katika

ngazi za Mikoa na Wilaya pamoja na wataalam **sita** (**6)** wa Maabara za Ubora wa Maji.

**(iii) Ubora wa Maji kwa Matumizi Mengine**

**60. Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi unahitaji maji yanayokidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi husika. Katika kuhakikisha maji hayo yanakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayotumika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya sampuli **444** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake ambapo sampuli **212** ni kwa ajili ya matumizi ya viwandani, ujenzi **(60)**, umwagiliaji **(23)** na sampuli **149** kwa ajili ya shughuli za utafiti. Matokeo yalionesha sampuli **418** zilikidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa isipokuwa sampuli **12** za maji kwa ajili ya matumizi ya viwandani, ujenzi **10** na umwagiliaji sampuli **4** hazikukidhi viwango vya ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**(iv) Uhakiki wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji**

**61. Mheshimiwa Spika**, Serikali ina jukumu la kuhakikisha madawa yanayotumika katika kusafisha na kutibu maji yanakidhi viwango vya ubora na yanakuwa na ufanisi katika kusafisha na kutibu maji. Katika kutimiza jukumu hilo, hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imehakiki ubora wa madawa ya kusafisha maji aina ya *Aluminium Sulphate*. Matokeo ya uchunguzi yalionesha madawa hayo yanakidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji. Aidha, katika kuhakikisha madawa yanawekwa kwenye maji kwa ufasaha, Serikali imehakiki ufanisi wa mitambo rahisi **338** ya kutibu maji katika skimu za maji vijijini na mitambo **29** ya kusafisha na kutibu maji katika skimu za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Vilevile, Serikali imefunga jumla ya mitambo

ya kutibu maji **11** katika skimu za maji vijijini na kuboresha mifumo ya uwekaji dawa za kutibu maji katika skimu **25** za maji vijijini katika Wilaya za Kakonko, Buhigwe Mufindi, Chunya na Njombe .

### (v) Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira

**62. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa ubora wa majitaka kutoka majumbani, viwandani na katika taasisi mbalimbali ni muhimu katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla. Katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira ambapo hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya **sampuli 475** zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi kutoka kwenye mifumo **10** ya kusafisha majitaka ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na mifumo **57** ya kusafisha majitaka ya viwanda na taasisi. Matokeo yalionesha **asilimia 49** ya sampuli zilikidhi viwango vya ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Aidha, Mamlaka za Maji, viwanda pamoja na taasisi ambazo majitaka yake hayakukidhi viwango, ushauri wa kitaalam ulitolewa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kusafisha majitaka.

### (vi) Uimarishaji wa Maabara za Maji

**63. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha huduma za ubora wa maji nchini kwa kuzijengea uwezo maabara za ubora wa maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imeziwezesha maabara saba (7) za ubora wa maji (Dar es Salaam, Singida, Shinyanga, Mwanza, Musoma, Kigoma na Bukoba) kudumisha hadhi ya ithibati baada ya kufanyiwa ukaguzi na Bodi ya SADCAS. Hadhi hiyo, inadhihirisha kuwa matokeo yanayotolewa na maabara hizo yanakubalika kimataifa. Aidha, Wizara ipo katika hatua za awali za kuziwezesha maabara za Mbeya, Morogoro, Mtwara, Iringa na

Sumbawanga kupata ithibati. Vilevile, Wizara imeendelea kuongeza wigo wa uchunguzi wa viashiria vya ubora wa maji; madawa ya kusafisha na kutibu maji; pamoja na majitaka kwa kuzipatia maabara vitendea kazi vya kisasa.

**64. Mheshimiwa Spika**, kuhakiki ubora wa maji kabla ya kuyatumia ni jambo la msingi katika shughuli za kiuchumi na kulinda afya ya jamii. Nitumie fursa hii, kutoa wito kwa wadau wote kuhakiki ubora wa maji kabla ya kuyatumia katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, viwanda na taasisi nyingine zenye shughuli zinazozalisha majitaka zihakikishe maji hayo yanasafishwa na kufikia viwango vinavyokubalika kabla ya kurudishwa kwenye mazingira ili kulinda afya ya ikolojia.

### 4.2.3 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

**65. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini, katika mwaka 2022/23 Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,029** katika maeneo ya vijijini. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa miradi **586 (Kiambatisho Na. 2)** katika vijiji **1,293** vyenye jumla ya vituo **5,748** umekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi wapatao **4,086,442.** Vilevile, utekelezaji wa miradi mingine unaendelea na upo katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa 13 ya kuvuna maji ya mvua.

**66. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa shughuli zinahusu huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini ni kama ifuatavyo:-

### 4.2.3.1 Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya Maji Vijijini

#### (i) Mradi wa Maji wa Kagongwa – Isaka kwenda katika Vijiji vya Mwalugulu, Kilimbu, Jana, Butondolo na Itogwanholo

**67. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji katika vijiji vya Mwalugulu, Kilimbu, Jana, Butondolo na Itogwanholo katika Wilaya ya Kahama kwa kutumia maji kutoka bomba kuu la mradi wa IsakaKagongwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 4.256**. Mradi huo unahusisha ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 18.4, ujenzi wa matanki matatu (3) yenye jumla ya mita za ujazo 470, ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 36.2 na ujenzi wa vituo 31 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa **asilimia 50** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha wananchi wapatao 28,699 wa vijiji hivyo.

#### (ii) Mradi wa Maji Ziba – Nkinga

**67. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa maji Ziba – Nkinga katika Wilaya ya Igunga kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.349.** Mradi huo utahudumia vijiji **tisa (9)** vya Ndembezi, Itulashilanga, Mwanzelwa, Nkinga, Ikunguipina, Njiapanda, Ulaya, Barazani na Kitangiri. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ununuzi na ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 21.4; ujenzi wa ofisi ya CBWSO kwa ajili ya uendeshaji wa mradi; na ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 85** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023 na kuwanufaisha wananchi wapatao 29,780.

### (iii) Mradi wa Maji Ruangwa - Nachingwea

**69. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa Mradi wa maji wa Ruangwa - Nachingwea kwa gharama ya **Shilingi bilioni 119.6**. Mradi huo mkubwa utatumia chanzo cha mto Nyangao kupeleka maji kwenye jumla ya vijiji 56 ambapo vijiji 34 vipo Wilaya ya Ruangwa, vijiji 21 vya Wilaya ya Nachingwea na kijiji kimoja (1) kipo Wilaya ya Lindi. Mradi huo unahusisha ujenzi wa banio; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa tanki la kukusanyia maji (*Sump well*); ujenzi wa matanki matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 4.675; ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 85; ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 105; ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi; ujenzi wa ofisi tatu (3) za CBWSO kwa ajili ya uendeshaji wa mradi; ununuzi wa magari mawili (2) na pikipiki 10; na ujenzi wa vituo 70 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Wakandarasi wamekabidhiwa eneo la mradi na wanaendelea na maandalizi ya vifaa na wataalam kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi. Mradi huo unatarajia kunufaisha wananchi wapatao 128,657 wa vijiji hivyo.

### (iv) Mradi wa Maji Mkinga - Horohoro

**70. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mkinga – Horohoro unaotoa maji kutoka bomba kuu linalopeleka maji katika Jiji la Tanga kwa gharama ya **Shilingi bilioni 35.5**. Mradi utahudumia jumla wananchi wapatao 74,795 wa vijiji 37 vya Wilaya ya Mkinga pamoja na mji wa Horohoro. Mradi huo unahusisha ujenzi wa matanki nane (8) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 1.29; ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 95; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 101; ujenzi wa ofisi ya CBWSO kwa ajili ya kuendesha mradi; na ujenzi wa vituo

60 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 10**.

**(v) Mradi wa Maji Morunganya – Morogoro Vijijini**

**71. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Morunganya uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa gharama ya Shilingi **bilioni 23**. Mradi huo utahudumia vijiji 19 vya Kalundwa, Kibwaya, Tandai, Mkuyuni, Madamu, Luholela, Mwarazi, Kivuma, Kungwe, Kikundi, Lukonde, Vuleni, Lubungo, Muhunga-Mkola, Newland, Kibuko, Maseyu, Kinonko na Gwata. Mradi huo unahusisha ujenzi wa banio la maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 117; ujenzi wa wa Ofisi ya CBWSO kwa ajili ya uendeshaji wa mradi; ujenzi wa matanki 12 yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 1.84; na ujenzi wa vituo 100 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 55** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha wananchi wapatao 52,000 kupata huduma ya maji safi na salama.

**(vi) Mradi wa Maji Ukiliguru, Sumve hadi Koromije**

**72. Mheshimiwa spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kimkakati wa Ukiliguru, Sumve hadi Koromije ambao unatoa maji Ziwa Victoria kuhudumia miji ya Usagara, Ukiliguru, Sumve na Koromije na vijiji 19 kwa gharama ya S**hilingi bilioni 38.4**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa choteo la maji; ujenzi wa matanki sita (6) yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 5.625; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa nyumba moja (1) ya watumishi na ofisi mbili (2) za CBWSO kwa ajili ya uendeshaji wa mradi; ununuzi na ufungaji wa pampu; ujenzi wa jengo la pampu; ulazaji wa bomba kuu

umbali wa kilomita 39.3; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 221.8; na ujenzi wa vituo 80 vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkandarasi amekabidhiwa eneo la mradi na anaendelea na maandalizi ya vifaa na wataalam kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao 162,377.

### 4.2.3.2 Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

**73. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Program - SRWSP*) yenye lengo la kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwenye Halmashauri za wilaya 86 katika mikoa 17 nchini na pia kujenga uwezo kwa taasisi zinazosimamia utoaji wa huduma ya maji vijijini ili kufanya huduma hiyo kuwa endelevu.

**74. Mheshimiwa Spika,** Programu hiyo ilitengewa jumla ya **Dola za Marekani milioni 350** (sawa na takribani **Shilingi bilioni 822.5**) na ilipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/20 - 2024/25. Programu hiyo inatekelezwa kwa utaratibu wa Malipo kwa Matokeo (*Program for Results – PforR*) iliyotengewa jumla ya **Dola za Marekani Milioni 330** (sawa na takribani **Shilingi bilioni 775.5)** na utaratibu wa *Mipango Wezeshi ya Programu - Investment Project Financing - IPF*) kwa **Dola za Marekani Milioni 20 (**sawa na takribani **Shilingi bilioni 47).** Programu hiyo ililenga kuongeza idadi ya wananchi wapatao **3,000,000** waishio vijijini kupata huduma ya majisafi, salama na toshelevu.

**75. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita, kuanzia mwezi Machi 2021 hadi

mwezi Machi 2023, Serikali ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **571** ya maji vijijini ambapo katika kipindi hicho, imefanikiwa kutekeleza miradi **399** yenye jumla ya vituo **7,107** vya kuchotea maji na kunufaisha wananchi wapatao **4,755,035** waishio vijijini katika vijiji **2,487**. Utekelezaji huo umewezesha Serikali kuvuka lengo la Programu hiyo la kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma kufikia zaidi ya milioni 3 ndani ya miaka mitatu ya utekelezaji wa Programu. Matokeo hayo yamewezesha kuongezeka kwa fedha kutoka **Shilingi bilioni 119** mwaka 2020/21 hadi kufikia **Shilingi bilioni 385** mwaka 2022/23.

**76. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hiyo kwa ufanisi, umesababisha Benki ya Dunia kuongeza muda pamoja na fedha za utekelezaji wa Programu kutoka **Dola za Marekani Milioni 350** hadi kufikia **Dola za Marekani Milioni 654.9.** Vilevile, idadi ya mikoa inayopata fedha za PforR imeongezeka kutoka mikoa **17** hadi **25** na Halmashauri za wilaya zinazoshiriki katika utekelezaji wa Programu imeongezeka kutoka **86** mwaka 2019/20 hadi kufikia **137** katika mwaka 2023/24.

**77. Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuongezeka kwa halmashauri za wilaya zinazoshiriki katika utekelezaji wa Programu hiyo na pia kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa Programu, kutaongeza kasi ya kufikia malengo ya Ilani ya CCM ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi waishio vijijini kwa zaidi ya **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025.

#### 4.2.3.3 Mradi wa Matumizi ya Dira za Maji za Malipo ya Kabla

**78. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufanisi wa matumizi ya maji na ukusanyaji wa maduhuli, RUWASA kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilisaini mikataba tarehe 21 Juni 2022 na **Chuo cha Ufundi Arusha** (ATC), **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya** (MUST) na **Dar es Salaam Teknohama Business Incubator** (DTBi) kwa ajili ya

kubuni, kutengeneza na kufunga dira za maji za malipo kabla ya matumizi kwenye skimu za maji vijijini. Mradi huo umelenga kubuni, kutengeneza na kufunga dira 300 za majaribio. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya dira **150** zimetengenezwa na dira **69** zimefungwa katika skimu mbalimbali za maji. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023.

### 4.2.3.4 Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*)

**79. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Benki ya Uwekezaji Tanzania (*TIB*) inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa kupunguza gharama za uendeshaji kwa kubadilisha mitambo ya dizeli kwenda mitambo inayotumia nishati ya jua. Gharama za mradi ni takriban **Shilingi bilioni 19.85** ambapo utekelezaji wake umeanza katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mtwara na Tabora. Lengo la mradi huo ni kutatua changamoto za gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini hususan miradi inayotumia nishati ya mafuta ya dizeli ambayo ni ghali. Hadi mwezi Aprili 2023, ufungaji wa mitambo ya kufua umeme wa jua umekamilika katika skimu **62** kati ya 74 ziliyopangwa katika mikoa ya Dodoma na Singida; kujenga vituo vya maji **369** kati ya 597 vilivyopangwa pamoja na kufunga dira za malipo ya kabla *(pre-paid water meter)* katika vituo hivyo.

### 4.2.3.5 Uimarishaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii

**80. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali ilipanga kuunda na kusajili Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply Organizations - CBWSOs*) 704 na kuzijengea uwezo zilizopo ili kuimarisha uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Hadi mwezi Aprili 2023, CBWSOs **111** zimeundwa na kusajiliwa na hivyo kuwa na jumla

ya CBWSO 2,543 zilizosajiliwa. Pia, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo CBWSOs **125** kwa kutoa mafunzo maalum (*tailor-made training*) kuhusu utunzaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji vijijini; kununua vitendea kazi; na kujenga majengo ya ofisi. Vilevile, CBWSOs zimeajiri wataalam wapatao 5,296 ambapo Mafundi Sanifu ni 1,837, Wasaidizi wa Hesabu 1,529 na Wasaidizi wa Ofisi 1,930. Kuwepo kwa wataalam hao kumewezesha shughuli za kiufundi kufanywa kwa weledi zaidi ikilinganishwa na hapo awali na hii imesaidia kuwa na huduma endelevu.

### 4.2.4 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**81. Mheshimiwa Spika**, lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira inawafikia zaidi ya asilimia 95 ya wakazi wote wa maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025. Katika kutimiza lengo hilo, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka katika maeneo ya mijini ikiwa ni pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini. Katika mwaka 2022/23, jumla ya miradi **175** ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2023, miradi **40** imekamilika (**Kiambatisho Na. 3)** na miradi **135** inaendelea na ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, na Miradi ya Kitaifa ni kama ifuatavyo:-

#### 4.2.4.1 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa

### (i) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya

**82. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza utekelezaji wa Mradi wa kutoa maji katika chanzo cha Mto Kiwira kupeleka katika Jiji la Mbeya kwa gharama ya **Shilingi bilioni 117**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa banio katika chanzo cha Mto Kiwira litakaloweza kuchukua kiasi cha lita milioni 117 kwa siku; ulazaji wa bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi Sisitila umbali wa kilometa 26.3; ujenzi wa miudombinu ya kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ukubwa wa lita milioni 5; ulazaji wa bomba kuu la mserereko kutoka kwenye chujio la maji hadi Mwashaali umbali wa kilomita 22.5; ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 11 kutoka Sisitila hadi eneo la *New Forest*; kujenga matoleo ya bomba kutoka kwenye bomba kuu yatakayohudumia wananchi wa vijiji 4 vya Isongole, Swaya Juu, Magao na Iyela ambavyo vitapitiwa na bomba kuu; kuunganisha mfumo wa usambazaji maji wa mradi mpya wa Mto Kiwira na uliopo; na kufanya tathmini ya athari za kijamii na kimazingira. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi amepatikana na maandalizi ya vifaa na wataalam kwa ajili ya kuanza ujenzi yanaendelea. Kukamilika kwa mradi kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 hadi lita milioni 184; na kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95. Vilevile, mradi unatarajiwa kuwanufaisha wananchi wapatao **1,452,751**.

### (ii) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha

**83. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu takribani **Shilingi bilioni 520**. Hadi mwezi Aprili

2023, kazi zilizokamilika ni pamoja na uchimbaji wa visima **41**; ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya kutibu majitaka; upanuzi na ukarabati wa miundombinu na mifumo ya majisafi na majitaka maeneo ya katikati ya Jiji; ujenzi wa vyoo **42** vya mfano vyenye jumla ya matundu **184**; ujenzi wa mtandao mpya wa majitaka umbali wa kilomita **180.503**; ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji; ujenzi wa ofisi tatu (**3**) za kanda, Karakana na Bohari katika eneo la Safari *City*; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa ofisi kuu; na upanuzi wa mtandao wa majitaka nje ya maeneo ya katikati ya Jiji.

**84. Mheshimiwa Spika**, kazi zinazoendelea ni pamoja na upanuzi wa mtandao wa majisafi; uchimbaji wa visima 15; ufungaji wa mfumo wa mawasiliano; ujenzi wa matanki; na ujenzi wa mfumo wa kuchanganya maji (*blending*). Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 92.67** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023. Mradi unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 40** hadi lita **milioni 200** kwa siku; muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka saa 12 za sasa hadi saa 24 kwa siku; huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**; kupunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 48** hadi **asilimia 25**; na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kufikia **asilimia 100.**

### (iii) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani

**85. Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na:-

### a) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi

**86. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani. Mradi huo umezinduliwa na **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa** tarehe 16 Machi, 2023 na umegharimu **Dola za Marekani milioni 86**. Kazi zilizotekelezwa zimehusisha ujenzi wa matanki **matatu (3)** ya kuhifadhi maji yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita **milioni tano (5)** kila moja katika maeneo ya Tegeta, Mbweni na Vikawe; ujenzi wa matanki **mawili (2)** ya kupunguza mgandamizo wa maji yenye uwezo wa lita **540,000** kila moja; ujenzi wa vituo viwili **(2)** vya kusukuma maji katika maeneo ya Wazo na Mapinga; uunganishaji wa wateja wapya **37,142**; ununuzi wa dira za maji **50,000**; na upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita **1,252**. Aidha, Wizara yangu itaendelea na upanuzi wa mradi huo ili kuwafikia wananchi walio karibu na eneo la mradi.

### b) Mradi wa Maji wa Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera

**87. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji na Mpera. Hadi mwezi Aprili 2023, kazi zilizokamilika ni ujenzi wa tanki la **lita milioni 15** katika eneo la Kisarawe II; kituo cha kusukuma maji katika eneo la Kimbiji; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 6.9** kutoka Kibada hadi Maweni kwa Mwingira; ulazaji wa bomba la kusafirisha maji umbali wa **kilomita 8** kutoka Kibada kupitia Daraja la Nyerere hadi bomba la kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam; ulazaji wa bomba umbali wa **kilomita 6.3** kutoka kwenye visima kupeleka maji kwenye tanki; na ulazaji wa bomba umbali wa **kilomita**

**15.8** kutoka kwenye visima hadi kwenye kituo cha kusukuma maji. Kazi inayoendelea ni ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 95**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023 na utawahudumia wakazi **250,000** wa Chanika, Luzando, Mpera, Chamazi, Kitunda, Kinyerezi, Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Keko na Chang'ombe.

**(iv) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mwanza**

**88. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development AgencyAFD*) imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa chujio la Butimba kwa gharama ya **Euro 26,165,102**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo kipya cha majisafi; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji; ununuzi na ufungaji wa pampu. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 71**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023 na utawanufaisha wakazi wapatao **105,649**.

**(v) Ukamilishaji wa Mradi wa Majisafi katika Manispaa ya Kigoma**

**89. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo KfW imetekeleza mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma na wananchi wanapata huduma ya maji. Hadi mwezi Aprili 2023 ujenzi wa choteo jipya uliogharimu **Euro milioni 3.61** umekamilika**.** Kukamilika kwa mradi huo, kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9.5** kwa siku hadi **lita milioni 42** kwa siku na kuwanufaisha wakazi **384,500** wa Manispaa ya Kigoma.

**(vi) Mradi wa Upanuzi wa Huduma kupitia mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi**

**90. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji maji kutoka Mjini Lindi hadi Mchinga kwa gharama ya Shilingi 12,419,342,808.31. Mradi huo unahusisha uchimbaji wa visima vitatu (3); ujenzi wa tanki la lita 680,000; ujenzi wa uzio kuzunguka tanki; ujenzi wa jengo la mlinzi; ujenzi wa vioski 20; ulazaji wa mabomba katika njia kuu umbali wa kilomita 30; ufungaji wa pampu mbili (2); na ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 80. Hadi mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 71. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2023 na utawanufaisha wananchi wapatao 40,000.

**(vii) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Manispaa ya Morogoro na Maeneo ya Pembezoni**

**90. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency* - AFD) inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Morogoro kwa gharama ya **Euro milioni 84**. Mradi unahusisha kuongeza kimo cha tuta la Bwawa la Mindu kwa mita 2.5; ujenzi wa mtambo mpya wa kusafisha na kutibu maji wa Mafiga wenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 54 kwa siku; ujenzi wa matanki ya maji; ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji kwa umbali wa kilomita 30; ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majitaka wa Mafisa; na ujenzi wa jengo jipya la ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro. Hadi mwezi Aprili 2023 kazi zilizotekelezwa ni uandaaji wa Mpango Kabambe wa Rasilimali za Maji *(Water Resource Master Plan)* katika Manispaa ya Morogoro; tathmini ya kimazingira na kijamii; ubainishaji wa mpaka mpya wa bwawa utakaotokana na kuongeza kimo

cha tuta; ununuzi wa wakandarasi wa ujenzi na mtaalam mshauri wa usimamizi wa ujenzi; na uhakiki wa makazi yaliyopo kwenye mpaka wa awali kwa ajili ya fidia. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2026 na utawanufaisha wakazi wapatao 722,010 wa Manispaa ya Morogoro.

**(viii) Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji wa Babati**

**92. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Dareda-Singu-Sigino-Bagara kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.77**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa matanki matano (5) ya kuhifadhi maji yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 4.1; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 63.31; ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 26.83; ujenzi wa vituo viwili (2) vya kusukuma maji; ununuzi na ufungaji wa pampu mbili (2) za kusukuma maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; na ujenzi wa chanzo. Hadi mwezi Aprili 2023, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki matatu (3) ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita milioni 2.45; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji umbali wa kilomita 10; na ujenzi wa chanzo ambapo utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 85.** Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023 na utawanufaisha wananchi wapatao 60,000.

**(ix) Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma**

**93. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa kutekeleza mradi wa maji Nzuguni kwa gharama ya Shilingi bilioni 5. Mradi huo unahusisha uchimbaji wa visima vitano (5) vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita **million 7.6** kwa siku; ujenzi wa matanki mawili (2) yenye ukubwa wa lita milioni 3.5; ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza

maji umbali wa kilomita 7; kujenga jengo la pampu; na kufunga Pampu ya kusukuma maji. Hadi mwezi Aprili 2023, uchimbaji wa visima vitano (5) umekamilika na utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 10**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2023 na utawanufaisha wakazi wapatao 37,000 wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa. Kukamilika kwa mradi kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka wastani wa lita milioni 68.7 kwa siku hadi lita milioni 76.3 kwa siku. Vilevile, Serikali imeanza mradi wa maji Bihawana ambao utahusisha uchimbaji wa visima 23, ulazaji wa bomba kuu la kupandishia maji, ujenzi wa matanki, ulazaji wa mabomba ya kusambazia maji na ujenzi wa vichoteo vya maji.

**94. Mheshimiwa Spika,** aidha, katika mpango wa muda wa kati na muda mrefu, Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika kwa ajili ya Jiji la Dodoma ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Farkwa na kuangalia uwezekano wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Dodoma.

**(x) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa VwawaTunduma**

**95. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) imeanza kutekeleza Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Vwawa na Tunduma. Katika hatua za awali, upembuzi yakinifu utafanyika katika Miji ya Vwawa na Tunduma kwa gharama ya **Euro 892,500.00**. Hadi mwezi Aprili 2023, taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri atakayefanya kazi hiyo zinaendelea. Katika mpango wa muda mfupi wa kutatua changamoto ya maji katika miji ya Vwawa na Tunduma, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi wa maji wa kutoa maji katika chanzo cha Mto Momba kupeleka katika miji ya Tunduma na Vwawa baada ya kubaini kuwa maji ya mto Bupigi hayatoshelezi mahitaji ya miji hiyo.

### (xi) Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Shinyanga na Maeneo ya Pembezoni

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(French Development Agency-AFD)* imeanza utekelezaji wa mradi wa usambazaji majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Shinyanga kwa gharama ya **Euro milioni 70**. Hadi mwezi Aprili 2023, upembuzi yakinifu wa mradi huo umekamilika na Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina. Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi na Mkandarasi atakayetekeleza ujenzi wa mradi. Mradi utaimarisha huduma ya majisafi kutoka asilimia 58 hadi asilimia 95, na huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 0.5 hadi asilimia 33.

### (xii) Kuboresha Huduma ya Maji katika Manispaa ya Mtwara na Maeneo ya Pembezoni

**97. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chujio la maji katika eneo la Mangamba kwa gharama ya **Shilingi 3,451,853,994**. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki la maji ya huduma ya zimamoto, ununuzi na ufungaji wa mabomba na viungio; ujenzi wa jengo la pampu; ufungaji wa pampu; ukarabati wa karakana; na ujenzi wa mifumo ya usalama ya umeme. Hadi Mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 96**. Kukamilika kwa mradi huo, kutawezesha wakazi wa Mji wa Mtwara kupata huduma ya maji yaliyosafishwa na kutibiwa kwa viwango vinavyokubalika.

**98. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha mfumo wa maji Mtwara Mjini awamu ya kwanza na ya pili kwa jumla ya gharama ya **Shilingi 20,361,599,950**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi matanki

matatu (3) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 7.5; ukarabati wa njia kuu ya kusafirisha maji; na ukarabati njia kuu ya kusambaza maji. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji kwa awamu ya kwanza umefikia **asilimia 60** na awamu ya pili umefikia **asilimia 5**.

**4.2.4.2 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

**(i) Miji ya Tinde na Shelui**

**99. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India kwa gharama ya **Shilingi bilioni 24.75**. Hadi mwezi Aprili 2023, awamu ya kwanza ya mradi imekamilika ambapo kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa matanki **matatu (3)** yenye jumla ya ujazo wa **lita 700,000** ambayo yamejengwa Shelui na tanki la **lita milioni 1.15** ambalo limejengwa Tinde; ukarabati wa matanki **mawili (2)** katika eneo la Shelui; na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji. Vilevile, Wizara inaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi ambayo inahusisha ulazaji wa mabomba kwenye mtandao wa kusambaza maji umbali wa kilomita 8.4 katika Mji wa Tinde. Hadi mwezi Aprili 2023, ununuzi wa bomba umekamilika na utekelezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023. Mradi unatarajiwa kuwanufaisha wananchi **86,983** wa miji ya Shelui na Tinde.

**(ii) Maeneo yanayohudumiwa na Mradi wa Kitaifa wa HTM**

**100. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji Segera-Kabuku wenye gharama ya **Shilingi 25,585,976,283.13.** Mradi huo ni wa kimkakati wenye lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wa vijiji 15 vya Kwamgwe, Chanika Kofi, Seza Kofi, Bondo, Kwadoya, Ngojoro, Kwedizinga, Ugweno, Taula, Kwedibago, Kabuku Nje, Kabuku Mjini,

Komsanga, Kabuku Kaskazini na Kabuku Ndani pamoja na Kambi ya Jeshi Mgambo-Kabuku wanapata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huu ni kama ifuatavyo; ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji wenye uwezo wa lita milioni 6.27 kwa siku; ujenzi wa jengo la mitambo na jengo la maabara; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita milioni 2; na ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 106. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkandarasi amekabidhiwa eneo la mradi na maandalizi ya vifaa na wataalam kwa ajili ya kuanza ujenzi yanaendelea. Mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha wananchi wapatao **120,055**.

**(iii) Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari - Butiama**

**101. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia *(Saudi Fund for Development – SFD)* inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji utakaohudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa choteo la maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa tanki kubwa la maji safi eneo la Mugango pamoja na mantaki **matano** (**5**) katika maeneo ya Kong, Kiabakari, Butiama Hill na Bumangi; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama umbali wa **kilomita 48**; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa **kilomita 140**; ujenzi wa ofisi na nyumba za wasimamizi wa mitambo; ukarabati wa matanki **mawili** (**2**) katika maeneo ya Kyatungwe na Bisarye; ujenzi wa vioski **40** vya maji na ununuzi wa dira za maji **2,000**. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 79** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023. Mradi huo utawanufaisha zaidi ya wakazi **100,000**

waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka bomba kuu.

**(iv) Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

**102. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na BADEA, OFID na Kuwait Fund inaendelea kutekeleza mradi wa maji Same-Mwanga-Korogwe ambao umelenga kusambaza maji katika Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji **38** kwenye Wilaya za Same na Mwanga na vijiji vitano **(5)** katika Wilaya ya Korogwe. Hadi mwezi Aprili 2023, kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kuzalisha maji, choteo la maji; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 81.7**, ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; na ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji. Vilevile, ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa **kilomita 105** katika Mji wa Mwanga umefikia **asilimia 97**; na ujenzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 102 katika Mji wa Same umefikia **asilimia 99.2**. Aidha, kwa upande wa kipande kutoka kwenye chanzo hadi Kisangara kilichokuwa na changamoto ya Mkandarasi, majadiliano baina ya Wizara na Mkandarasi yamefanyika na kufikia muafaka wa Mkandarasi kurejea eneo la mradi kukamilisha kazi zilizobaki. Hatua hiyo imefikiwa baada ya pande zote kusaini Mkataba wa Makubaliano tarehe 13, Machi 2023. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2024.

**(v) Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Sengerema**

**103. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa maji Nyasigu – Lubungo – Ngoma kwa gharama ya **Shilingi 13,742,895,491.14**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa jengo la mtambo wa kusukuma maji; ufungaji wa pampu; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji wenye uwezo lita milioni

12 kwa siku; ujenzi wa matanki matatu (3) yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 2.6; ulazaji wa mabomba ya mtandao umbali wa kilomita 108.4; ujenzi wa vituo 70 vya kuchotea maji; ununuzi wa gari na pikipiki saba (7); ujenzi wa chemba; ujenzi wa jengo la ofisi kuu na jengo la ofisi ya uendeshaji eneo la Ngoma; ujenzi wa njia ya umeme mkubwa kutoka Nyasigu hadi katika chanzo cha Mabiru; na uunganishaji wa wateja wa majumbani. Hadi mwezi Aprili 2023, Mkandarasi ameanza maandalizi ya awali ya kuleta vifaa na wataalam.

### 4.2.4.3 Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28

**104. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma ya maji katika miji 28 ambapo miradi katika miji 24 inatekelezwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim na miradi katika miji minne (4) inatekelezwa kwa fedha za ndani. Hadi mwezi Aprili 2023, Wakandarasi wameanza utekelezaji wa miradi.
Aidha, msamaha wa kodi umepatikana kwa miji yote 28.

### 4.2.4.4 Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu

**105. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unatekelezwa kwenye Wilaya tano (5) za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kwa niaba ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*) kwa gharama ya **Shilingi bilioni 444.6**. Hadi mwezi Aprili 2023, kiasi cha **Shilingi bilioni 1.97** kimetumika kulipa fidia kwa wananchi wapatao **1,364** kati ya **1,395** waliofanyiwa uthamini. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi zinaendelea na utekelezaji unatarajiwa kuanza katika mwaka

2023/24. Mradi utawanufaisha wananchi wapatao **495,000** wa Wilaya hizo.

### 4.2.4.5 Mtandao wa Taifa wa Usambazaji Maji (National Water Grid)

**106. Mheshimiwa Spika**, Mtandao wa Taifa wa Usambazaji Maji (*National Water Grid*) unalenga kuhakikisha maji yanapatikana kwenye maeneo yote nchini na katika kipindi chote cha mwaka bila kujali iwapo eneo husika lina vyanzo vya maji au lina uhaba wa maji. Mtandao huo unahusisha ujenzi wa mtandao wa kusafirisha maji kutoka maeneo yenye maji mengi na kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba (*Inter Basin Water Transfer - IBWT*). Utekelezaji wa mtandao huo unawezekana kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na maziwa makuu matatu (3) ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, na imepitiwa na mito mikubwa 11 ya Ruvuma, Rufiji, Kilombero, Pangani, Wami, Ruvu, Malagarasi, Ruhuhu, Kiwira, Kagera na Mara ambayo hutiririsha maji kipindi chote cha mwaka. Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka maeneo mbalimbali ya Shinyanga, Tabora na Simiyu ni mfano mojawapo wa mtandao unaotoa maji kutoka kwenye eneo lenye maji mengi kuyapeleka kwenye maeneo yenye uhaba.

**107. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha maeneo mengi zaidi yananufaika na mpango wa *National Water Grid*, Wizara inaendelea na maandalizi ya kutekeleza miradi mikubwa kwenye maeneo mengine nchini. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu wa awali na inaendelea na taratibu za kumpata mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni. Mtaalam Mshaur huyo anatarajiwa kuajiriwa katika mwaka wa fedha 2023/2024.

### 4.2.5 Miradi ya Usafi wa Mazingira

**108. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka katika maeneo ya mijini ambayo hutolewa kwa njia ya mfumo wa mabomba na magari ya majitaka. Uboreshaji huo umeongeza mtandao wa majitaka kutoka kilomita 1,385.8 mwezi Aprili 2022 hadi kilomita **1,416.93** mwezi Aprili 2023. Pia, maunganisho yameongezeka kutoka wateja **53,428** mwezi Aprili 2022 hadi wateja **56,923** mwezi Aprili 2023. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

**(i) Kuboresha Huduma ya Uondoshaji Majitaka katika Jiji la Mwanza**

**109. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka katika maeneo ya Mabatini, Kilimahewa A, Kilimahewa B na Pasiansi unaogharimu **Shilingi 3,720,864,077.92**. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa mabomba ya majitaka umbali wa kilomita **15.79**; ujenzi wa chemba, ujenzi wa ngazi, uboreshaji wa *squatting pan* na kuunganisha wateja **900.** Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji umefikia **asilimia 82**.

**110. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali inatekeleza mradi wa upanuzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la Ilemela kwa gharama ya **Shilingi 6,739,048,681.80**. Mradi unahusisha ujenzi wa *settling tank*; ujenzi wa chemba mbili (2) za mgawanyo *(splitting chamber)*; na ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya kusafisha majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 51**.

**111. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka sehemu za milimani katika maeneo ya Igogo – Sahara, Kabuhoro, Isamilo, na Ibungiro Jijini Mwanza kwa gharama ya **Shilingi 3,844,768,482.50**. Kazi

zinazoendelea ni pamoja na kutandaza mabomba ya ukusanyaji majitaka na kufanya maunganisho ya wateja wa majitaka sehemu za milimani. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 85** na utawanufaisha wakazi **355,000**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2023.

**(ii) Mradi wa Ukarabati wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneo ya Area C na D katika Jiji la Dodoma**

**112. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa mfumo wa majitaka katika maeneo ya Area C na Area D yaliyopo Jijini Dodoma unaogharimu **Shilingi bilioni 4.96**. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa chemba 1,005 za majitaka; na ukarabati wa bomba za majitaka umbali wa kilomita 19. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 82** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

**(iii) Mradi wa Upanuzi wa Mfumo wa Majitaka katika Maeneo ya Korongoni na Longuo "A" Manispaa ya Moshi**

**113. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Manispaa ya Moshi kwa kujenga mradi wa upanuzi wa mfumo wa majitaka katika Kata za Korongoni na Longuo "A" kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1**. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa bomba la majitaka umbali wa kilomita 12.99 na ujenzi wa chemba 171 za majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80**.

**(iv) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Nzega**

**114. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Mji wa Nzega kwa gharama ya **Shilingi 1,586,916,242**. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa chemba ya kupokea majitaka; ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka; ujenzi wa jengo la mlinzi; ujenzi wa eneo oevu; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; uwekaji wa *geomembrane*; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti 2023 na utawanufaisha wananchi wapatao 133,000.

**(v) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka katika Manispaa ya Singida**

**115. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafisha majitaka katika Manispaa ya Singida kwa gharama ya **Shilingi 1,764,606,000**. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka; ujenzi wa jengo la walinzi; ujenzi wa eneo oevu; ujenzi wa maabara, ujenzi wa jengo la ofisi; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 10**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024 na utawanufaisha wananchi wapatao 112,934.

**(vi) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Muheza**

**116. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika mji wa Muheza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.03.** Utekelezaji wa mradi

unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kutibu topekinyesi; ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka; ununuzi wa gari la usimamizi wa mradi, ujenzi wa barabara ya kufika eneo la bwawa; na ujenzi wa vyoo shuleni na stendi. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 60**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023 na kuwanufaisha wananchi wapatao **38,131**.

(vii) **Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka Omurushaka/Kayanga**

**117. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la Omurushaka/Kayanga kwa gharama ya **Shilingi 1,071,954,550.84**. Utekelezaji wa mradi unahusisha kusafisha eneo la ujenzi wa mabwawa; ujenzi wa barabara kutoka barabara kuu kwenda kwenye mabwawa yenye urefu wa kilomita 1.2; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *Facultative*; ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya *maturation*; ujenzi wa jengo la walinzi; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majitaka; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 65** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023. Mradi ukikamilika utawanufaisha wananchi wapatao **45,000**.

(viii) **Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Kutibu Majitaka Kyaka-Bunazi**

**118. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la KyakaBunazi kwa gharama ya **Shilingi 970,355,684**. Utekelezaji wa mradi unahusisha kusafisha eneo la ujenzi wa mabwawa; ujenzi wa barabara kutoka barabara kuu kwenda kwenye

mabwawa yenye urefu wa mita 800; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *anaerobic*; ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya *Facultative*; ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya *maturation*; ujenzi wa jengo la walinzi; ujenzi wa mfumo wa kukausha topekinyesi; ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 5** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kukamilika kwa mradi kutawanufaisha wananchi wapatao **35,000**.

**(ix) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Mji wa Chato.**

**119. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Mji wa Chato kwa gharama ya **Shilingi 1,594,256,565**. Mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya majitaka; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa; na ununuzi wa magari mawili (2) ya uondoshaji majitaka. Hadi mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 5**.

**(x) Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Majitaka Eneo la Ngalanga katika Mji wa Njombe**

**120. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Ngalanga katika Mji wa Njombe kwa gharama ya **Shilingi 1,240,186,800**. Mradi unahusisha ujenzi wa mabwawa ya kupokea na kuchakata majitaka; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la mabwawa; ujenzi wa jengo la walinzi; na ununuzi wa gari la uondoshaji majitaka. Hadi mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 3**.

**(xi) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Usafi wa Mazingira katika Kata ya Sinde Jijini Mbeya**

**121. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuboresha Huduma ya Usafi wa Mazingira katika kata ya Sinde Jijini Mbeya kwa gharama ya **Shilingi milioni 167.07**. Mradi unahusisha ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 1.5; ujenzi wa chemba 71 za majitaka; ukarabati wa bomba umbali wa mita 220; na ukarabati wa chemba 12. Hadi mwezi Aprili, 2023 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 97**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023 na utawanufaisha wananchi wapatao **5,800**.

**(xii) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Majitaka katika Manispaa ya Musoma**

**122. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya uondoshaji wa majitaka katika Manispaa ya Musoma unaogharimu **Dola za Marekani milioni 13.28**. Mradi huo unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kukusanya majitaka katika Kata ya Kitaji, Iringo, Mwigobero, Mwisenge na Mkendo; ujenzi wa vituo vinne vya kusukuma majitaka; ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika Kata ya Makoko; na ujenzi wa vyoo katika shule za msingi na vyoo vitano (5) kwa ajili ya masoko na machinjio. Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 13**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2024.

### 4.2.6 Taasisi zilizo Chini ya Wizara

#### 4.2.6.1 Mfuko wa Taifa wa Maji

**123. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Maji yenye dhamana ya kutafuta na kutoa

rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini na Bodi za Maji za Mabonde. Mfuko huo unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 na chanzo kikuu cha mapato kwa Mfuko ni tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli.

**124. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Mfuko uliidhinishiwa **Shilingi 175,912,837,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Hadi kufikia Aprili 2023, Mfuko umepokea jumla ya **Shilingi 105,064,199,108.40** sawa na **asilimia 60** ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha hizo zimepelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maji kote nchini na kipaumbele kimekuwa ni miradi inayoendelea na iliyo katika hatua za mwisho kukamilika ili wananchi waweze kunufaika na huduma ya majisafi na salama. Vilevile, jumla ya miradi ya maji **225** imepokea fedha kati ya miradi **376** iliyopangwa ambapo utekelezaji wa **miradi 48** umekamilika. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Maji umetoa fedha kwa ajili ya kuwezesha vyanzo vya maji **67** kulindwa na kutunzwa.

**125.** Mfuko pia umeendelea kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza miradi ya maji nchini hususan katika kutoa mafunzo ya uandaaji wa maandiko ya miradi (*Bankable Project Proposals*) kwa ajili ya kutafuta fedha za uwekezaji katika miradi ya maji. Hadi mwezi Aprili 2023, Mfuko kwa kushirikiana na USAID kupitia Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira umetoa mafunzo ya kuandaa maandiko ya miradi kwa Mamlaka za Maji, RUWASA na Bodi za Maji za Mabonde kwa mikoa ya Ruvuma, Iringa, Rukwa, Morogoro, Songwe na Njombe.

**126. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini, Mfuko umezindua rasmi dirisha la mikopo ya riba nafuu mahususi kwa Mamlaka za Maji na taasisi zinazotoa huduma ya maji nchini zitakazokidhi vigezo. Dirisha hilo la mikopo lilizinduliwa tarehe 06 Februari 2023 na kwa sasa taratibu zote za utoaji wa mikopo zimekamilika. Mikopo hiyo ni mojawapo ya chanzo cha fedha za miradi kwa Mamlaka za Maji na itachochea kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Kupitia mikopo hiyo, fedha inayorejeshwa (*revolving funds*) itatumika kutekeleza mradi mingine na kuwezesha mfuko kufikia miradi mingi zaidi.

### 4.2.6.2 Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)

**127. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuijengea uwezo RUWASA ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Katika mwaka 2022/23 jumla ya magari 15 na pikipiki 395 zimenunuliwa ili kuiimarisha usimamizi, ufuatiliaji na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Magari hayo yalipelekwa katika mikoa 13 ya Tanga, Arusha, Njombe, Dodoma, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Kagera, Morogoro, Shinyanga, Mara, Tabora na Iringa na magari mawili yalibaki RUWASA makao makuu. Vilevile, pikipiki zilizonunuliwa zilipelekwa katika ofisi za RUWASA wilaya na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii.

**128. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza kasi ya uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji nchini, Serikali imenunua mitambo (*Drilling Rigs*) 25 ya kuchimba visima; na seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa. Mitambo hiyo ilikabidhiwa kwa Wizara ya Maji mwezi Novemba 2022 na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Mitambo hiyo

itaharakisha kazi ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa nchini.

**129. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa RUWASA ambapo ukarabati wa majengo **matano (5)** ya ofisi katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga umekamilika. Vilevile, taratibu za kuwapata wakandarasi watano (5) kwa ajili ya kujenga ofisi mpya katika mikoa ya Mara, Njombe, Geita, Manyara na Morogoro zimekamilika. Pia, Wakandarasi watano (5) wamepatikana kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za RUWASA Wilaya katika miji ya Nyasa, Kalambo, Kongwa, Kahama na Tanganyika.

### 4.2.6.3 Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira

**130. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini umekasimiwa kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Mamlaka hizo zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019. Utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira unasimamiwa na Bodi za Wakurugenzi zinazoteuliwa na Waziri mwenye dhamana na Maji.

**131. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma, Wizara ilifanya tathmini na kuunganisha baadhi ya Mamlaka. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara ina jumla ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira **87** nchini. Idadi hiyo ya Mamlaka imegawanyika katika makundi manne (4) ambayo ni Mamlaka 25 za Miji Mikuu ya Mikoa, Mamlaka 49 za Miji Mikuu ya Wilaya, Mamlaka sita (6) za Miji Midogo na Mamlaka saba (7) za Miradi ya Kitaifa. Vilevile, Serikali imeendelea kuziimarisha mamlaka za maji kwa kujenga ofisi katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Arusha, Maswa, Sengerema,

MugangoKiabakari na Biharamulo. Aidha, Serikali imetoa mafunzo ya kujenga uwezo wa menejimenti na Bodi za Wakurugenzi kwa Mamlaka **33** za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa mamlaka hizo.

### 4.2.6.4 Chuo cha Maji

**132. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Maji ni taasisi yenye jukumu la kuandaa wataalam wa maji. Majukumu mengine ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Sekta. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada. Mafunzo yanayotolewa katika ngazi za Astashahada na Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*); Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*); Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*); Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (*Sanitation Engineering*) pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada mafunzo yanatolewa katika fani za Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*); Uhandisi wa Usafi wa Mazingira (*Bachelor of Sanitation Engineering*); Maendeleo ya Jamii na Uhandisi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (*Community Development for Water Supply and Sanitation Engineering*); Haidrojiolojia na Uchimbaji (*Hydrogeology and Drilling*) na Uhandisi wa Haidrolojia (*Engineering Hydrology*). Vilevile, Chuo kinaendesha kozi mbalimbali za muda mfupi katika sekta za maji na umwagiliaji.

**133. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, wanafunzi **864** wa Astashahada na Stashahada wamedahiliwa ambapo **704**

wamedahiliwa Kampasi ya Ubungo na **160** Kampasi ya Singida. Vilevile, wanafunzi wapatao **500** wa Shahada ya kwanza walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 247 katika mwaka 2021/22. Hadi mwezi Aprili 2023, Chuo kina jumla ya wanafunzi **2,835** ambapo **1,912** ni wa Astashahada na Stashahada na wanafunzi **923** ni wa Shahada ya kwanza. Aidha, katika mahafali ya Novemba 2022, jumla ya wanafunzi **464** walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi **133** ni wa Shahada, **269** wa Stashahada na wanafunzi **62** walikuwa wa ngazi ya Astashahada.

**134. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika ngazi za Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu. Hadi mwezi Aprili 2023, watumishi **13** wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (PhD); Watumishi **watano (5)** Shahada ya Uzamili (*Masters*) na watumishi **Watatu (3)** Shahada ya kwanza. Vilevile, Chuo kimekamilisha ukarabati wa hosteli **tano (5)** zenye uwezo wa kulaza wanafunzi wapatao **916** na ujenzi wa majengo yenye madarasa **15** na ofisi **17**.

### 4.2.7 Masuala Mtambuka

#### (i) Rasilimali Watu katika Sekta ya Maji

**135. Mheshimiwa Spika**, rasilimali watu ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Maji. Mahitaji ya rasilimali watu katika Sekta ya Maji ni watumishi 10,276 ikilinganishwa na watumishi **9,422** waliopo na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **854**. Kati ya watumishi waliopo wahandisi (*Engineers*) ni 704 na mafundi sanifu **2,647** ambapo wahandisi 499 sawa na asilimia 70 wamesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi nchini (*Engineers Registration Board* - ERB) kama wahandisi wataalam na wahandisi 205 sawa na asilimia 30 wapo kwenye hatua mbalimbali za kusajiliwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa wahandisi

wote wanasajiliwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu walipoajiriwa ili kuimarisha usimamizi wa miradi ya maji inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**136. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika fani mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya watumishi **1,898** walipatiwa mafunzo ambapo watumishi **1,700** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **198** walipata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Pia, Taasisi zilizo chini ya Wizara zimeendelea kujengewa uwezo wa kutayarisha Ikama na Makisio ya Mishahara (PE), kuandaa Mipango ya Rasilimali watu na kupitia Miundo ya Taasisi, Utumishi na mishahara kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma.

(ii) **Jinsia**

**137. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia katika Taasisi zilizo chini yake. Uwiano huo ni muhimu kwenye vyombo vya maamuzi, usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi nchini. Hadi mwezi Aprili 2023, idadi ya watumishi wanawake ni **2,827** sawa na asilimia **30** ikilinganishwa na wanaume **6,595** sawa na asilimia **70**. Aidha, viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara na Taasisi waliopo, wanawake ni **201** sawa na asilimia **24** na wanaume ni **622** sawa na asilimia **76**. Vilevile, uteuzi wa kamati mbalimbali huzingatia uwiano wa jinsia ili kuhakikisha watumishi wote wanashiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao.

**(iii) Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**138. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendeleza juhudi za mapambano dhidi ya rushwa kwa kutekeleza Mkakati wa Taifa

Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP III*) kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Mkataba huo unahakikisha wananchi wanatambua haki na wajibu wao katika kupokea huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake. Vilevile, vikao viwili (2) vya Kamati ya Maadili vilifanyika kwa ajili ya kutathmini mafunzo ya mapambano dhidi ya rushwa na maadili yaliyofanyika katika Taasisi 17 zilizo chini ya Wizara. Kwa ujumla, tathmini hiyo inaonesha kuwa hali ya mapambano dhidi ya rushwa imeendelea kuimarika na hivyo kupunguza viashiria vya rushwa.

**(iv) UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

**139. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mwongozo wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya watumishi **3,283** walipata mafunzo maalum kuhusu kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza. Aidha, posho kwa ajili ya kununua lishe bora na usafiri kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kutolewa.

**Ujenzi wa Majengo ya Wizara**

**140. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu – Mtumba linalogharimu kiasi cha Shilingi **bilioni 22.97** na ujenzi wake ulianza rasmi tarehe 3 Novemba, 2021. Hadi mwezi Aprili 2023, ujenzi umefikia **asilimia 88** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023. Vilevile, Wizara imekamilisha ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi za Bodi za maji za mabonde ya Ziwa Nyasa katika Mji wa Njombe; Ziwa Rukwa, Wami - Ruvu na ofisi za Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini katika miji ya Lindi na Mtwara. Aidha, ujenzi wa Ofisi ya

Bonde la Rufiji umefikia **asilimia 98** na ofisi ya Bonde la Nyasa katika mji wa Songea umefikia **asilimia 33.**

**141.** Kwa upande wa Maabara za Maji, Wizara imekamilisha ujenzi wa majengo ya Maabara za Iringa, Mbeya, Sumbawanga, Songea, Mtwara na Morogoro pamoja na ununuzi wa samani za maabara hizo. Vilevile, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kupitia michoro na kusimamia ujenzi wa majengo ya Maabara za Arusha, Tanga na Dodoma zimeanza.

**(v) Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA**

**142. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (*e-Government Authority*) imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuboresha huduma zinazotolewa na Sekta. Katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mifumo ya Pamoja kwa kuziunganisha na kutoa mafunzo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara kuwezesha kutumia mifumo hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 na Kanuni Zake za Mwaka 2020. Mifumo hiyo ni Mfumo wa Pamoja wa Ankara za Maji (*Unified Maji Billing System)* unaofahamika kama '*MAJIIS*' kwa ajili ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na Bodi za Maji nchini; Mfumo Jumuishi unaosaidia Kusimamia Rasilimali za Taasisi (*Enterprise Resource Management Suite*) kwa ajili ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira; na Mfumo wa Taarifa za Miradi unaopatikana kwa njia ya Simu za Kiganjani unaofahamika kama '*Maji App*'. Mfumo wa Taarifa za Miradi kwa njia ya Kiganjani unarahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi iliyokamilika na inayoendelea katika kila mkoa pamoja na kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi yote ya maji nchini.

**143. Mheshimiwa Spika**, mfumo wa *MAJIIS* umetengenezwa mahususi kwa ajili ya kusimamia ankara za maji zinazotolewa pamoja na utoaji vibali vya watumia maji, umwagaji wa majitaka na uchimbaji visima. Mfumo huo umeanza kusaidia katika kudhibiti ubambikizaji wa Ankara za Maji kwa sababu Mteja anashirikishwa wakati wa usomaji wa Mita za Maji kwa kutumiwa Arafa (SMS) mara usomaji unapofanyika ukionesha usomaji wa sasa, usomaji wa mwezi uliopita na kiasi cha matumizi yake ya maji. Ujumbe huu unamtaka Mteja kuhakiki usomaji huo kabla ya Ankara yake kuandaliwa na ikiwa hajaridhika au kuhitaji ufafanuzi, basi awasiliane na Msoma Mita au Mamlaka husika kupitia Namba ya Simu inayowekwa kwenye Ujumbe huo ili ahudumiwe. Hivyo, natoa wito kwa wananchi wote wawe wanahakiki usomaji kwenye Mita zao pindi wanapopokea ujumbe mfupi kupitia simu za mkononi mara usomaji unapofanyika. Mfumo huo pia umerahisisha huduma za kupokea bili za maji na kufanya malipo kupitia njia za kielektroniki/miamala ya simu za viganjani popote pale mtu alipo.

**144. Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya taasisi **96** zimejiunga na mfumo wa Kusimamia Ankara za Maji nchini (MAJIIS). Taasisi hizo ni Mamlaka **86** za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji Mikuu ya Mikoa, Miji ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na Miradi ya Kitaifa. Vilevile, Bodi za Maji za Mabonde tisa (9) zimejiunga na kutumia Mfumo huo. Aidha, Mfumo huo unatarajia kuunganishwa na Mifumo mingine ya Serikali kama vile NIDA na BRELA ili kuwezesha maombi ya kuunganishiwa huduma ya maji yafanyike kidijitali.

**145. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi (*Enterprise Resource Management Suite – ERMS*) tayari Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira **28** zimeanza kutumia mfumo huo unaolenga kuwezesha Mamlaka hizo kutekeleza majukumu yake kwa njia ya kidijitali na

kupunguza gharama za matumizi ya karatasi. Mamlaka nyingine zilizobakia zitaungwa kwenye Mfumo huo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

## 5. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

**146. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zinazochukuliwa kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:-

### (i) Uchafuzi na Uharibifu wa Vyanzo vya Maji

**147. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na uchafuzi, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii na hivyo kunachangia kwa sehemu kubwa kupungua na kuzorota kwa ubora wa rasilimali za maji hali hii huathiri uendelevu wa rasilimali za maji nchini.

**148.** Katika kukabiliana na changamoto ya uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendeleza uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji kupitia mipango mbalimbali inayojumuisha kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji; pamoja na kutambua, kuweka mipaka, kutangaza kwenye Gazeti la Serikali na kurejesha vyanzo vya maji vilivyoharibika. Wizara yangu inaendelea kutoa wito kwa jamii na wadau wote kutii sheria na kanuni zinazosimamia rasilimali za maji, kuhamasisha matumizi bora ya maji kwa shughuli za kijamii na kiuchumi ili kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

**(ii) Mahitaji Makubwa ya Fedha kwa ajili ya Uwekezaji wa Miradi Mikubwa ya Maji**

**149. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ya kimkakati kama vile ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Ndembera/Lugoda umechelewa kutekelezwa kutokana na uhitaji wa fedha nyingi. Hali hiyo imesababisha miradi hiyo kuendelea kuwekwa kwenye mipango ya utekelezaji ya kila mwaka wa fedha. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia fedha za ndani ili kutekeleza miradi hiyo mikubwa na muhimu katika Sekta ya Maji.

**(iii) Mabadiliko ya Tabianchi**

**150. Mheshimiwa Spika,** athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwemo ukame wa muda mrefu, kuchelewa kwa mvua pamoja na mafuriko zimeendelea kuathiri sekta ya maji kwa kuchangia kukauka kwa vyanzo vya maji, kuongezeka kwa migawo ya maji pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji. Katika kipindi cha karibuni, athari za mabadiliko ya tabianchi zimedhihirika katika vyanzo vingi vya maji kwa mfano Mto Ruvu ambao ulipungua sana kina cha maji hali iliyosababisha kuchukua hatua za dharura kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**151.** Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuhimiza ushiriki wa wananchi katika utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na mazingira. Vilevile, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa na maziwa na ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua.

## 6. VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/24

### 6.1 Vipaumbele vya Sekta

**152. Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na kuendelea na utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria; kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji; kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa ikiwemo miradi ya maji katika miji 28; kuendelea na ujenzi wa bwawa la kimkakati la Kidunda na kuanza ujenzi wa bwawa la Farkwa; na kusanifu na kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwemo maziwa makuu na mito mikubwa ili kuyapeleka maeneo yenye uhaba mkubwa wa maji.

### 6.2 Mpango wa Utekelezaji

**153. Mheshimiwa Spika**, mpango wa utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2023/24 umeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuibua miradi ya kipaumbele. Aidha, mpango umejikita katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; usimamizi wa ubora wa maji; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira vijijini; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira mijini; utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara; na masuala mtambuka kama ifuatavyo:-

### 6.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

#### (i) Utunzaji wa Vyanzo vya Maji na Uhifadhi wa Mazingira

**154. Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kuendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kuweka mipaka inayoainisha maeneo ya hifadhi katika vyanzo vya maji ili kudhibiti shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo na mengine kuyatangaza katika Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu. Katika mwaka 2023/24, jumla ya vyanzo 84 vitawekewa mipaka na kutangazwa kama maeneo tengefu. Aidha, Serikali itafanya ukaguzi wa miundombinu ya utupaji majitaka katika migodi, viwanda pamoja na maeneo mengine.

#### (ii) Ujenzi wa Mabwawa

**155. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa uvunaji maji ya mvua na kuanza utekelezaji wa ujenzi wa bwawa moja kwa kila wilaya yenye mazingira yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa; kuongeza kasi ya ujenzi wa mabwawa ya maji ya ukubwa wa kati hususan katika maeneo yenye ukame; na kujenga mabwawa ya kimkakati. Katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kujenga mabwawa **27** ya ukubwa wa kati na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati kwa ajili ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

#### (iii) Usimamizi wa Rasilimali za Maji

**156. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara itakarabati vituo **135** na kujenga vituo **51** vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji, kutoa vibali 450 vya matumizi ya maji, kutoa vibali 30 vya kutupa majitaka, kuunda Jumuiya 10 za Watumia Maji pamoja na kuzijengea uwezo Jumuiya 87 na kuunda kamati **9** za vidakio (*Catchment Committees*).

Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia shughuli za uchimbaji wa visima vya maji, kuendesha majukwaa na vikundi kazi vya wadau wa sekta mtambuka wa rasilimali za maji, kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi, kuimarisha taasisi zinazosimamia rasilimali za maji nchini na kufanya tathmini ya thamani ya maji kiuchumi.

### 6.2.2 Usimamizi wa Ubora wa Maji

**157. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuimarisha uhakiki na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji **2,091**; skimu **4,600** za usambazaji maji mijini na vijijini pamoja na mifumo **150** ya majitaka; kuziwezesha maabara tano (**5**) kupata ithibati; kuhakiki ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji kabla ya manunuzi na wakati wa matumizi; kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji inayohimili mabadiliko ya tabianchi kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira **34** na Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamiii **100**; kutoa elimu kuhusu viwango vya ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali; na kuendelea kuimarisha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi pamoja na kujenga na kukarabati majengo ya maabara.

### 6.2.3 Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

**158. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi ya maji vijijini **1,546** (**Kiambatisho Na. 4).** Vilevile, Serikali itaendelea na ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali ya vijijini (**Kiambatisho Na. 5)**.

**159. Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kuimarisha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya

vijijini, Serikali imepanga kuzijengea uwezo CBWSOs **2,543** na kusajili CBWSOs mpya **111**.

### 6.2.4 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi **244** ya maji mijini. Orodha ya miradi ya majisafi na usafi wa mazingira mijini itakayotekelezwa imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 6**.

#### (i) Miradi ya Kimkakati ya Majisafi katika maeneo mbalimbali ya Miji

**161. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wananchi wengi wanapata huduma ya maji, Serikali imepanga kutekeleza miradi mikubwa itakayotumia vyanzo vya uhakika. Katika mwaka 2023/24, Serikali itafanya mapitio ya usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara – Mikindani pamoja na vijiji na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya bomba kuu; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa kutoa maji mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya mkoa wa Pwani; na kuanza ujenzi wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Malampaka na Malya.

#### (ii) Mpango wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma

**162. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Jiji la Dodoma inayotokana na ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2023/24 Serikali imepanga kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa kukarabati na kupanua mtandao wa majisafi Jijini Dodoma; na Mradi wa ujenzi wa

Bwawa la Farkwa. Vilevile, Serikali itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Mikoa ya Singida na Dodoma.

### 6.2.5 Mpango wa Kuimarisha Huduma ya Usafi wa Mazingira

**163. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uondoshaji wa majitaka katika maeneo mbalimbali ili kuboresha huduma ya usafi wa mazingira nchini. Miradi hiyo ni pamoja na kupanua mtandao wa kupitisha majitaka Jijini Dodoma; kujenga miundombinu ya mfumo wa majitaka eneo la Kurasini Jijini Dar es Salaam; kujenga miundombinu ya mfumo wa majitaka eneo la Mbezi Beach; kujenga miundombinu ya mfumo wa majitaka eneo la Buguruni; kupanua mtandao wa kupitisha majitaka katika Manispaa ya Moshi; kujenga mtandao wa majitaka katika Manispaa ya Bukoba, Misenyi na Kayanga; na kusanifu miradi ya usafi wa mazingira katika miji mikuu 10 ya Vwawa, Kigoma, Lindi, Sumbawanga, Singida, Njombe, Mtwara, Katavi na Tabora. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya usafi wa mazingira katika miji ya Igunga, Chato, Babati, Musoma, Tabora, Dodoma, Mbeya, Iringa, Tanga, Muheza, Njombe, Pangani na Singida.

### 6.2.6 Taasisi za Wizara ya Maji

**164. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kukiimarisha Chuo cha Maji kwa ajili ya kutoa wataalam watakaotumika katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji pamoja na kufanya tafiti za kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Maji. Katika mwaka 2023/24, Chuo kimepanga kujenga majengo matatu (*Lecture theatre, Boardroom Block na High tech Laboratory Block*); kukarabati majengo ikiwemo maktaba katika Kampasi Kuu ya Ubungo - Dar es Salaam; kuanza ujenzi wa Kampasi ya Singida katika eneo la Mwankoko; kukimarisha

kituo cha utafiti cha Ngurdoto, Arusha kwa kujenga jengo la utawala, maabara, jengo la kuhifadhi malighafi za utafiti na kuajiri watumishi; na kutumia jarida lake la kitaalam (*The Journal of Water Resources, Engineering, Management and PolicyJWEMPO*) ambalo litatoa fursa kwa watafiti na watendaji ndani na nje ya nchi kuchapisha taarifa na tafiti mbalimbali za kutatua changamoto kwenye Sekta ya Maji, na pia kusambaza elimu na maarifa yenye tija kwa jamii.

**165. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Chuo kimepanga kununua vifaa vya TEHAMA, pamoja na mtambo mmoja wa kuchimba visima (*Drilling Rig*) ikiwa ni mkakati wa kuhakikisha ufundishaji kwa vitendo unaboreshwa ili kuendana na uhitaji wa Sekta ya Maji nchini. Aidha, Chuo kitaongeza udahili wa wanafunzi wapya wapatao 3,000; kuongeza programu mpya sita (6) ngazi ya Shahada na kuanzisha programu nne (4) za ngazi ya Uzamili. Chuo pia kimepanga kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma, pamoja na kuajiri wakufunzi ili kuendana na kasi ya ongezeko la udahili na programu.

### 6.2.7 Masuala Mtambuka

**166. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, kuandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Maji (*National Water Master Plan*); kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali chini ya Sheria za Maji ili kuhakikisha kuwa sheria za maji zinatekelezwa kikamilifu; kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili kuleta tija katika Sekta ya Maji; kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Jinsia wa Sekta ya Maji; kutoa elimu na kuhamasisha watumishi kuendelea kupima afya zao; na kusambaza vifaa kinga katika vituo vya kazi ili kudhibiti maambukizi mapya ya *VVU*.

## 7. SHUKRANI

**167. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote wanaochangia kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Maji. Michango, maoni na mapendekezo ya wadau wote yamezingatiwa na yamesaidia kuboresha maandalizi ya bajeti na hotuba ya Wizara yangu katika kuweka vipaumbele vinavyolenga kutatua changamoto na kuboresha utoaji wa huduma katika Sekta ya Maji. Hii inadhihirisha wazi kuwa mchakato wote wa maandalizi ya bajeti na hotuba yetu umezingatia dhana ya ushirikishwaji wa wadau na makundi yote ya jamii kwa maendeleo ya Sekta ya Maji na Taifa.

**168. Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii pia kukushukuru wewe na wawakilishi wa wananchi ambao ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuwawakilisha vyema wananchi, kuisimamia na kuishauri vizuri Wizara yangu katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya Sekta ya Maji. Ninasema ahsanteni sana.

**169. Mheshimiwa Spika,** naendeleza shukrani zangu kwa Nchi Rafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Misaada ya Kimataifa, Sekta Binafsi, Taasisi za Kiserikali, Mashirika ya Kidini na wadau wengine kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Serikali ya Awamu ya Sita ambayo ina dhamira kubwa ya kuwaletea wananchi wake maendeleo hususan katika Sekta ya Maji. Kipekee ninapenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo tunashirikiana nazo kwa sasa zikiwemo Uingereza, Ujerumani, India, Marekani, Korea Kusini, Uholanzi, Hispania, Misri, Ufaransa, Kuwait, Ubelgiji, Italia na Saudi Arabia.

**170. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninayashukuru Mashirika ya Maendeleo na Taasisi za Kimataifa kwa misaada ya kitaalam

na kifedha katika kuiwezesha Sekta ya Maji kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund),* Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD), Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO),* Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GiZ),* Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), *Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF),* Shirika la Afya Duniani *(WHO),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Maendeleo la Ubelgiji *(BTC),* Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID)*.

**171. Mheshimiwa Spika**, pia ninapenda kuwashukuru Viongozi na Waumini wa Dini zote kwa kuliombea Taifa na viongozi wa Taifa letu, kwa unyenyekevu mkubwa naendelea kuwaomba na kuwasihi waendelee kuliombea Taifa letu na viongozi wetu. Vilevile, nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kidini ambazo zimeendelea kusaidia Sekta ya Maji kufikia malengo yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation,* Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

**172. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza Sekta ya Maji. Taasisi hizo

ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS), OIKOS, Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET),* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA), World Vision*; *Worldwide Fund for Nature (WWF*), *Netherlands Volunteers Services (SNV), Plan International*, *Concern Worldwide*, WaterAid Tanzania, *Water Mission* (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Maliasili (*IUCN*) na Mashirika mengine mbalimbali.

**173. Mheshimiwa Spika**, ninaomba nitumie fursa hii kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara nikianza na Naibu Waziri wa Maji **Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi (Mb)** ambaye amekuwa akifanya kazi kubwa kuhakikisha Sekta ya Maji inasonga mbele na wananchi wengi zaidi wanafikiwa na huduma ya maji. Vilevile, naomba kuwapongeza **Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Mhandisi **Mhandisi Cyprian John Luhemeja** kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Imani na dhamana waliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa na ninaamini katika utendaji wao tutafanya mageuzi makubwa katika kuongeza kasi ya maendeleo katika Sekta ya Maji. Aidha, kipekee napenda kuwashukuru Viongozi wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wote wa Wizara ya Maji na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatimizwa.

**174. Mheshimiwa Spika,** Natumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na nguvu ya kuwatumikia Watanzania katika Sekta ya Maji na kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Pia, naishukuru familia yangu na wananchi wa Jimbo la Pangani kwa maombi, dua, upendo, ushirikiano, faraja, uvumilivu na kuendelea kunilea na kuniamini katika kutekeleza majukumu

yangu na ninaahidi kuendelea kutumia maarifa yangu yote katika kujenga jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

**8. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24**

**175. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 756,205,106,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 60,375,474,000** ambapo **Shilingi 18,035,561,000** sawa na **asilimia 29.87** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (*OC*) na **Shilingi 42,339,913,000** sawa na **asilimia 70.13** ni kwa ajili ya kulipa Mishahara (*PE*) ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 695,829,632,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 407,064,860,000** sawa na **asilimia 58.50** ni fedha za ndani na **Shilingi 288,764,772,000** sawa na **asilimia 41.50** ni fedha za nje.

**176. Mheshimiwa Spika**, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.maji.go.tz*

**177. Mheshimiwa Spika**, NINAOMBA KUTOA HOJA.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa Waziri kwa kusoma vizuri.

**WAZIRI WA MAJI:** Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Maryprisca, Naibu Waziri wa Maji ambao ni Ndugu Rufina Mtega - mke wa kaka yake, Ndugu Yutus Mbunda ambae ni kaka yake, Ndugu Dorwin Bahati - dada yake, Ndugu Edith Mgoto - dada yake, Ndugu Anthony Chondu - mtoto, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tano ambazo ni: -

a) Sehemu ya kwanza inatoa maelekezo ya jumla, na kubainisha msingi na muundo wa taarifa;

b) Sehemu ya Pili inachambua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji na upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

c) Sehemu ya Tatu, inaonesha uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ya maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne, inaonyesha maoni na ushauri wa Kamati na;

e) Sehemu ya Tano inahitimisha, taarifa kwa ushauri wa Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Maji aliyoitoa mapema hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Wizara hii katika Mikoa ya Shinyanga, Singida, na Manyara. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa miradi ya maji Kagongwa – Isaka. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi 4,256,000,000 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa mradi wa maji wa Kagongwa – Isaka iliyopo Wilaya ya Kahama. Hadi Machi 23 utekelezaji wa mradi huu ulifikia asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao 28,700 katika vijiji vitano. Aidha Kamati ilibaini changamoto zifuatazo katika mradi huu:-

a) Ucheleweshaji wa upatikanaji wa bomba za chuma kutoka katika kiwanda kinachozalisha bomba za aina hii kuwa kipo kimoja tu hivyo kusababisha kuchelewa kwa kukamilisha kwa mradi huu; na;

b) Vijiji viwili ambavyo viko jirani na mradi wa maji wa Kagongwa – Isaka kutopatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji katika Miji ya Tinde na Shelui. Mradi huu unahusu upanuzi wa bomba la Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Tinde – Igunga – Shelui - Singida na Vijiji vilivyomo pembezoni mwa bomba kuu kupelekea maji katika miji hiyo. Mradi umetekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 24.94 fedha kutoka Exim Benki ya India.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 99 na wananchi wapatao 108,000 wanatarajiwa kufikiwa na mradi huu katika Miji ya Tinde na Shelui pamoja na Vijiji 34 ambapo Vijiji 22 vipo Tinde na Vijiji 12 vipo Shelui.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzindua mradi huu pamoja na namna anavyofuatilia na kuhakikisha kwamba lengo la Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kumtua Mama ndoo kichwani linafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Ziba kwenda Nkinga. Mradi wa maji wa Ziba – Nkinga unaotekelezwa kwa gharama ya shilingi 5,349,328,135.14, fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia *Program* ya Lipa kwa Matokeo *(PforR)* kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za maji katika vijiji tisa. Hadi Machi 2023, utekelezaji wa mradi ulifikiwa asilimia 85 na wananchi wapatao 29,780 watanufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Orkesumet Wilaya ya Simanjiro. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 41.5 na tayari umekamilika tangu tarehe 30 Agosti,

2022 kwa asilimia 100, hivyo wananchi wapatao 52,000 na mifugo watapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji safi Dareda, Singu, Sigino na Bagara. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara kwa gharama ya shilingi 12,724,407,807.55. Hadi Februari 2023, utekelezaji wa mradi huu ulifikia asilimia 80 na utakamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kujivunia katika mradi huu ni kwamba utekelezaji ni kwa fedha za ndani, asilimia 100 na kusimamiwa na Watanzania (BAWASA). Serikali imeokoa zaidi ya shilingi bilioni 15 kutoka gharama za awali zilizokadiriwa kutumika kiasi cha shilingi bilioni 27 kwa ubora ule ule. Mradi huu ukikamilika, utawezesha wakazi zaidi ya 82,000 kunufaika na huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maji iliyokaguliwa. Hata hivyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi katika miradi ya maji. Serikali iharakishe upatikanaji wa bomba za chuma zinazohitajika katika mradi wa Kagongwa – Isaka ili ahadi ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2020 Ibara ya 100 ukurasa 149 ya kufikisha huduma ya majisafi na salama asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo 2025 iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji iendelee kuwatumia watalaam wa ndani kutekeleza sera ya kuwatumia wakandarasi wa Kitanzania katika utekelezaji wa miradi ya maji. Wananchi ambao ndio wanufaika wa miradi husika,

washirikishwe vizuri katika hatua zote za mradi kuanzia kuibua, kupanga, na utekelezaji wa miradi yenye tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji inayoligharimu Taifa fedha nyingi za walipa kodi ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya maji, na kuifanya iwe endelevu, Serikali ione umuhimu wa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha usalama wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya maendeleo yaliyotembelewa na kukaguliwa, yanapatikana katika ukurasa wa 4 - 14 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, tarehe 27 na 28 Machi, 2023. Uchambuzi katika sehemu hii ulijikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji katika bajeti ya 2022/2023, ukusanyaji wa maduhuli na utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitoa maoni na ushauri katika maeneo tisa. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa ukusanyaji maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maji - Fungu 49 liliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,200,000,000 kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji na ada kwa huduma za maabara. Hadi mwezi Februari, 2023, Wizara ilikusanya kiasi cha shilingi 772,666,497 sawa na asilimia 64.4 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara ya Maji. Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo katika maeneo makuu matatu ya sekta ya maji. Maeneo hayo ni usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya maji safi na mazingira vijijini, uratibu wa kujenga uwezo wa Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi hiyo ni pamoja na kukamilika kwa jumla ya miradi 420 ya maji ambapo vijijini ni 382 na mijini ni miradi 38. Kuzinduliwa kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Awamu ya Tatu na kuanza kutumika rasmi kwa Mfumo wa Pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji *(Unified Billing System)* kwa mamlaka 80 za maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji huo, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge na Waziri wa Maji, pamoja na Watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, *Engineer* Nadhifa Kemikimba kwa usimamizi madhubuti wa utawala bora na kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023, zipo changamoto zilizosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa

baadhi ya miradi ya maji. Changamoto hizo ni pamoja na ucheleweshaji wa upatikanaji wa misamaha ya kodi kutoka mamlaka za mapato; upungufu wa wataalam wa kada mbalimbali. Kwa sasa sekta ina Watumishi 9,422 ambapo mahitaji ni Watumishi 10,276, hivyo kuwa na nakisi ya Watumishi 854; pamoja na mahitaji makubwa ya fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maji Fungu 49 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 708,761,598,600. Kati ya fedha hizo, shilingi 657,899,338 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, na Shilingi 51,461,260,600 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi mwezi Februari, 2023 jumla ya shilingi 575,945,210,657.26 sawa na asilimia 81.3 ya fedha yote ilipokelewa. Kati ya hizo, shilingi 542,789,767,774.55 sawa na asilimia 94.2 ni fedha za maendeleo, na shilingi 33,755,442,884.71 sawa na asilimia 5.9 ni fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha hadi mwezi Februari ni asilimia 81.3. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa mwenendo huo ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 unapatikana kuanzia ukurasa wa 14 mpaka wa 24 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa malengo na vipaumbele vilivyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, vinaendana na majukumu ya msingi ya Wizara ya Maji, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Awamu ya Tatu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2021/2022 – 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Malengo ya

Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 na ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maji - Fungu 49 linatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1,200,001,000, kutokana na vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maji - Fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 756,205,106,000. Kati ya fedha hizo shilingi 60,375,474,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 695,829,632,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi 407,064,860,000 sawa na asilimia 59 ni fedha za ndani na shilingi 288,764,772,000 sawa na asilimia 41, ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kwamba, fedha za maendeleo zinazoombwa ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya kipaumbele. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Bwawa la Kidunda na miradi ya maji vijijini, miradi na kazi zinazohusu uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji ikiwemo ujenzi na ukarabati wa mabwawa, uboreshaji wa huduma za maji ikiwemo kujenga uwezo wa maabara za maji na kujenga uwezo wa taasisi pamoja na watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo. Ni maoni ya Kamati kwamba kiasi hicho kama kitatolewa kama ilivyopangwa na kwa wakati, tutaimarisha huduma ya majisafi na salama na kuwafikia wananchi waliopo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kwamba Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji ni asilimi 4.6 ya Bajeti

Kuu ya Serikali ya Maendeleo ni asilimia 34.1. Uchambuzi huo unaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha huduma ya miundombinu ya majisafi na salama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika sekta ya maji. Uchanganuzi wa takwimu hizi ni ishara ya hatua ya kutimiza ahadi ya Serikali ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 Ibara ya 100 ukurasa wa 149 ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi na kuwafikia wakazi asilimia 85 vijijini na asilima 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kina kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maji ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 unapatikana kuanzia ukurasa wa 25 hadi 34 wa taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji – Fungu 49 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba kubainisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni asilimia 82.5 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge, upatikanaji wa fedha za ndani ni asilimia 77.2 na fedha za nje ni asilimia 91.1 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo, hali hii inayoleta matumaini kwa Kamati kwamba miradi ya maendeleo itakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maji katika kufanikisha azma ya kuwa na usalama wa maji

na kuimarisha huduma ya maji safi na salama, pamoja na kuwafikia wananchi zaidi ya asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo 2025 kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inastahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mizuri ya kuendeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya Kidunda, Farkwa na Ndembera, inahitaji fedha nyingi kuitekeleza. Ucheleweshaji wa upatikanaji wa misamaha ya kodi kwa ajili ya vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya maji, ni kikwazo katika kutekeleza miradi ya maji. Upungufu wa mabomba ya chuma unachelewesha utekelezaji wa miradi ya maji inayohitaji mabomba ya aina hiyo. Upungufu wa wataalam wa kada mbalimbali katika sekta ya maji unakwamisha ufikiwaji wa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Chuo cha Maji ambacho ni hazina ya watalaam wa sekta ya maji kinahitaji kuongezewa bajeti ili kuzalisha watalaam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya upatikanaji wa uhakika wa huduma ya majisafi na salama katika Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya nchi, inahitaji mikakati mahususi. Hakuna mkakati mahususi na wa uhakika wa uvunaji wa maji ya mvua. Yapo malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta ya maji kwamba baadhi ya maeneo ambayo miradi ya miundombinu inapita, hawapati huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kubwa kati ya uwezo wa utendaji na ufanisi wa wafanyakazi wa Taasisi za Wizara ya Maji. Kutokuwepo kwa mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ya maji na *grid* ya Taifa kunaathiri utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maoni yaliyobainishwa hapo juu, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati zinapatikana inavyostahili. Aidha, kutokana na uhitaji mkubwa wa fedha katika miradi hii, Serikali iangalie namna ya kupata fedha kutoka vyanzo vingine ikiwemo, kuandika maandiko ya kutafuta fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Serikali iweke mfumo mzuri utakaowezesha kuharakisha upatikanaji wa misamaha ya kodi ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itafute ufumbuzi wa changamoto ya upungufu wa mabomba ya chuma ili kukwamua miradi ambayo imekwama. Serikali iharakishe kuajiri watalaam katika sekta ya maji ili kukabiliana na upungufu wa watalam 854 katika sekta hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha, Chuo cha Maji kiimarishwe kwa kutengewa fedha za kutosha katika bajeti na kuzalisha watalaam wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na chagamoto ya upungufu mkubwa wa maji safi na salama katika Jiji la Dodoma, Serikali na Wizara iweke mikakati madhubuti ya kupata maji kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uchimbaji visima na kuanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa kutumia maji ya Bwawa la Mtera kuhudumia Jiji la Dodoma, Kamati inashauri utafiti na tathmini ya kina ufanyike ili kubaini kama mradi huo utakuwa endelevu na hautaathiri maslahi ya wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wa maji iandae mkakati mahususi na wa uhakika wa uvunaji wa maji ya mvua. Mkakati huo uzingatie haja ya kutoa elimu kwa umma kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, usanifu wa majengo ya umma, utengaji wa bajeti kwa

ajili ya uvunaji wa maji, na ujenzi wa mabwawa katika maeneo yenye mvua nyingi ili kulinda miundombinu ya barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni maoni ya Kamati kwamba, Wizara iweke mwongozo utakaoelekeza vijiji vinavyopitiwa na miradi ya maji kuwa wanufaika wa kwanza na miradi hiyo; Wizara iweke utaratibu wa watalaam kutoka maeneo mbalimbali kutembeleana na kubadilishana uzoefu ili kuongeza ufanisi katika miradi ya maendeleo; Wizara iandae mpango kabambe wa uendelezaji wa Sekta ya Maji *(National Water Master Plan)* pamoja na Gridi ya Maji ya Taifa *(National Water Grid)* ili kuimarisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wake madhubuti. Kamati yangu inaahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunamwombea afya njema, maisha marefu na mafaniko katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika na kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hususan wakati wa uchambuzi wa bajeti. Naomba majina yao wote yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* pamoja na taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard* za Bunge kama Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge; na Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, Mbunge; Katibu Mkuu Mhandisi Nadhifa Kemikimba; Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Cyprian Luhemeja; pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu bila kukwama. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, pamoja na Makatibu wa Kamati, Ndugu Angelina Langisisi Sanga na Ndugu Nyamwanja Chipanda Chilemeji kwa ushauri, uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**10 MEI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tano ambazo ni: -

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa Maelezo ya jumla, na kubainisha Msingi na Muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya **Pili** inachambua Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Taarifa za Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya **Tatu**, inaonesha Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iv) Sehemu ya **Nne,** inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati; na

(v) Sehemu ya **Tano**, inahitimisha, taarifa kwa kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Maji aliyoitoa mapema leo.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Kwa madhumuni ya taarifa hii, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** inahusika**.** Aidha, Masharti ya Kanuni ya 118 (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 yanazitaka Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Maji na Mazingira kuchambua Taarifa za Bajeti kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti hayo, tarehe 27-28 Machi, 2023, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa Msingi huo, ninaliomba Bunge lako Tukufu ipokee Taarifa hii na kuijadili sambamba na Hoja ya Waziri wa Maji iliyotolewa mapema hii leo.

## 1.3 Mawanda (Scope) ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji ina Fungu Moja **(Fungu 49).**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inafafanua Uchambuzi wa maeneo matatu ambayo ni, Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii katika Mikoa ya Shinyanga, Singida, na Manyara. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo kama ifuatavyo: -

**a) Upanuzi wa Mradi wa Maji wa Kagongwa – Isaka**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 jumla ya **Shilingi Bilioni 4.256** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Mradi wa Maji wa Kagongwa – Isaka uliyoko Wilaya ya Kahama. Ujenzi wa Mradi huu ulianza tarehe 16 Machi, 2022 na ulikusudiwa kukamilika mwezi Machi, 2023. Mradi huu unajengwa na Kampuni ya PNR Services Ltd ya Dar es Salaam kwa fedha za nje kutoka Benki ya Dunia kupitia program ya Malipo kwa Matokeo (PForR).

**Mheshimiwa Spika,** kazi zilizofanyika mpaka sasa katika Mradi huu ni pamoja na; Ujenzi wa Matenki matatu ya kuhifadhia maji

yenye lita za ujazo 470,000 katika Vijiji vya Jana, Itogwanholo na Mwalugulu, Uchimbaji wa Mitaro na ulazaji wa bomba zenye kipenyo tofauti kuanzia Mm 32 hadi Mm 160 umbali wa Kilomita 37,108 kati ya Km 54,225 za Mradi wote na Ujenzi wa Vituo 31 vya kuchotea maji. Mradi umefikia asilimia 80.

**Mheshimiwa Spika,** kazi zinazoendelea katika Mradi huu ni pamoja na, Ukamilishaji wa matenki yote matatu; ufungaji wa viungio na bomba za kuingiza Maji kwenye Matenki, ujenzi wa ukuta na upakaji wa rangi, Uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba umbali wa Km 17,117 na Ujenzi wa Chemba za valves na usimikaji; gate valves, Washout na air valves, na Uunganishaji wa huduma ya Maji kwenye maeneo ya kuchukulia Maji (off take points Isaka na Mwalugulu).

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 15 Machi, 2023 Kamati ilipotembelea Mradi huu Mkandarasi alikuwa ameshalipwa kiasi cha **Shilingi 1,408,004,932.66 sawa na asilimia 33** ya Mkataba. Kamati ilielezwa kuwa Utekelezaji wa Mradi umefikia **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika, Mradi huu ukikamilika unatarajia** kuhudumia Wananchi wapatao **28,700** katika Vijiji vitano vya **Mwalugulu, Kilimbu, Jana, Butondolo na Itogwanholo**. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Maji Na. 5 ya mwaka 2019, Chombo cha Watoa Huduma ngazi ya Jamii (CBWSO) kimekwishaundwa kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa uendelezaji wa Mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliarifiwa kuwa hakuna changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Hata hivyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

i) Ucheleweshaji wa upatikanaji wa bomba za chuma kutokana na Kiwanda cha kuzalisha bomba za aina hii kuwa

kimoja tu ambacho ni Tanzania Steel Pipe (TSP), hivyo kusababisha kuchelewa kwa ukamilishaji wa Mradi; na

ii) Vijiji Viwili ambavyo viko jirani na Mradi wa Maji wa Kagongwa – Isaka kutopatiwa Maji.

**b) Mradi wa Maji katika Miji ya Tinde na Shului**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Upanuzi wa bomba la Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Tinde – Igunga –Tabora na Shelui Singida na Vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba Kuu linalopeleka Maji katika Miji hiyo tarehe 15 na 16 Machi, 2023. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 24.94** fedha kutoka Exim Benki ya India.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mradi huu umefikia **asilimia 99** ambapo kwa sasa upo katika muda wa matazamio. Aidha, Wananchi wapatao **108,000** wanatarajia kunufaika na Mradi huu katika Miji ya Tinde na Shelui pamoja na Vijiji 34 ambapo Vijiji 22 vipo Tinde na Vijiji 12 vipo Shelui.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uzinduzi wa Mradi huu pamoja na namna anavyofuatilia na kuhakikisha kwamba lengo la Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kumtua Mama ndoo kichwani linatekelezwa.

**c) Ujenzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Ziba kwenda Nkinga**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa maji wa Ziba – Nkinga unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 5.349,328,135.14,** fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Program ya lipa kwa Matokeo

(PforR) kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Vijiji Tisa.
Mradi unatekelezwa na Mkandarasi Helpdesk Engineering Tanzania Limited na kusimamiwa na Watalaam wa RUWASA.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusisha ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa Kilomita 21.4, ujenzi wa Ofisi ya watumia maji (CBWSO) kwa ajili ya uendeshaji wa Mradi na ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuchotea maji. Kamati iliarifiwa kuwa Utekelezaji wa Mradi ulianza tarehe 18 Aprili, 2022, na unatarajia kukamilika tarehe 31 Machi, 2023. Hadi Machi 2023 utekelezaji wa Mradi ulifikia **asilimia 85**. Aidha, Wananchi wapatao **29,780** watanufaika na Mradi huu, hivyo kupunguza adha ya Maji kwa Wananchi wa Vijiji Tisa (9) vya Nkinga, Njiapanda, Ikunguipina, Kitangili, Barazani, Ulaya Ndembezi, Mwanzelwa na Itulashilanga.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa baada ya Awamu ya kwanza kukamilika, utekelezaji wa Awamu ya pili utaendelea ambapo itahusisha Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Maji katika Vijiji vyote vya Mradi kwa kujenga Matenki manne yenye ujazo wa jumla ya Lita 450,000, kulaza bomba lenye urefu wa Km 48.6, na kujenga Vituo 37 vya kuchotea Maji.

**d) Mradi wa Maji Orkesumet Wilaya ya Simanjiro**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mradi huu unalenga kupunguza tatizo la maji kwa Wananchi wa Mji wa Orkesumet ambalo limedumu kwa muda mrefu. Chanzo cha Maji ya Mradi wa Orkesumet ni kutoka Mto Pangani (Ruvu) na unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazozalisha Mafuta (OPEC Fund for International Development – OFID) kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 41.50**. Mradi huu ulikamilika tangu tarehe 30 Agosti, 2022 kwa asilimia 100 na

tayari Wananchi wapatao **52,000** na Mifugo wanapata huduma ya majisafi na salama.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu umetekelezwa kwa Awamu mbili. Awamu ya kwanza ya Mradi inahusu mapitio ya usanifu wa awali na kuandaa makabrasha ya Zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mradi yalifanyika na kukamilika mwezi Agosti, 2015. Awamu ya pili ya ujenzi wa Mradi imegawanyika katika vipande viwili (Lot I na Lot II). Kipande cha kwanza kilihusisha ujenzi wa Chanzo na Mtambo wa kutibu Maji, na kipande cha pili kinahusisha ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, kuhifadhi na kusambaza maji. Mkandarasi wa Vipande vyote viwili ni Jandu Plumbers Limited ya Arusha, chini ya usimamizi wa Kampuni ya Shoura Consultant Co. Ltd ya Jamhuri ya Watu wa Sudan ikishirikiana na Interconsultant ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kazi zilizofanyika katika Mradi huu ni pamoja na:

a) Usanifu na ujenzi wa Miundombinu ya chanzo yenye uwezo wa kuchukua maji mita za ujazo 7,500 kwa siku,

b) Ujenzi wa Mtambo wa kutibu maji wenye uwezo wa kuzalisha maji safi na salama Mita za ujazo 6,720 kwa siku;

c) Ujenzi wa njia yenye urefu wa Kilomita 2.5 kutoka kwenye chemba hadi kwenye mtambo wa kutibu maji.

d) Ujenzi wa nyumba sita za Watumishi;

e) Ununuzi na ujenzi wa bomba kuu Kilomita 36.5 lenye kipenyo cha Milimita 400,

f) Ujenzi wa Vituo vitatu vya kusukuma maji

g) Ujenzi wa Matenki mawili ya Mita za Ujazo 1600

**e) Mradi wa Maji Safi Dareda- Singu –Sigino – Bagara**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara, kwa gharama ya **Shilingi 12,724,407,807.85,** hadi mwezi Februari, 2023 kiasi cha **Shilingi 3,396,882,500** kilitumika na Mabomba yenye gharama ya takriban **Shilingi Bioni 8** yapo eneo la Mradi na fedha ya kulipia ipo.

**Mheshimiwa Spika,** Kitu cha kujivunia katika mradi huu ni kwamba unatekelezwa kwa fedha za ndani kwa **asilimia 100** na kusimamiwa na Watanzania (BAWASA). Mradi unajengwa kwa force akaunti hivyo, Serikali imeokoa zaidi ya **Shilingi Bilioni 15** kutoka gharama za awali zilizokadiriwa kutumika kiasi cha **Shilingi Bilioni 27** kwa ubora ule ule**.**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mradi ulianza mwezi Novemba, 2021na ulitarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja, hata hivyo haukuweza kukamilika kutokana na changamoto ya zuio kutoka kwa Viongozi na Wananchi wa Kata ya Ayalagala juu ya matumizi ya chanzo cha maji cha mto Endala kilichopo Bacho. Kamati ilielezwa kwamba changamoto hii ilitatuliwa na Waziri wa Maji kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara hivyo Mradi unaendelea na umefikia asilimia 80 na utakamilika mwezi Juni 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa faida/manufaa ya Mradi huu ukikamilika ni pamoja na:-

a) Zaidi ya wakazi 82,000 watanufaika na huduma ya majisafi na salama;

b) Kuondoa kero ya maji chumvi kwa wakazi wa Kata ya Bagara na Hospitali ya Mkoa wa Manyara;

c) Kupunguza gharama za uendeshaji kutokana na kuwa na chanzo kimoja kikubwa *(Centralized*);

d) Kupunguza magojwa ya mlipuko na gharama za matibabu.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Maji, Kamati ilipokea taarifa za Utekelezaji wa Miradi na kuona hali halisi uwandani (*in the field*) kwa Miradi iliyotembelewa. Kwa ujumla, Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa Miradi hii, hata hivyo, Kamati inaona kuwa ipo haja ya Serikali kuwashirikisha Wananchi kabla ya kuweka Mradi ili waweze kuwa sehemu ya Mradi. Hii itasaidia kuondoa migogoro baina ya Serikali na Wananchi wa eneo husika, lakini pia itasaidia kuleta tija iliyokusudiwa na kuwawezesha kuilinda, kuitunza, kuisimamia na kuifanya kuwa endelevu.

### 2.2.1 Yaliyobainika kwenye Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Ukaguzi wa Miradi hiyo yamebainisha mambo yafuatayo: -

a) Kwa ujumla hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa kwa mujibu wa Mpango kazi ni wa kuridhisha;

b) Kuchelewa kwa upatikanaji wa mabomba ya chuma kunachelewesha utekelezaji wa Miradi

c) Serikali ikitoa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge, Miradi itatekelezwa na kukamilika kwa wakati;

d) Watalaam wa Uhandisi wa Maji kutoka Chuo cha Maji wameonesha uwezo mkubwa endapo watapewa fursa na kutumiwa vizuri na Serikali. Hali hii imedhihirika katika Mradi wa Maji Dareda-SinguSigino- Bagara. Ni maoni ya Kamati kwamba Serikali itoe motisha kwa Watalaam wanaofanya kazi vizuri na kwa uzalendo.

e) Kuna haja ya Wizara ya Maji kuendelea kujitangaza ili kazi nzuri inayofanywa na Wizara iweze kujulikana kwa Wananchi;

f) Ushirikishwaji wa Wananchi katika Miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao, ni muhimu kwani unasaidia kuzuia mkwamo unaoweza kuchelewesha utekelezaji na tija ya Mradi.

g) Baadhi ya maeneo yanayopitiwa na Mradi kutopata maji;

h) Ni muhimu Wananchi wa endelee kupatiwa Elimu juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji;

i) Baadhi ya Wananchi Vijijini kushindwa kumudu gharama za kulipia maji.

**2.2.2 Maoni kutokana na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kutokna na yaliyobainika katika Miradi ya Maendeo iliyotembelewa, Kamati ina maoni yafuatayo:-

a) Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi katika Miradi ya Maji. Aidha, Kamati inampongeza Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso na Watendaji wote wa Wizara kwa kutekeleza Miradi kwa ubora unaolingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

b) Serikali iharakishe upatikanaji wa bomba za chuma zinazohitajika katika Mradi wa Kagongwa – Isaka ili ahadi ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2020 Ibara ya 100 Ukurasa 149 ya kufikisha huduma ya Majisafi na salama asilimia 85 Vijijini na asilimia 95 Mijini ifikapo 2025 inatimia;

c) Wizara ya Maji iendelee kuwatumia Watalaamu wa ndani kutekeleza Sera ya kuwatumia Wakandarasi wa Kitanzania katika Utekelezaji wa Miradi ya maji, kwa kuwa wale waliopewa Miradi hiyo wameonesha uwezo mkubwa wa kiutendaji.

d) Wananchi ambao ndio wanufaika na mradi husika wakishirikishwa vizuri katika hatua zote za mradi kuanzia kuibua, kupanga, na utekelezaji wa miradi tija iliyokusudiwa hupatikana. Ni mtazamo wa Kamati kuwa Serikali itaendelea kuwahusisha na kuwashirikisha Wananchi inavyostahili katika uibuaji, upangaji na utekelezaji wa Miradi ya maji;

e) Elimu kwa Umma kuhusu ulinzi, utunzaji wa Mazingira na vyanzo vya Maji uendelee kutolewa;

f) Wizara na Watalaamu wake waendelee kushirikiana na Wananchi ili kuhakikisha kuwa kasoro ndogondogo zilizozopo katika Utekelezaji zinapatiwa ufumbuzi na kuboreshwa. Kwa kufanya hivyo Miradi hii itakuwa endelevu.

g) Vijiji ambavyo Miradi imepita vipatiwe Maji kwanza kwani hawa ndiyo walinzi wa kwanza wa rasilimali za maji;

h) Miradi ya maji inaligharimu Taifa fedha nyingi za walipa Kodi. Ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya maji, na kuifanya iwe endelevu, Serikali ione umuhimu wa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha usalama wa miundombinu hiyo.

i) Vyombo vya Watoa Huduma ngazi ya Jamii vione namna ya kuwasaidia Wananchi wasio na uwezo wa kulipa gharama kupata maji.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, tarehe 27 na 28 Machi, 2023. Uchambuzi katika sehemu hii imejikita kwenye maeneo yafuatayo: -

a) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji katika Bajeti ya 2022/2023;

b) Ukusanyaji wa Maduhuli na;

c) Utekelezaji wa Bajeti ikilinganishwa na Upatikanaji wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la Uchambuzi ni kuliwezesha Bunge kupata ulinganisho utakaosaidia katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Ulinganisho huo unafanyika kwa njia ya asilimia, na Vielelezo, ili kubainisha taswira ya mlingano uliopo.

### 2.3.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2022/2023, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo

Tisa (9). Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mfano wa Ushauri uliozingatiwa unahusu Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kimkakati zinapatikana inavyostahili. **Utekelezaji ulioripotiwa unaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2023, Serikali ilitoa asilimia 77.2 ya Bajeti ya fedha za ndani za Maendeleo.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya Ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo, ni rai ya Kamati kwamba Serikali iendelee kutekeleza kikamilifu na kwa haraka maeneo ambayo utekelezaji wake umefanyika kwa kiwango cha chini. Mfano wa Ushauri huo ni Serikali kuongeza juhudi za kuwaelimisha Wananchi kutumia utaratibu wa kuvuna maji ya mvua wakati wa majira ya mvua ili yasaidie wakati wa kiangazi.

### 2.4 Uchambuzi wa Ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Maji **(Fungu 49)** iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,200,001,000.00** kutokana na mauzo ya Nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya Leseni kwa Makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji na Ada kwa huduma za Maabara. Hadi mwezi Februari 2023, Wizara ilikusanya kiasi cha **Shilingi 772,666,497.00** sawa na **asilimia 64.4** ya lengo. Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2023 ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 1**

**Kielelezo Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2023**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2022/2023 | MAKUSANYO HADI FEBRUARI,2023 | ASILIMIA YA LENGO |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Nyaraka | 1000.00 | 00 | 00 |
| Malipo ya Leseni kwa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji | 250,000,000.00 | 183,103,382.00 | 73.24 |
| Ada kwa huduma za Maabara. | 950,000,000.00 | 589,563,115.00 | 62.06 |
| **JUMLA** | **1,200,001, 000.00** | **772,666,497.00** | **64.4** |

**Chanzo: Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** uchanganuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

**a)** Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Wizara ya Maji kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa Bajeti **ni asilimia 64.4** ya lengo la mwaka. Hali hii inahitaji msukumo wa Serikali ili lengo la Makusanyo ya Maduhuli lifikiwe ifikapo Juni 2023;

**b)** Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji ulifikia asilimia **73.24**. Hali hii ni dalili nzuri kwamba Wizara itaweza kufikia lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kutokana

na chanzo hicho ifikapo mwezi Juni, 2023. Vile vile hali hiyo, inaonesha kwamba, upangaji wa lengo ulifanyika kwa uhalisia;

**c)** Mwenendo wa ukusanyaji Ada kwa Wateja wanaopata huduma za Maabara za ubora wa maji ulifikia **asilimia 62.06.** Hali hii inatia shaka iwapo Wizara itaweza kufikia lengo la makusanyo ifikapo mwezi Juni, 2023**.** Hata hivyo, mwenendo huu unaashiria kuwa iwapo huduma za Maabara zitaboreshwa na kusimamiwa ipasavyo, makusanyo ya Maduhuli yanaweza kuongezeka, hivyo kufikia lengo lililokusudiwa.

**d)** Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia hali halisi ya ukusanyaji wa Maduhuli katika mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, uwekezaji wa kutosha katika Leseni za Kampuni za Utafiti na Uchimbaji wa Visima vya Maji utachangia kuongeza Mapato ya Serikali, na hivyo kuleta tija iliyokusudiwa kwa Wananchi. Aidha, huduma za Maabara za ubora wa maji zikiboreshwa na kusimamiwa ipasavyo zinaweza kufikia lengo lililokusudiwa ifikapo mwezi Juni, 2023. Ni maoni ya Kamati kwamba Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yapangwe kulingana na uhalisia wake ili kuweza kufikia malengo. Aidha, msukumo zaidi unahitajika ili kufikia lengo lililokusudiwa kwa mstakabali wa Wananchi.

## 2.5 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2022/2023

### 2.5.1 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa Mipango na majukumu ya Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Ili kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa Bajeti hiyo, Kamati ilidadisi utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika maeneo Makuu matatu ya Sekta ya Maji. Maeneo hayo ni: -

a) Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji;

b) Huduma ya Maji safi na usafi wa mazingira Vijijini na Mijini;

c) Uratibu na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi katika Sekta ya maji ni pamoja na: -

a) Kukamilika kwa jumla ya Miradi 420 ya maji ambapo ya Vijijini ni 382 na Mijini ni Miradi 38;

b) Kuzinduliwa kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Tatu na;

c) Kuanza kutumika rasmi kwa Mfumo wa Pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji (Unified Billing System) kwa Mamlaka 80 za Maji na Usafi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utekelezaji huo, Kamati inampongeza kwa dhati Mhe. Juma Awesso (Mb) Waziri wa Maji pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Eng. Nadhifa Kemikimba kwa usimamizi madhubuti wa utawala bora na kizalendo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, zipo changamoto zilizopelekea kuchelewa kwa Utekelezaji wa Miradi ya Maji. Changamoto hizo ni pamoja na;

a) Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi. Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imepewa siku sitini (60) kushughulikia maombi ya misamaha ya Kodi. Utaratibu huo uliowekwa kisheria unaathiri kwa kiasi fulani, utekelezaji wa Miradi ya maji. Athari hiyo inachelewesha upatikanaji wa huduma za Maji kwa Wananchi;

b) Upungufu wa Wataalam wa Kada mbalimbali. Kwa sasa Sekta ina Watumishi **9,422** ambapo mahitaji ni Watumishi **10,276** hivyo kuwa na nakisi ya Watumishi **854.** Hali hii inapunguza ufanisi katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa Miradi ya Maji.

c) Mahitaji makubwa ya fedha za kutekeleza Miradi ya maji. Uwekezaji kwenye Miradi ya Maji unahitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja, lakini upatikanaji wa fedha umekuwa si kwa kasi iliyokusudiwa. Kwa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati kama vile Bwawa la Kidunda, Farkwa na Ndembera/Lugoda umechukua muda mrefu kuanza kutekelezwa kutokana na kuhitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja wakati upatikanaji wa fedha hizo umekuwa si kwa kasi iliyokusudiwa. Hali hiyo

imesababisha Miradi hii kuchukua muda mrefu kuanza kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kwamba, ili ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati kama Bwawa la Kidunda, Ndembera na Farkwa uweze kuanza kuna haja ya kuweka Mkakati maalumu/madhubuti wa kupatikana kwa fedha kwa ajili hiyo. Vinginevyo, kuna hatari ya kuwa na Mipango kila mwaka isiyokelezeka hivyo kushindwa kukidhi matarajio ya Wananchi.

### 2.5.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Maji **Fungu 49** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 657,899,338,000** kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kati ya fedha hizo **Shilingi 407,064,860,000** sawa na **asilimia 61.87** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,834,478,000** sawa na **asilimia 38.13** ni fedha za nje. Hadi mwezi Februari 2023, jumla ya Shilingi **542,789,767,774.55** sawa na **asilimia 82.5** ya fedha zote za Bajeti ya Maendeleo zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 314,228,279,947.31** sawa na **asilimia 77.2** ni fedha za ndani na **Shilingi 228,561,487,827.24 sawa na asilimia 91.12** ya Bajeti ya fedha za Maendeleo za nje. Kwa upande wa fedha za nje, utaratibu wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji unafanyika kwa kutumia namna mbili ambazo ni kutoka kwa wadau mbalimbali kupitia katika mfumo wa Exchequer na baadhi ya Washirika wa Maendeleo kulipa moja kwa moja (Direct to project funds) wakandarasi na wataalam washauri na baadae malipo hayo hutambuliwa kwa kuingizwa kwenye mfumo wa exchequer. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,063,444,078.17** zimetolewa kupitia exchequer na **Shilingi 225,498,043,749.07** zimelipwa moja kwa moja kwa Wakandarasi na Wataalam Washauri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Uchanganuzi zaidi unaonekana katika **Kielelezo Na.2**

**Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti na kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo hadi Februari, 2023**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2022/2023 | | FEDHA ILIOPOKELEWA HADI FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 407,064,860,000.00 | 314,228,279,947.31 | **77.2** |
| **FEDHA ZA NJE** | 250,834,478,000.00 | 228,561,487,827.17 | **91.1** |
| **JUMLA** | 657,899,338,000.00 | 542,789,767,774.48 | **82.5** |

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti katika **Kielelezo Na. 2** unaonesha kuwa: -

a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili kugharamia Miradi ya Maendeleo inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ulifikia **asilimia 82.5** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. **Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati ni kiashiria kwamba Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa itakamilika kama ilivyokusudiwa ifikapo Juni, 2023;**

b) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **aslimia 77.2** ya Bajeti iliyoidhidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. **Hali hii inaonesha dhamira nzuri ya Serikali ya kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na kuhakikisha kuwa Wananchi wananufaika na Miradi hii na kuondokana na kero za kukosa maji**.

c) Kwa upande wa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka nje upatikanaji wake ni **asilimia 91.12** ya Bajeti iliyoidhinidhwa

na Bunge kwa ajili hiyo. **Hali hii inaonesha kwamba Bajeti iliyopangwa ni halisia na inaonesha ushirikiano wa dhati wa Washirika wa Maendeleo wa kutoka nje.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa wakati na hivyo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 ya kuona kwamba nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kuimarisha huduma ya Majisafi na Salama na kuwafikia Wananchi kama ilivyokusudia na Ilani hiyo. **Ni rai ya Kamati kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kitatolewa mapema kabla ya mwezi Juni ili Miradi iweze kukamilika kwa asilimia 100.** Aidha, ni matarajio ya Kamati kuwa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha 2022/2023 utafaa kutumika katika upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ili miradi itakayokuwa imepangwa kutekelezwa ikamilike kwa wakati.

### 2.5.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Fungu 49 liliidhinishiwa Shilingi **51,462,260,600.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 34,761,735,600** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na wa Chuo cha Maji, na **Shilingi 16,700,534,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia mwezi Februari 2023, fedha zilizotolewa ni **Shilingi 33,755,442,884.71** sawa na **aslimia 65.6** ya Bajeti yote ya Matumizi ya Kawaida. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na kupokelewa hadi Februari, 2023**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2022/2023 | | FEDHA ILIYOPOKELEWA HADI FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA MISHAHARA** | 34,761,735,600.00 | 25,103,893,918.15 | **72.2** |
| **FEDHA ZA OC** | 16,700,534,000.00 | 8,651,548,966.56 | **51.8** |
| **JUMLA** | **51,462,260,600.00** | **33,755,442,884.71** | **65.6** |

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi katika kielelezo hiki unaonesha kwamba utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaidi ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za uimarishaji wa huduma za Maji Mijini na Vijijini hadi kufikia mwezi Februari 2023, ni **asilimia 65.6** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Upatikanaji huo wa fedha uko chini ukilinganishwa na kiasi kilichopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hiki ambao ni **asalimia 66.6.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo na Vipaumbele

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Malengo na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, vinaendana na majukumu ya Msingi ya Wizara ya Maji, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Awamu ya Tatu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano wa mwaka 2021/22 – 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya

mwaka 2030; na ahadi mbalimbali za Viongozi wa Kitaifa. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009 na maboresho yake ya mwaka 2022; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 pamoja na Kanuni zinazoelekeza utekelezaji wa Sheria hizo. Wizara imepanga kutekeleza kazi katika maeneo yafuatayo: -

a) Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
b) Usimamizi wa ubora wa maji;
c) Usambazaji wa Majisafi Vijijini;
d) Usambazaji wa Majisafi na usafi wa Mazingira Mjini na;
e) Kuimarisha Uwezo wa Kitaasisi.

## 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024

### 3.2.1 Makadirio ya Maduhuli yatakayokusanywa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Maji (Fungu 49) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 1,200,001,000,** kutokana na vyanzo vya mauzo ya Nyaraka za Zabuni, Leseni kwa Kampuni za Utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, Tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma ya maabara za ubora wa maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilifanya ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Maduhuli yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoisha. Uchanganuzi wa ulinganisho huo unaonekana katika **Kielelezo Na. 04**.

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Maduhuli yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| CHANZO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2022/2023 | MAKUSANYO HALISI HADI MWEZI FEBRUARI, 2023 | % LENGO | MAKADIRIO YA MADUHULI 2023/2024 | % ONGEZEKO/PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mauzo ya Nyaraka za Zabuni** | 1,000.00 | 00 | 0 | 1,000.00 | **0** |
| **Leseni za Kampuni za Utafiti** | 250,000,000.00 | 183,103,382.00 | 73.2 | 250,000,000.00 | **-** |
| **Ada - Huduma za Maabara** | 950,000,000.00 | 589,563,115.00 | 62.06 | 950,000,000.00 | **-** |
| **JUMLA** | **1,200,001,000.00** | **772,666,497.00** | **64.4** | **1,200,001,000.00** | **-** |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa: -

(i) Lengo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka 2023/2024 halijaongezeka, kiasi kilichopangwa kukusanywa mwaka wa fedha unaoisha ndio kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka huu wa fedha.

(ii) Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Lengo la Mwaka wa Fedha unaoisha ni wa chini ikilinganishwa na lengo kwa robo tatu ya mwaka ambapo ilipaswa kuwa **asilimia 66.6;**

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli kutokana na Leseni za Kampuni za Utafiti ni **asilimia 73.2**

(iv) Makadirio ya Mapato kutokana na ada za huduma ya Maabara za ubora wa maji ni **asilimia 62.06**. Ulinganisho umeonesha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa ada hizo hadi mwezi Februari 2023 siyo wa kuridhisha. Hali hiyo inaonesha mashaka iwapo kiasi kinachokadiriwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kinaweza kupatikana. Ni rai ya Kamati kwamba juhudi za makusudi zifanyike ili kiasi kilichokadiriwa kiweze kukusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, lengo la Ukusanyaji wa Maduhuli linahitaji usimamizi wa kutosha wakati wa utekelezaji ili kufikia malengo yaliyowekwa.

**3.2.2 Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024,**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maji (**Fungu 49)** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 756,205,106,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 60,375,474,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 695,829,632,000** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. kati ya fedha hizo za Maendeleo **Shilingi 407,064,860,000** sawa na **asilimia 59** ni fedha za ndani na **Shilingi 288,764,772,000** sawa na **asilimia 41** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba Fedha za maendeleo zinazoombwa ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya kipaumbele. Miradi hiyo ni pamoja na: -

a) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda na Miradi ya Maji Vijijini;

b) Miradi na kazi zinazohusu Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali za Maji ikiwemo ujenzi na ukarabati wa Mabwawa,

c) Uboreshaji wa huduma za ubora wa maji ikiwemo kujenga uwezo wa Maabara za Maji na;

d) Kujenga uwezo wa Taasisi na Watumishi.

**Kielelezo Na. 5: Mchanganuo wa Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Fungu 49 unabainishwa kwenye Kielelezo Na. 5**

| MCHANGANUO | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA | | ASILIMIA YA BAJETI YOTE |
|---|---|---|---|
| **FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA** | Mishahara | 42,339,913,000 | 5.6 |
| | OC - | 18,035,561,000 | 2.4 |
| **JUMLA NDOGO** | | **60,375,474,000** | **8** |
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | Fedha Ndani | 407,064,860,000 | 59 |
| | Fedha za Nje | 288,764,772,000 | 41 |
| **JUMLA NDOGO** | | **695,829,632,000** | **92** |
| **JUMLAYA BAJETI YOTE** | | **756,205,106,000.00** | **100** |

**Chanzo:** Randama Fungu 49, Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

a) Kwa ujumla Bajeti ya Wizara ya Maji inayoombwa kwa ajili ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama ni ya kuridhisha.

Hata hivyo kutokana na majukumu makubwa ya Wizara hii ni mtazamo wa Kamati kwamba Bajeti hii haitoshi;

b) Bajeti ya Wizara ya Maji inayoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 92** ya Bajeti yote ya Wizara**,** Fedha ya ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 59.** Takwimu hizi zinaashiria kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo iliyopangwa kwa mwaka huu wa fedha. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha ya ndani kwa ajili ya Maendeleo. Ni Maoni ya Kamati kwamba kiasi hicho kitatolewa kama kilivyoombwa na kwa wakati hivyo kuimarisha huduma ya majisafi na salama na kuwafikia Wananchi wa Mijini na Vijijini.**

c) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika Utekelezaji wa Bajaeti inayoisha, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kupatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Mchanganuo na ulinganisho unaonekana katika **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2022/2023 na mwaka wa Fedha 2023/2024**

| MCHANGANUO | Aina ya Matumizi | FEDHA ILIYOIDHINISHWA 2022/2023 | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA 2023/2024 | ONGEZEKO / PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | **MISHAHARA** | 34,761,735,600 | 42,339,913,000 | **7578177400.00** | **22** |
| | **OC** | 16,700,534,000.00 | 18,035,561,000 | **1,335,027,000.00** | **8** |
| | **JUMLA NDOGO** | **51,462,269,600.00** | **60,375,474,000** | **8,913,204,400.00** | **17.3** |
| **MATUMIZI YA MAENDELEO** | **Fedha za ndani** | 407,064,860,000 | 407,064,860,000 | **-** | **-** |
| | **Fedha za nje** | 250,834,478,000 | 288,764,772,000 | **37,930,294,000.00** | **15.1** |
| | | **657,899,338,000** | **695,829,632,000** | **37,930,294,00.00** | **6** |
| **JUMLAYA BAJETI YOTE** | | **709,361,607,600** | **756,205,106,000.00** | **46,843,498,400.00** | **7** |

**Chanzo:** Randama Fungu 49, Wizara ya Maji

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa: -

(i) Makadirio ya Bajeti yote ya Wizara ya Maji yameongezeka kwa **asilimia 7** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(ii)

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo yameongezeka kwa **asilimia 6** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. **Ni mtazamo wa Kamati kwamba ongezeko hilo la Bajeti ya Maendeleo litafanikisha utekeezaji wa Miradi iliyopangwa kwa mwaka 2023/2024;**

(iv) Mkadirio ya Matumizi ya shughuli za Kawaida yameongezeka kwa **asilimia 17.3. Hali hii inaashiria kwamba shughuli za usimamizi na uendashaji wa Shughuli za uendelezaji wa rasilimali za maji zitasimamiwa kwa ukamilifu.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imeridhika kwamba Bajeti hii imezingatia azma ya Serikali iliyotamkwa katika Ibara ya 100, Ukurasa wa 149 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Azma hiyo ni kuona kwamba, nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia Wananchi zaidi ya asilimia 85 Vijijini na 95 kwa Mijini ifikapo mwaka 2025. Ongezeko hilo la Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 linaakisi lengo hilo. Msistizo wa Kamati kwa Serikali ni kuhakikisha kuwa Bajeti inayoidhinishwa na Bunge inatekelezwa ipasavyo.

### 3.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 ili kubaini ongezeko/ pungufu la Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti ya Kuu ya Serikali.

Ulinganisho huo unaonekana kwenye **Kielelezo Na.7**

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maji dhidi ya Bajeti Kuu ya Serikali 2023/2024**

| MCHANGANUO | BAJETI KUU YA SERIKALI | BAJETI YA WIZARA YA MAJI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| OC | 6,396,900,000,000.00 | 18,035,561,000.00 | **0.3** |
| MISHAHARA | 10,882,126,000,000.00 | 42,339,913,000.00 | **0.7** |
| DENI LA SERIKALI | 12,771,533,000,000. | - | **-** |
| **JUMLA NDOGO** | **29,232,100,000,000.00** | 60,375,474,000.00 | **0.2** |
| MAENDELEO NDANI | 11,873,894,000,000 | 407,064,860,000 | **3.4** |
| MAENDELEO NJE | 3,282,081,000,000 | 288,764,772,000 | **8.8** |
| **JUMLA NDOGO MAENDELEO** | **15,155,975,000,000.00** | **695,829,632,000** | **4.6** |
| **JUMLA KUU** | **44,388,067,000,000.00** | **756,205,106,000.00** | **1.7** |

**Chanzo:** Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Randama ya Wizara ya Maji 2023/20234

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Ulingansho huo unaonesha kuwa: -

a) Bajeti ya Wizara ya Maji ni **asilimia 1.7** ya Bajeti Kuu ya Serikali. Hali hii inaashira kwamba kwa kiasi fulani Bajeti Kuu ya Serikali imezingatia umuhmu wa majukumu ya Wizara ya Maji;

b) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji ni **asilimia 4.6 ya** Bajeti Kuu ya Serikali ya Maendeleo ambayo ni **asilima 34.1**. Uchambuzi huo unaonesha dhamira ya Serikali ya kuendeleza na kuimarisha huduma ya Miundombinu ya Majisafi na salama nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mtazamo huo wa kimaendeleo katika Sekta ya Maji nchini. Uchanganuzi wa Takwimu hizi ni ishara ya hatua za kutimiza ahadi ya Serikali ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020 Ibara ya 100 Ukurasa wa 149 ya kuimarisha huduma ya majisafi na salama kwa Wananchi na kuwafikia wakazi asilimia 85 kwa Vijijini na asilima 95 kwa Mijini ifikapo mwaka 2025. Msisitizo wa Kamati ni Serikali kuendelea kuiwezesha Sekta hii kupata fedha kadiri inavyoidhinishiwa na Bunge.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji –Fungu 49 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba kubainisha Maoni ya Kamati ambayo yamezingatia changamoto zinazoikabili Sekta ya maji. Changamoto hizo ni pamoja na: -

a) Mahitaji makubwa ya fedha za kutekeleza Miradi ya maji;
b) Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi;
c) Upungufu wa Wataalam wa Kada mbalimbali;
d) Uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za binadamu, mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira; na
e) Uhaba wa maji kutokana na ongezeko la Idadi ya watu.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

a) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 82.5** ya fedha zote za Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge, upatikanaji wa fedha za ndani ni **asilimia 77.2** na fedha za nje ni **asilimia 91.1** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Hali hii inaleta matumaini kwa Kamati kwamba Miradi ya Maendeleo itakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa;

b) Kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maji katika kufanikisha azma ya kuwa na usalama wa maji na kuimarisha huduma ya majisafi na salama, pamoja na kuwafikia Wananchi zaidi ya asilimia 85 Vijijini na asilimia 95 Mijini ifikapo 2025 kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 inastahili pongezi;

c) Mipango mizuri ya kuendeleza Miradi ya Kimkakati ikiwemo Ujenzi wa Mabwawa ya Kidunda, Farkwa na Ndembera inahitaji fedha nyingi kuitekeleza;

d) Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Misamaha ya Kodi kwa ajili ya vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya maji ni kikwazo katika utekelezaji wa Miradi ya Maji;

e) Upungufu wa mabomba ya Chuma unachelewesha Utekelezaji wa Miradi ya Maji inayohitaji mabomba ya aina hiyo;

f) Upungufu wa Wataalam wa Kada mbalimbali katika Sekta ya Maji unakwamisha ufikiwaji wa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Chuo cha Maji ambacho ni hazina ya Watalaam wa Sekta ya Maji kinahitaji kuongezewa Bajeti ili kuzalisha Watalaam wa kutosha;

g) Changamoto ya upatikanaji wa uhakika wa huduma ya majisafi na salama katikaJiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Nchi, inahitaji Mkakati mahususi;

h) Hakuna Mkakati mahususi na wa uhakika wa uvunaji wa maji ya mvua;

i) Yapo malalamiko kutoka kwa Wadau wa Sekta ya Maji kwamba baadhi ya maeneo inapopita miundombinu ya kusafirisha maji hawapati huduma;

j) Kuna tofauti kubwa katika uwezo wa utendaji na ufanisi wa
Wafanyakazi wa Taasisi za Wizara ya Maji;

k) Kutokuwepo kwa Mpango Kabambe wa uendelezaji wa Sekta ya Maji na Grid ya Maji ya Taifa kunaathiri utoaji wa huduma ya Majisafi na salama nchini;

**4.2 Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na Maoni yaliyobainishwa hapo juu naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:

a) Serikali iendelee kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo ya Kimkakati zinapatikana inavyostahili. Aidha, Kutokana na uhitaji mkubwa wa fedha katika Miradi hii, Serikali iangalie namna ya kupata fedha kutoka vyanzo vingine ikiwemo, kuandika maandiko ya kutafuta fedha kwa Washirika wa Maendeleo;

b) Serikali iweke Mfumo mzuri utakaowezesha kuharakisha upatikanaji wa misamaha ya Kodi ili kufanikisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa wakati;

c) Wizara itafute ufumbuzi wa changamoto ya upungufu wa mabomba ya chuma ili kutokwamisha Miradi ya Maji;

d) Serikali iharakishe kuajiri Watalaam katika Sekta ya Maji ili kukabiliana na upungufu wa Watalam 854 katika Sekta hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha, Chuo cha Maji kiimarishwe kwa kutengewa fedha za kutosha katika Bajeti ili kuzalisha Watalaam wa wengi;

e) Ili kukabiliana na chagamoto ya upungufu mkubwa wa majisafi na salama katika Jiji la Dodoma Serikali iweke Mikakati madhubuti ya kupata maji kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya Uchimbaji visima na kuanza utekelezaji wa Mradi wa kutoa Maji kutoka Ziwa Victoria. Kuhusu Mradi wa kutumia maji ya Bwawa la Mtera kuhudumia Jiji la Dodoma, Kamati inashauri utafiti na tathmini ya kina ufanyike ili kubaini kama Mradi utakuwa endelevu na hautaathiri maslahi ya Wadau wengine;

f) Wizara kwa kushirikiana na Wadau wengine wa Maji iandae Mkakati mahususi na wa uhakika wa uvunaji wa Maji ya mvua. Mkakati huo uzingatie haja ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, usanifu wa majengo ya Umma, utengaji wa Bajeti kwa ajili ya uvunaji wa Maji na ujenzi

wa Mabwawa katika maeneo yenye mvua nyingi ili kulinda miundombinu ya Barabara na Reli.

g) Serikali iweke Sheria au Mwongozo utakaoelekeza Vijiji vinavyopitiwa na Miradi ya Maji kuwa wanufaika wa kwanza na Miradi hiyo;

h) Wizara iweke utaratibu wa Watalaam kutoka maeneo mbalimbali kutembeleana na kubadilishana uzoefu ili kuongeza ufanisi katika Miradi ya Maendeleo;

i) Wizara iandae Mpango Kabambe wa uendelezaji wa Sekta ya Maji (National Water Master Plan) pamoja na Grid ya Maji ya Taifa (National Water Grid) ili kuimarisha utoaji wa huduma ya Majisafi na salamanchini.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina pamoja na Maoni na Mapendekezo ya Kamati, naomba kuhitimisha hoja ya Kamati kama ifuatavyo: -

### 5.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, Maisha marefu na mafaniko katika utekelezaji wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hususan wakati wa Uchambuzi wa Bajeti. Hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wako tayari kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi wakati wowote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua na kuthamini umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ningetamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Maryam Omar Said, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Keneth Nollo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Joseph Kasheku Msukuma, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Jumah Aweso, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb), Katibu Mkuu Mhandisi Nadhifa Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Cyprian Luhemeja pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu bila kukwama. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, ndc, pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Angelina Langisi Sanga na Ndg. Nyamwanja Chipanda Chilemeji kwa Ushauri, Uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson Gedion Kiswaga (Mb),
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA.**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa sasa tunaingia kwenye awamu ya kuchangia na atakaechangia wa kwanza ni Mheshimiwa David Kihenzile, ajiandae Profesa Kitila Mkumbo, ajiandae Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae Mheshimiwa Paresso.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa ya kunipa nichangie wizara hii, kwa sababu pia ni wizara yangu ya kwanza kuchangia. Moja nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri lakini pia aina ya uwasilishaji ambao unavutia. Sisi sote tunafahamu kwenye maji yako mambo manne la kwanza tunajadili rasilimali, la pilli tunajadili uwezo wa kusambaza maji hayo, la tatu tunajadili hali ya maji taka na la nne tunajadili ubora wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kabla sijaanza huko, nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Amefanya mapinduzi makubwa kwenye sekta hii ya maji na hapa imeelezwa mambo aliyoyafanya sitoweza kusoma moja moja. Lakini amekamilisha miradi 1373, amekamilisha miradi kwenye miji 80 inayokwenda kuhudumia watu 4,000,000 lakini zaidi ya yote ametusaidia miradi vichefuchefu ikiwemo kule kwangu Sawala Mufindi Miradi 157 kati ya 177, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa usimamizi wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona mchakato wa miradi Miji 28 ambayo na Mafinga, Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Mufindi kwa Ndugu yangu Chumi unakwenda kuanza, hongereni sana Wizara. Lakini pia tumeona asilimia imefika asilimia 77 kwenye maji vijijini ambapo kimsingi ndiko ninakotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti *water utility performance review report for the financial* year ya mwaka 2021/2022 imejielekeza katika mambo mbalimbali kwa kina yameainishwa mle ndani. Naomba nisome kakipande kadogo sana anaesema *during financial year*... nitaitafsiri katika Mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 uzalishaji wa maji uliongezeka kwa asilimia 1.2 lakini *in stored water production capacity* uwezo ulikwenda mpaka asilimia 2.6 lakini upande wa pili mahitaji ya maji yaliongezeka mpaka kufika asilimia 9.8 kulinganisha na mwaka uliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo hoja zangu mbili zinapokwenda kuibuka.tunafahamu Taifa letu, tuna fursa nyingi ambazo tunazo na pengine kabla sikufika huko nimalizie kushukuru kwenye upande wa Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri, sina deni na wewe nakushukuru sana wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji hususani wa kinamama wale viongozi wangu meneja kwenye wilaya na mkoa kwa kazi kubwa ambayo mmenifanyia katika mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote niliyotamani kusema leo nitegemee niongee kwa bashasha nije na takwimu umenifilisi. Ninachokuombe kheri, naomba ukaitekeleze ikafanyike kwa ufanisi mwaka jana ulianza Mradi wa Igowole nilikuomba ufanye *extension* isiishie Mkalala, Ikwega na Igowole nimeona hapa unapeleka mpaka Itulituli, Kihanga, Mninga, Kisasa, Kidatu, Uvizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza juu ya umuhimu wa Kata ya Mtambula nimeona umeiweka humu ndani kwenye maji mwaka huu. Nimezungumza kuhusu mradi wa vijiji vya Sambalamaziwa nimeviona humu ndani, japo sijaona Iramba na Kindegebasi nitaomba utuongezee hapo pamoja na Namkangu kule Idunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Malangali niliulizia sana mwaka jana leo Mheshimiwa Tendaga amezungumzia, nimeoa amuweka hapa leo pia, mradi wa Itika – Horo na Idete nimeona pia umeukumbuka. Kwa ujumla maeneo karibu yote ambayo tulikubaliana umeyaweka kwa hiyo, kama mchangiaji wa kwanza pia sishiki shilingi yako, nakuombea kheri ukatekeleze Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwako na Wizara yako, kuna changamoto kubwa sana na uchelewaji wa kuanza kwa miradi. Sisi Mikoa yetu mitatu tulikuwa na afisa manunuzi mmoja haiwezekani vijana wako wengi mtaani hawani kazi kwa nini mtu mmoja apewe jukumu la miradi yote hiyo? Lazima mkarekebishe hili mwaka wa fedha unaofuatia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili kwa Mheshimiwa Waziri ni moja tu ni uanzishwaji wa Gridi ya Taifa ya Maji. Kabla sijasema hiyo nikuombe nendeni mkarekebishe Sera ya Maji ya 2002 imepitwa na wakati. Hatuwezi kutumia sera ya miaka 10 iliyopita, miaka 20 iliyopita wakati muda umepita ebu karekebisheni, tusaidieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye hoja dhidi ya maji ya Taifa, Taifa letu lina bahati kubwa sana hapa umetuambia mvua zinanyesha kwa wastani milimita 1,000 kwenda mbele, hapa tumeelezwa tuna maji ya bahari, tuna Ziwa Victoria, tuna Tanganyika, tuna Nyasa. Katika Ziwa Victoria sisi kama moja ya watu wenye *majority shares* zaidi ya *utilization* kubwa inafanywa na wenzetu wa Kenya sisi tupo tunaangali. Mikoa jirani tunaambiwa hapa jana kwamba ina changamoto ya ukame na itakosa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanganyika sisi tuna *majority share* kwenye ziwa lile lakini tunao mradi mmoja tu maji nenda

Nyasa maji yake yanafaa kwa kunywewa na mwanadamu hakuna mradi hata mmoja, acha maji ya mvua Mheshimiwa Waziri wakati umefika wa kutekeleza kuanzisha gridi ya maji tukusanye maji yote ya nchi hii yaingizwe ndani tuweke ma–*pipe* makubwa yasambaze maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nchi yetu katika nchi zenye *highest pick* Afrika, Tanzania ni moja wapo tunakwama wapi? Umetueleza mahitaji ya maji kwa sasa ni takribani bilioni 60 lita za ujazo, ume–*project* miaka 20 ijayo 2035 tutakuwa na bilioni 80 na wakati huo *capacity* ya maji tulizonazo ni 126 bilioni. Je, hayo mahitaji 2035 tutapata wapi maji? lazima twende tukaanzishe gridi ya Taifa ya maji kama ilivyo gridi ya Taifa ya umeme ili tuweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashe jana amekuja hapa na hoja ya *irrigation*, gridi ya Taifa ndiyo mkombo. Tutapata maji kwenye viwanda, tutapata maji ya kilimo, tutapata maji kwenye uvuvi, maji ya wanyama pori, maji ya kunywa na kadhalika Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika mambo takayoyazungumza ambayo nategemea mwisho wa siku…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Ahsante Kengele ya pili.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkumbo, jiandae Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwanza nianze kwa kutangaza maslahi kwenye Wizara hii siyo maslahi yale ya kikanuni maslahi ya kifedha ni

ukweli kwamba nilipata bahati ya kutumikia Wizara hii kama Katibu Mkuu kwa miaka mitatu na nusu na kwa nafasi hiyo nilifanya kazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Jumaa Aweso. Kwanza aitwi Juma anaitwa Jumaa Hamidu Aweso nilimpokea pale nataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nithibitishe kwamba Waziri huyu ni mtu makini, ni mzalendo sana, ni mchapakazi, ni mnyenyekevu lakini muhimu sifa za ziada ambazo siyo lazima uziseme na kazi yake ni mcheshi, ni mchangamfu sana na watu waliyofanya kazi Wizara ya Maji wanafahamu kwamba anafahamu kiswahili vizuri ndiyo maana katika hotuba yake zimejaa methali za kiswahili jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Mamlaka ya Maji Jijini Dar es salaam *DAWASA* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya Mkoa wa Dar es salaam, hususani Jimboni kwangu mimi nina kata 8, mitaa 46 zile 86 ambazo amezisema sisi tulishazivuka siku nyingi. Kwa hiyo, tuna bahati, tunashukuru kwa hilo. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri alikuja mtaa ulikuwa umebaki Mtaa wa Golani tulikwenda nae mpaka kule mlimani sana, wale wananchi wamenituma asubuhi hii nikushukuru sana wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana *Engineer* Edison Meneja wetu wa Ubungo na *Engineer* Julieth John Meneja wa Magomeni wanafanya kazi kubwa. Nichukue nafasi hii pia kumponeza mdogo wangu Cyprian Luhemeja kwa uteuzi ambao ameupata, amefanya kazi kubwa Dar es Salaam tunarajia kwamba atasaidia katika nchi na tumtakie *Engineer* Kiula na wengine wote waendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niombe *Engineer* Julieth tumeisha ongea, *Engineer* Lidya ile tumetengeneza

mradi mzuri wa maji taka, Mtaa wa Manzese, *National Housing* na Sinza na sehemu zingine lakini mitaa ni *critical* kwa sababu ina shida kubwa sana ya maji taka tumeisha zungumza hili niwaombee mlitekeleze vizuri ili wananchi wetu waweze kukaa vizuri pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maji hakuna shaka, katika miaka ya hivi karibuni imepata mafanikio makubwa ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaeleza. Nataka nitumie dakika ambazo zimebaki kueleza mafunzo ambayo tunayapata yanayotokana na mafanikio katika sekta ya maji na wale ambao wapo humu ndani muda mrefu wanafahamu ni nikiwa Katibu Mkuu tukija hapa Mwaka 2017 palikuwa hapakaliki. Tukikaa pale mlikuwa mnatupiga nyundo za kutisha, ukitoka hapo unamuomba waziri likizo ya wiki nzima baada ya bajeti kupita lakini hii kazi ilikuwa ni kubwa lakini baada ya muda mfupi kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mafunzo matano kama muda ukiruhusu moja; ni umuhimu wa kuwa na taasisi imara katika usimamizi wa shughuli za Serikali. Sekta ya maji inasimamiwa na taasisi kubwa tatu tunayo mabonde ya maji, mamlaka za maji ambazo zipo kwenye mijini na miji midogo na tuna *RUWASA* hii ambayo mmeipigia makofi mengi. Hizi ni Taasisi ambazo zinafanya kazi kubwa, kwa hiyo, nikusii Mheshimiwa Waziri uendelee kuzipa nguvu taasisi hizi kwa sababu kwakweli ndiyo miguu yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, funzo la pili; ni umuhimu wa kuwa na mipango ya muda mrefu na kuishikilia. Sekta ya maji inaongozwa amesema Mheshimiwa Waziri na *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *water sector development program*. Sekta hii imekuwepo kwa takribani miaka 20 na kila Waziri akija anakabidhiwa nyaraka hii na anatembea nayo, tofauti tu ni kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa pale Mawaziri kadhaa alikuwepo Mheshimiwa Jumanne Maghembe, akaja Mzee wangu Kamwelwe akaja Profesa Mbarawa na wengine tofauti ni kwamba, wanatekeleza *program* hii hii hawabadilisha hata nukta. Tofauti kubwa ni kasi, kijana anakasi kubwa huyu, anakimbia zaidi, na kwa sababu yeye amevunja rekodi ya Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, amevunja rekodi, kwa sababu yeye ndiye mdogo kuliko wote sasa hivi katika Mawaziri wote wa Wizara ya Maji tangu Wizara hii iundwe. Alikuwa anashikilia rekodi Mheshimiwa Jakaya ameishapitwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, funzo la tatu; muhimu ni muhimu wa kuheshimu, kuwajali na kuwapenda watalamu wetu. Sekta ya maji ni moja ya sekta ambazo zina heshimu sana watalamu wake. Kwa hiyo, ni jambo muhimu tuwape nafasi, tuwaheshimu, kwa sababu ukweli ni kwamba mkono mmoja hauchinji ngo'mbe. Mheshimiwa Waziri, yuko hapa ana ng'ara lakini nyuma yake kuna vijana wakakamavu, waliyosoma vizuri, wanafanya kazi yeye anawapa nafasi. Hili ni jambo la msingi ambalo lazima aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne; ni umuhimu wa uwekezaji. Sekta ya Maji inapata fedha kutoka mfuko wa maji jambo hili ni jambo zuri la kushukuru kwa kweli liendelee, kwa sababu hii ndiyo hasa nguzo ambayo inafanya miradi wa maji itekelezwa kwa ukubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano; sekta ya maji na sekta za huduma zingine zinahitaji utulivu na tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuipa sekta hii maji utulivu mkubwa sana kwa kiwango ambacho watalam wanafanya kazi yao kwa kutulia, kwa kutumia utaalam wake, sekta hizi ni ngumu. Katika hilo tatizo la sekta ya maji ni kwamba inapambana ni kama kila mara goli linapanuka kwa sababu leo anazungumzia asilimia 86

lakini kesho inaweza ikashuka kwa sababu ya ukuaji wa idadi ya watu hiyo ndiyo changamoto kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuendelee kuwekeza fedha katika sekta hiii ili tuendelee kushughulikia miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la miwisho nichukue nafasi hii kuiba muda wako kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo moja kuwapongeza vijana wetu wa yanga kwa mechi yao ya leo. Kwa sababu wamefanya kazi kubwa, wapo nusu fainali na la pili kuwatakia kila kheri katika mechi yao ya leo, leo ni siku kubwa katika… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Zungumzia hoja iliyoko mbele yako. *(Vicheko)*

**MHE. PROF. KITILA M. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo najua hilo utakuwa umelizingatia hata wewe mwenyewe tunawapongeza vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar. Jiandae Mheshimiwa Paresso, jiandae Mheshimiwa Shabani Taletale.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara Maji. Pia nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha uhai na afya njema kwa siku ya leo nakuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya maji na hususani Wilaya ya Nyang'hwale. Tumeendelea kupokea fedha nyingi sana kwenye sekta hii ya maji hongera

sana Mama tuko pamoja wana Nyang'hwale 2025 zako ni za kumwagika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alivyofanya ziara yake Mwaka 2018 pale Wilayani kwetu Nyang'hwale na kuweza kuja kukuta mradi huu wa kichefuchefu Nyamtukuza aliweza kutoa maneno makali na maelekezo makali na mradi huo leo umeweza kukamilika. Ombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamuomba sasa aje auzindue mradi huo ambao tayari umeishakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na wizara yote kwa ujumla. Kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya na walizozifanya katika Jimbo la Nyang'hwale kwa kweli mradi huu ulikuwa ni kichefuchefu. Alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu akawa anasema Nyang'hwale Oyee wanamwambia maji, akaja Waziri Aweso akasema Nyang'hwale Oyee wanamwambia maji. Lakini leo hii tatizo la maji Wilaya ya Nyang'hwale tumelipunguza kwa kiwango kikubwa sana. Hongereni sana Waziri Aweso pamoja na Prisca pamoja na timu nzima ya Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze ma–*manager* wangu hasa ma–*manager* wa *RUWASA* Mkoa wa Geita Jabir pamoja na Moses wa Wilaya Nyang'hwale kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya tunashirikiana nao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja, kwanini naunga mkono hoja? Kwa kweli tulikuwa nashida ya maji katika Wilaya ya Nyang'hwale kwa kipindi kikubwa sana. Mwaka 2020 tulikuwa na asilimia 39 tu ya upatikanaji wa maji lakini kufikia mwaka 2023 tumefikia asilimia 65 kwa kiwango kikubwa tunatoa pongezi kwa wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna vijiji 40 ambavyo tayari tumeishafikiwa na maji lakini vijiji vilikuwa ni 62 bado vijiji 22. Maji yaliyopatikana ni kupitia visima virefu na vifupi lakini pia kupitia Mradi wa Maji Nyamtukuza lakini kutoka Mahando – Ilogi kwakweli maji tumeyapata hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu Waziri lakini pia pongezi nyingi zimuendee Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yaliyopatikana kwa kupitia Bomba la Mangu – Ilogi ni vijiji 20 mpaka sasa hivi vinanufaika na bomba hilo lakini watu wanaonufaika na maji katika Wilaya ya Nyang'hwale ni watu 133,000 kati ya watu 207,000. Mradi wa Mahando – Ilogi ifikapo 2022/2023 ampapo tunaenda kumalizia baadhi ya vijiji vitakavyokuwa vinanufaika ni vijiji vifuatavyo ikiwemo Karumwa, Busengwa, Izinya, Kayenze, Bukwimba, Mundu, Mwamakiliga, Lugwa, Kafita, Mushimba, Ikangala, Kitongo, Kakola, Nyaudele, Bungombela, Bukungu, Bulangale, Igeka pamoja na Nyamtukuza vijiji hivi vitaendelea kunufaika baada ya kukamilisha Mradi huu wa Mangwi – Ilogi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Bajeti yetu hii ya 2023/2024 tunatarajia kukamilisha baadhi ya vijiji vifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vijiji vilivyokamilika Jimbo la Nyang'wale ama Wilaya ya Nyang'wale itakuwa imeshakamilisha na kumaliza kabisa tatizo la maji. Vijiji hivyo sitaki kuvitaja niseme kwa sababu ya muda. Tuna bilioni 15 ambazo tulitengewa kwa ajili ya mradi wa Nyamtukuza. Mpaka sasa hivi tumeshatumia bilioni 10.3, ina maana bado kuna bilioni nne na *point*. Mradi huo umekamilika, tunaziihitaji fedha hizo ziendelee kutolewa ili tutweze kusambaza maji kwenye vijiji ambavyo nilikuwa nataka kuvitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo ni takribani bilioni nne na kitu. Lakini pia tulitengewa bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa *tank* la chujio. Tumeahirisha kujenga chujio hilo sasa hivi tunaziomba fedha hizo ziendelee kutolewa kwa ajili ya kusambaza mabomba kwenye vijiji vingine vilivyobaki. Kwa nini tumesitisha hilo zoezi la kujenga hilo *tank,* ni kwa sababu sasa hivi tunatumia maji ya kutoka Mangu Kwenda Ihugi, maji safi na salama, hivyo hatuhitaji tena kujenga *tank*. Tunaziomba fedha hizo zitoke ili tuweze kukamilisha vijiji vyote ambavyo vimebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja, lakini ombi langu la mwisho, nakuomba Mheshimiwa Waziri; kwa sababu mradi huo ulikuwa ni kichefuchefu na wewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wengine walifika kwa ajili ya mradi huo. Ninakuomba sasa nikuombe uje uuzindue mradi huo. Mwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu tunawasubiri kwa hamu mje muuzindue. Lakini pia fedha hiyo niliyoiomba iendelee kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa namuita Mheshimiwa Paresso, ajiandae Mheshimiwa Hamisi Shabani.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama amabvyo msemo maarufu unavyosemwa, kwamba maji ni uhai kweli maji ni uhai, na kwa ajili ya ustawi wowote wa jamii ni lazima kuwepo na uhakika wa upatikanaji maji safi na salama. Suala la upatikanaji wa maji safi na salama mdau wa kwanza kuhakikisha wananchi wanapata

maji ni Serikali, ihakikishe wananchi wanapata maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi kwenye baadhi ya maeneo, kama endapo Serikali kama inachelewa kupeleka huduma hii wananchi wanaamua wenyewe kujianzishia miradi yao kwa mujibu wa taratibu ili mradi wapate maji kwa ajili ya wa ustawi wa jamii yao. Miaka ya 1990 katika Wilaya ya Karatu kulikuwa kuna shida kubwa sana ya upoatikanaji wa maji. Ulipofika mwaka 1999 wananchi wa Karatu waliamua wenyewe, pamoja na viongozi wao wa wakati huo kujitafutia ufumbuzi kuhakikisha wanapata maji katika maeneo yao. Katika vijiji sita katika Mji Mdogo wa Wilaya ya Karatu, waliamua kuchangisha wenyewe fedha zao, kuchimba maji na kutafuta maji. Walihakikisha kwamba wanataka kupata uhakika wa maji. Ilipofika mwaka 2002 wananchi wa Karatu wakaanzisha mradi wa maji maarufu kwa jina la *KAVIWASU*. Ni mradi ambao ulikuwa umebeba na unatoa huduma katika vijiji sita ndani ya Mji wa Karatu. Wananchi hawa walihakikisha kwamba wanaendeleza mradi huu kwa fedha zao na kwa gharama zao wenyewe, na walisajili mardi huu kama bodi ya wadhamini chini ya vijiji hivyo sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipofika mwaka 2022 mradi huu ulitimiza miaka 20 kwa huku wananchi wakiendelea kujiendesha wenyewe kwa kuhakikisha wanasambaza maji, wanapata maji na mradi unaendelea kukua. Lakini mradi huu mara ya kwanza ulikuwa unatumia maji mtiririko, kwa maana ya maji ya msimu wa mvua, lakini baadaye wananchi wakajiongeza wakaanza kuchimba na visima virefu ili kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu katika miaka 20 uliodumu kabla ya mwaka jana maamuzi yaliyofanyika ambayo nitayaeleza uliweza kuhakikisha ndani ya vjiji hivyo sita

katika Mji wa Karatu asilimia 76.8 ya wananchi wanapata maji. Lakini kama haitoshi mtandao wa maji uliweza kufikia kilomita 478.4, na wananchi ambao wamejivutia maji majumbani walifika takriban kaya elfu tatu na zaidi. Vilevile mradi huu ulikuwa unazalisha lita milioni nne kwa saa, katika mji wa Karatu. walikuwa na ma-*tank* ya kuhifadhia maji 23, ma-*tank* ambayo yanakidhi lita tofauti tofauti kuanzia elfu thelathini na tano, elfu kumi na tano, elfu saba na kuendelea. Lakini walikuwa na visima virefu nane vya uhakika vya kuhakikisha maji yanapatikana mwaka mzima na wananchi katika vijiji hivi wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walikuwa wana *Public DP,* yaani machoteo ya maji ya wananchi wa kawaida 128, na yote yalikuwa ni *active* na yanapatikana bila shida. Sasa shida ikaja mwaka jana, Mheshimiwa Waziri amekwenda Karatu amevunja mradi huu. Wananchi wa karatu wanauliza; kwa mafanikio haya ambayo wao wenyewe kwa fedha zao mradi huu umechangiwa na wananchi asilimia 100 hakuna hata shilingi 10 ya Serikali iliyokwenda pale; ni sababu zipi zilifanya Wizara Kwenda kuvunja mradi huu? Wananchi hawa walikuwa na tatizo la maji miaka yote hawakupata hata shilingi 10 kutoka Serikalini, wakaamua wenyewe kwa jitihada zao wakajiletea mradi wa maji, wakausajili kwa utaratibu unavyotakiwa, kwa nini Wizara mmeend akuvunja mradi huo wa wananchi?

Mheshimiwa Naibu spika, lakini kama haitoshi kuwepo miradi kama hii Karatu si ya kwanza, kuna miradi mingine ambayo imefanya vizuri sana katika Jimbo la Hai. Nilikuwa naongea na Mheshimiwa Mbunge pale asubuhi kuna mradi wa Uroki, Bomang’ombe, kuna mradi wa Losaa-Kia kuna mradi wa Machame kuna mradi wa Lyamungo. Miradi hii inafanana kabisa na mradi ule ule ulioko Karatu, na miradi hii na inafanya vizuri sana. Mheshimiwa Mbunge amenipa taarifa pale asubuhi miradi hii bado ipo kwa upande wa Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunataka kujua Karatu wamewafanya nini mkaenda kuvunja huu mradi? Na kama kulikuwa kuna shida kwa nini hamkukaa na wananchi, mkawafuata na mkapata maoni mkataka kujua? Mheshimiwa Waziri mmeenda na hoja nyepesi sana, mmesema mradi wa *KAVIWASU* ulikuwa unatoza maji ghali, mkaanziha mradi wa Serikali unaitwa *KARUWASA* mwaka 2014. Wakati mnaanzisha mradi wa *KARUWASA*, *KAVIWASU* ilikuwa inashida gani? Sisi wananchi tunajua kulikuwa hakuna shida, nyinyi mkaanzisha mradi mwingine wa Serikali ndani ya eneo lile lile ambalo wananchi walijipatia maji wenyewe. Huu mradi wa *KARUWASA* mliouanzisha Serikali ulikuwa unatoa huduma kwa asilimia 30 tu. Ilikuwa ina mtandao wa maji kilomita 58, ilikuwa inazalisha maji lita 1,000,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** …Aaaaa! Jamani Mheshimiwa Naibu Spika. Kengele bado ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili, kaa chini. (*Kicheko)*

Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale. Utajiandaa Mheshimiwa Shonza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi kwanza kabisa ningependa nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mema anayoyafanya na kwa neema aliyoileta ndani ya Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki. Lakini pia nimpongeze kaka yangu Aweso, wana Morogoro Kusini Mashariki wanakupenda sana.

Na nikwambie, kwa sababu wanajua uwezo wako ukitaka kuongeza wanne karibu Morogoro Kusini Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza timu yangu ya Simba kwa kuendelea kufa kiume, na naamini tutafufuka kiume, na leo timu yao inacheza tuiombee mema. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendele kuipongeza Wizara ya Maji, hapa niseme kidogo mimi wazazi wangu wote walikuwa wafanyakazi wa Wizara ya Maji, kwa hiyo mimi nimelelewa na Wizara ya Maji. Kwetu sisi kwenye Kata ya Tegetero ambako tunazalisha mradi wa Morong'anya. Na kwa mradi huu niendelee tena kumpongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan, mradi wa bilioni 23, huu mradi unakwenda kulisha vijiji zaidi ya 24. Vilevile Mama Samia hajawa mchoyo akaleta pale Kata yangu ya Mkambarani, mradi wa bilioni 4, nani kama Mama Samia? (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niongee; wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Wizara ya Maji imefanya makubwa sana kwenye Tarafa yangu ya Mikese na Tarafa ya Mkuyuni. Sasa tunakwenda kwenye Tarafa ya Ngerengere ambapo ndipo pana mlango wa kupeleka maji zaidi ya asilimia 50 Dar es salaam, hii mimi inanitia aibu kusema sana kwa sababu zaidi ya asilimia 50 maji yanakwenda Dar es Salaam, wana Dar es Salaam wanakunywa maji baridi ambayo tunatunza sisi wana Morogoro Vijijini, Tarafa ya Ngerengere inapata maji kwa asilimia 31. Na hiyo asilimia 31 maji yote ni chumvi, na asilimia 69 watu hawapati maji. Sasa hapa ndugu yangu Aweso ndio utakosa mke Morogoro Vijijini. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme ukweli tunamuona ndugu yangu Aweso anasema wali wa kushiba unaonekana

kwenye sinia lakini niongee ukweli wana Ngerengere kwenye hiyo sinia bado hawajaiona mpaka leo. Nikuombe kaka yangu Aweso, najua unaweza. Leo hii tunaona umetangaza Mradi wa Kidunda ambao unatoka kwenye Tarafa ya Ngerengere, lakini huu mradi wa Kidunda sisi kwetu hatuna faida nao. Muda wa ukame tutaona mnapanda helkopta mpaka vijijini kutuswaga kule, sisi tunaowalindia maji mpate watu wa Dar es Salaam lakini sisi kama wana Tarafa ya Ngerengere hatujui maji baridim maji yote tunayokunywa ni ya chumvi. Basi angalia ule mradi ambao unakweNda Dar es Salaam tuma wataalamu wako na sisi basi tupate maji baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo hii ninavyoongea katika Kata ya Tununguo hawana mradi wowote tangu uhuru umeanza, kwa hiyo sisi tunakunywa maji tunayaita maji ya Nzasa, yale maji meupe. Kweli! zama hizi! zama za Rais jembe, Rais shupavu Mama Samia Suluhu Hassan, nikwambie kaka yangu tunajua, tunajua nguvu ya Mama Samia na tunajua nguvu ya Chama Cha Mapinduzi, hatuwezi kuona sisi tunakunywa maji ya Nzasa halafu tunawapelekea maji Dar es Salaam wanakunywa maji baridi, hilo ndugu yangu leo naweza nikaondoka na shilingi yako nikaenda nayo Ngerengere.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa ndugu yangu anayechangia kwamba sera ya maji inasema. Pale ambapo maji yanaanzia kwenye chanzo cha maji wale watumiaji wanaozunguka eneo lile anatakiwa kupata maji kwa hiyo huo mradi wake watu wake wanapaswa

kupata maji kama wale wa mradi unaopeleka maji Arusha pale Hai, nao wanatakiwa kupata maji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea taarifa ya ndugu yangu Saashisha lakini naendelea kusema kwamba nakumbuka Mheshimiwa Waziri alikuja kwenye kata yetu ya Tegetero wakati anafuata kutembelea mradi wetu wa Morong'anya pale ule mradi wa Morong'anya unapoanzia kwenye kata ya Tegetero, kata nzima ya Tegetero haina mradi wa maji. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri umeacha maagizo na sisi pale katika kata ya Tegetero tuwe wanufaiika. Basi hicho kikafanyike kwenye ule mradi wa Kidunda. Leo hii mimi naona maajabu na miujiza, ule mradi wa Kidunda yale maji hauendi kuyamwaga baharini unakwenda kuwauzia wananchi. Pale hatupati shilingi kumi kipande, tumeridhika *Alhamdulillah* sasa basi hata tukose na maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba, mmetunyima shilingi kumi kipande basi tupeni maji. Tunaomba Tarafa ya Ngeregere nayo iwe sehemu ya unafaika ipate maji baridi Mheshimiwa Aweso. Hakuna kitu kinachoniuma, mimi wakati naingia kwenye nafasi hii ya Ubunge ku ukweli kabisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** *Alhamdulillah Rabbil Alamin. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shonza, jiandae Mheshimiwa Robert Chacha.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanafanya hasa katika upelekaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni siku chache tu zimepita tangu Mheshimiwa Waziri aje kwenye Mkoa wetu wa Songwe na amekuja pale Mlowo ametupatia mradi mkubwa wa shilingi milioni 601. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wenzangu wa kata ya Mlowo kukushukuru sana. Lakini pia tunafahamu kwamba kwenye Mkoa wetu wa Songwe tunao mradi mkubwa sana wa maji wa kutoa maji kwenye Mto Momba kuyasambaza kwenye Miji ya Tunduma, Vwawa Pamoja na na mji wa Mlowo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwamba kwneye bajeti ya mwaka jana alutuahidi kwamba mradi huo ungeanza mwaka huu, lakini mpaka sasa hivi mradi huo haujaanza. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri mradi huo uweze kuanza. Sote tunafahamu kwamba azma kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejionesha kwa namna ambavyo anavyotafuta fedha na kuzipeleka kwenye miradi mikubwa ya maji. Miongoni mwa Wizara ambazo Mheshimiwa Rais amepleka fedha nyingi ni Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima azma hiyo njema ambayo anayo iendane sambamba na kuondoa vikwazo vyote ambavyo vinaweza vikachelewesha azma ambayo anayo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nasema hivyo kwa sababu miongoni mwa matatizo makubwa ambayo tunayo kwneye Wizara ya Maji, na niseme kwamba ni jambo ambalo bado halijapewa umuhimu na Wizara, ni suala la upotevu mkubwa wa maji; hii ni changamoto. Hata ukiangalia, kwenye Ripoti ya *EWURA*

ambayo imetolewa ya mwaka 2021 imeonesha namna gani ambavyo mamalaka mbalimbali za maji hapa nchini zina kiwango kikubwa sana cha upotevu wa maji. Hali hiyo inasababisha kwamba wananchi wanakosa maji lakini vilevile Serikali inapoteza mapato mengi kutokana na tatizo hilo la kutokudhibiti hali ya upotevu wa maji katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika hiyo ripoti ya *EWURA*, na sisi tunafahamu kwamba kiwango cha kimataifa cha upotevu wa maji ambacho kinakubalika duniani kote ni asilimia 20, lakini mamlaka nyingi za maji hapa Tanzania zimevuka hicho kiwango cha asilimi 20. Nikianza, mamlaka namba moja ambayo inaongoza kwa upotevu mkubwa wa maji ni Mamlaka ya Mbozi kwenye Mkoa wa Songwe, Mkoa ambao mimi natoka. Ile ripoti imezungumza kwamba kwenye Mji wa Vwawa Pamoja na Mji wa Mlowo ndiko kwenye changamoto kunbwa sana ya upotevu wa maji. Ukiangalia kwenye hii miji mikubwa ndiko ambako shida ya maji ni kubwa sana. Hata huo mradi ambao tunauomba wa kuoa maji Momba ni kuja ku–*cover* hili *gap* la changamoto ya maji katika huu Miji ya Tunduma, Vwawa Pamoja na Mji wa Mlowo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu mojawapo kubwa ni uchakavu wa mabomba; na ninaamini kwamba hiyo changamoto haipo tu kwenye mkoa wa Songwe ni nchi yote kuna uchakavu mkubwa sana wa miundombinu. Lakini ukiacha kwenye Halmashauri hiyo ya Mbozi kuna Mkoa wa Arusha, wao upotevu wa maji ni asilimia 51, Dar es salaam 39, Lindi 37, Mwanza 36, Moshi peke yao ndio wako kwenye20.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba ni lazima sasa Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri uje na mkakati Madhubuti wa kumaliza tatizo la upotevu wa maji katika nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Waziri

umesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge wote wameonesha namna gani ambavyo kwanza tunakuamini na tuajua kwamba wewe ni jembe kweli kweli. Kama Mheshimiwa Waziri umeweza kudhibiti mabomba ambayo yanapaa usiku na sasa hivi yanatoa maji mimi naamini Mheshimiwa Waziri huwezi kushindwa kukabiliana na tatizo la upotevu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe ushauri wangu katika maeneo machache. Ushauri wangu wa kwanza, niombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa hii ni bajeti mpya jambo la kwanza ambalo nataka nishauri Mheshimiwa Waziri kuwe na ajenda maalumu ya kudhibiti suala la upotevu wa maji. Niombe Wizara ibebe jambo hili kama ajenda ili fedha za Serikali zisipotee, lakini vile vile wananchi wapate maji kwa wakati, na ile azma ambayo Mheshimiwa Rais anayo ya kumtua ndoo mwanamke kichwani iweze kutekelezwa. Lakini jambo la pili, nataka niishauri Wizara ifanye utafiti wa kina nchi nzima ili kuweza kubaini maeneo yote ambayo yana uchakavu wa mabomba ya maji. Mimi naamini wakishafanya utafiti, kwa sababu tayari tunayo taarifa *EWURA*, itasaidia sana kuweza kujua ukubwa wa tatizo uko vipi ili Wizara iweze kujipanga kuweza kukabiliana na hiyo changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu, niishauri Wizara itenge bajeti maalumu kwa ajili ya kukarabati miundombinu yote nchini Tanzania. Katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umetaja miradi mikubwa mbalimbali ambayo mmeifanya na ambayo mnakwenda kuifanya kwenye mwaka huu wa fedha. Miradi hiyo tukiendelea kutenga, tukijenga miradi mikubwa ya maji kama hatutengi bajeti kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya maji bado tatizo la maji litabaki pale pale. Kwa hiyo niombe tuanze kutenga bajeti ili tuweze kuzisaidia zile mamlaka ambazo zinashughulika na matatizo ya maji katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo jingine, nadhani ni wakati muafaka sasa tuhame kwenye mfumo wa kutumia bili za maji. Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukishauri sana kwa miaka mingi, kwamba tuanzishe luku za maji. Kwani changamoto ya kuwa na luku za maji ni nini? Kama kwenye umeme tumefanikiwa kwa nini kwenye maji tushindwe? leo hii kuna changamoto kubwa sana wananchi wanalalamika kwanza wanabambikiziwa bili za maji. Leo hii kuna taasisi zina madeni kubwa ya maji. Mwarobaini wa haya yote ni sisi kuwa na luku za maji kama ambavyo tuna luku za kwenye umeme tuwe na luku za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hili likifanikiwa, tutaondoa tatizo kubwa la ukosefu wa maji na changamoto kubwa ya fedha za Serikali kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu, watumishi wake huko mikoani wana imani kubwa sana naye. Kwenye Mkoa wangu wa Songwe mara zote nikiongea na watumishi, kwa maana ya Mameneja, wale wa Mikoa, Mameneja wa Wilaya, mara zote wananiambia kwamba, Mheshimiwa Shonza tunaomba pamoja na yote, msiache kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu, msiache kumshauri kwa sababu, jamaa anafanya kazi kubwa sana, ndio kauli yao siku zote. Kwa hiyo, hii inaonesha watumishi wa Mheshimiwa Waziri kule chini wana imani kubwa sana naye. Nimwombe Waziri jambo moja, wanazo changamoto kubwa ikiwemo changamoto ya ukosefu wa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unakuta mabomba yamepasuka sehemu, kuna changamoto sehemu, lakini wanashindwa kufika kwa sababu hakuna magari. Hivi juzi kuna mtumishi mmoja wa Wizara amefariki kwa sababu ya kukosa

usafiri. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri alichukue hili katika bajeti yake ya mwaka huu anunue magari, kama ambavyo wamefanya kwenye elimu, kama ambavyo wenzetu wa *TARURA* wamefanya na kwenye afya, naamini hata kwenye Wizara ya Maji anaweza kuwapatia vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa sababu tunajua kwamba, Waziri ni mtu wa kazi, nimwombe tu, tumekuwa tukimwona mara kwa mara akishughulika na wakandarasi na mameneja ambao hawafanyi kazi yao ipasavyo; nimwombe Mheshimiwa Waziri aweke *target* kwamba, kigezo mojawapo cha mtu kuwa *promoted* kwenye kazi yake ni kudhibiti tatizo la upotevu wa maji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hiyo ni kengele ya pili.

Mheshimiwa Robert Chacha, wajiandae Mheshimiwa Sylvester Francis Koka na Mheshimiwa Ester Lukago Midimu.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara ya Maji, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii kwa kunipa pumzi mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameendelea kutusaidia katika Halmashauri ya Mji Bunda katika kuhakikisha kwamba, Mradi mkubwa wa Maji wa Nyabehu umekamilika, ambapo mpaka sasa Mradi wa Nyabehu umekamilika kwa asilimia 99, ulikuwa una thamani ya karibia shilingi bilioni 10 na sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi ambao wananufaika na mradi huu ni zaidi ya wakati 178,000. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu, wakati anaingia kwenye nafasi hii, mradi huu bado ulikuwa hautoi matokeo ambayo wananchi wa Bunda Mjini wanayategemea. Kwa sasa tumeshapata matumaini kwa sababu, mradi huu unatoa maji safi na salama kwa kiwango kikubwa. Sasa ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Maji, ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, ni kuhakikisha kwamba, atusaidie mambo madogo madogo yale yaliyobaki ya usambazaji maji kwenye maeneo yale ambayo bado maji hayajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Mradi wa Ujenzi wa Tanki la Maji Misisi-Zanzibar ambapo tenki hili litahakikisha kwamba, wananchi wote wa Kata ya Sazira na wengine wa Kata hii ya Kabasa watapata maji mara baada ya kuwa tenki hili limekamilika. Mpaka sasa tumepata zaidi ya shilingi milioni 733 ambazo naamini Mheshimiwa Waziri tumeshapokea kwako fedha milioini 583 kwa ajili ya utekelezaji wa tenki hili ambalo litabeba maji zaidi ya lita laki moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba, jambo hili likishakamilika maeneo hayo tutapunguza uhaba mkubwa wa maji na malalamiko kwa wananchi wetu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiona mradi mkubwa wa maji kwao na maji yako karibu kilometa tatu, tano hivi kuingia Ziwa Victoria, halafu wakawa wanashangaa maji hawayaoni, lakini sasa wananchi wa Bunda Mjini wameanza kunufaika na mradi huu mkubwa ambao unatekelezwa pale Bunda. Mradi huu nakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Rais alikuja kuuzindua na baada ya kuuzindua umeleta matokeo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ni ujenzi wa tenki la maji ambalo litasambaza Manyamanyama na Mugaja. Lenyewe hili lina thamani ya shilingi bilioni moja na milioni 65 ambazo sasa mchakato unaendelea. Ombi langu ni kwamba, Waziri aweze kutuwezesha sisi ili tuweze kupata fedha hizo Halmashauri ya Mji wa Bunda, ili mradi huu uweze kutekelezwa na wananchi wetu waendelee kunufaika na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ujenzi wa tenki la maji ambalo litasambaza maji Kata ya Balili, Rubana na Kunzugu. Maeneo haya tukishawatengenezea tenki la maji, mradi ambao utakuwa unagharimu karibu zaidi ya milioni 759, naamini Mheshimiwa Waziri anafuatilia jambo hili vizuri, tunamwomba tuendelee kupata fedha ili tenki likamilike na wananchi wetu wale wapate maji vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jiografia ya Mji wa Bunda ilivyo na jinsi ambavyo tuko karibu na ziwa, lilikuwa ni jambo la kushangaza kwamba, sisi ndio tulikuwa tunakuwa walalamikaji wa kwanza kukosa maji, lakini sasa namhakikishia kwamba, atakapokuja Bunda kwa mara nyingine ataona furaha iliyopo kwa wananchi wake kutokana na kwamba, wamepata huduma nzuri ya maji wanapata maji safi na maji salama kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu ni kuhakikisha kwamba, jambo hili…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa mzungumzaji Taarifa kwamba, anapozungumza Bunda azungumzie Jimbo la Bunda Mjini. Jimbo la Bunda la kwangu bado lina ukame mkubwa sana wa maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert, Taarifa hiyo.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Getere anafahamu jimbo lake na mimi nafahamu jimbo langu. Mimi Jimbo langu ni la Bunda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la upotevu wa maji na jambo hili nimeona tatizo kubwa liko kwenye ile mipira ya kuvutia maji. Hawa ndugu zetu wenye viwanda vya kusambaza mipira hii naamini mipira hii haiko katika viwango vile ambavyo vinatakiwa. Yale mabomba yale ya maji wananchi wanayanunua, wakiyatumia kwa muda mfupi, ndani ya miezi mitatu mabomba yalishapasuka ambayo yanawaingiza wananchi kwenye gharama nyingine tena ya kununua mabomba mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naamini jambo hili na kwa sababu, wale ni wadau wa maji ni vizuri Waziri akawawekea mkazo kwenye mabomba haya ya maji. Yawe mabomba ambayo yanalingana na thamani halisi ya fedha ambazo wananchi wetu wanazitoa. Kwa sasa jambo ambalo litakuja kujitokeza pale kubwa ambalo ni baya ni hilo la mabomba ya maji kupasukapasuka kwa sababu, tumekuwa tukipata malalamiko mengi sana kwa wananchi wetu kwamba, mabomba wanayoyatumia kwa muda mfupi yanakuwa yalishapasuka, halafu wanaingia tena gharama za kununua mabomba yale kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tuna mradi pale wa kutibu majitaka na maji safi, pale Bunda, lakini tulishapata eneo pale karibu eka 100, kule Butakare, kilichobakia tu ni kupata fedha za fidia ili kwamba, eneo lile na kutokana na mwingiliano wa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini, ni vizuri tukapata fedha hizi za kulipa fidia maeneo haya, ili mradi ule uweze kutekelezeka ili uweze kuleta manufaa makubwa katika Mji wa Bunda. Kwa sababu jiografia ya Mji wa Bunda ndio picha halisi ya Mkoa wa Mara kwa mtu yeyote anayekwenda Mkoa wa Mara, picha nzuri ya Mkoa wa Mara anaianzia kwa kuona Bunda. Kwa hiyo, akikuta jiografia ya Bunda imekaa vizuri hasa kwenye miundombinu ya maji anajua hata huko anakokwenda lazima atakuta hali halisi ni nzuri zaidi. Kwa hiyo, ombi langu ni kuhakikisha kwamba, jambo hili linafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo lingine nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, yule Mkurugenzi wetu wa *BUWASA* aliyeko pale Bunda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili, ahsante.

Mheshimiwa Koka, jiandae Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi uliyonipangia ya kuchangia. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta zote za kuwahudumia wananchi wa Tanzania. Pamoja na kazi nzuri

sana inayofanywa na Serikali katika usambazaji wa maji, bado tuna matatizo madogo madogo ambayo hakika wananchi wangu na hususan wa Kibaha Mjini wanakumbana nayo ambapo inawaondolea nafasi ya kufurahia matunda haya ya usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kibaha Mjini, Kata ya Pangani na hususan Mtaa wa Pangani, lakini vilevile Mtaa wa Lumumba, Mtakuja na Miwale wao hawajafaidika na usambazaji wa maji, licha ya bomba kubwa la maji kupita, ambapo linapopita ni chini ya kilometa tatu hadi nne kufikia maeneo hayo. Jambo hili tumelijadili sana na Wizara na kuna mpango wa ujenzi wa tenki la lita 6,000 ambalo litaondoa tatizo katika ule Mtaa wa Pangani na hii mingine kiasi kwamba, hata machinjio yetu ya kisasa yatapata maji. Huu ni mwaka wa tatu kwenda wa nne, kila mwaka mkandarasi anakuja, kila mwaka tenda inatangazwa, jambo hili bado halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu na ni mchapa kazi, lakini wananchi wa Pangani wanasema bado zile cheche zake za kuchapa kazi hawajaziona. Nimwombe sana, ili tunapofunga bajeti hii tusigombane kwa kushika mshahara wake, basi namwomba atoe majibu sahihi ni lini tenki hili linajengwa, ili wananchi hawa waondokane na adha hiyo kubwa ambayo wamekuwa nayo kwa takribani miaka mitatu minne sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na Kata ya Pangani, lakini tuna maeneo mengine ambayo nayo yana changamoto ya maji ukizingatia Kibaha Mji ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani. Kata ya Viziwaziwa kuna uchakavu na kuna msukumo mdogo wa maji. Kwa hiyo, maeneo ya Mitasa, Gare, Viziwaziwa na Mikongeni hawapati maji kwa sababu ya msukumo mdogo, lakini vilevile Kata ya Msangani usambazaji wa maji na hususan,

Mitaa ya Kumba, Miembeni na Garagaza nako kuna tatizo kubwa wananchi hawajafikiwa na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maili Moja usukumaji wa maji ni mdogo kwa hiyo, wananchi hawapati maji ya kutosha, lakini Visiga, tuna Mitaa ya Saheni, Yerusalemu, Gaza pamoja na Bwawa la Chumvi na kwenyewe bado hawajapata maji licha ya kwamba, hizi ni kata zilizoko katika mji ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani. Ombi langu kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba, pamoja na kazi nzuri ambayo imeshafanyika ya kupeleka mabomba makubwa na kwamba, bomba kubwa linalokwenda Dar-es-Salaam vilevile linapita maeneo haya, sasa basi mgawanyo wa maji haya kwenda katika maeneo haya na msukumo wa maji uzingatiwe, ili wananchi wafurahie matunda ya Mradi mkubwa wa Ruvu Juu na Ruvu Chini kwa ajili ya wananchi wa Pwani na Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu mita za maji. Wananchi wengi wanapata adha kubwa kwa sababu ya kupata bili ambazo sio sahihi. Hili limekuwa ni tatizo kubwa kwa muda mrefu katika maeneo mbalimbali. Napenda niishauri Wizara kwamba, kama itachukua hatua zifuatazo nina imani tutaondokana na tatizo hili na hatimaye bili za maji zitakuwa sahihi, hatutakuwa na malalamiko na wananchi watakuwa wanalipa bila kuwa na foleni kubwa ya malalamiko na marekebisho ya bili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tujikite katika teknolojia, kwamba, twende kwenye mita ambazo ni za LUKU. Vilevile ununuzi wa mita na wenyewe una changamoto. Kwa hiyo, ningeishauri Wizara ifanye *consolidation* kama ni mita ambazo tutakubaliana kwamba, ni kweli zinafaa na ni sahihi, basi zinunuliwe kwa pamoja ili kila mamlaka iweze kupata mita zile na kila mahali katika nchi yetu ambako wanasambaza maji

kusiwe na mita ambazo ziko tofauti, hizi zinasoma vizuri, zile zinasoma vibaya, angalau tuwe na mita ambazo zinakubalika na zitakuwa zinatoa usahihi wa ujazo wa maji ambayo yanakwenda kwa wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, kwanza tutaondoa tatizo la upotevu wa maji, lakini pili tutaondoa tatizo la malalamiko na kuwaonea wananchi kwa kuwapelekea bili ambazo hakika hawajatumia maji kiasi kikubwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, itafanya hizi mamlaka zetu za maji ziweze kupata fedha bila kutumia gharama kubwa ya kusambaza maji kwamba, kuna watu wanapita kwenda kusoma mita na kutoa makadirio saa nyingine kwa utashi wa mtu kulingana na alivyoona. Kwa hiyo, ningeomba sana hili litiliwe mkazo ili sasa na upande wa maji na yenyewe yasambazwe katika utaratibu wa teknolojia kama tunavyofanya kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo machache na naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja. Tuko bega kwa bega na Wizara kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata maji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Midimu, jiandae Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati ya kumtua mama ndoo kichwani. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waheshimiwa Wabunge ni ukweli usiopingika Waziri Mkuu anazunguka nchi nzima kukagua miradi ya maendeleo. Nampongeza sana Mungu ambariki. Tatu, nampongeza Waziri Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu

Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Wizara ya Maji wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali yangu kwa kutuletea miradi mingi midogo midogo ya maji, nashukuru sana. Wilaya ya Maswa kuna Mradi wa Chujio, Kata ya Zanzui umegharimu bilioni tatu. Naishukuru sana Serikali, lakini pia naishukuru Serikali kwa kutuletea tenki la maji Maswa Mjini. Watu wa Maswa Mjini wanakunywa maji mazuri, safi na salama sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Maswa, kuna Vijiji vya Mwamashindike, Budekwa, Mwabalaturu na Busilili, kuna changamoto sana ya maji. Naiomba Serikali ituchimbie visima. Nasema hivyo kwa sababu gani, juzi tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkoa wa Simiyu amezindua gari la kuchimba visima, hicho ni kishindo cha Mama Samia Suluhu. Naomba hilo gari liweze kutuchimbia visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Busega naipongeza Serikali, Kata ya Mukura kuna mradi mkubwa wa bilioni 2.7, naipongeza sana. Kata ya Kabita kuna mradi unaendelea kujengwa na Serikali, tumeanzia bilioni sita naipongeza sana Serikali. Ombi langu kwa Busega, naomba Kata ya Shigala na Igalukilo kuna shida kubwa sana ya maji, naomba Serikali iweze kutuchimbia visima virefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda Kata ya Bariadi. Naipongeza sana Serikali kwa Mradi mkubwa wa Maji wa Ngulyati, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameuzindua juzi, umegharimu bilioni 1.3, naipongeza sana Serikali kwa hilo. Watu wa Kata ya Ngulyati wanaishukuru sana Serikali, wamenituma, sasa hivi hawana shida ya maji tena, wenyewe sasa hivi wanatafuta pesa tu hawana shida na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Bariadi, naomba kuna changamoto kubwa Kata ya Sapiwi, Kata ya Sakwe, Kata ya Lukindwabiye, Kata ya Mwasuguya na Kata ya Likungulyabashashi. Tunaomba waweze kuchimbiwa visima kwa sababu, muda mwingi wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Itilima, naipongeza sana Serikali kwa Mradi wa Gangabiriri, ni mradi mkubwa na ni mradi mzuri, lakini Wilaya ya Itilima, Gangabiriri ni Makao Makuu, Wilaya inaendelea kupanuka, naiomba Serikali ituongezee tenki, lakini vilevile naomba Serikali ichimbe kisima kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iweze kufanya ukarabati katika mabwawa; la kwanza, Noghbora, Mwamapalala, Sawida, Habia na Nkoma. Nikija Wilaya ya Meatu, kuna Bwawa la Mwanjoro limepasuka na halijaanza kufanya kazi, naiomba Serikali iweze kukarabati. Bwawa hilo likikamilika litahudumia vijiji vitano. Mheshimiwa Aweso ananisikia, Meatu kuna ukame mkubwa sana, naomba ajitahidi ikiwezekana Meatu kila tarafa wachimbe bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali yangu kwa mradi mkubwa wa maji. Mheshimiwa Waziri ametupa matumaini na namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kwa kutoa zaidi ya bilioni 444 kwa ajili ya Mradi wa Ziwa Victoria, ahsante sana mama kuwajali wanawake. Wanawake wa Mkoa wa Simiyu muda mwingi walikuwa wanaupoteza kutafuta maji kuliko kufanya kazi za maendeleo. Mama suluhisho la ukame Mkoa wa Simiyu ni Mradi wa Ziwa Viktoria, hongera sana mama yangu. Hicho ndio kishindo cha Mama Samia Suluhu, nani kama mama? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri, akija hapa kutoa majibu, aniambie mradi huo unaanza lini? Kwa sababu, maeneo ambayo mradi unapita tayari fidia zimeshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Mkoa wa Simiyu sio wavivu, ni wakulima wazuri na ni wachapakazi. Maji yale yakifika tutalima kilimo cha umwagiliaji, tutalima mbogamboga, tutalima michicha, tutalima kabichi, tutalima bilinganya, tutalima nyanya, tutalima vitunguu. Tutalima mazao ya chakula na tutalima mazao ya biashara, lakini vilevile tutasaidia na mikoa ya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Serikali sasa hivi ni kuwa na uwanja wa ndege kila Mkoa. Nina imani na Simiyu utajengwa na eneo tayari tumeshatenga, tutauza mbogamboga zetu na nje ya nchi. Tutauza mbogamboga zetu Dar-es-Salaam, Mbeya na kila sehemu watakula mboga za kutoka Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mohamed Monni, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambae ametujalia afya njema na amekuwa akitujalia uhai. Naomba nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hakika asilimia 96 ya fedha zilizotoka ni kubwa sana. Wabunge wa muda mrefu wataona ni muujiza kidogo kwamba siyo rahisi

fedha nyingi kiasi hicho zitoke kwa pamoja kwa ajili ya miradi ya maji.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri. Ndugu yangu, Mheshimiwa Aweso, amekuwa akifanya kazi kubwa na Naibu Waziri wake, lakini pamoja na kazi kubwa leo itabidi niseme maneno machache kidogo. Nashukuru kwa mradi wa Farkwa, mradi mkubwa kabisa ambao naamini unaweza kutosheleza maji Dodoma. Changamoto ni moja tu katika mradi ule, andiko la mradi ule linaonesha maji yale yanakuja Dodoma maana yake sisi Chemba hatuna tunachopata katika mradi mkubwa ule. Sasa sijui hao walioandika wanawaza nini, yaani sisi tuna ng'ombe tunamlisha, tunakamua maziwa, tunapeleka watu wakanywe sisi tusipate, hii haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasema mara kadhaa, nimesema kwenye vikao vya ndani, lakini bado kila kikao mnaeleza maji haya ni kwa ajili ya Dodoma. Sasa sisi wananchi wa Chemba kwa nini tuwe na lile bwawa, la nini, linatusaidia nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri alisema ndugu yangu pale kwamba na yeye kwenye bwawa lake maelekezo ni hayo hayo, kwamba maji yanapatikana kwenye Jimbo lake lakini eti maji hayo yakatumike sehemu nyingine, hii haikubaliki. Ninataka niwahakikishie Mheshimiwa Waziri, mkiweka mabomba pale tutaenda na vijana wetu kwenda kuyakata, kwanza tuanze kutumia sisi halafu ndiyo watu wengine waende kutumia. Mheshimiwa Waziri, naomba ninukuliwe hivyo na hivyo ndivyo ninavyoamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nina jambo la pili, umekuwa ukitupa miradi mingi sana ya maji na Chemba ni moja ya maeneo ambayo yanapata miradi mingi ya maji,

2021/2022 tulipata visima 11 lakini mpaka leo kwenye visima hivyo vilivyochimbwa ni vitatu. Tume-*carry* mwaka huu tulikuwa na visima vitano, hakuna kilichochimbwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini tuje hapa kwenye bajeti tujadiliane kwamba bwana tumekupa visima hivi, mimi niende vijijini nikaseme halafu fedha hizo, yaani visima hivyo havipo, hii haiwezi kuwa sawa. Mimi nafahamu namna ambavyo ninyi ni wachapakazi na mnafahamu nimetembea kila mahali kuhakikisha – na mimi naambiwa fedha zimetoka asilimia 96, ukiwauliza Wakandarasi kwangu wanasema hawajapata fedha ndiyo maana hawatekelezi miradi, hili jambo linaumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafahamu kwamba mkiniambia kuna maji naenda kule kuwaambia ndugu zangu hapa kwenye Kijiji X maji yanakuja. Sasa nabaki naonekana mimi Mbunge mwongo wakati fedha tumepitisha hapa lakini kule hazifiki. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, ninafahamu namna ambavyo unafanya kazi vizuri, katika hili kidogo tunaweza kupishana kwa nia njema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi miwili ya siku nyingi sana,Mradi wa Machije ambao una milioni 700 na mradi wa Chandama ambao una milioni 500. Mradi huu ulikuwa ni kabla *RUWASA* haijaanzishwa, mpaka leo mkandarasi kaweka bango hakuna kinachoendelea na kila siku tunau-*carry over* kwenye bajeti nyingine. Maana yake ni nini? uki-*carry over* unanipunguzia mimi *ceiling* ya kuendeleza miradi mingine. Wakati mwingine ukisema sana unaonekana kama unaleta vurugu. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri, mimi ni katika watu wanaokupenda sana na kukuamini, unafanya kazi kubwa, lakini wakandarasi wa namna hii wa nini? Na kwa nini iwe Chemba tu, kwa nini kwamba Chemba ndiyo miradi haiwezi kukamilika? Nataka nikuombe sana uingilie. Nikuombe baada

ya kumaliza bajeti yako hii, najua tutakupitishia vizuri, twende kule ukamalizie na wewe hii miradi ambayo inakera zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la muhimu sana na hili ni la nchi nzima kwamba ni lazima tuweke sera ya uhakika. Amesema Mheshimiwa Taletale kwamba pale kwake upatikanaji wa maji ni asilimia 31, yapo maeneo upatikanaji wa maji ni asilimia 92, nchi hii moja haikubaliki. Wewe mwenyewe mara kadhaa umesema kupata maji ni haki ya mwananchi yeyote yule, haikubaliki! Kwangu pia ni asilimia 36, ukienda Jimbo la jirani ni asilimia 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima hao wanaopanga bajeti waangalie namna gani wanaweza walau ku-*balance* ili maeneo yote haya tuwe na uwiano unaofanana, walau unaokaribiana, hii haikubaliki. Kwamba una asilimia 36, mlipakodi huyohuyo kuna mlipakodi mwingine ambaye ana asilimia 92 na huyo mwenye asilimia 92 ndiye anayepewa miradi mikubwa mingi zaidi ya maji, haya mambo lazima tuyaweke sawa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kuwe na mpangilio na uwiano wa namna gani tunaweza kugawana hizi rasilimali za nchi yetu haiko sawa kabisa, niliomba kulisema hilo ili wakati mwingine muangalie namna ambavyo tunaweza kwenda mbele kwa uelewano mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye miradi ya UVIKO walinunua magari na Mheshimiwa Waziri tulikubaliana, tuliongea vizuri, kwamba kwa sababu Chemba kuna changamoto kubwa ya maji kuliko eneo lolote la Dodoma magari yale yakaanzie Chemba. Ninataka wakati unajumuisha ujibu maswali mawili maana kuna changamoto kidogo, utaniambia tangu yamekuja yamechimba visima vingapi. Maana lile gari tukimpa raia mwingine atachimba visima 100

kwa mwaka, lakini likiwa Serikalini linachimba visima 10 kwa mwaka mzima, haiwezi kuwa sawa na tija yake itakuwa ni ndogo sana, lazima tufike mahali tuangalie namna sahihi na bora ya kuyatumia hayo magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mara kadhaa nimekusikia ukisema kwamba yako maeneo ambayo ukichimba maji ni ngumu kuyapata na moja ya maeneo hayo ni la Chemba. Tuna mradi wa Chemchemi ya Ntomoko kule, kuna eneo la pale Igunga, kidogo kilometa kama tano, sita hivi. Tumechimba mara nne hatujapata maji lakini tunaweza kuyaleta pale kwa gharama ndogo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nikuombe sana, unajua namna ambavyo nakuheshimu, najua wewe ni mdogo wangu, lakini naomba katika hili tuweze kusaidiana. Hatuwezi kuendelea kila mwaka kuja hapa Bungeni mimi nisimame niseme upatikanaji wa maji ni asilimia 32 na mwakani uwe asilimia 32, hii haiwezi kukubalika kabisa na uwezekano wa kupanda unakuwa ni mdogo kwa sababu tunapitisha miradi ambayo haitekelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba nitumie nafasi hii kukushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Rweikiza, jiandae Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie Wizara hii ya Maji, Wizara muhimu kwa mustakabali wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, kwa kazi kubwa na nzuri

sana anayoifanya ya kuboresha maisha ya Watanzania, mchapakazi, mpenda watu na kwa kweli tunajivunia kuwa nae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na wasaidizi wake kwa kazi nzuri, kwa wepesi wake na usikivu na kazi inasogea mbele. Kazi kubwa sana inafanywa na huduma za maji safi na salama na ya kutosha inasogezwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu miradi mingi ipo mikubwa na midogo na inakwenda vizuri. Mradi mmoja wapo kati ya miradi mikubwa ni ule wa Kemondo wa kata saba. Kata hizo Saba ni Kata ya Kemondo yenyewe, Kata za Katerero, Bujugo, Kanyangereko, Maruku na Kata mbili ziko kwa jirani yangu Mheshimiwa Charles Mwijage Mayondwe na Muhutwe. Mradi umesogea umefika asilimia 80 na zaidi ni kazi nzuri inasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umekuwa wa zamani una umri wa miaka minne, sasa hivi tuko awamu ya pili inatakiwa shilingi bilioni 4.8 ili awamu ya pili ikamilike. Kata kadhaa zipate maji na ninaomba hizi fedha zitolewe shilingi bilioni nne na milioni mia nane ili maji yasonge kwenye vijiji vya jirani pale ambavyo vinahusika na hiyo awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kuna vifaa vinatoka Dar es Salaam, vingine vinatoka Uturuki, pampu za maji, imekuwa ni hadithi ya muda mrefu tunaomba ziletwe ili kazi hiyo isonge mbele na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingine miradi ipo lakini Mradi wa Kata ya Karabagaine umekuwa ni kizungumkuti. Pale tumepeleka maji Vijiji vitatu vya Kizuru, Kitwe na Kawa. Serikali ya mama Samia imesogeza maji kwenye vijiji hivyo, na pale ni

Bukoba Vijijini lakini ule mradi umekabidhiwa Mamlaka ya Mjini, *BUWASA*. Kwanza sielewi kwa nini hiki kinafanyika, wajenge *RUWASA* wakamilishe kazi halafu mradi ukabidhiwe watu wa mjini waendeshe. Watu wa mjini wana bei kubwa. Sasa hivi kuna tatizo la kuunganisha maji kwa wananchi, maji yameshafika vijijini lengo ni kuwatua wanawake ndoo kichwani, lakini wanawake hawawezi kumudu yale maji, wanakwenda na ndoo zao mbali huko walikozoea maji yale hawayafaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ni nini hawa *BUWASA* wanaweka gharama kubwa sana. Gharama yao ni kuanzia shilingi 200,000 hadi shilingi 1,300,000 ya kuunganisha maji kwenye nyumba ya mtu, 200,000 ndiyo gharama za chini wengine mpaka 1,300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lengo la Serikali ya mama Samia ni kwamba watu wapate maji safi na salama na ya kutosha, lakini hawa *BUWASA* wanaweka gharama kubwa ambayo wananchi wa vijijini hawawezi kuimudu. Niombe hili Mheshimiwa Waziri uliangalie na uingilie kati. Kwa nini mradi uhamie mjini wakati ni wa vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja ametumiwa bili ya kuunganisha maji kwenye nyumba yake, ngoja noisome, imeandikwa hivi, Ndugu Charles Tibenderwa gharama zako za kuunganishiwa maji ni shilingi 464,396.40 na Kumbukumbu Na. ya malipo ni 994440341104, tafadhali lipa mapema kufuatana na maelezo uliyopewa na mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu bwana yuko mita 80 toka maji yalipofikia, anaambiwa gharama ni shilingi 464,000 na zaidi. Sasa kwa kweli hili ni tatizo kubwa, lazima wananchi wapate maji kama Serikali inavyokusudia. Serikali ya CCM inafanya kazi kubwa sasa kusitokee watu ambao wanataka faida kubwa kuzuia mafanikio ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yanayotokea Karabagaine yametokea tena vijiji vingine kwa mfano Kijiji cha Burugo, Kata ya Nyakato, hivyohivyo. Hii iko vijijini mradi umekabidhiwa kwa watu wa mjini wa *BUWASA,* matokeo yake gharama inakuwa ni kubwa, hawawezi kuimudu, naomba hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama hizi za kuunganisha maji, kushimba mtaro na kulaza mabomba, kwa nini wananchi wasiruhusiwe kuchimba mitaro wenyewe? Mabomba yanajulikana yapo madukani, kwa nini *BUWASA* isisimamie kama inataka iendelee na huu mradi, isimamie tu uchimbaji wa mtaro wa kutosha, mabomba mazuri *class c*, bei iwe himilivu wananchi wapate maji kama walivyokusudiwa badala ya kupandisha bei wananchi wakashindwa kupata hayo maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine uko pale Kata ya Katoma, maji yamekamilika pale katika Kijiji cha Ilogero, Kijiji cha Kashenge na kwingineko. Lakini kuna vita ya chini kwa chini. Huu mradi umejengwa na *RUWASA,* umekamilika, kazi ni nzuri, maji yako ya kutosha mazuri kwa wananchi. Kuna vita vya ndani kwa ndani, wanataka wauhamishie *BUWASA* mjini. Mradi uko vijijini kwa nini wanapambana kuupeleka mjini, ili wapandishe bei wananchi washindwe kupata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kwa kuomba, kuna mradi mwingine wa Kata sita za Izimbya, Kaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja. Mradi huu umesemwa siku nyingi sana, miaka mingi unasemwa, tunaambiwa hadithi ileile upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Usanifu huu hauishi? Miaka zaidi ya mitatu, minne, tunaambiwa usanifu wa kina na upembuzi yakinifu. Naomba upembuzi ukamilike, usanifu ukamilike mradi uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kuna ziwa Ikimba, maji mengi ya kutosha lakini watu hawawezi kupata maji. Katikati ya hizi Kata sita kuna Ziwa Ikimba, kubwa la kutosha lakini maji hayawezi kuwafikia wananchi kwa sababu ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Tunaomba mradi huu ukamilike nao uanze kujengwa wananchi wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Rweikiza. Sasa namwita Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, wajiandae Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Martha Festo Mariki.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya pekee ambavyo anaisimamia Serikali, kwa namna ambavyo Bunge linapitisha bajeti na yeye anaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri wa Maji na Naibu wake. Sina shaka na vijana hawa kwa sababu ya kazi wanazozifanya ni kielelezo kwa Umma; kwa kweli mnafanya kazi nzuri. Nimpongeze Katibu na Naibu Katibu wake kwa namna ya pekee ambavyo kwa kweli tunashirikana nao vizuri, unapohitaji ufafanuzi mara moja wanakusikiliza. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa *RUWASA, Engineer* Clement Kivegalo, kwa kweli huyu amekuwa ni mtu wa mfano, wakati wote ukimpigia simu *Engineer* Clement anakupokea, wakati wowote ukitaka kwenda ofisini anakuruhusu kwenda. Kwa kweli nakupongeza sana kwa kazi nzuri unayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Miji ya Kisesa, Bujora, Bukandwe pamoja na Bujashi. Kwa kweli hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nikushukuru sana Waziri wa Maji, alipokuja Makamu wa Rais kwa kweli ulisimama kidete kusema kwamba sasa kazi zinaanza. Naomba nikutaarifu kwamba tenki ambalo ulisema linaanza mwezi huu wa tano bado halijaanza. Ninayo matumaini kwamba labda litaanza baadaye kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, hili nikuombe tu kama mradi huu hautakwenda haraka mwaka kesho kitaumana humu ndani ya Bunge. Lazima kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika. Hili nasema kwa sababu nina uhakika kwamba wananchi wale wameteseka siku nyingi na idadi ya watu tayari ni 100,000 kwenye miji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe, nimeona miradi hii kwenye Kata ya Lutale, huu mradi umesanifiwa na unaweza kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 19. Huu mradi ukikamilika unakwenda kutatua changamoto ya vijiji vinane katika kata tatu. Kwa hiyo, niombe sana kwa kweli kama ambavyo umesanifiwa uweze kutekelezwa ili yasiwepo mabadiliko ya usanifu kwa sababu tunapochelewesha miradi hii baadaye kunakuwa na mabadiliko ya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Lugeye, Kigangama ambao umeanza kutekelezwa, kwa kweli huu unakwenda kutatua changamoto kubwa ya Kata za Kitongosima, Nyanguge, Mwamanga pamoja na sehemu ya Kata ya Kahangala. Kwa hiyo niombe sana mkandarasi ameanza, asimamiwe vizuri ili aweze kukamilisha miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, tunao mradi ambao umekamilika Magu Mjini, lakini hamjaufungua. Nikuombe umlete Rais ili aweze kuufungua huu mradi. Umekamilika vizuri, una mapungufu machache. Mwaka jana

mamlaka ya maji iliomba shilingi bilioni moja mkapitisha hapa Bungeni na ipo kwenye bajeti. Tunaomba sasa hiyo shilingi bilioni moja ipelekwe Magu ili vifaa na namna ya kutekeleza vifaa ambayo imebaki iweze kutekelezwa. Kwa sababu akija Mheshimiwa Rais kufungua siyo vizuri wananchi ambao hawajapata maji wakasimama na mabango. Niombe sana jambo hili liweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Waziri, tunayo Tarafa ya Ndagalu yenye Kata tano, vijiji 18 ambayo ina ukame kila mwaka wananchi wanapata shida. Mto Simiyu unapokamilika wananchi wanapata shida kubwa sana ya kuchota maji. Niombe mwaka huu sasa, *Engineer* Clement kwa sababu nakuamini, bahati nzuri Mkurugenzi huyu *Engineer* Clement, hataki miradi midogomidogo, ukienda kwake anakushauri mradi mkubwa ambao unaweza kutatua changamoto ya wananchi wengi, sasa Tarafa hii ya Ndagalu yenye vijiji 18 nikuombe sana Waziri umruhusu Mkurugenzi ili aweze kufanya usanifu na vijiji hivi viweze kupata maji ndipo tutakapo kuwa tumewasaidia wananchi watanzania, ndipo tutakapokuwa tumepunguza magonjwa kwa wananchi wetu lakini pia tutampa heshima Mheshimiwa Rais kwa sababu kazi kubwa anayofanya ni kuhakikisha kwamba na wakina mama anawatua ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi inayoendelea katika Kata ya Mwamabanza, Kata ya Sukuma na Kata ya Uhumbi, miradi hii imebakiza fedha kidogo sana na kwa kweli miradi hii ikikamilika, Tarafa yote ya Itumbili itakuwa na maji ya bomba kwenye kila Kijiji. Kwa hiyo, naomba fedha ambazo zimebaki Wizarani, na wakandarasi wapo asilimia 80, ziweze kuja ili waweze kuikamilisha miradi hii, ikiwezekana kabla ya kuanza mwaka mpya wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Kwa kweli nawapongeza sana Wizara hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango. Sasa namwita Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, jiandae Mheshimiwa Martha Festo Mariki.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Juma Aweso, Waziri wa Maji kwa uwasilishaji wa Bajeti ya 2023/2024, bajeti ambayo ina mipango mikubwa ya kimaendeleo katika kuleta mapinduzi makubwa nchini Tanzania na kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea kufurahia huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanalindi mjini hatuna umasikini wa maji, tuna mradi mkubwa ambao umekamilika uligharimu Shilingi bilioni 33 pale Ng'apa. Mradi ule unazalisha maji kwa siku lita bilioni 7,500,000,000 na matumizi yetu ni bilioni 7,250,000,000. Katika miradi ambayo imekamilika ni mradi wa Tandangongoro, Ncheleweni Ng'apa uliogharimu shilingi 2,800,000,000 na mradi wa Mitoyo, shilingi 3,600,000,000, mradi wa Kiduni wa fedha za *Covid-19* shilingi milioni 600, lakini na miradi mbalimbali ambayo bado inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu wanalindi ni mapinduzi makubwa sana katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kutekeleza miradi hii ya maji na kuwafanya wanalindi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. Hata hivyo, Lindi Mjini pamoja na fedha nyingi zilizotekeleza miradi ya kujenga matenki ya maji na usambazaji wa mabomba, bado tunayo changamoto. Wananchi wetu wanashindwa kuvuta

maji majumbani kwao. Sisi wanalindi tunatamani kuichangia Serikali yetu kwa kulipa bili za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, na nimwombe ndugu yangu Juma Aweso, ninaamini kwamba anaumiza kichwa sana juu ya Manispaa ya Lindi kwa sababu hatujakamilisha kusogeza miundombinu ya maji kwenye mitaa yetu ili wananchi wetu waendelee kuvuta maji majumbani na watumie kadri wanavyoweza kutumia waweze kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imechangia fedha nyingi sana, na tunatamani hizi fedha zirudi zikafanye kazi nyingine za kimaendeleo kuhakikisha kwamba tunaendeleza miradi hii ya maji. Hatuwezi kuchangia kama wananchi wetu hawataweza kuingia kwenye mpango wa kuvuta maji majumbani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kuitazama Lindi kwa jicho la huruma. Katika miradi mipya ambayo tunategemea kwamba inaendelea kutekelezwa, ni mradi wa Ngaza ambao unagharimu fedha shilingi 1,130,000,000. Pia tuna mradi wa Mkundi upande wa pili wa bahari wa shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Jumaa Aweso, asubuhi hapa ametangaza kutuingizia *advance* ya fedha na tumeona zimesoma kwenye *account* za maji. shilingi milioni 100 imekuja Lindi Mjini kuhakikisha kwamba mradi huu Ngaza unaogharimu shilingi 1,130,000,000 unaendelea kutekelezwa. Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana kwa huruma yako na kwa mapenzi yako makubwa ya kuhakikisha kwamba sasa wanalindi tunapata mapinduzi makubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi mkubwa sasa hivi unaotoka Mitero kuelekea Jimbo jirani la Mchinga. Mradi huu unapita Kata ya Mbanja kwa maana ya Mtaa wa Mbanja, Mtaa wa Kipetu, unapita Masasi ya Leo, unapita Likong'o kwa maana ya Kata ya Mbanja, kata ambayo tunategemea kutekeleza mradi mkubwa wa *LNG*. Vile vile mradi huu unakwenda Jimbo jirani la Mchinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, tuhakikishe kwamba mitaa hii niliyoitaja inapata huduma ya maji, kwa sababu hawa ndio walinzi wa mitaro ile iliyopita bomba kubwa la maji lakini walishiriki kuchimba mitaro ya maji kuhakikisha kwamba mabomba yanalazwa na kuelekea katika Jimbo la Mchinga. Maeneo haya yana changamoto kubwa sana ya maji safi na salama. Nina uhakika na usikivu wake mkubwa Mheshimiwa Waziri atahakikisha wananchi hawa wanaendelea kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kila Wilaya anatuletea fedha katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya maji. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, ziko Wilaya zina majimbo zaidi ya mawili. Lindi tuna majimbo matatu; tuna Jimbo la Mtama, tuna Jimbo la Lindi Mjini, na tuna Jimbo la Mchinga kwenye Wilaya moja. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie majimbo haya ambayo kwenye Wilaya moja yana zaidi ya jimbo moja kuhakikisha kwamba fedha hizi anapeleka kila jimbo na siyo kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi mpya ambao tunauombea fedha kwa bajeti hii ambayo tunaipitisha hivi leo. Tuna mradi mkubwa wa maji kutoka Ruaha kwenda Mnazi Mmoja utakaogharimu shilingi 1,229,000,000. Ndugu zetu wa Ruaha wamekuwa na changamoto kubwa ya maji kwa muda mrefu. Hawajawahi kuona hata bomba la maji kule kwenye Mtaa wa Ruaha. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wetu

Jumaa Aweso kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakuja na tunakwenda kuwatekelezea wananchi wa Ruaha Mnazi Mmoja ili waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna upanuzi wa mradi mkubwa ambao tunao kule Kitumbikwela, upande wa pili wa bahari, wananchi kule wanakosa maji safi na salama. Tunajua kwamba tumetengewa fedha za awali za kujenga matenki, Shilingi milioni 800, lakini tunahitaji kusambaza mabomba katika maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wa kule Kitumbikwela, wanaendelea kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo ambayo tunatamani wawe na visima. Wananchi wanaendelea kutaabika kutopata maji safi na salama. Mheshimiwa Naibu Waziri katika safari yake Waziri wa Maji alitoa ahadi ya kutupatia visima vitano Lindi Mjini. Visima hivyo hakuna hata kimoja kilichochimbwa.

*(Hapa kengele ililila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono, nakushukuru sana, nikutakie kila la kheri katika mapinduzi makubwa tunayoyategemea katika Wizara hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kupambania Taifa hili la Tanzania katika nyanja zote kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana napenda kumpongeza Waziri wa Maji pamoja na Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi katika Wizara hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi katika Mji wetu wa Mpanda tuna changamoto kubwa sana ya maji. Ukizingatia Mji wetu wa Mpanda ni mji ambao unakua sana kwa kasi na ongezeko kubwa sana la watu katika Mji wetu wa Mpanda. Katika Mji wetu wa Mpanda na Mkoa wetu wa Katavi, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana wa bandari, lakini changamoto ya maji katika mji huu bado ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Katavi tulikuwa tunaomba, tunafahamu kabisa mwarobaini wa kutatua changamoto katika Mji wetu wa Mpanda na Mkoa wetu wa Katavi ni kutoa maji katika Ziwa Tanganyika na kuyaleta katika Mji wetu wa Mpanda na kuhakikisha kwamba yanasambazwa katika Mkoa wetu wa Katavi. Mheshimiwa Waziri anatambua kabisa mradi huu muhimu utaenda kuikomboa mikoa mitatu, ukiwemo Mkoa wetu wa Katavi, Mkoa wetu wa Kigoma pamoja na Mkoa jirani wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka yote tangu tumeingia hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri amekuwa akituchenga sana kuhusiana na mradi huu. Sasa hivi tuko Bungeni tuna karibu takribani miaka mitatu. Tunataka aje atueleze sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, wananchi wa Mkoa wa Kigoma, na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, ni lini mradi utaanza; na ni lini mradi huu utatekelezwa katika Mkoa wetu ili wananchi waweze kuondokana na kadhia kubwa wanayoipta ya kupata maji yasiyo safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni shahidi, amekuwa akifanya ziara katika Mkoa wetu wa Katavi, ameona changamoto ya maji ni kubwa sana, na Serikali imekuwa ikileta pesa nyingi sana katika Mkoa wetu wa Katavi, lakini pesa hizo zimekuwa hazileti matunda kutokana na kwamba miradi mnayoenda kuielekeza ni miradi ambayo haiendi kuwa endelevu katika Mkoa wetu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2022 tulimwambia Mheshimiwa Waziri, tulikuwa tunaomba kwamba mradi wa Milala usitekelezwe, na badala yake hii pesa ambayo tunakwenda kuielekeza katika mradi ule, ni kwa nini Serikali isiwekeze kitu ambacho kitakuwa ni uhakika, ambapo ni kutoa maji haya kutoka Ziwa Tanganyika ambapo ni takribani kilometa 100 mpaka mji wetu wa Mpanda? Jambo hilo limekuwa kimya. Sasa Mheshimiwa Waziri ni kijana mwenzangu, tunaheshimiana sana. Tunaomba sisi wananchi wa mikoa hii mitatu aje atueleze, mradi huu utawezekana au hauwezekani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa imewezekana kutoa maji katika Ziwa Victoria na kuleta katika Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Shinyanga na sasa hivi mna mpango wa kuleta katika Mkoa wa Dodoma. Nini kinashindikana katika Mkoa wetu wa Katavi, katika Mkoa wetu wa Kigoma na katika Mkoa wetu wa Rukwa?

Mheshimiwa Waziri hapa ni lazima kije kieleweke, utueleze ni lini mradi huu utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kuhusiana na wakandarasi chechefu. Katika Mkoa wetu wa Katavi kuna Wakandarasi ambao kwa kweli wamekuwa wakiwakwamisha sana wananchi wa Mkoa wa Katavi, hususan mama zangu wa Mkoa wa Katavi. Wakandarasi ambao mnawapa miradi ya maji, wengi wamekuwa hawakamilishi miradi hiyo kwa wakati. Hapa nina mifano ya baadhi ya Wakandarasi ambao kwa kweli wamekuwa wakitukwaza sana wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, ni mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji maeneo ya Mishamo eneo la Ifumbulwa. Mkandarasi huyu anaitwa *HAMWA Construction* ana mradi wa thamani ya shilingi milioni 886. Mkandarasi huyu imefikia kipindi mpaka anawatelekeza vijana wale ambao wanafanya vibarua hawalipi, na amekuwa akiwaudhi sana wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuzungumza na watendaji wa maji waweze kushughulika na mkandarasi huyu. Mkandarasi mwingine anaitwa *HAMATEC* mwenye mradi wa zaidi Shilingi milioni 480. Mkandarasi huyu anatekeleza mradi wake katika Kata ya Katuma, Wilaya ya Tanganyika. Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi ni shahidi, Makamu wa Rais alipofanya ziara katika eneo hili alisisitiza kwamba mkandarasi huyu achukuliwe hatua, na mpaka sasa hivi mkandarasi huyo hamjamchukulia hatua, na wananchi wa kata ya Katuma na Wilaya ya Tanganyika mpaka sasa hivi wanashindwa kupata maji. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri naomba watakapokuja kuhitimisha watueleze nini kinakwamisha kumshughulikia Mkandarasi huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi mwingine, ni yule anayekamilisha mradi wake katika eneo la Milala katika Mji wetu wa Mpanda. Zoezi lile limesimama hamna kinachoendelea pale *site*. Mheshimiwa Waziri nakujua wewe ni mchapakazi, naomba ushughulike na wakandarasi hawa wanaokuwekea doa. Tunakujua wewe ni mchapakazi mzuri sana, ila ukiwashughulikia wakandarasi hawa, wananchi wa Mkoa wa Katavi tukapata maji. Hakika tutaiona kazi ambayo unaifanya wewe kama kijana, na vijana wote wa Taifa hili ambao tunakuona wewe kama mfano, tutaamini kweli vijana ukiwapa kazi, inafanyika kwa usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, sisi wananchi wa Katavi hususan ni Jimbo la Kavuu katika Kata ya Majimoto na Kata ya Chamaland. Mji wa Majimoto ni mji ambao unakua sana kutokana na kilimo cha mpunga. Mji huu umekuwa ukiongezeka sana, watu ni wengi wanaoenda kufanya shughuli za kununua mazao katika mji wa maji moto. Mheshimiwa Waziri nakuomba katika Kata hii ya Majimoto, mama zangu wa Mkoa wa Katavi wanaotoka kata hii, tunakuomba uweze kutupatia kisima kimoja kiweze kukaa Kata ya Majimoto na kingine katika Kata ya Chamaland.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ni kengele ya pili.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwakumbusha Wabunge wote kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendesha semina kuhusu Mapitio ya Sera ya Elimu ya Mafunzo ya Mwaka 2014 leo saa 7.00 mchana baada ya Bunge kusitishwa. Kwa hiyo, nawakumbusha tu ili mweze kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka jana wakati ulipoombwa mwongozo wa kiti kutoka kwa Mheshimiwa Chege kuhusu taharuki iliyotokea kutokana na mjadala na mambo yaliyofanywa na Mheshimiwa Waitara Bungeni. Kiti kilitoa mwongozo kwa kutumia kanuni ya 83(1)(c) ambayo nitaisoma. "Mbunge atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu ikiwa atakiuka kanuni hizi kwa namna nyingine yoyote ambayo kwa maoni ya Spika ataona kuwa ni utovu wa nidhamu."

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile Mheshimiwa Waitara hakuwepo Bungeni jana, kiti kilishindwa kutoa na Mwongozo wa kanuni. Sasa leo kwa vile Mheshimiwa Waitara yupo; na mtakumbuka hiki kitendo ni mara ya pili; kuna kipindi Mheshimiwa Waitara alikuwa anachangia, akakiuka maagizo ya kiti, na akakataa maagizo ya kiti, kwa zaidi ya dakika mbili akaendelea na michango yake wakati kiti kilimzimia mpaka *mic*. Vitendo kama hivi, siyo vya kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, humu Bungeni hata ukihama kwenye kiti chako kwenda kwenye kiti cha mtu mwingine, ni kosa. Ni kosa, someni kanuni ya 73. Ukitoka kwenye kiti chako kwenda kiti kingine ni kosa. Hiyo inaitwa kutangatanga ndani ya Bunge. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile Mheshimiwa Waitara yupo Bungeni sasa, kiti kinatoa onyo kwa kutumia kanuni ya

83(2)(a) ambayo inasema, kumwonya Mbunge huyo na kumtaka ajirekebishe kwa matendo ya utovu wa nidhamu.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba, tumeletwa humu na wananchi kuja kuwafanyia kazi. Hasira ni hasara. Unapopambana kwa hasira, hutafanikiwa kuwasaidia wananchi wako. Kwa hiyo sasa, Mheshimiwa Waitara kiti kinakupa onyo na kinakutaka ujirekebishe kwa mujibu wa kanuni ya 83(2)(a).

Waheshimiwa Wabunge, jioni saa 10.00 wataanza, Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Ally Makoa, Mheshimiwa Mwantumu Dau, Mheshimiwa Francis Ndulane, Mheshimiwa Simon Songe.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Alasiri Bunge lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Ally Makoa na Mheshimiwa Mwantumu Dau ajiandae. Mheshimiwa Issa Mtemvu, hayupo? Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu ambae ametupa afya njema na uzima leo tuko hapa tukiendelea kujadili mambo ya maendeleo ya watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kupitia Wizara ya Maji. Tumeona kazi kubwa, Miradi mikubwa ambayo tumeiona katika nchi yetu ikiendelea kujengwa na wananchi wakiendelea kufaidika na maji hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri Aweso, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya usiku na mchana anawahangaikia Watanzania. Naomba nimpongeze Naibu Waziri wa maji Mhandisi Maryprisca nae vilevile anafanya kazi kubwa sana kuzunguka na kuhakikisha matatizo ya maji yanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Katibu Mkuu, Kemikemba, kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha miradi yote na pesa zote zinakwenda kwa ajili ya miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Naibu Katibu Mkuu, Cyprian Luwemeja, kwa Kazi kubwa, tunajua alifanya kazi kubwa sana *DAWASA* na Rais kamuona sasa aje kusaidia wizarani aweze kukimbia na yale aliyoyafanya makubwa *DAWASA* sasa aweze kuyafanya katika miradi yote ya nchi nzima. Naibu Katibu Mkuu, Cyprian, hongera sana kwa kazi kubwa, watanzania tunakutegemea utahangaika kuhakikisha watanzania tunapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Meneja wangu wa Mkoa wa Katavi pamoja na Meneja wa Wilaya, wanafanya kazi kubwa. Lakupendeza zaidi wanapenda kushirikisha, wanashirikisha Wabunge, hakuna kitu wanweza kufanya wao bila kuwashirikisha Wabunge. Ninaomba niwashukuru sana na niwape pongezi kubwa kwa sababu ushirikishwaji ndio unaofanya mambo yanakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze waziri pamoja na Katibu Mkuu, kupitia maelekezo ambayo wamewapa watendaji wao wote katika nchi nzima. Tuseme tu kutokana na maelekezo haya, *Managers* wote wa mikoa pamoja na wilaya tunafanya nao kazi Vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Jimbo langu la Nsimbo, miradi yote ambayo niliyopewa na kama kuna changamoto wananishirikisha kwa ukaribu tunafanya kazi kwa pamoja. Naomba niwapongeze sana Meneja wa Mkoa pamoja na Meneja wa Wilaya, kila jambo lazima wanishirikishe na miradi yote ya Mkoa wetu wa Katavi lazima watushirikishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru hapa karibuni gari limekuja katika Jimbo langu la Nsimbo, visima vimechimbwa. Nilikuwa naomba nishauri, kazi kubwa inafanywa na watendaji na visima vinachimbwa na tumeona mara nyingi visima vingi vikichimbwa vinaachwa muda mrefu. Vinaweza vikakaa hata miezi sita pengine visima vinakaa mwaka mzima.

mhesh ninaomba nitoe ushauri wangu, basi sasa hivi tuchimbe visima kwa sababu wananchi wanaona visima vinachimbwa wanakuwa wana matumaini ya kuwa tunapata maji kesho, lakini hatimaye kile kisima kinakaa muda mrefu, ile hali tena inapungua. Ninaomba nishauri tuchimbe visima, muda huo huo tuvijenge ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. Tusikawie kwa sababu tayari mmeshafanya utafiti, watu wa bonde wamepita wameona na mmekuja kuchimba mmeona maji. Basi tuchukue hatua sasa ya kujenga ili wananchi wale waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Mkoa wa Katavi, suluhisho la maji ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, tupate maji kutoka Ziwa Tanganyika. Kwa sababu yale maji ndiyo yatakayofanya maeneo yetu ya Mkoa wetu wa Katavi wakapata maji safi na salama. Lakini naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri, umesema kuwa tutatumia sasa hivi maziwa, tutatumia mito kuhakikisha watanzania wanapata maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikupongeze sana ili basi hatua hii tuichukue haraka. Tunajua hii miradi ni mikubwa ambayo itachukua muda mrefu ili wananchi waweze kupata maji. Tunakutakia kila la heri kuhakikisha maji haya ya maziwa yanafika sasa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kuhusu miradi mbalimbali mikubwa inayopita katika maeneo yetu. Miradi hii mikubwa inaweza ikapita katika vitongoji na vijiji. Ninaomba sana miradi hii inayopita katika maeneo mbalimbali inasafiri, tunaomba yale maeneo ya vijiji na vitongoji husika ambako mradi ule unapita, wale wananchi waliopitiwa na ule mradi wapate maji. Kwa sababu tunapita wale wananchi wanakuwa hawana maji, matokeo yake uharibifu unatokea. Lakini tukiwapatia maji vitongoji vile vinavyopitiwa na mradi ule pamoja na sehemu nyingine kuna wafugaji, wafugaji wale wanaona bomba lile kubwa limepita na hawana maji, ile mifugo inahangaika matokeo yake wanapasua yale mabomba ili wanyama wale waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kuishauri wizara, tuhakikishe yale maeneo ambayo miradi ile mikubwa inayopita kama kuna wananchi wanaishi pale, kuna mifugo, tujenge mabwawa na wale wananchi waweze kupata maji safi na salama ili ule mradi tuulinde na yale mabomba tuweze kuyalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya mabomba makubwa na viwanda vyetu havitoshelezi. Leo hii ukiwauliza wakandarasi wanakwambia kuwa tuko kwenye foleni tunahitaji mabomba. Kuna miradi mingi mikubwa imechelewa kwa ajili ya malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba, kwa sababu tumekwishaona kuna malighafi mbili, kuna mabomba ya *plastic* na mabomba ya chuma na mabomba yale ya chuma makubwa kupitisha miradi mikubwa mikubwa viwanda vyetu havitoshelezi. Nilikuwa naomba aidha tushawishi wawekezaji waje kwenye nchi yetu wawekeze ili tuweze kupata mabomba kwa ajili ya malighafi au basi tuainishe nchi ambazo tunaweza tukapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja naomba nipongeze kwa kazi kubwa ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na safu yake yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Makoa, Mheshimiwa Mwantum Dau ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyowatendea wananchi wa Jimbo la Kondoa, *especially* kwenye hii sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Kaka yangu Mheshimiwa Aweso Waziri wa Maji, Naibu Waziri, nawashukuru wizara kwa ujumla Katibu Mkuu na watendaji kwa sababu wote hawa ni watu wema sana na ni msaada mkubwa sana katika muda ule ambao tunahitaji huduma kwa ajili ya wananchi wetu. Mungu awabariki awape nguvu waendelee kuchapa kazi na waendelee kuiheshimisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwanza kwa kukubali maombi yetu wana kondoa mjini kuweza kutenga fedha kwa ajili ya miradi yetu ambayo inaendelea. Mradi wa Hachwi, Murua na Mradi wa Bicha pamoja na Mradi mkubwa wa Kondoa Mjini. Pia naishukuru Serikali kwa kuweza kutukamilishia uchimbaji wa visima nane kwenye mitaa nane ambayo kwa kweli natoa pongezi nyingi sana kwa miradi hii na kwa kweli imekamilika, ispokuwa kisima kimoja na ambapo si tatizo la wizara ni tatizo la kule kwetu nadhani tutalifanya vizuri, mkandarasi alipata changamoto kidogo Kisima cha Itiso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali yangu kwa kukubali maombi yetu wana kondoa Mjini, kupanua mradi wetu wa maji Kondoa Mjini kwa ajili ya Mitaa yetu ya Kwapakacha, Mtaa wa Bicha, Tura pamoja na Mitaa ya kichangani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kutenga fedha kwa ajili ya kutuchimibia visima kwenye maeneo matatu, mitaa ambayo kwa kweli ilikuwa haina mradi wa maji ambao ni Mtaa wa Chang'ombe ambao uko Kondoa Mjini maarufu Serengenyi, lakini Mulua pamoja na Mtaa wa Damai. Ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutukubalia maombi yetu sasa wametenga fedha kwa ajili ya kwenda kutoa huduma hiyo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani ni nyingi kwa sababu miradi ni mikubwa sana. Hapa sasa baada ya kuipongeza Serikali ninaushauri wa mambo kama matatu ambayo kwa kweli yakifanyiwa kazi haya yataleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri namba moja; tumekuwa tukichimba hivi visima kama alivyotangulia kusema mwenzangu halafu vinachukua muda mrefu sana. Kwa sababu tunachimba kisima mwaka huu, mwaka ujao tunafanya *designing* lakini mwaka mwingine pengine ndio tunaweza kuanza kuwasambazia wanachi. tumechimba vizima vinane ambavyo kwa kweli wananchi wamepata matumaini kubwa sana lakini mpaka leo hatujaanza kuvisambazia. Visima hivi vipo Chora, Ausia, kwamtwara, Tamkori, Chemchem, Hurumbi, Dumi pamoja na Seria, Munguli na Msoi. Nimeona hapa kuna baadhi ya visima ambavyo tayari vimetengewa fedha kwa ajili ya usambazaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nashauri hapa Serikali, kwa sababu wananchi wana kiu ya maji na wananchi wanapata shida na wanakwenda mbali, Serikali inapopanga

kwenda kuchimba visima basi japo wakati tunasubiria kufanya usambazaji mkubwa ule wa fedha, fedha nyingi kwa ajili ya usambazaji, basi watuwekee japo sehemu moja kwa ajili ya wanachi kuchota maji wakati tukisubiria kuja kusambaziwa, lakini na sehemu moja kwa ajili wananchi kuweza kunywesha mifugo yao. Itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe na miradi ambayo tunafanya *designing and building* kwa wakati mmoja japo tuwe na eneo dogo la wananchi kupata maji. Natolea mfano, kuna huu Mtaa wa Chora, huu wanapakana na hifadhi, wanapokosa maji hasa kipindi cha kiangazi inawalazimu kuingiza ng'ombe kwenye hifadhi. Sasa tunaleta mgogoro kati ya wananchi na hifadhi na wananchi wetu wanaonewa kwa kupigwa faini kubwa hali ya kuwa wanatafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hawa watu wa Hurumbi, wanapakana na Pori hili la Swagaswaga. Kipindi cha kiangazi wanapata sana shida ya maji matokeo yake wanaingiza ng'ombe kwenye hifadhi. Hata hivyo, ni hekima za watu wa pale Swagaswaga wanawaruhusu wakati mwingine kwenda kunywesha kwenye hifadhi lakini hii pia ni mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuwasaidia watu hawa inabidi basi kisima tumechima basi watolewe maji japo wapewe *DP* moja pamoja na eneo la kunywesha mifugo litakuwa linawasaisia, huo ni ushauri wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili; tuna mfuko wa maji ambao unafanya vizuri. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri, juzi wakati tunafuatilia fedha kwa ajili ya mkandarasi wetu wa Kondoa Mjini, tulizungumza mambo mengi na tulikubaliana na nimeona matumaini ndani ya wiki hii. Mungu awabariki sana, maana yake mkandarasio wetu atapata fedha zake na ataendelea na mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna mfuko huu wa maji, ambao kwa kweli kwa nini mfuko huu usingekuwa unapeleka fedha kwa wasimamizi wa huduma moja kwa moja kama wanavyofanya watu wa barabara? Ili kuepuka kuchelewa kuwalipa wakandarasi ambapo sasa hivi mpaka wa-*arise certificate* itembee kwenye ofisi nyingi inachukua muda mrefu wakandarasi wasio na uwezo wanashindwa kumalizia miradi. Tukifanya kama wanavyofanya watu wa barabara, fedha hizi za mfuko wa maji zikaenda kwa wale wasimamizi wa huduma mikoani au wilayani inaweza ikasababisha wakandarasi wakawa wanalipwa kwa wakati na miradi ikakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; ambalo nataka nitoe ushauri kwa Serikali. Kuna changamoto kwenye vile vyombo vya watumiaji wa huduma za maji wanaita *CBWCO*. Unakuta vyombo hivi vinatumia gharama kubwa kuliko makusanyo ambayo yanafanywa na watumiaji wa maji vijijini. Kwa sababu wachangiaji wa vijiji vingi sio wengi sana kitendo ambacho kinafanya mapato yanakuwa madogo matumizi yanakuwa makubwa, tunawalipa mafundi na wanalipa pia wahasibu. Kwa nini Serikali isingeajiri watu hawa ili kupunguza *burden* (mzigo) kwa wananchi ambapo kweli maeneo mengi ambayo wanatumia hiki chombo cha maji wanalipwa, wamekuwa wakishindwa kuendesha miradi kwa sababu makusanyo ni kidogo matumizi ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaombi ambalo Mheshimiwa Waziri, unapaswa ulichukue na ulifanyie kazi. Tunafanya Mradi mkubwa pale Kondoa Mjini na tumeuongezea ukubwa wa takribani bilioni Nne. Kwa sababu Mkandarasi wetu yule ambae tunashukuru mlitupatia mkandarasi mzuri pamoja na changamoto lakini mpaka sasa ameweza kufikia zaidi ya asilimia 72.  Sasa kwa sbabu ukame na hali mbaya ya maji

ilikuwa kwenye Jimbo la kondoa Mjini… ilifikia Waziri Mkuu alikuja…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Makoa, ahsante sana.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa tu na ombi dogo kwamba Mradi huu ukikamilika basi Mheshimiwa Aweso, amlete Waziri Mkuu, auzindue ule Mradi kwa sababu wananchi walipata shida na sasa wana neema kubwa. Ni hilo tu na baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Makoa, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Francis Ndulane na Mheshimiwa Simon Songe, wajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Rahim*, ahsante sana.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya lakini niwashukuru na Wabunge wenzangu pia kwa hali hii hapa nawaona bado wazima na wana afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuanzia kwanza nimpongeze Baba yangu hapo Waziri wangu wa Maji pamoja na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa sana, wanafanya kazi kubwa sana isiyo na kifani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Rais, wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na yeye amefanya kazi kubwa katika Wizara hii ya Maji

hakuna asiyeona na kila anayesimama hapa anampongeza Mheshimiwa Rais, kutokana na kazi aliyoifanya katika Wizara hii ya Maji. Kwa kweli huyu Mama ni mfano, Mwenyezi Mungu ampe hekima, busara, ampe imani azidi kuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha huduma ya maji safi katika Jiji la Dodoma. Mimi ni mkazi wa Dodoma, nimejenga Manispaa ya Makulu, nina nyumba na nina Watoto pale nakaa nao katika kiji kile cha Mkalama. Nyumba yangu imeandikwa namba sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhia hii ya maji katika kijiji changu pale ninachokaa, katika mtaa wangu ninaokaa; ni kadhia kubwa imeingia, na ilifika mpaka kutoa swali la nyongeza hapa na Mheshimiwa Waziri alijibu vizuri tu yakapungua kidogo lakini yameanza kasi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya Mkalama tyana kasi kubwa yanapasua mabomba, maji ya makalama yanapasua maomba yana kasi, na kasi ile yanapopasua yale mabomba basi wewe huna haja ya kutafuta fundi ukasema uende ukampeleke pale azibe mabomba yale, sheria ile watu wa maji kama wako huku juu sijui wamaipata wapi, huna ruhusa ya kwenda kuziba lile bomba, uache yamwagike mpaka waje wenyewe waje wazidi kuyafunga; maana wakija wanayafunga. Kama limepasuka karibu na wewe unakosa maji. Nina changia hili isiwe hii kasi ya maji katika mji wetu pale iwe tena yale maji yapungue kasi, Hapana, yawe na kasi lakini yapunguzwe kidogo angalau yaweze kuingia vizuri na tuyatumie watu wote katika mtaa ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kadhia nyingine katika Chuo cha *UDOM*. Chuo cha *UDOM* mimi nipo hapa Mkalama, Chuo cha *UDOM* pale majasi unapanda juu, ndiko

ninakofanyia mazoezi mie, kila siku asubuhi, ukipita njia ile basi unanikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha *UDOM* hakina maji, watu wanahangaika, wanafunzi wanahangaika, walimu wanahangaika. Mheshimiwa Waziri hili suala analijua lakini mwanangu! Kwamba pale *UDOM* maji hayapatikani, mtoto akivuliwa nepi haiwezi kufuliwa maana maji hana, anafutwa na karatasi anavikwa nepi nyingine; wengine wanyonge, ni maskini hawana kitu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hili suala ulijue, kwamba kule *UDOM* maji hayapatikani

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Mwantumu, Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI**: Muda wangu huo ukipungua atanipa yeye maana nina dakika nane tu hapa.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa.

Ningependa kumpa taarifa mkwe wangu pale sisikitiki sana namuongezea kidogo kwenye hotuba yake ili iweze kukaa vizuri. Tatizo lililokuwepo *UDOM, UDOM* ni karibu na Mkalama anapokaa yeye lakini kuna tatizo la maji. Hili tatizo ni sawasawa na pale Mlimwa C, nje kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu anapata maji ya kutosha, hivi Mheshimiwa Aweso watendaji wako hawaoni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anagombanishwa na majirani zake? Hawaoni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inagombanishwa na wananchi wapiga kula wake?

Haiwezekani kwa Waziri Mkuu maji yapatikane ya uhakika halafu nje maji hayapatikani kwa uhakika na ukifika nyumba ya tatu maji yanatoka yaani nyumba hii maji yanatoka baada ya nyumba nne maji hayatoki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Neema, tayari dakika mbili zimekwisha, Mheshimiwa Mwantumu unapokea hiyo taarifa? *(Makofi)*

**MHE. MWANTUMU D. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu utanilindia usije ukaninyima kidogo, na hiyo taarifa aliyoitoa mama yangu hapo mimi naiunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UDOM* maji hayapatikani. ninakwenda kwenye mazoezi watoto wanasikitika, hawanijui kwamba mimi ni Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wananiona mimi ni kama mama yao tu, lakini mie yale maneno wanayosema mimi naya-*note* leo ninayatoa hapa wakisikia watasema kumbe yule mama Mbunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasikitika hakuna maji kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba chonde chonde fanya kazi muhimu ili maji yapatikane katika Chuo cha *UDOM* ili watoto wetu waweze kuyatumia maji ya *UDOM*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, kuna mpango hivi sasa wa wezi, wanaingia majumbani wanafungua mabomba tulisharushiwa mpaka kwenye mitandao. Likitoka bomba maji huna ruhusa ya kutoka ukitoka unapingwa nyundo kali unaanguka wanaingia ndani wanaiba hiyo ndio staili yao waliyokuja nayo majambazi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naliomba hili nalo lichukuliwe nba litiliwe maanani. Serikali yangu ifanye kazi kwa hawa majangili wanaopita katika nyumba kwenda kutuhujumu ndani ya nyumba zetu; hili suala nalo lifanyiwe kazi; na Mlimwa C nalo Mheshimiwa Waziri uende ukalifanyie kazi maji yapatikane. Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye apate maji atumie kwa vizuri na mama nyumbani lakini na wananchi wake waliokuweko pale wapate maji watumie na wao ili wapate kufanya kazi ya Chama cha Mapinduzi. (makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana baba piga kazi *big up*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau, tunaendelea na Mheshimiwa Francis Ndulane, Mheshimiwa Simon Songe Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na Mheshimiwa Issa Mtemvu, wajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali yetu ya awamu ya sita kwa kazi kubwa ambayo imekuwa ikiifanya katika kuhakikisha kwamba inamtua mama ndoo kichwani. Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri rafiki yangu bwana Aweso pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya. Nakumbuka wamepita hadi kwenye jimbo langu mara kadhaa kwa ajili ya kuhimiza na kuisimamia miradi ya maendeleo ya sekta hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kuanza kuchangia kwa kupongeza zaidi Serikali kwa sababu ndani ya miaka mitatu iliyopita imewekeza zaidi ya shilingi bilioni tano katika Wilaya yetu ya Kilwa yenye vijiji tisini, na tayari miradi

katika vijiji vinne tayari imekamilika; maji yanamwagika katika Kijiji cha Chapita, Chumo, Likawage pamoja na Somanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo miradi ambayo ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji ikiwemo uchimbaji wa visima pamoja na kuweka mtandao wa mabomba katika Vijiji vya Marendego, Nasaya, Masaninga, Kisima Mkika Zinga Kibaoni, Matandu, Hoteli Tatu, Mbwemkulu, Nainokwe, Kipimbimbi, Kilwa Masoko, Kikole, Nakiu, Kilwa Kisiwani, Hoteli Tatu pamoja Nakinjumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna maeneo ya vijiji 32 kati ya vijiji 90 bado vina changamoto kubwa ya maji na bado havijafikiwa na mtandao wa maji wa *RUWASA*. Nitavitaja baadhi ya vijiji; kipo kijji cha sehemu fulani za baadhi ya vitongoji vya Zinga Kibaoni. Pia vipo vijiji Vya Ngalambi; Lienga Kijiji cha Namatewa; Mwengei; Pungutini pamoja na Nandete, Nandembo pamoja na vijiji vingine, kama nilivyosema vijiji 32 kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa hapa napitia ukurasa wa 55, 56 kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na majedwali ya miradi ya maendeleo ambayo inakwenda kutekelezwa katika mwaka huu ujao. Nimeona pale katika ukursa huu wa 55, 56 amehimiza kuhusu uwepo wa miradi ambayo itatokana navyanzo vikubwa vya maji ile miradi ya kimkakati ikiwemo mradi wa maji kutoka mto Rufiji. Lakini pia nimeenda mbele zaidi ukurusa wa 111 katika yale majedwali yanayofafanua kuhusu miradi ya maendeleo, nimekuta Kilwa pamoja na Wilaya ya Lindi mkoani Lindi imeeleza kwamba tutapata maji kutoka kwenye Mto Rufiji vijiji viwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitanabaishe hapa; kutoka *main stream* ya Mto Rufiji ni kilometa 52 mnalikuta jimbo

langu, yaani ni mpaka wa Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Lindi. Lakini pia uipita njia ya mkato kama unataka kwenda Kipatimu unatembea kilometa 47 tu unakuta tayari umeingia katika jimbo langu Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inanishangaza kidogo, au sijui kuna *typing error* kuona mradi huu utatambaa kutoka Mto Rufiji utakwenda mpaka Kilwa mpaka Wilaya ya Lindi lakini utagusa vijiji viwili tu. Nafikiri hii haiko sawasawa. Na kwa mujibu wa maelezo yao kwenye yale majedwali wanasema wananchi wa vijiji viwili wapatao elfu hamsini laki tisa arobaini na nne watanufaika na mradi huu wa maji ya Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka kidogo vijiji viwili kuwa na wananchi 50,000 kwa. Kwa hiyo naomba, kwanza hizi takwimu zikapitiwe upya ili kuona *accuracy* ya hivyo vijiji ambavyo vimezungumzwa hapa. Lakini, vijiji viwili ni vichache kwa umbali ambao bomba litatambaa. Na kwa kutokana na ukubwa wa tatizo nimeshasema hapa ni vijiji 32 bado vya Wilaya ya Kilwa havina maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo ningeomba Mheshimiwa Waziri wakafanye *review* katika utekelezaji wa mradi kutoka mto Rufiji ili ikiwezekana angalau mkazo hivu vijiji vyetu 32 ambavyo havina uhakika wa maji. Kwa sababu nina hakika chanzo cha uhakika cha kuweza kututoa kwenye tatizo hili la maji ni hiki cha Mto Rufiji. Na kama nilivyosema mwanzo, ni kiasi cha bilioni tano tu zimetengwa, na miradi ya kiasi cha bilioni 1.4 ndiyo ambayo imekamilika kwa miaka hii mitatu. Kwa hiyo tunahitaji sana maji kutoka Mto Rufiji ili yaweze kumaliza changamoto ya maji katika Wilaya ya Kilwa. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji na kumuongezea, kwamba maji ya Mto Rufiji yanahitajika sana kwenye Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla, tunahitaji maji kutoka Mto Rufiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis unapokea hiyo taarifa?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea kwa asilimia 100. Wiki moja iliyopita tulipewa taarifa hapa na Wizara, kwamba Wizara pamoja na kutekeleza huu mradi kwa vijiji viwili vya Wilaya za Kilwa na Lindi pia watatengeneza mabomba mawili kupitia njia ya Mkuranga na Kisarawe ili yapeleke maji Dar es salaam. Lakini tunaona uwekezaji wa kuelekea Dar es salaam ni mkubwa sana. Ni kwa nini uwekezaji kama huo usifanyike kwa mikoa ya Kusini kama alivyozungumza mwenzangu Mheshimiwa Kuchauka? Kwa hiyo niseme tu kwamba tunahitaji nguvu kubwa ielekezwe katika wilaya za Mkoa wa Lindi za Kilwa, Lindi vijijini, Lindi Mjini pamoja na Liwale kwa kuanzia ili wananchi wetu waweze kupata hii huduma ya maji safi na salama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Simon Songe, Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mheshimiwa Issa Mtemvu Mheshimiwa Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Wizara Maji. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya katika kuhakikisha kwamba sehemu nyingi zinaanza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Aweso kwa kazi kubwa anazofanya, anayaishi yale maneno yake ambayo amekuwa akiyazungumza kila siku. Pongezi hizo ziende pia kwa Naibu Waziri kwa kazi wanazofanya pamoja na kwenye Ofisi ya Katibu Mkuu na wasaidizi wake. Kipekee nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu wa *RUWASA* Bwana Clement kwa kazi kubwa anazofanya kuhakikisha kwamba anawasimamia mameneja wa mikoa na kuleta matokeo chanya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nimpongeze sana dada yetu *Engineer* Miriam Meneja wa Mkoa wa Simiyu kwa kazi kubwa anazofanya. Kwa kweli anatupa heshima kubwa sana kuhakikisha kwamba sehemu kubwa tunaendelea kupata maji pamoja na Meneja wangu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jambo kubwa alilofanya kuhakikisha kwamba wanaleta magari ya kuchimba visima katika mikoa yetu. Leo hapa naomba sasa nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba tumepokea gari katika Mkoa wa Simiyu tuneomba hizi gari sasa zikalete matokeo chanya kwa Watanzania. Tusinunue gari kuja kuzi-*park,* hakikisheni mnapanga bajeti kwa ajili ya kuendeleza gari hizi kwa ajili ya mitambo hii ambayo sasa tumeinunua na kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kuchimba visima. Tunataka wilaya zetu tuchimbe visima kwenye vijiji ambavyo nina shida ya maji. Kwa mfano pale Busega tunataka tuchimbe visima kwenye Kata za Shigala, Kata ya Igerukilo, Malili, Imalamate na Ngasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunaomba sasa gari hii itengewe bajeti ili iweze kufanya kazi. Kwa sasa tumeletewa lakini bado haijatengewa bajeti ya kuiendesha gari hii; na ili liende katika mikoa yote. Tutengenezee hivi sasa bajeti ili gari hzi ziweze kufanya kazi. Kila mkoa tupeleke bajeti kufanya kazi. Mfano tupeleke bajeti za mabomba na mafuta ili hizi gari sasa zilete tija kwa Watanzania na kwa kuleta tija ambayo Mheshimiwa Rais anaitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie jambo moja ambalo kila siku tumekuwa tukipata ahadi hapa. Mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mkoa wote wa Simiyu. Suluhisho kubwa Mheshimiwa Waziri hapa katika Mkoa wetu wa Simiyu ni mradi mkubwa wa Ziwa Victoria ambao utaanzia Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu. Mradi huu ndilo suluhisho la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nimekaa hapa Bungeni mwaka huu ni wa tatu napitisha bajeti, kila mwaka mnaandika kilekile kwenye bajeti. Mwaka 2021/2022 mliandika kilekile, mradi huu utaanza mwaka huu na haukuanza. Lakini bado 2021/2022 mkaandika hivyo hivyo na haukuanza mradi huu. Sasa hivi nimesoma hapa mmeandika hivyo hivyo na mradi sujui kama utaanza. Ninaomba sasa tuchukulie maanani katika mradi huu uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikukumbushe, mimi nimeuliza maswali mawili hapa kwenye huu mradi; mwezi Aprili, 2021 niliuza swali nilijibiwa hivi naomba ninukuu majibu yalikuwa hivi kwenye huu mradi; "Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi utaanza mwezi Agosti, 2021 na miji mikuu ya wilaya itakayonufaika ni Busega, Bariadi, Itilima Maswa na Meatu na vijiji vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu umbaliwa kilomita 12 kila upande. Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa miaka minne."

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni miaka miwili imeshamalizika na huu mradi haujaanza. Sasa nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapa niliuliza mwezi Februari, 2022 swali hili hili kwenye mradi huu huu. Majibu yalikuwa hivi, ninanukuu; "Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Nikiri maelekezo ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ni kutumia rasilimali toshelevu ikiwemo moto pamoja na maziwa kuhakikisha kuwa matatizo ya maji yanamalizika. Tumepata fedha naomba nirudie hapa tumepata fedha bilioni 400 kwa ajili ya kutumia Ziwa Victoria na kutatua tatizo la maji Mkoa wa Simiyu ikiwemo Busega, Bariadi na Itilima. Kwa hiyo mkakati wa Serikali sasa hivi tupo hatua ya kumpata mkandarasi na tupo hatua za mwisho. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi atapatikana mapema na kwa wakati ili utekelezaji wa mradi huu uanze mara moja."

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni mwaka na nusu nini maana yake? Lazima tuwe *serious* na kazi hii ambayo tunataka wananchi wetu tuone wanapata. Tunatamani wananchi wapate maji. Lakini bado, katika mwaka huu wa fedha inaandikwa tena hivi; ninanukuu; "Hadi mwezi Aprili 2023 kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kimetumika kulipa fidia kwa wananchi. Aidha taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi zinaendelea na utekelezaji unatarajiwa kuanza katika mwaka 2023/2024".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Habari ya mkandarasi itaisha lini? Kwa sababu kila mwaka ni mkandarasi kila mwaka ni mkandarasi Mheshimiwa Waziri mimi shilingi yako nakimbia nayo Busega, naomba kesho ukisimama utupe *commitment* ya Serikali kwenye huu mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria wa Mkoa wa Simiyu tunatamani wananchi wa Mkoa wa Simiyu tuondokane na tatizo la maji. Ni aibu leo kuzungumza Busega

haina maji wakati kata ya mwisho kwa umbali ni kilometa 42 haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha kesho atupe *commitment* ya Serikali, haya maneno yaliyoandikwa hapa yaliandikwa 2021 yaliandikwa 2022 yameandikwa 2023 leo tunataka *commitment* ya Serikali ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama kupitia Mradi wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka nichangie kwa Wizara ya Maji ni kuhusu wakandarasi. Sasa hivi wakandarasi wanalaamika hawajalipwa fedha. Sasa ni muda ambao tunatakiwa tutafakari tunapoingia kufanya kazi na wakandarasi tuhakikishe kwamba fedha zipo, wanapo-*raise certificate* tuwalipe kwa wakati ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni muda mrefu wakandarasi wetu wa miradi ya maji, miradi ya barabara hawajalipwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aangalie wakandarasi wake awalipe ili waweze kufanya kazi, kwa sababu kama hawatalipwa kwa wakati, tuta-*raise* riba, tuta-*raise* kucheleweshwa kwa kazi za wakandarasi. Ili kazi za wakandarasi zimalizike kwa wakati na ili wananchi wanufaike na miradi hii, ni lazima miradi hii imalizike kwa wakati. Ikiwemo kuwalipa wakandarasi kwa wakati ili waweze kufanya kazi ambazo tumewapa. Bila kuwalipa kwa wakati kwanza kunawarudisha nyuma, kunachelewesha miradi, kunaongeza gharama za miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na–*declare interest* kwamba niko Kamati ya *PAC,* kila miradi inaongezeka gharama zake kwa sababu ya kuchelewesha kuwalipa na tatizo hili sasa limeanza. Wakandarasi huko *site* wanalalamika, wengine

wameshafikisha asilimia 75 za miradi, asilimia 80 lakini wamesimama kwa sababu hawajalipwa fedha zao. Ni wakati muafaka sasa tuweze kuwalipa ili wafanye kazi ambazo tumewapa na kuwatuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa, maana bado nina muda dakika mbili naziona hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maji jioni hii. Kwanza nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza ndoto yake ya vitendo kwa kumtua mama ndoo kichwani kwa kupitia Serikali yake anayoongoza ya Awamu ya Sita, tumpigie makofi kwa wingi Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwapongeze Wizara ya Maji, kaka yetu Juma Aweso, lakini pia na Naibu Waziri Mheshimiwa Mahundi, Katibu Mkuu ambaye aliteuliwa hivi karibuni *Engineer* Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu ambaye alikuwa Mtendaji Mkuu wa *DAWASA* Luhemeja, lakini pia na wasaidizi wao wote wakiwepo Katibu wa Waziri Ndugu Gibson ambaye anaendelea kutupa sana ushirikiano na pia Mkurugenzi wa Mamlaka Maji, *CPA* Grace Msiru naye anatupa sana ushirikiano.

Kiukweli niwapongeza kama Wizara wanatupa ushirikiano mkubwa. Wasituchoke waendelee kutuvumilia, sisi siasa zetu zinabebwa na maji. Kwa hiyo, kwa kiwango kikubwa sana Wizara hii tunaitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowapongeza *RUWASA* Mkoa wa Tabora ambayo iko chini ya Mhandisi Kapufi, lakini pia Mamlaka ya Maja Igunga (*IGUWASA)* ipo chini ya Mtendaji Mkuu, ambaye tunamwita Murugenzi Mkuu pale Mhandisi Humphrey, lakini pia na Mamlaka ya Maji ya Vijijini Igunga *RUWASA* iko chini ya Meneja wetu pale anaitwa Mulaza. Wanatupa ushirikiano mkubwa kwa kweli, wanaendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa Ilani yetu kuhakikisha tunapeleka maji vijijini na mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni hii sitakuwa na mambo mengi sana ya kuchangia, lakini nina mambo takribani mawili, moja ni shukrani, lakini pia na mradi mkubwa ambao ningependa kuusemea ambao ningeomba Wizara wausimamie kwa makini kuhakikisha unakamilika. Mwaka jana walitupatia mradi mkubwa sana wa maji kwa kutumia maombi maalum wa kwenda Kijiji fulani kinaitwa Mwamashimba, ni takribani kilometa 45 kutoka Igunga Mjini kule ndio chimbuko langu mimi kama Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakunywa maji kutoka kwenye kitu tunaita *malonga*, mnachimba maji, mnatumia ng'ombe na binadamu. Tunashukuru tulileta *special request* Wizara, walitupatia fedha takribani milioni 800, ule mradi umekamilika na sasa tunapata maji. Tunashukuru sana kwa moyo wao wa upendo waliotujalia Wanaigunga. Pia nishukuru Mamlaka ya Mji Mdogo pale Igunga walitupatia fedha takribani bilioni 1.8 kwa ajili ya mradi wa maji taka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wetu wa Igunga unakuwa sana, ni moja ya miji inayokuwa kwa kasi na ni mji wa kijanja, biashara ni kubwa. Kwa hiyo tumepata mradi wa maji safi na maji taka pale, tunawashukuru Wizara kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi, nimpongeze Waziri, wamekuwa wasikilizaji wazuri wa maoni ya Wabunge. Mwaka jana moja ya eneo ambalo pia nililichangia sana ni suala la kubadilisha utaratibu wa manunuzi kwa Mamlaka ya Vijijini *RUWASA*. Nimeona hivi karibuni kuna taarifa ya Waziri inatembea, inasema kwamba wameruhusu manunuzi kwenda mpaka ngazi za mkoa kwa Mamlaka ya Maji *RUWASA*. Hongera sana kwa Wizara kwa hili wametusaidia, kwa sababu tulikuwa tukikwama, tulikuwa tunatoa mifano kwamba inahitajika hata *motor* ya milioni tatu, milioni nne, lakini idhini mpaka itoke Wizarani. Sasa wameamua kulishusha mpaka ngazi ya mikoa, naamini litaongeza ufanisi na miradi mingi itakwenda kwa wakati. Hongera sana kwa Wizara waendelee kufanya kazi kwa bidii wamsaidie Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi miwili ambayo tunategemea kwa mwaka huu wa fedha pale Igunga. Kwa Mamlaka ya Maji ya Mjini kwa maana *IGUWASA* kuna mradi mmoja unahitaji milioni 840. Tunafanya upanuzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka sehemu moja inaitwa Makomero kwenda Mgongolo. Kwa hiyo tunapitisha bajeti ya Waziri na naiunga mkono kwa asilimia 100 ili niweze kupata hizi fedha, tukakamilishe huu mradi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa pili pale wa kufanya maboresho. Tuna chanzo kimoja cha Bwawa la Bulenya ambapo tumeomba milioni 521. Naamini pia kwa kuwa naenda kuunga mkono hii bajeti kwa asilimia mia moja, basi na zenyewe tutazipata kupitia Mkurugenzi wa Mamlaka za Maji,

Ndugu Joyce ili tuweze kukimbizana tuweze kuendelea kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kuchangia jioni hii pale tuna mradi mmoja wa *RUWASA* ambao ni wa bilioni 20. Kuna kampuni moja inaitwa *Help Desk Engineering,* naona wapo *site* na wameshasaini nao mkataba lakini spidi yao sio nzuri sana. Naamini Mheshimiwa Waziri hili watalifanyia kazi, tusirudi kule kwenye ile miradi chechefu ambayo walipambana nayo takribani kwa miaka miwili. Haya makampuni au hawa wakandarasi ndio watamfelisha Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, ajitahidi kuwa makini. Tunapotoa ushauri kwa kuwa anaupokea, mimi ningeshauri kitu kimoja, aweke utaratibu kupitia Kitengo chao cha *Monitoring and Evaluation* Wizarani. Wanatoa mkataba, mkandarasi akipewa mkataba ndani ya miezi mitatu hajaanza kufanya utekelezaji kwa kiwango wanachoridhika nacho, wavunje mkataba, watoe tenda upya ili tuweze kwenda kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyeyere aliwahi aliwahi kusema; "*we must run while others are walking*", kwa lugha nyepesi ya Kiswahili ni kwamba lazima tukimbie wakati wengine wanatembea. Tunaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu, siasa yetu inabebwa na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus Ngassa. Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Stella Fiyao wajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Fungu 49 - Wizara ya Maji ya Ndugu yangu *Comrade* Aweso. Nisiwe mchoyo wa fadhila ya kuwapongeza sana. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kufanya na ni ukweli Wananchi wa Kibamba wanajua kabisa kazi kubwa ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais kwenye Jimbo letu la Kibamba. Ni kwa sababu maelekezo yake pia yanapokelewa vizuri na hawa ndugu zetu ambao wanatafsiri maelekezo, Ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, Waziri na Naibu wake, dada yangu Mheshimiwa Maryprisca Mahundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema, mwishoni kwenye shukrani. Sasa anayo timu nzuri hapo Wizarani, sina shaka kabisa juu ya Katibu Mkuu, Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Cyrpian Luhemeja, kaka yangu anao wasaidizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni shuhuda nimekwenda ofisini kwa Waziri mara nyingi na nyingine ambayo amenikutanisha na menejimenti yake yote juu ya changamoto ya Jimbo za Kibamba, lakini leo nieleze kidogo juu ya mafanikio ya Mheshimiwa Rais katika miaka yake miwili. Naingia hapa Jimbo la Kibamba lina changamoto chini ya asilimia 30 maji wanayapata, kabisa. Wananchi wengi hawana maji, wanapatapata maji pale barabarani, kwenye matanki makubwa Luguruni kwenye mita 20 au 30, lakini leo ninavyozungumza tayari Mheshimiwa Rais alikubali kilio changu humu ndani cha kujenga Tanki la Mshikamano kwa bilioni 5.4, lakini alitumia fedha za UVIKO bilioni 2.5 akazileta. Katika zile bilioni 139, bilioni 2.5 akasema mpeni Kibamba hata tanki lake la Mshikamano liweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tanki limeshajengwa limezinduliwa na wananchi wanaendelea kuunganishiwa maji, lakini pongezi nyingine kwa Mheshimiwa Rais, upo mradi wa zaidi ya bilioni 65 kutoka *World Bank*. Mradi wa chuo kikuu kuelekea Bagamoyo, lakini tumefaidika na tanki la Tegeta *A*, ujazo wa tanki ile milioni tano, tayari tanki limekamilika. Wananchi wa Goba yote wanaendelea kuunganishiwa maji. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, sana kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo mimi na Waziri hata jana nilimwomba niende na akanialika kwenye menejementi yake yote, yote kueleza changamoto mbili ambazo nijue kama amezifanyia kazi au bado. Moja ni wananchi wetu wa Msumi, Kata ya Mbezi, wananchi hawa ni wengi, ndio Jimbo lile lina watu 650,000, jimbo la tano Tanzania nzima kuwa idadi ya watu na wananchi ni wengi kweli, lakin hawana hata chanzo cha maji. Nimshukuru kwa majibu aliyonipa. Tayari wameelekeza fedha katika matanki mawili ya Mshikamano na Tanki la Tegeta *A* kuunganisha nguvu ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ili watengeneze matanki mawili ya bilioni 13.6. Nawashukuru sana. Najua sasa wananchi wa Mbezi, eneo la Msumi lote linaenda kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho lenye changamoto ni King'azi *A*, nimezungumza hapa miaka miwili mfululizo kwenye *Hansard* ipo. Niliwahi kusema viongozi watapigwa mawe humu, lakini leo Waziri amenipa majibu. Katika eneo lile kuna eneo linaitwa Bangalo Kilimahewa, eneo la kwao, watu wa *DAWASA,* sasa hivi wanaelekeza bilioni 42 pale. Sasa faida yake nini? Mradi mkubwa chini ya Benki ya Dunia, wananchi wa Kibamba, King'azi A na B wanaenda kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wananchi wa Bangulo, Kinyerezi Jimbo la dada yangu, lakini kuna wananchi wa Kinyerezi, Majohe, Pugu Kipunguni, Ukonga, tunaona mradi mkubwa unaenda kuwasaidia watu wa Dar es Salaam, wananchi wa majimbo matatu. Nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Aweso, sina sababu ya kusema mengine, ni kumpongeza kama kijana, anaendelea kuonesha vijana wakipewa nafasi wanavyoweza kufanya kazi. Nampa pongezi sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli katika muda nilionao baada ya hilo, Mheshimiwa Waziri taarifa yake yote kwa nafasi aliyonayo eneo lake ni maji safi na majitaka, lakini eneo hilo la majitaka halizungumzi vizuri sana kwenye taarifa zake kwa nyakati zote. Najua wameelekeza mitambo mizuri ya kubebea uchafu ule katika maeneo machache, lakini nimwambie takwimu zinavyosema kwenye taarifa yake, kwamba mpaka sasa ana kilometa 1,385 kwa mwaka uliopita mpaka sasa hivi 1,416. Huo ndio mtandao wa kilometa za maeneo za maji taka, lakini ameweza kuwaunganishia wateja 53,000… *(Makofi)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa Saashisha.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa kaka yangu taarifa tu kwamba, ni kweli eneo hili la maji taka limesahaulika. Hapo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna eneo wanamwaga majitaka, eneo la Swaswa. Serikali imejenga barabara nzuri mbele na nyuma na majumba yamejengwa mazuri ya ghorofa, lakini yale majitaka usiku yanatoa harufu kali, hawayatibu vizuri. Kwa hiyo, nilikuwa

nampa taarifa kwamba ni kweli, watazame na eneo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea na mchango wangu eneo hili, inawezekana ni gharama sana, sijui lakini niwashauri kwa sasa. Kwa sensa ya mwaka 2020, tumefikia takribani watu milioni sita ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, majumba mengi yamejengwa ya maghorofa Kariakoo na maeneo mengine, lakini ukweli miundombinu ya majitaka haijawekwa vizuri. Sasa niwashauri kwa sababu nyumba nyingi za Kariakoo zinajiunganishia katika mifumo ya maji taka katika mifereji ya majisafi, kwa hiyo ni changamoto, lakini kuna eneo lingine ni mfumo wa majitaka usiotumia chemba, jinsi unavyofanya kazi. Wanaweza kutoa elimu hii kwa watu wengi sasa hivi wanavyojenga, wajenge mifumo ile ya maji taka ambayo haihitaji kutumia chemba inaweza pia ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuna jambo hili ni changamoto sana, taka ngumu pia kutupwa kwenye vyanzo vya maji. Dar es Salaam hii hali mbaya na sasa niwaambie kipindupindu kimeanza kuingia, yote hii ni kwa sababu hatujajielekeza vizuri. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri achukuea na wataalam wake, eneo hili la kwake la pili, nashangaa sana hizi Wizara, nitakuja kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inakaa kwenye ardhi, makazi inaacha. Hili la kwake la maji na mambo ya taka, maji yuko vizuri, taka anaziacha. Ajielekeze huko vizuri, najua ameanza lakini aongeze nguvu, nina imani sana atafanikiwa kama alivyofanikiwa kwenye maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Maji kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu. Nilimtaja Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Sebastian Kapufi, ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kwanza kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja leo nilikuwa nauguza Muhimbili, lakini nikaona Wizara hii isinipite kwa sababu wananchi wa Simanjiro walinituma niseme maneno, nitakayoyasema. La kwanza, ni kuridhika kwa wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kwa kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba mradi mkubwa wa maji ambao sijui naweza kusema sijui ni mradi wa kielelezo, wa kimkakati ambao ulibuniwa na Hayati Edward Moringe Sokoine mwaka 1974 alipokuwa akimkaribisha Hayati Rashid Mfaume Kawawa kuzindua Wilaya ya Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa mmoja wa vijana chipukizi waliokuwepo wakati wilaya ile ilipokuwa inazinduliwa. Hayati Edward Moringe Sokoine alisema pamoja na kwamba Kiteto hakuna maji pale Kibaya ambalo tatizo liko mpaka leo, Makao Makuu ya Wilaya yatajengwa Orkesumet na tutachukua maji kutoka Mto Ruvu, kilometa 45 mpaka 50 kuleta Makao Makuu ya Wilaya ya sasa ya Simanjiro ambayo ni Orkesumet. Mradi huu umetekelezwa na uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa vitendo na umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana ya maji, Mheshimiwa Juma Aweso, wananchi wanamshukuru, wanampongeza kwa kazi nzuri kubwa aliyotufanyia. Wanampongeza kwa sababu yeye mwenyewe kwa kipindi cha Uwaziri wake, mimi nikiwa Mbunge katika kipindi hiki, amekuja pale zaidi ya mara sita, akihakikisha kwamba ule mradi unakamilika. Mara zote alipofika tuliona mabadiliko makubwa ya kukidhi kiu ya wananchi wa Jimbo la Simanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie kwamba kazi inayofanywa na Mheshimiwa Waziri Aweso ni kazi ya kupigiwa mfano, ni kijana mnyenyekevu, kijana muadilifu, kijana mchapakazi na ni kijana anayejishusha. Natamani viongozi wote wa CCM tungeiga mfano wa Mheshimiwa Juma Aweso ambaye hanyanyui mabega, siku zote yuko *down*. Nalisema hili kwa sababu si sifa njema sana kwa kiongozi kwamba Mungu amekupa madaraka ukiwa na umri mdogo, lakini unasahau kwamba wewe una umri mdogo hata kama una madaraka makubwa, lakini Mheshimiwa Aweso anajua nafasi yake katika jamii hasa akiwakuta waliomzidi umri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais amempa Naibu Waziri mzuri, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, anafanya kazi nzuri sana kwa kushirikana naye. Katibu Mkuu wa kupigiwa mfano, dada yangu Nadhifa Kemikimba, tangu amekulia kwenye Wizara ya Maji, nilimjua akiwa Mkurugenzi, nikamjua akiwa Naibu Katibu Mkuu amekuja kuwa Katibu Mkuu. Leo Wizara ile imekamatwa na viongozi ambao kwa kweli wanajua wajibu wao, wanawajibika vizuri na ni viongozi waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema leo kwamba, moja kati ya sifa ya kiongozi ni uadilifu na ndio maana huwezi kutenganisha uongozi wa umma na maadili kwa sababu sifa mojawapo ya kiongozi ni uadilifu. Kwa mafanikio haya

tunayoyaona yanatokana na kazi nzuri ya uadilifu wa wale waliopewa dhamana katika Wizara husika. Kwa hiyo, nataka niwashukuru kwa mradi huo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa pia wa pili ambao ni wa Mji wa Arusha ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Mji wa Arusha chini ya *Engineer* Rujomba pamoja na Mwenyekiti wake Dkt. Masika na Mheshimiwa Balozi Ole-Njoolay. Mradi ule Mheshimiwa Rais alielekeza maji yale yaletwe Mererani, yapelekwe kwenye Kata ya Endiamtu, yapelekwe kwenye maeneo mengine yanayozunguka Mji wa Mererani ambayo ni Kata ya Shambarai, Kata ya Naisinyai na Kata ya Oljoro Namba 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake. Nimesema nawapongeza na ndio hasa furaha yangu iliyopo leo na mengine nitaomba tu kwa unyenyekevu. Maelekezo ya Rais kupeleka maji katika maeneo haya niliyoyataja ni kwa sababu maji yaliyoko pale yana *fluoride* kubwa na yanapelekea watoto kupinda miguu na wengine meno kuoza, ukiwaona unaona meno ya watu ni mekundu na siyo hapo tu na Kata ya Msitu wa Tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuwa na maji ambayo watu wetu wanapinda miguu katika kizazi hiki siyo sifa njema kwa Serikali ambayo Rais wake anatafuta fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya watu. Kwa hiyo niendelee kumwomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yake watupie macho yao tena katika maeneo haya. Siyo kwamba sitambui miradi aliyonisaidia ambayo Wizara yake chini ya *RUWASA,* nampongeza sana Meneja wangu wa *RUWASA* wa Mkoa, Ndugu yangu Walter Kirita na Ndugu yangu Johanes *Engineer* wa *RUWASA,* Simanjiro ambaye kwa kweli nasema amekaa akikaimu nafasi ile kwa muda mrefu na amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ningeomba sana amfikirie, apitie tena muda aliokaimu na kazi nzuri aliyoifanya ikimpendeza amthibitishe, amefanya kazi nzuri Johanes, kazi ambayo ni ya mfano. Hakuna Diwani leo ambaye hamsifu kwenye halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekumbuka miradi ambayo Serikali ya Mama Samia imetusaidia sana. Wananchi wa Terrat wana furaha kwa sababu ya Mama Samia, wananchi wa Engonongoi wana furaha kwa sababu ya Mama Samia, wananchi wa Endonyongijape, Naberera, Okutu na Lemeshuko wana matumaini kwamba katika bajeti inayokuja watapelekewa maji. Wananchi wa Losoito na Naiborndet katika bajeti ya mwaka huu watapelekewa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwa upande wa, nilikuwa napitia Fungu namba 49 upande wa randama katika ukurasa wa 56 kwamba moja kati ya kazi atakazofanya ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya maji ya ukubwa wa kati hususani katika maeneo makame. Nataka niseme Wilaya ya Simanjiro ni miongoni mwa maeneo ambayo yapo katika nyanda kame na wote wanajua na Waziri juzi ameshuhudia alipokuja na Kamati. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maji walifika, walishangaa walivyofika katika yale maeneo wakasema, kabla ya mradi huu wa Mama Samia wa kupeleka maji Orkesumet, watu hawa walikuwa wanaishije?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Simanjiro ni miongoni mwa maeneo ambayo yapo katika nyanda kame na ninyi nyote mnajua na wewe mwenyewe juzi umeshuhudia ulipokuja na Kamati nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maji walifika, walishangaa walivyofika katika yale maeneo wakasema kabla ya mradi huu wa Mama Samia wa kupeleka maji Orkesumet, watu hawa walikuwa wanaishije?

Nikawaambia mmeona tu sehemu ndogo ya sehemu ya Wilaya ya Simanjiro ipo haja ya wakati mnagawa rasilimali hizi za nchi muangalie mazingira na jiografia ya maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachimba mpaka mita 200 chini hatupati maji ardhini, tupo katika nyanda kame, Simanjiro iko kwenye nyanda kame, Longido ipo kwenye nyanda kame, Monduli ipo kwenye nyanda kame. Watu wanapeleka maji kwa matrekta kilometa 50 kilometa 20, 30 ni jambo la kawaida kwenda kutafuta maji kilometa 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka leo Lerumo ambako leo ndiyo inapelekwa maji katika bajeti ya mwaka huu ni kilometa 30 kwenda Rovuremit lakini wananchi wa Lerumo leo Mkandarasi amepatikana na kazi imekwishaanza na hii kazi ni ya Mama Samia Suluhu Hassan, Waziri wake ni wewe Juma Aweso. Nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upo mradi….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo, hauwezi kuniongezea hata dakika hivi au ndiyo muda umeenda?

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ngoja nimalizie, ahsante nashukuru. Niombe basi ule mradi wa Mirerani, Endiyamtu, Shambarai, Olgora

Namba Tano na Isinyai ukamilishwe na wenzetu wa Mamlaka ya Maji wa Mji wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami kwanza nimshukuru Mheshimiwa hapa Ole-Sendeka amenisaidia kushukuru kwa niaba, kwa hiyo mimi nitaenda moja kwa moja kwenye *point*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya Waziri nikushukuru, kule Mpanda tumepokea zaidi ya shilingi bilioni tatu kuboresha kilometa 38 lakini kuna mtandao wa kilometa 105 ambazo tunategemea kupata shilingi bilioni 4.7, lakini nishukuru sana Mheshimiwa Waziri tumepatiwa kwa maana Miji 28 tumepatiwa kilometa 42. Niseme ukilinganisha miji mingine yote naona Mji wa Mpanda jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri umeufikiria katika eneo hilo ili tuweze kuongeza mtandao wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tuna miradi ya Kakese na Milala ambapo kuna fedha kutoka *National Water Fund*. Naomba fedha hizo zipelekwe kwa haraka Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ya shukrani na mimi niendelee kusema nafahamu siku zote Waziri amekuwa akituambia hakuna mbadala wa maji, nakubaliana na wewe katika hilo na ukiongelea maji kwa maana maji ni usalama wa nchi ni usalama wa Taifa. Watafiti mbalimbali

wanakwambia yawezekana vita vya tatu vya dunia vikatokana na tatizo hasa la maji katika maeneo mbalimbali duniani. Kwa hiyo, hayo yote yanaonyesha umuhimu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu najua tunaambiwa mpaka itakapofika mwaka 2025, kutakuwa na upungufu wa maji kwa maana ya 8,083 lakini mimi nataka kusema nini? Siku zote nikichangia hapa nimekuwa nikitoa mifano mpaka ya China, mito mbalimbali, vyanzo mbalimbali ambavyo vimekuwa ikiunganisha Kusini kuja Kaskazini, Mashariki kwenda Magharibi kwa maana ya Tanzania hii. Niombe sana sana sana, najua wakati nikiingia hapa uliniambia Kapufi mimi najua utakapoingia pale wazo lako ni moja tu kuhusu Gridi ya Taifa. Umeniambia pale, kwa hiyo maana yake suala hili wewe na Wizara yako mnalo akilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kwa maana ya nchi yetu hii njema, nafahamu umuhimu wa visima, nafahamu tumepeleka magari lakini twenda kushoto twende kulia, Waziri wa Kilimo juzi ameongelea namna ya kuigawa nchi hii kwenye kanda za kilimo. Nakuomba na wewe Mheshimiwa Waziri wa Maji igawe nchi hii kwenye kanda za maji. Kwa mfano, ukitumia tu Ziwa Victoria nilikuwa nikipiga mahesabu hapa kwa maana ya Mikoa yetu 26, Ziwa Victoria peke yake zaidi ya Mikoa 10 inakuwa *covered*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Ziwa Victoria tu lime-*cover* zaidi ya Mikoa 10, Ziwa Tanganyika? Hebu chukulia Mikoa mingine mitano, Ziwa Nyasa Mikoa mingine mingapi? Ziwa Rukwa Mikoa mingine mingapi? Kwa hiyo, tukiigawa nchi hii katika Kanda hatuna sababu ya kuyatafuta maji kwa tochi. Kisima ambacho hauna uhakika nacho wakati maji yale pale unayaona kwa wingi wake. Iwe ni Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Rukwa na ninajua Rais wa nchi hii ameongelea

habari ya kutumia vyanzo hivyo. Kupanga ni kuchagua, naomba tuje na vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu zilizopita tuliwahi kuambiwa tuna omba tuiunganishe nchi hii kwa barabara za lami na hili naliona likienda kuwa limetimia. Leo unaweza ukatoka Mtwara ukafika Bukoba kwa *taxi* au bajaji! Andika historia, Mheshimiwa Waziri aandike historia. Mimi niendelee kusema sibezi shughuli nyingine zote zinazofanyika, ununuzi wa magari, uchimbaji wa visima. Tugawe nchi hii, ukiigawa nchi hii nakuhakikishia kwa maji tu hayo tuliyonayo visima iwe ni ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hayo mabwawa tunayokusudia kukinga maji ni ziada. Maji tuliyonayo Victoria tu sisemi kwamba yamalize nchi nzima lakini hebu angalia kama Victoria imefanya miji 10, Tanganyika ikafanya mingine 10. Katika mikoa 26 tumebakiza mingapi? Najua Zanzibar watakuja na utaratibu mwingine kama ni visima tuseme sawa lakini bado ungeweza kuyavusha maji hata huko. Kwa hiyo mimi niendelee kusema naomba naomba, mimi sitaki kwenda mbali zaidi, katika hili hatuna sababu ya kulalamika, kupanga ni kuchagua na lazima tuje na vipaumbele. Tukisema tunakusudia kwenda kuiunganisha nchi kwa maji, kuwa na mtandao wa maji hilo linawezekana, hivi vyanzo vingine iwe ni ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru kama ambavyo tumesema hapo mwanzo ukizungumzia maji hata wenzako wengine wote awe ni mtu wa kilimo na wengineo, kwanza tuanze na maji. Ukizungumzia kilimo kwa maana ya umwagiliaji, *so long as* maji tumeyafanyia kazi, wewe ukienda ukaya-*tap* hata hayo maji mengine yanayotiririka ya mvua na mambo mengine ambayo yanapotelea baharini na kwingineko, sisi tuamue sasa kwamba haya maji mengine ndiyo yaende

kwenye kilimo, haya ambayo ni mengine yaende kuwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kwenda mbali zaidi ambako kuna nchi za wenzetu ukifungua tu maji ya bomba una uwezo wa kuyanywa. Sitaki kwenda huko kwa sababu kwanza tu ile mgawanyo wa maji hatujafika hapo lakini nilitamani pamoja na huduma hizi za maji tuendelee kuangalia ubora wa maji yenyewe. Nchi za watu huhitaji hata kwenda kununua maji dukani, unafungua *tap* yako unachota maji unakunywa. Kwa hiyo, mimi naamini tukianza kwanza na ufumbuzi huo wa kupatikana kwa maji hayo mengine yatafuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na wengine wote kuhusu suala zima la majitaka. Nilisema hapa majitaka wala siyo maji ya kubeza. Unaweza ukapitia majitaka yakakusaidia kufanya majukumu mengine. Miji mingi duniani inapendezeshwa kwa kupitia majitaka. Kwa hiyo, kwa kuzalisha majitaka ukaya-*purify,* maji hayo yanarudi kufanya shughuli hizi nyinginezo kupendezesha Miji kama hivyo, badala watu kupita na kusema kwamba mji ni mchafu, wapite wakiuona mji umependeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo niombe kwa maana ya huduma ya majitaka kutolewa kwa mfumo wa magari na kama siyo magari tu hata kwa maana ya hayo mabwawa mengine ambayo ni ya kutibu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la udhibiti wa uchimbaji holela wa visima ndiyo maana nakusudia ni bora tukaendelea kuangalia vyanzo hivyo tulivyonavyo tayari kwa sababu *study* zinasemaje? Hili nilikuwa naomba sana kwa maana ya muda mrefu haswa katika ile miji ya wenzetu tafiti zako zijielekeze pia. Unaweza ukafurahia kwa maana ya kuyachimba maji yaliyopo ardhini lakini ukazalisha tatizo jingine.

Kwa hiyo, naomba sana hilo likifanyika liende sambamba na tafiti. Sehemu nyinginezo duniani miji imekuwa ikizama kutokana na suala hilo hilo la uchimbaji visima bila kufanya tafiti. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri katika eneo hilo tuendelee kuyazingatia hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu kwa maana ya Chuo cha Maji kuzalisha wataalam. Haya yote tunayoyatamani naendelea kuomba tusiache kuboresha watu wetu katika fani hii ya maji ili waendelee kutoa huduma iliyotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata hii nafasi, nami niungane na wenzangu kwanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akifanya katika kutafuta rasilimali kwa ajili ya nchi yetu, pia katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maji. Ni kweli kabisa amefanya kazi kubwa sana na ndiyo maana tunaona miradi kila kona karibu kila Jimbo miradi mingi inaendelea. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya, kwa kweli mnastahili kupewa sifa kwa sababu sote tunajua Wizara ya Maji tulikotoka, miradi ilikuwa ni miradi chechefu kweli kweli na ilikuwa ni miradi

ambayo kwa kweli iliturudisha nyuma sana lakini sasa hivi kazi kubwa mmeifanya na sisi tunaona mwelekeo ni mzuri. Ninawapongeza sana kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimeona hata katika Jimbo langu mmenisaidia sana miradi. Kuna ule mradi mdogo ule wa Mlangali Mbewe pale unafanya vizuri, Mradi wa Itunga unafanya vizuri lakini kuna miradi mingine ya Msiya unaendelea kutekelezwa. Mheshimiwa Waziri nakubaliana na wewe kwamba maji ndiyo maisha. Maji ni uhai, maji ndiyo chakula chetu, maji ndiyo nishati, maji ndiyo usalama wa nchi na sote tunakubaliana na hayo. Kama hii ndiyo msingi kwamba maji ndiyo maisha yetu, ukiangalia nchi yetu ilivyo tumebahatika kuwa na mabonde, kuwa na mito, kuwa na maziwa makubwa, mpaka tunayo hata Bahari, sasa hatustahili kuendelea kulia kila siku kwamba tuna shida ya maji kwa ukubwa huu wa mambo yote haya ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachohitajika Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri ambayo umeifanya, kilichobaki ni uje na mpango wa matumizi bora ya maji *(water master plan)* ya muda mrefu. Ukija na *water master plan* ya muda mrefu utakuwa umeacha *legacy* katika nchi hii. Sasa hivi tunatekeleza miradi mingi, kila mahali inatekelezwa lakini hatuwezi kuiendeleza nchi hii kwa kutekeleza hii miradi namna hii. Tuje na mpango ule wa maji namna ya kuyatumia yale maji, ili tutengeneze gridi za kuunganisha sasa kwamba hapa itatoka wapi, hapa itatoka wapi, hapa tutaunganishaje? Hiyo ndiyo itakuwa mpango wa muda mrefu wa kutatua tatizo la maji katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yaliyoko katika nchi hii hatustahili kila Mkoa wala eneo lolote kukosekana kwa maji, kwa sababu tunayo mengi, tukiwa na gridi kubwa tukiwa na mpango huo wa matumizi basi kila kitu kitakwenda vizuri. Kwa

hiyo, nadhani hili ni eneo ambalo unatakiwa uache *legacy* kubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Waziri ulikuja kule Jimboni na wewe ni shahidi unaona Wilaya yetu ya Mbozi na Jimbo la Vwawa ambalo ni Makao Makuu ya Mkoa, upatikanaji wa maji ni chini ya asilimia 50. Sasa hivi maji katika eneo lile Mji wa Vwawa ni asilimia 49 wakati ndani ya nchi umesema upatikanaji wa maji umefikia asilimia 88.5 mijini. Mimi kwangu ni chini ya asilimia 50 Waziri na wewe ni shahidi ulikuja uliona. Kwa kweli hii haikubaliki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wilaya inavyozalisha katika uchumi wa nchi hii, ukiangalia wananchi wanavyofanya kazi katika nchi hii, hatustahili kuwa na maji chini ya asilimia 50. Ulikuja tukazungumza miradi kadhaa tukaangalia mahali tutakakopata miradi miaka karibu mitatu tunazungumza hilo. Uliniambia tutachukua maji kutoka Ileje kwenye Mto Bupigu na mimi nikakwambia Mheshimiwa Waziri lazima tuwe na mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na nikasema kule mnakosema uwe ni mkakati wa muda mrefu lakini nako inawezekana kuna changamoto na nikasema kuna maji yanapatikana kutoka kule Ilomba eneo la Mafumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni mengi yangeweza kuchukuliwa kule kwa mserereko yakaja mpaka Nyimbili, yakaja Idiwili, yakaja Nyimbili yakafika mpaka Vwawa kwa njia ya mserereko. Pale tunahitaji fedha kidogo tu. Mheshimiwa Waziri hebu hili liangalie. Nisingependa kwamba niwe Mbunge wa kulialia humu ndani. Pale maji unatega tu maji yanaserereka mpaka Vwawa pale Mjini. Kwa kweli hili naomba mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmekuja na mpango sasa hivi ule wa maji ya Momba, mimi nakubaliana nalo lakini ule hauji Vwawa sasa hivi. Mmesema unaishia Tunduma, kwa nini uishie

Tunduma? Halafu mseme utakuja kwenda Mbozi na mpaka Vwawa mpaka Mlowo baadaye? Kwa nini msingetafuta hizo fedha mkaunganisha huu mradi ukatufikia mpaka maeneo yote ili na sisi tuweze kutatua tatizo la maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, nakuomba nakuomba kama Kaka yako hebu lifikirie Jimbo la Vwawa. Hebu iangalie Wilaya ya Mbozi, hebu iangalie Wilaya ya Mbozi mtupatie maji katika maeneo hayo ili tuondokane na changamoto za maji. Ipo Kata ya Nanyara, Kijiji cha Songwe, Lusungo na Songwe vina shida kubwa ya maji. Vina mradi wa maji wa mwaka 1978. Mradi ule ulikuwa ni mdogo mpaka leo hii kuna shida ya maji unatakiwa upanuliwe ukarabatiwe ili uweze kutosheleza mahitaji ya maji. Tunaomba hilo mlifanyie kazi na muone namna mtakavyoweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Kijiji cha Ihowa, Kijiji cha Weru, Kijiji cha Shomora, Vijiji hivi vyote vinastahili kupata maji. Ije Igare kuna mradi mwingine ulikuwa mkubwa sana lakini maji hakuna. Mabomba yamepita maji hayajapatikana, maji hayapo. Sasa tunaomba mtufikirie muone namna mtakavyoweza kuboresha. Pale Vwawa, Ilolo tulichimba kisima, na wewe ulikuwa shahidi wakati ule ukiwa Naibu Waziri, tumechimba kisima. Kile kisima mmekuja kutuambia tena hakina maji mpaka leo. Sasa kama kisima tumewekeza tumechimba hakijapatikana maji, nini *solution* ya muda mrefu sasa? Sasa tunapataje maji maana tunahitaji haya maji. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kuangalia katika maeneo haya utusaidie hii miradi ya maji iweze kutatua matatizo yaliyoko katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Isango tunakushukuru sana mmeleta mradi wa kuchimba kisima ambacho kitasaidia sana kupunguza upatikanaji wa maji pale Kata ya Sanga lakini utakuja mpaka hapa Itengezya, nakushukuru kwa kazi hiyo

inaendelea vizuri lakini tunaomba sasa itekelezwe mtuunganishe katika mradi mkubwa ili kusudi tatizo la maji la Wilaya ya Mbozi, Mji wa Vwawa, Jimbo la Vwawa mpaka hadi Mlowo liwe ni historia, utakuwa umeacha *legacy* kubwa nasi tutasema alikuwepo Waziri mdogo anaitwa Aweso akisaidiwa na Maryprisca walifanya kazi nzuri sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri tusaidie na sisi naamini tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia Mheshimiwa Waziri, maji ni uhai, maji ni usalama wa nchi, maji ni chakula, maji ni nishati. Tunahitaji uje na *master plan* ya matumizi ya maji. Uje na gridi, ikiunganisha nchi hii tuione miaka mitano, miaka 10, miaka 20, miaka 50 ijayo naamini utakuwa umefanya kazi nzuri na Mungu akubariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Hasunga. Nilimtaja Mheshimiwa Stella Fiyao, Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo wajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Maji. Hii ni Wizara muhimu sana kama walivyotangulia kusema, uhai wa Taifa letu unategemea Wizara hii pia ya Maji kwa sababu ni muhimu katika kila sekta. Tukisema Ujenzi unagusa maji, tukisema nini kila kitu kinagusa maji, tukisema usafi, afya kila kitu kinagusa maji. Kwa hiyo ni Wizara muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa namna ambavyo bajeti yake inatekelezeka. Tukiangalia katika suala zima la bajeti ya miradi ya maendeleo katika fedha zilizokuwa zimetengwa shilingi

bilioni 657.899 fedha zilizotoka kufikia Aprili 2023 zilikuwa ni shilingi bilioni mia sita ishirini na tatu na milioni saba Hamsini na tatu na *point.* Kiukweli hii inatia moyo hata Wabunge tunapokaa hapa kupitisha bajeti kiuhalisia inatia moyo mpaka kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutia moyo huku bado kuna changamoto kubwa kwenye suala zima la usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa, hili ni tatizo kubwa sana kwenye maeneo yetu. Bajeti inapita huku inatekelezeka lakini ukienda kwenye suala la usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kumekuwa kunasuasua sana. Hii imepelekea miradi mingi kutokamilika kwa wakati na wakati mwingine kutokwenda kwenye lengo sawa sawa na vile inavyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Mji wa Tunduma pale sasa hivi utakuta kuna ma-*tank* ambayo yamepakwa rangi za kila aina, lakini hakuna maji. Utaona kuna miundombinu kila maeneo, ukifika utasema Mji wa Tunduma una maji, lakini ukienda kwenye uhalisia, wananchi wa Mji wa Tunduma asilimia kubwa hawapati maji safi na salama. Hii ni hatari sana. Wananchi wetu wanataka wanapoona yale ma-*tank,* wanavyoona miundombinu ya maji imetembea kila mahali, kitu kikubwa wanachokitaka siyo yale matenki, siyo mabomba yaliyopitishwa kila maeneo, wanachotaka ni uhalisia wa maji. Sasa tunataka tuone maji, tusione tu yale matenki ambayo yanabadilishwa rangi. Tunataka tuone uhalisia wa maji kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia kama walivyosema Wabunge wengine wa Mkoa wa Songwe, Mheshimiwa Waziri kuna hatari ya sisi Mkoa wa Songwe kukimbia na Shilingi yako. Kiukweli. Kwa sababu uhalisia hakuna kata hata moja ndani ya Mkoa wa Songwe ambayo ina uhakika wa kupata maji safi na

salama kwa uhakika, hakuna. Katika taarifa yako unasema kwamba hali ya upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 77, lakini ukienda Wilaya ya Momba, ukienda Halmashauri ya Mji wa Momba kuna vijiji 72. Kati ya vijiji 72, vijiji 28 tu ndiyo vyenye uhakika wa kupata maji. Kwa hiyo, napata shaka na hii asilimia 77, ni wapi? Ni wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata shida. Karne hii ya leo watu wana-*share* maji na mifugo. Ukienda Momba…

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wana-*share* maji na mifugo, ni kitu cha hatari sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwongezee taarifa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wetu wa Songwe, kwamba katika Jimbo la Momba kati ya vijiji 72, ni vijiji 22 tu ndiyo vinapata maji safi na salama ya kwenye bomba. Vijiji 50 havina maji. Kwa upatikanaji wa Jimbo la Momba ni sawasawa na asilimia 30 tu, lakini vijiji vilivyobaki 50 tunakunywa maji na nguruwe, punda, mbuzi na ng'ombe. Vijiji 50, na jambo hili linaendelea kushamiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao unaipokea taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa naipokea kwa mikono miwili kwa sababu huo ndiyo uhalisia wa Jimbo la Momba. Ni hatari! Kwa karne hii, leo wananchi wana-*share* maji na mifugo! Ni jambo la hatari. Ndiyo maana *typhoid* kwenye Mkoa wa Songwe haziishi, maana ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakapokuja hapa, atuambie mkakati wake katika Mkoa wa Songwe ni upi, kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunataka tujue, tumeendelea kusema hapa, kila inapofika Wizara ya Maji tunachangia na tunasema. Mmeendelea kutuahidi kipindi kirefu kwamba maji yatatoka kwenye Mto Songwe huko Ileje, yatakuja Tunduma, yataenda Vwawa, yataenda Mbozi, leo hii mmetubadilishia mpango, mnasema maji yanakwenda kutoka Momba. Tunataka mtuambie, kwa sababu tangu mwaka 2019 mlisema tayari mmeshafuatilia na mmejua gharama za mradi, mradi utagharimu kiasi gani. Leo hii mmetubalishia mpango, mnasema maji yanakwenda kutoka Momba, yanaenda Tunduma, yanaenda Vwawa, yanaenda Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri atakapokuwa anakuja hapa atuambie, ni lini mradi huo utatekelezeka? Ni lini mradi huo utatekelezwa? Kwa sababu tumechoka kuimba humu, tumechoka kusema, tumechoka kuzungumza. Tuambieni ni lini mradi huo mkubwa utatekelezeka kwa ajili ya kukomesha tatizo la maji katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Mbozi na Vwawa? Lini mradi utatekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, bado tumeendelea kuimba, kuna mradi ambao unahudumia Kata ya Mpemba na Kata ya Katete. Mradi huu unatoka Ukwire Wilaya ya Mbozi kuja Halmashauri ya Mji wa Tunduma na unahudumia

Kata hizo mbili, miundombinu yake ni mibovu. Miundombinu ilitengenezwa tangu mwaka 1971, mpaka leo kuna tatizo kubwa. Mradi huu ulikuwa unawakomboa sana wananchi wa Kata ya Mpemba na Kata ya Katete. Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unakuja hapa, utuambie ni lini mtafanya ukarabati mkubwa kwenye mradi huo ili wananchi wa Kata ya Mpemba na Kata ya Katete waweze kunufaika na maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, sisi watu wa Songwe tuangaliwe kwa jicho lingine. Tunachangia asilimia kubwa sana kwenye pato la Taifa, hebu tuangalieni kwenye suala la maji, tuondoleeni hizi changamoto. Ninaamini changamoto hizi zinatibika kama Mheshimiwa Waziri utaamua. Tusaidie wananchi wa Mkoa wa Songwe tuepushieni changamoto kubwa ya maji ambayo inaleta athari mpaka kwenye ndoa. Tusaidieni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Fiyao. Tunaendelea na Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge, halafu Dkt. Oscar Kikoyo, Mheshimiwa Augustine Vuma, na Mheshimiwa Agnes Hokororo wajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimpwekeshe Mwenyezi Mungu na kumhimidi kwa neema kubwa ya Rais wetu tuliyenaye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na watendaji wake mahiri, wazalendo, wenye kupambana kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa jitihada kubwa na mahangaiko makubwa mnayoyafanya kuhakikisha

rasilimali maji inakuwa chanzo kikuu cha maendeleo ya Taifa letu. Lazima tuwe wakweli kwamba Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu Waziri wake wamekuwa wanahangaika sana kipindi kirefu kwa sababu, ni miaka mingi miundombinu ya maji haikuwa inafanyiwa matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya maji ni chakavu Tanzania hii, na ndiyo sababu imesababisha katikakatika ya maji kila kukicha. Kwa hiyo, Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan inafanya jitihada kubwa kuanza kuboresha miundombinu ya zamani ya maji pamoja na miradi ile chechefu ambayo imeshafanyika, pia kutengeneza miundombinu mipya ya maji. Naipongeza sana sana Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan. Hakika imedhamiria kabisa kuleta huduma bora kwa wananchi wa Tanzania. Bila shaka, haihitaji tochi. Kazi kubwa ya Mama Samia Suluhu Hassan inafanyika, na watendaji wake wako mahiri kabisa kuhakikisha wanafanya kazi vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania amesema Waziri leo wakati anazungumza kwenye hotuba yake na Mheshimiwa Kapufi naye amezungumza, ni kwamba, sisi Tanzania ndiyo wa kwanza Afrika kuwa na maziwa makubwa Afrika nzima. Pia Tanzania ndiyo wa pili Afrika ukiacha *DRC* Kongo kwa *water bodies.* Vile vile, kiukweli *so far so good,* rasilimali maji hii tunavyoiangalia, ni kwa jicho la huduma tu zaidi, hatujaangalia *potential* kubwa ya maji tuliyonayo Tanzania katika upande pia wa kuongeza mapato ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Naomba niseme wazi, kaka yangu, Mheshimiwa Aweso, nakupenda sana, unajua; na umewasifia sana watendaji wako, ni vizuri kuwa na imani kubwa na watendaji wako, ni jambo jema, lakini mimi nasema hapa, Wahandisi wa rasilimali maji wa

Bodi za Mabonde ya Maji, bado hawajafanya *assignment* yao sawasawa kukusaidia kufanya kazi yako vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Mpaka leo, juu ya *potential* kubwa tuliyonayo ya maji, hatuna *Integrated Water Master Plan* Tanzania, hatuna. Kamati imezungumza hapa kwamba tunahitaji *National Water Master Plan. Master Plan* tulizokuwanazo mpaka sasa ni za mikoa mikoa; ya Mkoa wa Tanga ni ya mwaka 1976; ya Mkoa wa Ruvuma, Kigoma na Iringa ni ya mwaka 1982. Ukisoma *Water Master Plan* zile za mikoa, utagundua kwamba inaonesha tu maeneo ambayo unaweza kupata maji, lakini hakuna *details* za undani zaidi, kwa maana maji yale yako kwa kiwango gani? Maji yale yana ubora gani? Naamini wahandisi wa rasilimali maji, kama watafanya tafiti ipasavyo, hivi vitu vinaweza kujulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake ni nini? Madhara ya kutokujulikana kiwango cha maji kilichopo. Leo umetutajia uhitaji wa maji kwamba ni Shilingi bilioni 60 *meter cubic,* lakini hizo nina uhakika umeangalia *consumption per person,* ukazidisha na idadi ya Watanzania. Kwa hiyo, watu wa bodi za maji wanapaswa kufanya tafiti kujua *underground water scope* ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na kasumba kubwa ya kuchimba visima. Tunachimba sana visima na Wabunge hapa tunaonekana tunahitaji sana kuchimba visima, lakini bodi za maji ndiyo zinapaswa kututengenezea *mechanism* ya kuhakikisha visima vile vitaendelea kuwa na maji. Hiyo inawezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima wa-*establish coordinates* katika visima vilivyopo sasa na waweze kuonesha *underground water channel, relationship* yake na kisima kipya kinachojengwa. Kwa sababu mkondo wa maji una tabia wa

kunyang'anyana maji. Visima vingi vikichimbwa sehemu moja, bila kujua *capacity* yake kule chini, ina maana kwamba kisima kimoja kitanyang'anya maji upande mwingine, *at the end of the day* ni kwamba visima vinakauka na hakuna *sustainability. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimshauri sana kaka yangu kipenzi, watu wa bonde za maji wafanye tafiti ya kutosha, watuambie *scope* ya *underground water.* Kwa sababu huwezi kufanya *management* yoyote ya maji kama hujui *capacity* uliyonayo *underground.* Leo miji inatanuka, watu wanaongezeka, tunachimba visima kiholela, mwisho wa siku inaonekana miradi siyo *sustainable,* kwamba maji hayatoshi, maji yanakatika, ni kwa sababu bodi za maji; Wahandisi wa Rasilimali Maji hamjafanya tafiti za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mumsaidie ndugu yangu yule. Mheshimiwa Aweso ni mzalendo, anapambana, na ana maono mapana kwa ajili ya Wizara hii ya Maji. Msaidieni vya kutosha. Anaweza kufanya makubwa zaidi mkimpa mawazo. Ninyi ni wataalam, mko pale, fanyeni *assignment* yenu sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia, katika nchi ya Uholanzi, wenzetu sasa hivi, ile *distribution* ya *water supply,* anakaa ofisini, anai-*monitor through GSI Technic (Geographical Information System Technic),* inamwezesha ku-*monitor distribution* ya *water supply.* Hii ndiyo imesaidia ku-*manage* upotevu wa maji. Tuna maji mengi yanapotea lakini hatuna *proper management* ya upotevu wa maji. Sisi tuna wadau, tuna wahisani, tunashirikiana na nchi mbalimbali na wadau wako tayari, tunashirikiananao, watuwezeshe upande huu ili tuweze kudhibiti upotevu wa maji kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kufanya tafiti za kutosha, ina maana tutaweza hata kuvuna maji, tutaweza hata kuondoa chumvi kwenye maji, lakini watu wa mabonde ya maji bado hamjafanya *assignment* yenu sawasawa, na *potential* kubwa ya maji tuliyonayo Tanzania, bado hamjaiangalia kwenye jicho la kiuchumi. Miundombuni imekuwa chakavu muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga uwekezaji mkubwa ulifanyika kuanzia miaka 1990 na 1995. Wakati huo miundombinu yote imeshakuwa mibovu, maji yanakatika kila siku. Ina maana hakuna *proper strategic maintenance program* ya miradi ya maji. Kwa nini leo imeji-*accumulate* miradi mingi kwa wakati mmoja? Ni kwa sababu hiyo. Huko nyuma mmeshindwa kufanya ipasavyo. Sasa msimwangushe Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso amekiri wazi kwamba, ule usemi wako unasemaje? Ukinizingua, tutazinguana. Yuko *very serious* na anachokifanya, msimzingue. Tunatamani Wahandisi mfanye kazi zenu vizuri, kwa ueledi na maarifa. Fanyeni tafiti za kutosha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng. Mwanaisha.*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuwa…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili na tano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, wajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutuletea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Watendaji Wakuu wa Wizara na Watendaji wote wa *RUWASA* nchi nzima, lakini zaidi Meneja wetu wa *RUWASA,* Mkoa wa Kagera, Ndugu yangu Warioba, mtani wangu; na Meneja wetu wa Wilaya Muleba, Jerome. Ni watendaji wazuri sana, wanafanya kazi iliyotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea suala la upotevu wa maji. Mheshimiwa Waziri naomba hili uliangalie sana. Ukiangalia *standard* ya ulimwengu, upotevu wa maji haupaswi kuzidi asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya *PIC,* mamlaka nyingi ambazo tumezitembelea, unakuta wanaongelea upotevu wa maji zaidi ya asilimia kati ya 30 mpaka 40. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji wakati anachangaia hapa, amesema mabomba mengi yanapasuka, na yanapopasuka hatuchukui hatua za haraka kwenda kuyaziba. Hapa ndipo tatizo lilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, huu upotevu wa maji, mara nyingi sana sisi ambao tumefanya kazi ya kuwalinda

walaji, nimefanya kazi kwenye hiyo sekta. Unakuta unabebeshwa watumiaji kwa makosa ambayo yanafanywa na watu wengine, wanakuja kubebeshwa watumiaji. Naomba Waziri uliangalie hili, uwasisitize watendaji wako wawe wanachukua hatua za haraka kuziba mabomba ambayo yanapasuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, jana tulikutana na *management* yake pale Wizarani. Kilichonipeleka pale Wizarani ilikuwa ni Mradi wa Muleba wa kutoa maji Ziwa Victoria. Huu mradi nimeuongelea mara nyingi sana. Tangu nije hapa, ni mwaka wa tatu naongelea mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea mwaka huu nitakuta kwenye bajeti, lakini nashukuru kwa *commitment* aliyotoa Mheshimiwa Waziri jana, na kwa *commitment* hiyo nategemea bajeti ya mwaka kesho, tulishauriana tukakubaliana kwamba sasa tutautekeleza kwa awamu. Nami nakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Waziri. Sasa isiishie hapa, au pale mezani ofisini kwake. Naomba mwaka kesho nilione kwa vitendo, na hii itampa heshima sana Mheshimiwa Waziri, na zaidi itampa heshima sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kuona wilaya ambayo iko pembezoni mwa ziwa tunahangaika na maji. Tuna miundombinu ya maji, tuna maji pembezoni mwa kata zetu, lakini hatuna maji. Mheshimiwa Waziri nakuomba hili ulichukue kwa uzito wake, na tukipata mradi huu wa Ziwa Victoria wa kuhudumia kata sita, itatusaidia, hasa maji yanayotumiwa Kata ya Muleba, sasa yataweza kusaidia Kata za Ikondo, Kata ya Kibanga na Kata ya Biirabo na Kata ya Nshamba, tutakuwa tumehudumia hizo kata nyingi kwa mradi huo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara, tuna miradi mipya miwili. Tuna mradi wa Chebitembe Kisana kwenye hii bajeti, lakini tuna mradi mwingine wa Bushagara. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa miradi hii na miradi mingine ambayo inaendelea. Naomba hiyo miradi mingine ambayo inaendelea isije ikasimama. Kazi kubwa imefanyika, na inaendelea kufanyika, tunaomba sasa kama wachangiaji wengine walivyosema, wakandarasi wale wapewe fedha ili miradi iendelee kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kata zetu ambazo ziko visiwani. Tuna kata tano Wilaya ya Muleba. Tuna Kata ya Ikuza, Kata ya Mazinga, Bumbire, Kerebe na Goziba. Hizi ni kata ambazo ziko katikati ya Ziwa Victoria. Tunakuomba utengenezwe utaratibu mzuri, kwani wenyeji wa kule ni wavuvi lakini hawana maji safi na salama, wanatumia maji ya ziwa ambayo siyo salama kwao. Tunakuomba ututengenezee utaratibu mzuri, angalau bajeti ya mwaka kesho hizi kata ambazo ziko katikati ya ziwa na wenyewe tuwakumbuke, ni Watanzania wenzetu na wanastahili kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa hili, Wilaya ya Muleba, hasa Muleba Magharibi, tulikuwa na matatizo makubwa sana. Mheshimiwa Waziri tuliongea jana ofisini kwako na umetupa *commitment* kwamba gari likitoka Karagwe liende Wilaya ya Muleba kuchimba visima kwenye hizi kata ambazo zina uhaba mkubwa sana wa maji hususan Kata za Kyebitembe nashukuru kuna Mradi wa Kyebitembe sana.

Mheshimiwa Mweyekiti, umetupa visima kwenye hizo baadhi ya kata. Kata ya Burungura, Kasharunga na Kata ya Karambi, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa *commitment* hiyo natumaini sasa mwaka kesho tutakapokuja hapa hatutakuja kuimba wimbo uleule, kibwagizo kilekile

nakuomba tuendelee kufanya kazi tutakuunga mkono na bajeti yako mimi kwa *commitment* hii jana nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru na la mwisho kwamba nilikuwa na tatizo sana kwenye kijiji changu cha Msalala. Mheshimiwa Waziri kati ya visima ambavyo tumepata visima 10 Wilaya ya Muleba nakuomba na utoe maelekezo mahususi, kisima cha Chakaseni kuchimbwe Msalala, kule eneo la Msalala wana matatizo makubwa sana ya maji, wananunua ndoo moja ya maji mpaka shilingi 1,000 kwa sababu ya uhaba huo wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mmeishatoa *commitment* kwamba kisima kinakwenda kuchimbwa pale nikuombe Mheshimiwa Waziri utoe maelekezo wakati unatoa hotuba yako ya mwisho na natumaini na watendaji wako wa *RUWASA* Kagera wakachimbe kisima cha kwanza lile eneo la Msalala, umetupa kisima kimoja nadhani hakitoshi. Mheshimiwa Waziri kwa busara yako kwa sababu kuna watu wengi sana pale na ni mkusanyiko wa watu wengi hasa wavuvi na wanaokuja kununua dagaa ungetuongezea kimoja viwaka viwili watu wa Msalala watakushukuru sana na tutakutafutia samaki utakapo tembea Mkoa wa Kagera kuna *guest house* nzuri pale ukalale pale watakuandalia chakula kizuri sana kwa heshima utakayokuwa umewapatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, niwatakie utendaji mwema wa kazi haya maelekezo mahususi ulimpatia Katibu Mkuu dada yangu Nadhifa kuhusu suala la kata sita kutoa maji Ziwa Victoria waandae kazi hiyo kwa haraka iweze kutekelezeka mwaka kesho niione kwenye bajeti. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Oscar Kikoyo. Nilimtaja Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Agnes Hokororo ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara ya Maji.

Kwanza niseme tu Wizara hii imesheheni vichwa sana kuna *brain* kubwa sana kwenye Wizara ya Maji kuanzia kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, msikivu, mchapakazi ana *brain* ubunifu wa kutosha, usimamizi mzuri lakini Naibu Waziri wake Mheshimiwa Maryprisca, timu Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wote wako sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mchango. Jambo la kwanza nishukuru sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Rais na Waziri na Wizara kwa ujumla kwa miradi mingi ambayo wameendelea kuniletea jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokea mradi kwenye Kata ya Rusesa kata ambayo ilikuwa na shida kubwa sana ya maji mradi ambao kwa ujumla wake zinahitajika milioni 984 lakini nimeishapokea milioni 566 kwa hiyo, bado wakiniongezea milioni 300 namalizia ujenzi wa *tank* kuweka na *sora* na pampu ili wananchi wa Kata ya Rusesa wapate maji ya kutosha

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyamnyusi nimepata milioni 977, Kagera Nkanda bilioni 1.300, Mvugwe milioni 353, Chekenya milioni 817, Kaboranzuri milioni 962 hii siyo hatua ya kubeza nashukuru sana sana wananchi wa Kasulu wanashukuru sana sana hata leo asubuhi nimekutana na Mheshimiwa Profesa Ndalichako siyo mbaya kwa sababu ni Waziri mmemfunga

mdogo hawezi kuzungumza lakini alikuwa anafurahi sana kwa sababu mradi wake mkubwa wa maji Kasulu Mjini umeanza kutekelezwa angekuwa na yeye anaweza kuzungumza angezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la kwanza nataka Waziri unisikilize vizuri sana, Kigoma tunahitaji Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika yaani kama kuna kuna *legacy broo* utaiacha ukiwa kama waziri ni kuhakikisha kwamba tunapata Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi unajua *URUWASA* unaendelea na uchambuzi wa awali na wanasema chanzo kitakuwa kwenye kitongoji cha Shakachakara kijiji cha Kabwera Kata ya Nsimbo halafu tenki kubwa litajengwa Heru Juu Kasulu hii ukijenga tenki pale kama jina lake linavyosema anavyosema Heru Juu maana yake ni sehemu ambayo ina muinuko mkubwa. Maji unaweza ukayatupa kwenda wilaya yeyote Kakonko, Kibondo, Kasulu yenyewe, Kigoma Vijijini, Uvinza kote itaenda mpaka Kaliua na Sikonge kote. Kwa hiyo, nakuomba *brother, is a very very big project* hata Katavi watapata mpaka Rukwa. Tunaomba sana utusaidie sana sana, kwa kuanzia angalau mwaka ujao wa bajeti tuone kuna usanifu unaanza *please over please. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Mfuko wa Maji wa Taifa. Kwanza hapa nimpongeze bila kumung'unya maneno *CEO* wa Mfuko wa Maji tena kwa bahati mbaya anakaimu sijajua nyiye mtajua mnavyofanya lakini tumewaita mara kadhaa kwenye kamati tukaangalia *progress* zao ni ukweli usiyopingika mfuko wa maji umepeleka fedha nyingi sana kwenye kila kona ya nchi hii na kama haitoshi miradi ile hasa ambayo ilikuwa ni kichefuchefu wewe unafahamu umekuwa Waziri. Mfuko wa maji umekusaidia kuikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nisema la kupongezwa kubwa sana kwenye mfuko wa maji ni hili la ubunifu wao wa kukopeshwa mamlaka kubwa za maji zile ambazo zinajiendesha kwa faida. Aingii akilini eti Waziri uumize kichwa eti kutafuta hela ukawape *DAWASA no thank you, DAWASA database* yao ya walaji wa maji kubwa *purchasing power* watu wa Dar es Salaam ni kubwa iko wazi huwezi kuwapelekea hela za ruzuku wale. Wale wanajiendesha kwa faida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakopeshwa na mfuko wa maji zile hela ambazo mnazipeleka za ruzuku zile zipeleke Kasulu, zipeleke Kibondo, zipeleke Uvinza, zipeleke Kigoma Vijijini *yes* lakini haya *ma–giants* hawa wakopeshwe kwa sababu wanajiendesha kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutegemei kuona unawapelekea kama kwa ndugu yangu pale Mwanza na *RUWASA* inajiendesha kwa faida kubwa sana naamini wanaweza kukopeshwa na mfuko wa maji wakawa wanalipa. Kwa hiyo, nipongeze sana ubunifu huo lakini tuongezewe pesa sasa mfuko wa maji ili uendelee kukwamua miradi mingi ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameguswa kuhusu *DUWASA*. *DUWASA* sisi tumewasimamia kama Kamati ya *PIC*. *DUWASA* tutawapiga tu madongo bure tunataka Wizara iwasaidie kuongeza miradi ili *production* ya maji iwe kubwa. Kwa sababu baada ya ile ongezeko la watu Serikali ilivyohamia Dodoma wanasema *production* yao nusu ya mahitaji ya Mji wa Dodoma sasa unawezaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nadhani wanajitahidi angalau tunakuja hapa tumeoga, tunakuja tumefua suti

zinakaa vizuri *I am telling you*. Lakini katika hali ya kawaida *production fifty percent* ya mahitaji. Mradi kama huu ambao nimekuona Mheshimiwa Aweso juzi unaenda kuzindua Nzuguni ya vile midogo midogo ya dharula ifanyike wakati tunasubiri mradi mkubwa wa maji kutoka wapi? Ziwa Victoria kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Aweso jitahidi sana kuhakikisha kwamba unawasaidia watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso pale ninae Kaimu *Manager* wa *RUWASA* wa Wilaya ya Kasulu Kijana kama wewe, anachapa kazi vizuri japo ana gari bovu kweli kweli kuliko watumishi wa Serikali wote Wilaya ya Kasulu. Kijana anajitahidi sana kweli kweli lakini bado anakaimu, nimekwambia mara mbili mara tatu moja ya jambo la kufanya watu wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa ni kuwapa haki yao wanayostahili, yule kijana anatusaidia sana, sana Kasulu sana sana Kasulu hebu mpeni haki yake anatusaidia sana Kasulu, Madiwani wanampenda, Mbunge nampenda, Watumishi wanampenda anasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi ameisimamia kwa nguvu kubwa ni mbunifu anashirikisha sasa anakaimu leo mwaka wa pili hata yenyewe ile sheria ya kukaimu si miezi sita peke yake Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Augustine vuma ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais

wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu naamini Watanzania wengi wanajua hili neno la kumtua Mama ndoo kichwani, yeye ndiye Muasisi aliyeasisi alipokuwa Makamu wa Rais. Sasa hivi yeye anaitekeleza akiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na anatekeleza kwa kasi. Kwa hiyo, nadhani wote tuna kila sababu ya kumpongeza kwa sababu hata tumeona kwenye bajeti hii imeongezeka kwa asilimia saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri anayoifanya, Mheshimiwa Naibu wake *Engineer* Maryprisca Mahundi, Katibu Mkuu *Engineer* Nadhifa na Naibu wake Watendaji wote lakini bila kusahau Mameneja wa *RUWASA* hasa Meneja wa *RUWASA* wa Mkoa wa Mtwara *Eng*ineer Primy Damas na mameneja wetu wa wilaya kwa kuwa nafanya kazi Mkoa wote wa Mtwara. Kwa nini nampongeza Mheshimiwa Waziri? Kwa sababu ni kweli kabisa kwamba amekua akijua mihemo ya wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati nachangia hapa nadhani moja ya Wabunge waliyolia hapa kuhusiana na maji ya kuokota nilikuwa ni mmoja wapo na hasa nilipowapa ile hisroria ya kwamba watu walikuwa wanatumia maji ya tikitiki wakati fulani kwa sababu ya shida ya maji katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimshukuru Mheshimiwa Aweso, kwa sababu waswahili wanasema kushukuru ni kuomba tena. Namshukuru sana Waziri kwa sababu kuna miradi kadhaa ambayo imetekelezwa kwenye Mkoa wetu wa Mtwara. Hivyo nitakwenda kuishukuru hiyo nianze kwanza kwa kuunga mkono mapendekezo yote, ama maoni ya kamati kwa kuwa ni mjumbe wa kamati na yeye amekuwa ni msikivu na timu yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye yale maoni kumi naomba nisisitize kwenye mambo mawili; la kwanza, ni Wizara haina namna nimuhimu sana ikatengeneza mpango kabambe wa maji hii tunayosema kwa kilugha chetu cha kimakua *National Water Master Plan,* hili lazima lipatikane lakini pia Wizara lazima iwe na gridi ya maji na hili linawezekanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema; Mheshimiwa Waziri, unganisha vyanzo vikubwa vya maji kwa maana ya Maziwa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na mito mikubwa kama Mto Ruvuma na Mto Rufiji na hapo sasa utaona namna ambavyo mambo ama azma ile ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani itawezekana. Kwa sababu utakuwa tumeweza kuya–*tap* hayo maeneo muhimu na unakuwa na gridi ikinyofoka huku unawasha huku, hilo ndiyo jambo ambalo litakutoa na nadhani utaweka historia katika maisha yako ya kuwahudumia watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili kwenye yale mapendekezo kumi ya kamati, nisisitize kwenye kutumia watalamu wa ndani. Tulipokuwa kwenye kamati tumetembelea miradi, tumeona ule wa Babati pale namna ulivyokuwa mzuri na umetekelezwa na watalam wa ndani sina shaka watalamu wa ndani wa wizara yako wanaweza wape nafasi wakatekeleze miradi mingine kule ambako Waheshimiwa Wabunge wanakuomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee kukushukuru Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa kipindi kirefu sisi mradi wetu wa Makonde tangu enzi hizo ulivyojengwa ulikuwa unaingia kwenye vitabu lakini ulikuwa hautekelezeki. Kwa mara ya kwanza safari hii wewe na Naibu wako na Katibu Mkuu pale mmeweka alama, kwa nini? Kwa sababu mradi ule wa bilioni

84.7 tayari fedha bilioni 12 ikiwa ni malipo ya awali zimeishakwenda na mkandarasi yuko *site* kazi ya kusafisha maeneo ya kujenga matenki kwenye majimbo manne inaendelea. Newala Mji, Newala Vijijini, Tandahimba na Nanyamba hapa ninaomba tu kama nilivyotangulia kukushukuru na ninakuomba tena kwamba *phase one* ya mradi huu ni muhimu ikaunganisha maji katika maeneo yote muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ule mchoro wa maji utakuta kwa mfano pale Nanyamba inapitia kata kumi lakini kata tatu ndiyo zinaonekana zitakwenda hali kadhalika Tandahimba. Kwa hiyo, ni muhimu *phase one* hii ikaenda maeneo yote ya mradi ili *RUWASA* waje kuwa na kazi ndogo. Kwa sababu unajua fedha zao pia haziwatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili kwa sababu umeweka alama na unakusudia kutuwekea alama ili mimi mwakani nisije tena kusema habari ya kuokota maji hapa ni vizuri mradi ukatekelezwa kwa kasi na fedha ikaenda ili tuone matokea ya kazi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ninalo kushukuru Mheshimiwa Waziri sisi tuna Mamlaka pale *MANAWASA* Masasi kwa fedha za 2021/2022 tayari umepeleka milioni 434 kati ya 738 nikuombe kwa zile fedha za 2022/2023 milioni 940 peleka kaka wakaweze kusambaza maji mjini Masasi na Nachwingea lakini na vijijini ambako ndiyo tunatoka sisi kule vijiji ambavyo vinazunguka kwenye ule mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu; ambalo namshukuru Mheshimiwa Waziri kweli umejua shida za watu wa Mtwara. Kwa sababu jambo ambalo lilikuwa linaniliza mwaka jana la kutekeleza mradi wa Mto Ruvuma angalau umeonyesha kwa hatua za awali kwenye bajeti hii ipo miradi inayotekelezwa.

Pia ukuachia hapo kuna mpango wa kuchimba mabwawa, sasa ninakushukuru kwamba kwenye usanifu kwenye miradi ya kuchimba mabwawa yatakayohifadhi maji ya mvua yale 27 kwenye ukurasa wako wa 77 umeonyesha kuna usanifu katika Lukuledi – Masasi, Namasobo – Nanyumbu, Chilunda – Nanyumbu, Mikangaula – Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa sasa mradi unaoendelea Sengenya – Nanyumbu tunakushukuru sana lakini yatakayojengwa kwa *force account* Namasobo – Nanyumbu. Nakushukuru kipekee unajua Lukuledi imezungukwa na kata nyingi ambazo hazina maji. Ule Mradi wa Manawasa hautatosheleza kwenye zile kata ambazo inazunguka lakini utafanya usanifu na utajenga umenihakikishia hivyo niseme nini ninakushukuru Mheshimiwa Waziri kwamba kwa bilioni 1.7 na ushehe uko ukienda kutekeleza ile hata Mwenyezi Mungu ataendelea kukubariki kwa sababu umewatibu waliyo wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kwamba kwenye ule utaratibu wakuchimba visima. Visima vilivyochimbwa na bonde kwa mwaka huu uliopita 2022 lakini vile visima vyako vitatu kwenye kila jimbo, kwenye majimbo kumi ya Mkoa wa Mtwara tayari umechimba na bado nane una uhakika utakwenda kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niombe, sasa vile visima ambavyo vimechimbwa tayari ni muhimu sasa wananchi wakayanywa yale maji hasa kwenye maeneo yote nawaombea lakini nimeona kwenye vijiji kadhaa kule Sululu ya leo, Masiku, Chingulungulu umechimba lakini maji hawajaanza kuyanywa maana yake ni kwamba wataenda kule kuyaokota maji sasa na maji haya wanaenda kuyaokota mbali mtoni. Ninajua unajua adha za mama zako na sasa una Naibu mwanamke, nimruhusu kwanza kipindi hiki mwezi ujao ule

twende akaone adha ambayo inapatikana katika Mkoa wa Mtwara ili tuweze kwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme kuna suluhisho la kudumu la upatikanaji wa maji katika Mkoa wetu wa Mtwara na lenyewe si jipya ni suala la kutumia maji ya Mto Ruvuma. Kuna mambo mengi watalamu wanasema maji yanapungua, sijui yanafanyaje? Lakini kama utatengeneza *master plan* ile inamaana unaweza kuunganisha Ziwa Nyasa na Mto Ruvuma kwa hiyo, wananchi wa Mkoa wa Mtwara, wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, wananchi wa Mkoa wa Lindi hii changamoto ya upungufu ama kukosa maji safi na salama tutakuwa tumeondokana nayo. Ukifanya hivyo kwakweli utakuwa si tu kwamba umesikiliza mihemo ya wagonjwa sisi lakini utakuwa umetutibu hata kama ujasomea udaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninawatakia kila kheri, chapeni kazi nyingi wote ni vijana na kazi endelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana Mheshimiwa Agnes Hokororo. Nilimtaja Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweke mchango wangu kidogo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanda chema huvikwa pete, hapa leo tunaona, toka tumeanza kuchangia Waheshimiwa Wabunge wote wanatoa sifa kubwa na shukurani kubwa nikiwemo mimi kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waziri wetu mwalimu wa misemo mbalimbali ya kutufundisha na

kutusaidia katika maisha Jumaa Aweso lakini pia Naibu Waziri wake *Engineer* Maryprisca pamoja na Katibu Mkuu *Engineer* Kemikimba lakini kiujumla wake kwakweli wizara hii watumishi wake wote wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mambo mengi mazuri yameishachangiwa na Waheshimiwa Wabunge lakini kwa umuhimu wa wizara hii nashindwa kutoa jina langu inabidi niendelee kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba wizara imejitahidi kufanya shughuli mbali mbali za kiuwekezaji wa maji katika maeneo mbalimbali nami kwangu nawashukuru sana kwa mradi wa maji Wangingama, Litui *group*, Ngumbo *group* na nikiruka mradi wa Pururu Songa mbele ambao kidogo haujanifurahishwa haujaanza lakini kuna Liuli…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa mchango wako mzuri apitie hapo kwamba Taifa linawakilishwa vyema *Young African* imeshinda goli mbili bila. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naipokea taarifa hii kwa sababu mimi ni

Simba, lakini Yanga wamechukua *jersey* za CCM, kwa hiyo tunawapenda tu hata kama wakifanya vyovyote vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba nilikuwa naendelea kushukuru kwa ajili ya mradi ambao utaendela pale Kilosa, Nangombo ambao utaenda mpaka Malinyi na Chihulu na miradi mingine michache itakayoendelea. Lakini kama ambavyo mwalimu amesema, ulitufundisha kwamba pilau la sherehe mvua ikinyesha huliwa wima. Sasa kwa mazingira hayo mimi sasa hivi nanyeshewa naomba nipate maji Mtupale, Chinyindi, Ruhangalasi, kata ya Lumeme, kata ya Mipotopoto, yaani eneo la Uhuru na Mipotopoto yenyewe, na Luhindo leo wamenipigia tena simu na kule Mseto Lipalamba, kote huko kuna shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea katika masuala mengine yanayotuhusu kitaifa, pamoja na hizi shukrani nyingi nilizozisema. Tunamaliza Dira yetu ya Taifa ya Mwaka 2025. Dira hii ilisisitiza zaidi katika kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na Maisha bora, tuwe na jamii ambayo itakuwa na Maisha bora, lakini pia tuwe na amani, utulivu na umoja; utawala bora, jamii iliyoelimika na uchumi wenye ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mambo haya pamoja na kwamba tumeshaanza mchakato wa kuandaa dira mpya ya mwaka 2050 bado masuala haya ya msingi siamini kama yatatoka katika mtazamo wa dira hii ambayo tunaiandaa. Mambo hayo yote ili yaweze kutekelezeka kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi ulio imara na wenye ushindani, kwa vyovyote vile suala la maji haliwezi kuwekwa pembeni. Na ndiyo maana sasa unakuta hata Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la kuwa na Mpango kabambe ambao kwa Kingereza lugha nzuri ni hiyo *Water Master Plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa sababu Pamoja na kwamba sasa hivi tunatafuta maji hapa lakini bado kuna haja ya kuangalia utoshelezi endelevu wa suala la maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza hapa watu wanavyoshukuru miradi inayotajwa. Utasikia tumepata bilioni arobaini, bilioni hamsini, bilioni ngapi, lakini kule kwangu mimi sihitaji bilioni kumi, nahitaji milioni milioni kwa sababu vyanzo vya maji viko vingi tunahitaji tu kuvuvta maji kufikisha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo kama Simanjiro tulikoenda mara ya mwisho kukagua mradi. Mradi ni mkubwa sana lakini ukiangalia mradi ule umekuwa mkubwa kwa sababu ya kuhangaika kutengeneza vituo vikubwa, kusafirisha kwa umbali mrefu kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya maji vya kutosha katika maeneo yanayohusika. Kwa misingi hiyo kwa nini tunataka kuwa na hiyo mpango kabambe wa kuona kwamba ni namna gani tunaangalia maji yetu kwa mbali lakini vile vile namna gani tunaweza kuunganisha hivyo vyanzo, hasa vyanzo vikubwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna mikakati mingi ya nchi ambayo yote kila Waziri hapo unaona anakuja anachemka, wa kilimo anachemka anasema anataka mashamba sijui ya aina gani, wa Kifugo anakwambia mimi nachemka anataka sijui ng'ombe wa aina gani. Wote hawa wanagombania maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa humo humo kuna kutumia dawa, humo humo kuna kutumia, kwamba hilo hilo bonde moja mwingine anatafuta maji ya kunywa, mwingine anatafuta maji ya kilimo, mwingine anatafuta maji gani. Matokeo yake tutajikuta kwamba tuna hali ambayo baadaye tutakuja kuanza kupigana sisi. Lakini vile vile tukumbuke kwamba tumeshaingia

mkataba na umeanza kufanya kazi wa nchi za Afrika kuweza kufanya biashara pamoja; na ninaamini wengi watakuja kufanyia kazi Tanzania kwa sababu ndiko kwenye amani, kuna furaha na rasilimali nyingi ziko huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama maji hayataonesha dira ya kuweza kutosha, kama maji hatutayawekea mipango maalumu, kama maji yatakuwa kwamba yoyote yule afanye analojisiskia, hiyo itakuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo tunaona kwamba maadam tumeshtuka mapema, tuwaombe si kwamba walikuwa hawafanyi kitu kabisa, tunaboresha mipango ile ambayo tayari wanayo; tunaomba sasa hata katika mpango huu mkuu wa dira ya Taifa ya 2050 suala la maji lionekane vizuri kinagaubaga ili hata tunapoiangalia dira yetu nyingine pia ya 2063 zote hizo ziweze kuwa pamoja ikihakikisha kwamba Tanzania tunakuwa na usalama wa maji, Tanzania inakuwa ni nchi tuitakayo sawa mabavyo Afrika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hayo pia kwa kusisitiza hili suala la mfumo wa *grid* ya taifa ya maji, hayo yamefanyika. Kwanza Mungu mwenyewe ametuumba kwa mfano ambao hata mishipa ilivyounganishwa ndio hizo *grid* zenyewe, sivyo? Kwenye umeme tumeshaona, na mambo mengine mengine. Kwa hiyo tunaposisitiza suala la kuchukua maji kwenye maziwa yetu kwenye mito mikubwa na maeneo mengine hatumaanishi kwamba sasa tumpe *pressure* Waziri, kwamba kesho apate fedha za kufanya mambo yote haya kwa mara moja, tunachohitaji ni kuwa na mipango inayoonesha kabisa kwamba eneo hili nitachukua maji kwa muda fulani, lakini baada ya hapo nitatakiwa nichukue huku na huku. Ikifika muda niwe nimeshajiandaa kwa ajili ya kuingiza maji kutoka katika chanzo fulani, lakini pia kuhakikisha kwamba hata mtumiaji mwingine hajakiharibu kile chanzo. Kwa hiyo hizi Wizara zikae pamoja katika kupanga hiyo mikakati mwisho wa yote tuwe na

mapango wa maji endelevu ambao utatuongoza huko katika dira kuu ya mwaka 2050 na maisha yetu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, nilikuwa napenda pia kuwaomba wenzetu wa Wizara ya Maji kuangalia suala la upatikanaji wa maji kwa bei nafuu. Kwa upande kama *TANESCO* kuna umeme unapataikana wa gesi, kuna umeme unapatikana wa maji, kuna umeme unaptikana wa *diesel* ukijumlisha pamoja unakuta bei ya umeme inapungua, kwa hiyo wananchi wote wanapata bei ambayo inafanana. Sasa kitendo hiki cha kuwa na sehemu za upatikanaji wa maji kila eneo kivyake, na *system* ya mapato imekuwa kila watu kivyao matokeo yake kuna maeneo kunakuwa na bei kubwa sana za maji wakati maeneo mengine wana – *enjoy* maji kwa bei nafuu zaidi. Kwa hiyo iko haja ya kuangalia mfumo wetu wa ukusanyaji mapato iili uweze kutoa unafuu katika baadhi ya maeneo ambayo yanapata maji kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya ulikuwa unataka kumalizia, muda wako kengele ya pili imelia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Basi nizidi kushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili mimi niweze kuchangia hoja

iliyoko mezani kwetu. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli amefanya kazi nzuri sana katika kuhakikisha kwamba mwanamke anatuliwa ndoo kichwani. Zamani tulifikiri siasa lakini tunaona kabisa ana nia na anadhamira ya kweli kuhakikisha kwamba wanawake sasa tunatuliwa ndoo kichwani, na amejua kutuheshimisha sisi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza Waziri wetu, Mheshimiwa Jumaa Aweso, amefanya kazi nzuri sana Pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Prisca Mahundi. Ana misemo yake usione vinaelea vimeundwa. Mheshimiwa Aweso anafanya kazi nzuri kwa sababu kuna mchango wa akina mama wale wawili ambao leo alitutambulisha pale juu, tena akina mama shupavu; wamemfanya atulie na kuzingatia kazi na Wizara inaenda vizuri. Tunawapongeza sana, utupelekee salamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona kobe yuko juu ya mti ujue amepandishwa. Niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumpandisha *Engineer* Kemikimba kuwa Katibu Mkuu, lakini vilevile kumpa unaibu Katibu Mkuu Cyprian Luhemeja. Tuseme sasa upele umepata wakunaji na Wizara itaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijawatendea haki kama sitampongeza Mkurugenzi Mkuu wa *IRUWASA Eng*. Kidegalu, lakini pia Meneja wetu wa Iringa *Eng*. Joyce, wanafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba vijiji vyetu vya Iringa vinapata maji na wanatekeleza miradi yao vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mkurugenzi wa *IRUWASA Engineer* Kalanje wameubeba Mkoa wetu wa Iringa.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa tu mzungumzaji, na nimuongezee tu taarifa yake kwamba ni sehemu ya Mawaziri wa ukituma *message* wanajibu, ukipiga simu wanapokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hata usiku wa manane tukimtumia *message* anapokea. Mkoa wa Iringa umekuwa wa kwanza katika utoaji huduma za maji safi na mazingira kati ya mikoa 26, ndiyo maana nimewapongeza sana viongozi wetu wa Mkoa wa Iringa. Tunashukuru Wizara kwa kuipatia *IRUWASA* miradi mikubwa ya kuboresha huduma za maji katika Manispaa ya Iringa, katika Miji ya Kilolo na Ilula kupitia chanzo cha Mto Mtitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wametoa kibali cha kutekeleza miradi ya kuongeza chanzo cha maji kata ambazo zilikuwa hazijapatiwa maji, nawapongeza sana Wizara ya Maji. Kwa mfano mji wa Ilula tumeweza kupata milioni 445.7, Mji wa Kilolo milioni 413.8. Tunaomba sasa tupatiwe sasa hiyo *advance payment* ya milioni 413.3 ili sasa mabomba yanunuliwe ili kazi ya usambazaji iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na suala la upotevu wa maji. Nimeona Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia upotevu wa rasilimali ya maji. Pamoja na rasilimali za maji kuwa adimu lakini kuna upotevu kati ya asilimi 30 na 40. Hii itaweza kudhibitiwa endapo kutafanyika matengenezo, kwa sababu kumekuwa na matengenezo ya mara kwa mara. Mabomba mengi yamekuwa chakavu sana na miradi mingi imekuwa ya muda mrefu, haikarabatiwi. Sasa, kama itakarabatiwa basi angalau tutapunguza upotevu wa maji mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto nyingine ni pamoja na upungufu wa watumishi, hasa fani ya ufundi sanifu na wahandisi. Lakini tunacho Chuo cha Maji, tena sasa hivi vijana wengi sana wanakwenda kusoma pale. Tunaomba sasa Serikali iwatumie wale vijana ili wapunguze upungufu ambao uko katika mikoa yetu ikiwepo hata na Mkoa wa Iringa. Pia kuna wafanyakazi wengi sana wana vibali tu, hawaajiriwi. Siku nyingi sana tumekuwa tukisema, kwamba saa ifike sehemu Serikali itoe vibali, kwa sababu hizi mamlaka zina uwezo wa kuwalipa mishahara, ili vijana hawa wasiendelee tu kuwa kwenye zile mamlaka miaka miwili mikataba miaka mitatu; na hasa Dar es Saalam ulikotoka Naibu Katibu Mkuu, na wewe unajua. Sasa waajirini wale vijana basi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia kuna tatizo la changamoto ya vitendea kazi zikiwepo gari, hasa Mkoa wetu wa Iringa pia kuna tatizo kabisa la ukosefu wa magari katika wilaya zetu zote. Tunaomba sasa Mheshimiwa Aweso awe na mkakati wa kuhakikisha kwamba vitendea kazi vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Wizara kwa kuanza mradi wa maji katika miji 28, hongera sana. Mradi huu ni wa siku nyingi, tumeuliza maswali mpaka tumechoka; lakini sasa hivi tunaona sasa umeanza kutekelezeka. Tumeona mkandarasi

ameanza kazi hata pale katika Mji wa Mafinga tumepata *tank* la lita 2,000,000 pale Changarawe, kwa hiyo tunaapongeza sana. Vilevile kuna mradi wa Matanana na Itimbo, visima vimeshachimbwa bado fedha ya usambazaji. Sasa, tunaomba basi Wizara ituletee ili wanawake waendelee kufaidika na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Jimbo letu la Isimani kwa Mheshimiwa Lukuvi tunaeona kuna mradi ule wa Kilolo – Isimani, tayari asilimia 90 umetekelezeka, na ule mradi unaanzia katika Kata ya Lugalo tunaomba pale kata zote au vijiji vyote vipatiwe maji sasa fedha ya usambazaji ndiyo inahitajika pia. Kuna mradi wa Pawaga unahitaji *treatment plant,* wananchi wanakunywa maji machafu sana. Hiyo yote ni fedha tunaihitaji Mkoa wa Iringa. Tuna miradi mingine tena bado kama mradi wa Kilolo. Mradi wa Kimara tunashukuru kwamba angalau umeshakamilika na wenyewe bado usambazaji. Mradi wa Uwambingeto unaendelea, na sasa uko asilimia 51, mradi wa Ifuwa tulipata bilioni 2.2 mkandarasi kalipwa asilimia 20 tu na maradi umesimama. Tunaomba pesa ende pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Kihesa – Mgagao – Masege wananchi wanapata shida mno, lakini bado uko kwenye uzabuni kila siku wanarudia tunaomba kazi ifanyike. Mradi wa Kata ya Kalenga kwa Mwenyekiti wetu. Kuna mradi wa Tanangozi – Tosamaganga mpaka Lupalama unahitaji ukarabati tu, tunaomba fedha ipatikane. Kata ya Nzii ma – *tank* mawili tayari tunaomba kazi ya usambazi maji. Lakini pia tunayo kata Mufindi Kusini, Ihoanza Malangali, Igunda. Mradi wa vijiji tisa, mradi wa Mtambula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee sasa kuhusu upungufu wa rasilimali maji. Takwimu zinaonesha upatikanaji wa maji kwa Mtanzania tangu tumepata uhuru hadi sasa. Wakati wa upatikanaji wa uhuru maji yalikuwa wastani wa lita za ujazo

10,000 kwa mtu mmoja kwa mwaka, lakini wastani huo umepungua sasa hivi ni lita za ujazo huo huo 2,250, ambao ni sawa sawa na upungufu wa lita 7,750 sawa sawa na asilimia 77.5. Upungufu huo umechangiwa na sababu zifuatazo; ongezeko la watu na mifugo, uharibifu wa mazingira, uchafuzi wa vyanzo vya maji, shughuli za binadamu, kilimo, ufugaji na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2022 Serikali ilifanya mabadiliko ya sheria, lakini sasa tunaomba Serikali ione umuhimu wa kuzingatia zile sheria ili wananchi tuweze kupatiwa. Haya maji bila kufanya hizi sheria zikawa zinafanyika kazi; maana tunaona sheria zinatungwa lakini utekelezaji wake unakuwa sio mzuri sana. Kwa hiyo tunajitahidi vyanzo vingi vinakuwa vinaharibiwa. Tunaomba sasa Serikali isimamie kikamilifu ili tuweze kulinda vyanzo vya maji na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampongeza Mkurugenzi wa Dodoma wa Maji *(DUWASA)* amejitahidi sana, kuna *population* kubwa sana hapa Dodoma. Lakini juzi tulienda pale Mtera tulienda na Waziri wa Maji, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mazingira na Waziri wa Nishati. Tumeona kabisa mambo ni mazuri pale tunaweza tukachukua maji kuyaleta Dodoma, kuliko kwenda kuchukua maji kule Mwanza kuyaleta hapa Dodoma gharama itakuwa kubwa sana. Mimi naona tuangalie huu mradi, kwanza hapa Jirani, kutoka Mtera kuja hapa. Sisi zamani tulikuwa tunafikiri labda itakuwa tatizo kubwa sana kuchukua yale maji ya Mtera, lakini jinsi tulivyoelezewa, alivyoelezea Waziri wa Nishati, wa Mazingira na wa Maji tumeona kumbe inawezekana. Kuna maji mengi sana yanafunguliwa yanapotea pale. Sasa basi yaletwe hapa Dodoma ili yaweze kusaidia wananchi, ili wananchi wa Dodoma waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba sasa Serikali iangalie hizi mita za maji, tuwekewe mita za maji kama ilivyo *TANESCO,* kwa sababu wananchi wengi wanalalamikia kwamba *prepaid meter…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mkono asilimia 200.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Nilimtaja Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Joseph Kamonga wajiandae.

**MHE. STANSALUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nitumie fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Vilevile nimshukuru sana Mungu wetu wa Mbinguni anayeishi kwa kuendela kutupa uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumza maneno machache sana. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, na katika ile hesabu ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja ya maika miwili ya mafanikio kwenye sekta ya maji ya Mheshimiwa Rais, sisi watu wa Nyamagana Pamoja na Jimbo la Ilemela kwa mama yangu pale Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula tunayo kila sababu ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu katika mafanikio ya miaka miwili Nyamagana tunaenda kuopata chanzo kingine kipya cha maji baada ya miaka 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tupigie mstari baada ya miaka 43 iliyopita ndipo tunaenda kupata chanzo kingine cha maji. Lakini pale Ilemela tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu pale Kabangaja tunategemea kuwa na chanzo kingine cha maji, tangu Ilemela imeanza, tangu Mwanza imekuwepo. Tafsiri ya vyanzo hivi viwili ni kwenda kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la maji kwenye Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela. Kwa hiyo tunamshukuru sana Rais na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu, yeye ndiye anayelala na mgonjwa na kwa sababu yeye ndiye anayelala na mgonjwa anajua matatizo mengi. Nimpongeze yeye na timu yake kwa sababu, ya kuokoa muda. Kila aliyeko kwenye Wizara ya Maji atambue kwamba, nimempongeza kutokana na kazi kubwa wanayofanya, wakiongozwa na Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu nchi hii, wamesema pale Mheshimiwa Hokororo na Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, tumekuwa na matatizo ya maji toka miaka mingi iliyopita. Nikizungumza leo Nyamagana hapa, miaka 43 iliyopita tulikuwa tunategemea chanzo kimoja peke yake kilichojengwa miaka ya 80 kikiwa na uwezo wa kuhudumia watu laki moja peke yake. Leo, miaka 43 baadaye tunazungumza chanzo kipya kinachojengwa kitakuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 48 kwa siku na kitahudumia ongezeko la watu zaidi ya 105,000. Hapa nataka kusema nini Mheshimiwa Aweso? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika pamoja na changamoto nyingi tulizonazo, safari aliyoianza Waziri toka amekuwa kwenye Wizara hii, sisi wenzake inatupa matumaini na faraja ya kwamba, iko kazi kubwa anayoifanya na Wizara yake. Nina hakika ni lazima tumuunge mkono na kumtia moyo kwamba, miradi ya maji siyo sawa na ujenzi wa nyumba, unaweza kufikiri asubuhi, ukajenga jioni, kesho umekamilisha na matokeo

yakaonekana. Kazi kubwa anayoifanya ndio itakayotupa sisi dira ya kule tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nyamagana kama nilivyosema, chanzo chetu cha kwanza kimejengwa miaka ya 80. Leo tunaongeza lita milioni 48 kwenye chanzo kipya, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita, mpaka hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake umesema mwenyewe tuko takribani asilimia 71. Ukweli usiopingika, kukamilika kwa chanzo hiki itakapofika Julai, tarehe 30, tutakuwa tumefanikisha kupata lita zipatazo jumla yake Kapri *Point* na Butimba zitakazofikia milioni 148 peke yake. Bado tunahitaji lita milioni 22 ili kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Nyamagana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoutaja mradi huu Mheshimiwa Waziri akumbuke ndio utakaowasaidia watu wa Magu na Misungwi, lakini maeneo yetu yote kwa sasa ambayo yanapata changamoto ya maji, ukienda kule Buhongwa, Rwanima, Kishiri, Igoma, Nyegezi, Mkolani, Luchelele, kote huko changamoto hii inategemea kukamilika kwa chanzo hiki. Sasa ushauri wangu Mheshimiwa Waziri; tunafahamu, Ilemela nimetaja chanzo cha Kabangaja, Nyamagana tunacho chanzo cha *Capri Point*, ili tuweze kuwa na uhakika wa maji kwa wakazi wetu wote kwa maeneo haya, tunahitaji uzalishaji wa chanzo cha Kabangaja pale kwenye Manispaa ya Ilemela, lakini tunahitaji uboreshwaji wa chanzo cha Butimba kitoke kuzalisha lita milioni 48 kwa siku mpaka lita milioni 160 ili tuweze kufikia malengo ambayo tumekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu na kila mmoja anajua Serikali yetu bado ni himilivu sana kwenye ukopaji na bado inazo sifa za kuendelea kukopa. Kama tuna uwezo wa kukopa au kushawishi na kushirikisha mashirika mbalimbali, kama tulivyofanya kwenye huu mradi ulioko Nyamagana leo,

tuendelee kuchukua fedha kwa sababu, tukikamilisha miradi hii tutakuwa tumeliokoa Taifa hili, tumewasaidia wanawake wa Taifa hili, tumeimarisha ndoa kama wanavyosema akinamama za Taifa hili na tumejenga umoja kwenye Taifa hili kwa sababu, tutakuwa na uhakika wa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kadri tunavyofanya nusunusu tafsiri yake ni kwamba, leo tumelaza bomba kilometa 17 kutoka Butimba kwenda Sahwa ambapo maji yatakuwa yanapokelewa kutoka kule Butimba, lakini kutoka Sahwa kwenda Igoma kwenye tenki linalozalisha lita milioni tano. Maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukilazimika kuja kuongeza miaka miwili baadaye itatulazimu kuweka mfumo mpya wa ulazaji bomba, ili liweze kuendana na chanzo tutakachokuwa tumekijenga. Tukikamilisha vyanzo hivi sio mbaya, tunahitaji takribani bilioni 400 kwa mujibu wa wataalamu walivyofanya na bilioni 400 sio nyingi kwenye kuzalisha maji kwa sababu, Mamlaka ya Maji ya *MWAWASA* inao uwezo mkubwa wa kujiendesha yenyewe kama itakuwa na uhakika wa kusambaza maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, watendaji wake wote wa Mamlaka ya Maji ya *MWAWASA,* nafahamu wananchi wa Nyamagana wanazo changamoto, lakini hakuna safari tunayoweza kufika bila kutembea. Hakuna safari tunayoweza kufika bila kuchukuliana. Kazi hii ni kubwa, haijaanza leo na ndio maana nimesema, Waziri Mheshimiwa Aweso chini ya Serikali ya Awamu ya Sita anaingia kwenye rekodi ya Jimbo la Nyamagana na Wilaya na Jiji la Mwanza kwa kuwa wa kwanza kuhakikisha chanzo cha lita milioni 48 kinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka kazi hii aliyoianza kwa muda mrefu itawasaidia sana, lakini hatuwezi kukamilisha chanzo peke yake bila kukamilisha maeneo yatakayopokelewa maji na usambazaji. Nafahamu tunatarajia au tunakusudia kujenga tanki moja kule Rwanima, Mtaa wa Kagera, litakalobeba lita milioni 10, lakini kule Rwanima yenyewe lita milioni tano, Mtaa wa Kasese kule Mkolani lita milioni tano, ili tuweze kuwahudumia watu wa Luchelele. Pale tuna Chuo cha *SAUT* peke yake kinahitaji maji yasiyopungua lita milioni 10 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri alitazame Jiji la Mwanza ambalo ni kilometa zisizopungua saba kutoka kwenye maji mpaka kwenye chanzo na usambazaji wake, ukichukua eneo lote la Nyamagana, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri ni eneo ambalo linawezza likatushangaza na likatuletea mapato mengi kupitia Mamlaka ya Waziri ya Maji na akafanya kazi nyingine na mamlaka hii inaweza kusaidia kuzalisha fedha zitakazotoa huduma kwenye maeneo mengine. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeupiga mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema nampongeza sana Mheshimiwa Aweso. Miradi ya maji ni safari na safari hii ameianza vizuri na anaenda nayo vizuri, ni wajibu wetu kumuunga mkono, ni wajibu wetu kumuunga mkono sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, malengo na mafanikio yanaonekana. Mabadiliko tunayoyaona kwenye bajeti ya kila mwaka ndio tafsiri ya utekelezaji na matokeo yake. Nimshukuru sana na nimpongeze, watu wa Nyamagana wanamsubiri Waziri kwenye uzinduzi wa chanzo hiki cha maji pamoja na Mheshimiwa Rais, ili waje waone faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe babu, unajua Waziri Mheshimiwa Aweso ni babu yetu, unajua Waziri ni mjukuu wa

Wasukuma, kwa hiyo, kila analolifanya ahakikishe babu zake wasimtie laana mzee na safari hii umepata Naibu Katibu Mkuu hapo na yeye ni mjukuu wake, kwa hiyo, ahakikishe kazi hii inakwenda vizuri sana. Mungu awabariki sana, nawashukuru sana, ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Nilimtaja Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Maimuna Mtanda ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko Mezani ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumpongeza kidhati Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Bwawa la Kidunda shilingi bilioni 329.46 limesainiwa. Bwawa la Kidunda linaenda kuwa Suluhu ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye Mkoa wa Dar-es-Salaam. Kazi hii ni kazi kubwa, Mheshimiwa Rais anastahili pongezi kubwa sana. Katika miaka yake miwili moja kati ya mambo makubwa aliyoyafanya ni kuhakikisha tunapata chanzo cha uhakika cha maji kwenye Mkoa wa Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kidhati Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso. Waziri huyu tukianza kutaja sifa zake hapa muda wangu utaniishia, niruhusu nitaje chache. Mheshimiwa Aweso ni mtu mnyenyekevu, Mheshimiwa Aweso ni mtu mpole, Mheshimiwa Aweso anafikika, Mheshimiwa Aweso ni Waziri ambaye ukikutana naye barabarani unaweza ukasema sio Waziri, hajakivaa cheo. Mtu hajapata cheo bali cheo kimempata mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo methali ya Kichina kwamba, kiongozi bora uongozi wake unaanzia nyumbani kwenye familia yake. Mheshimiwa Aweso huyu anaongoza familia mbili vizuri sana na ndio maana Wizara hii haimpi tabu. Sisi hatuna kubwa zaidi ya kumwombea dua; "*Rabbana aatiina fii dduniya hassana wafil akhirat hassana.*" Mwenyezi Mungu ampe neema yote ya hapa duniani na hata akhera, aendelee kufanya kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amepata Katibu Mkuu mzuri, *Engineer* Nadhifa Kemikimba ni mtu aliyekulia kwenye Wizara ya Maji. Kama lile suala la *institutional memory* hapo ndio mahali pake. Mama mpole, mnyenyekevu ana sifa zote za utumishi wa umma. Tunaona timu hii inaenda kutekeleza ajenda ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kiasi kikubwa na Ilani ya Uchaguzi itatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi pale Dar-es-Salaam tulikuwa na mtu bingwa kabisa, *Engineer* Cyprian Lwemeja aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa *DAWASA*. Ingekuwa ni usajili labda sisi tungemkatalia kumsajili huku Wizara ya Maji, mtu bingwa, mtu mzuri, anacheza kama Aziz Ki alivyofanya leo pale Uwanja wa Taifa. Naibu Katibu Mkuu huyu naamini ataisaidia Wizara na Taifa hili katika kutekeleza kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kwenye Mkoa wa Dar-es-Salaam imefika asilimia 95, lakini kwenye Jimbo la Ukonga, jimbo ambalo ndio linaongoza kwa watu kwenye nchi hii, watu 921,957 tuko asilimia 57, lakini Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ziada ya ule mradi uliotoka Ruvu Juu ukapita Kibamba, ukaenda Kisarawe, ukaja pale Pugu, sasa kuna mradi mwingine kule Zingiziwa, Somelo, Ndiole Juu kwenda Msongola, lakini *DAWASA* wanaenda kutekeleza mradi mkubwa wa thamani ya shilingi bilioni 42, Kata

ya Kitunda, Kata ya Kivule, Kata ya Mzinga, Kata ya Kipunguni mpaka kule Chamazi kwa Mheshimiwa Chaurembo na Temeke kwa Mheshimiwa Kilave, wanaenda kupata maji haya na sisi Jimbo la Ukonga tunaenda kufikia hii asilimia 95 ya maji kwenye upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii kule naomba nichukue fursa hii vilevile kumpongeza *Engineer* Sirila, Mwanamama huyu Mhandisi, Meneja wa Wilaya ya Ukonga ya maji na *Engineer* Alex Wandu ambaye anahudumia Wilaya ya Kisarawe, lakini anahudumia maeneo ya Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, kazi hii inayofanywa inaenda kuheshimisha Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Serikali hii iliahidi upatikanaji wa maji kwa asilimia 95 mijini, kazi inayofanyika bilioni 42 hizi za mradi mpya, bilioni saba zile za Mradi wa Pugu - Kisarawe, bilioni 11 za ule Mradi wa Somelo, bilioni 60 zinaenda kuwekezwa kwenye Jimbo la Ukonga ni kazi kubwa sana. Sisi watu wa Ukonga tunasema ahsante sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kweli wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, bilioni 60 hili sasa ni sinia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni kubwa, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri mwaka 2021, amesoma Pugu kama mimi na amepata shida ya maji, *no wonder* anafanya kazi ya maji vizuri. Alikuja Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais pale Pugu na aliendá pale *Pugu Secondary* kuona maji yalivyofika kwenye shule ile ya historia ya nchi yetu. Aliahidi mradi ule atakuja kuufungua yeye mwenyewe. Tunaomba Waziri afikishe salamu zetu, tungefurahi kumwona anakuja kuzindua mradi ule wa maji maana ameahidi kufikia Disemba, 2023, Jimbo zima la Ukonga litakuwa limepata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawili madogo ya mwisho, niwapongeze sana. Kama alivyosema Mheshimiwa Mabula, watendaji wote wa Wizara ya Maji, wako wengi, lakini ninaamini watendaji wengi wamepata unyenyekevu na uchapakazi kutoka kwa Waziri wao. Ukienda *RUWASA* ingawa haihudumii Dar es Salaam, Clement, Kivugalo Mtendaji Mkuu, ni mtu mwema hata alivyotambulishwa asubuhi niliona Wabunge wengi wakipiga makofi, aendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wangu, Haji Nandule, *CEO* wa Mfuko wa Maji, amesema pale anafanya kazi nzuri. Ni watu ambao Mheshimiwa Aweso kwa ukaaji wake kwenye Wizara hii ametengeneza timu nzuri na anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe kusema naunga mkono hoja. Naomba sana tupitishe bajeti hii kwa mikono miwili, ili kazi hizi za maji ziende zikamguse Mtanzania na kumtua mama ndoo kichwani, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerry Silaa. Nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia machache yanayohusiana na masuala ya maji.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli, kazi anayoifanya ni kubwa na sisi Watanzania na sisi Wanamtwara na sisi Wananewala tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema sisi Wanamtwara, sisi Wananewala? Ametoka kuongea hapa Mheshimiwa Hokororo akautaja Mradi wa Maji ule wa Makonde ambao ni mradi wa muda mrefu, uliasisiwa na watu wa Finland muda mrefu, ukachoka, ukawa hauhudumii wananchi ipasavyo, mabomba yalishachoka sana. Awamu kwa awamu tukawa tunaomba fedha ili mradi huu ukapate kuboreshwa, lakini ilishindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso amefika Newala akaliliwa na wazee, yeye mwenyewe ni shahidi, kwa kero ya maji ambayo wananchi wa Newala walikuwa wanaipata, lakini tunashukuru sana Serikali ikatupatia bilioni 84.7 kupitia Mradi wa Miji 28. Kwa kweli, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha tumezipata. Matarajio ya Wananewala, Wanatandahimba na watu wa Nanyamba ambako mradi huu unapita ni kwamba, wanachotaraji ni kuona mradi unatekelezwa ipasavyo, unatoa maji, ili wananchi wa maeneo niliyoyataja sasa na wenyewe waanze kutumia maji ya bomba, maji yaliyo safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupeleka fedha hizo tunajua kazi zimeshaanza, maeneo ya kujenga matanki yameshaanza kusafishwa kwa kila eneo. Kwa mfano Newala, Newala Mji, pale Nambunga, Newala Vijijini, Nanda, Tandahimba, lakini pia na kule Nanyamba, tunatakiwa kuweka usimamizi wa dhati pamoja na kupeleka fedha kama usimamizi hautakuwepo, tija ya mradi hatutaipata. Sisi tunategemea kwamba, ifikapo Juni, 2024 wananchi wa maeneo yanayopitiwa na mradi huu waanze kunufaika na mradi huu, lakini tukiacha kusimamia ipasavyo matokeo hatutayaona. Ipo miradi ambayo tunaishuhudia kwa macho haisimamiwi ipasavyo, matokeo yake ni kwamba, huduma kwa wananchi hazifiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mradi ukasimamiwe, lakini kusimamiwa huko kutategemea wale watu wa Makonde hawana gari la uhakika la kufuatilia huu mradi kwa uhakika. Niiombe Wizara, nilisikia kulikuwa na tetesi ya kupatiwa gari, watu wa Makonde wapatiwe gari ili waweze kusimamia vizuri mradi huo ukalete manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa lazima niongee kwa sababu, kupata fedha bilioni 84 kwa mkupuo sio jambo rahisi. Ni kazi kubwa sana ilifanyika mpaka na sisi tukawa wanufaika wa mradi huo. Mradi huu ili ukafanye kazi itakayoonekana vizuri na wananchi wote waweze kupata maji, ukienda kwenye Jimbo la Newala ipo miradi mingine ambayo kama itakamilika na kufanya kazi vizuri, basi tija ya mradi mkubwa huu itaenda kuonekana kwa wepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Mlima Miuyu, upo unatekelezwa katika Jimbo la Newala Vijijini. Mradi huu ni wa muda mrefu. Ulikuwa ni mradi wa miezi tisa kuanzia mwaka 2018/2019, lakini mpaka leo haujakamilika na haujakamilika, inawezekana kuna changamoto za wakandarasi, lakini Wizara pia, hawajawakamilishia fedha. Mradi ulikuwa wa bilioni 1.3 lakini fedha ambazo zimelipwa ni milioni 614 pekee. Niiombe sana Wizara itafute kwa nini fedha hazijaenda, kama shida iko kwa wakandarasi tuwasimamie wakandarasi wetu, kama shida ni ya Wizara, Wizara pelekeni fedha na waje watuambie ni lini fedha zitaenda. Mradi wa miezi tisa wa 2018 mpaka leo tunaongea, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu pamoja na mimi mwenyewe kwenye maeneo yetu, hatujawahi kuona maji ya bomba. Sasa hii miradi ambayo imeshaanza kwenda angalau basi, ikasimamiwe vizuri. Kwa kiasi fulani nashukuru kwenye huu Mradi wa Miyulu, angalau msimu wa mwaka jana, kaingazi cha mwaka jana, ile *pressure* kali, fedha ambazo tulikuwa tunalipa

kule nyuma kwa ndoo ya lita 20 kulipa kwa shilingi 2,000, msimu wa mwaka jana ilipungua kwa sababu, angalau hii miradi kidogo ilikuwa inaanza kutoa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri asimamie, kumbe inawezekana, mambo mengine ni masuala tu ya umeme, mara umekatwa, ukiuliza kwa nini fedha hazikupelekwa umeme ukirejeshwa maji yanatoka. Niombe sana, tusimamie, tuone tija ya miradi ambayo inakwenda

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kutopatikana kwa maji ni nyingi, ukienda leo Jimbo la Newala Vijijini pamoja na Newala Mjini, kuna miradi ambayo haikamiliki kwa wakati kwa sababu tu ya ukosefu wa maji. Mradi unapelekewa fedha, wananchi wako tayari kutoa nguvu zao, wanahangaika kumaliza maji kwenye visima. Kule kwetu kwa sababu ya changamoto ya maji kila nyumba inayojengwa inakua na kisima, tunavuna maji, lakini maji yale kwa bahati mbaya hayatibiwi, tunayatumia hivyohivyo, ni yale maji ya kuokota, ndiyo maji ambayo sasa inapotokea miradi kwenye kijiji wananchi wanajikusanya wanaenda kuchukua maji yao kwenye visima wanaenda kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine yale maji yanaisha, kwa hiyo miradi unakuta haitekelezeki kwa wakati sahihi kwa sababu ya ukosefu wa maji. Tunakuja tunawalaumu sana Wakurugenzi wetu lakini wakati mwingine wana changamoto hiyo ya maji. Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie, maji Newala sasa ije ibadilike historia, mmeshaanza kuandika hiyo historia kwa kupeleka fedha nyingi, tunaomba sana wananchi wa Newala nao wanataka kuondokana na kero ya maji, kuondokana na kero ya maji ya kuokota kwa kupatiwa maji ambayo yatatoka kwenye mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingine midogomidogo kwenye maeneo yetu. Miradi ambayo ikienda nayo kupelekewa fedha basi changamoto kubwa sana tutakuwa tumeipunguza Mheshimiwa Waziri wetu. Kwa mfano, kuna mradi wa usambazaji wa maji wa vijiji vya Mkudumba – Mnyengachi na Mdimba – Mnyambe – Mnima na Bahati. Pia upo mradi mwingine ambao unajumuisha Vijiji vya Mikumbi, Mkongi, Nyamangudu, Nangujane, Chirende, Mkomato pamoja na Lihanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ipo kwenye mpango lakini tunaiombea sana ipate fedha. Kukamilika kwa miradi hii kutakuwa na sura nyingine ya Newala, sura ya Newala haitakuwa ile ambayo tumeizoea siku zote. Kuna watu wanarudi Newala wanakataa kufanya kazi kwa sababu ya shida ya maji. Mtu anafika Newala unatumia maji kwenye kile kikopo, kinaitwa kidosho, anapewa kile aoge, hawezi. Atakaa siku ya kwanza, mwezi wa kwanza anaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni afya, maji ni uhai, magonjwa mengi yanatokana na ukosefu wa maji. Tunaipa Wizara ya Afya mzigo mkubwa wa kutibia wagonjwa, magonjwa ambayo kumbe yangeweza kuzuilika kama maji safi na salama yangeweza kupelekwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuombe sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na mtani wangu Mheshimiwa Mahundi, chondechonde, tunaomba usimamizi na upelekaji wa fedha uende ili wananchi wa Newala wapate maji, tuigeuze Newala, maji Newala ni shida kwelikweli. Kila mtu atashangaa kama watayaona maji Newala kwa hali ya Newala jinsi ilivyo miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mvua zimeanza kukata tumeshaanza kupata hofu, kwa sababu kuna maeneo mvua hazikunyesha vya kutosha kwenye maeneo hayohayo ya Newala, kwa hiyo hata visima vyao vile vya asili havina maji. Kwa hiyo hapa sasa hivi mvua inavyoanza kukata tunaanza kupata hofu. Hivi sasa hivi mvua imekata tutaishije kwa miezi yote mpaka masika yaje, kwa sababu masika ndiyo mkombozi wetu, lakini kwa dunia ya sasa ilivyo kutegemea masika peke yake hapana Mheshimiwa Waziri. Tunaomba tuondokane na suala la kutumia visima, tuondokane na maji ya kuokota, wakati sasa umefika nasi tufaidi, tuone raha ya kutumia maji ya bomba.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi yako, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda. Nilimtaja Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Joseph Kamonga ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa uhai kuweza kusimama hapa kwa siku nyingine. Pili, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Jumaa Aweso, kwa kutuletea bajeti nzuri na kwa kazi yake nzuri. Niwapongeze vilevile Naibu Waziri, Dada yangu Mheshimiwa Mahundi na Watendaji wote ndani ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Injinia Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu. Kwa namna ya pekee, Jimbo la Njombe, mimi ndiye Mwakilishi wao, naongea kwa niaba ya wananchi wa Njombe, ninawapongeza sana Maafisa wa *RUWASA* ambao nimekuwa nikifanya nao kazi

kwa karibu sana katika siku zote hizi. *Resident Manager* Ndugu Shaka na Injinia Malisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Njombe lina mjini na vijijini na nitaiongelea hiyo kama moja ya sehemu yangu kubwa ya mchango wangu wa leo. Kwa hiyo nimpongeze Injinia Kyauri ambaye ni *MD* wa *NJUWASA* kwa maana ya kwamba yeye ana-*cover* eneo la mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo makubwa sana ya Mji wa Njombe toka nimeingia hapa Bungeni ilikuwa ni ukosefu wa maji katika Mji wa Njombe na katika vijiji vyake, jambo hili lilikua linaleta sintofahamu kubwa kwa sababu Njombe tuna vyanzo vingi vya maji, nami ninapenda toka ndani ya roho yangu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mtu wa kwanza kutukomboa kwenye matatizo ya maji. Maji bado hayajaanza kutoka lakini tuna miradi ambayo inaleta matumaini makubwa sana kwa Mji wa Njombe kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mikubwa mitatu pale Njombe Mjini ambayo italeta maji kwenye eneo la mji, pia tuna mradi mkubwa sana, naishukuru sana Serikali, mradi wa Benki ya *Exim* - India, mradi huu tumeungojea kwa hamu, sasa tunajua Wakandarasi wameanza kazi, kwa hiyo tuna uhakika sasa ahadi ambayo Chama cha Mapinduzi kilitoa kupitia Ilani, mimi Mbunge niliitoa na Mheshimiwa Rais akitembelea Njombe aliitoa kwa wananchi, kwamba utakapofika wakati wa uchaguzi tutakuwa na maji yanayomwagika, kwa lugha ya kwetu tunaita maji bwerere pale Njombe. Nafurahi sana kwamba mambo haya tutakwenda kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mradi mwingine nimeuona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Aweso wa majitaka. Mji wa Njombe unakua kwa haraka sana na sasa tuko katika

maandalizi ya kuomba kuwa manispaa. Kwa hiyo kwetu mradi wa majitaka ni mradi muhimu sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa Aweso na timu yako nzima kwa kuona umuhimu wa kuipa Njombe mradi huu kwa wakati huu, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo la pili ambalo ni kubwa sana kwangu. Nashukuru sana nina ushirikishwaji mzuri sana katika kupanga miradi hasa ya vijijini, katika kufuatilia nikagundua kwamba baadhi ya miradi ambayo tulitegemea tungeipata mwaka huu katika vijiji vyetu haijaingizwa kwenye mpango, nilivyozidi kudodosa na kuuliza nikakuta kwamba tuna mradi mkubwa wa Benki ya Dunia unaitwa *P4R* (Utaratibu wa Malipo kwa Matokeo) bilioni 350. Nilikuwa na matumaini makubwa sana kwamba vijiji vyetu vitaingia katika mradi huo, lakini kwa bahati mbaya sana havimo, maelezo yanaonekana kama yana-*make sense* lakini nilipenda nieleze na Mheshimiwa Aweso anisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumeondolewa kwenye mradi huu ambao ni muhimu sana kwa wananchi wa Njombe. Njombe ni Njombe Mjini lakini asilimia 40 ya Njombe Mjini iko mjini, asilimia 60 iliyobaki yote ni vijijini, vijiji zaidi ya 40. Sasa *complication* hiyo na mradi huo mkubwa ambao una-*cover* maeneo ya vijijini, Njombe Mjini haimo kwa sababu ina jina linaitwa mjini, lakini Njombe *actually* asilimia kubwa ni vijiji. Inayo Kata 13, lakini Kata 10 zote ni maeneo ya vijijini, Kata tatu ndiyo za mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, umbali wa vijiji vya Njombe vijijini, niite sasa vijijini ili ieleweke vizuri, unakwenda kilometa 120 nje ya Mji wa Njombe, lakini siyo hilo tu katika Halmashauri zote za mji katika Tanzania, Njombe ndiyo Halmashauri ya mji iliyo kubwa kuliko zote, ina *square kilometers* 3,210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira hayo ni kwamba lengo la kupeleka maji vijijini kwa asilimia 85, Mheshimiwa Aweso kwa ku-*exclude* Halmashauri ya Mji Njombe na Jimbo la Njombe Mjini, unakwenda ku-*distort* hiyo *figure* kwa sababu unabakia na vijiji vingi unavyoviona kwamba viko mjini lakini vyenyewe viko vijijini. Kwa hiyo ni vizuri sana jambo hili likaangaliwa upya tukawa *realistic*. Kuna majina hapa mimi nimeyakuta tu yako kisiasa, kuita Jimbo la Vijijini Mjini na hili jambo nimeshalifikisha TAMISEMI, tutaangalia huko mbele ili tusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, hili ni ombi mahsusi kutoka kwa wananchi wa Njombe, kwamba tunaomba sana tufikirie upya kwenye ule mradi mkubwa ambao una-*cover* maeneo ya vijijini. Tulikuwa na vijiji kama vitatu au vinne ambavyo tayari vilikuwa vinaingia kwenye hiyo *program,* kuna Kijiji cha Lilombwi, Kijiji cha Ihanga hakina maji ni kijiji kikubwa na kina uwekezaji mkubwa, hivi vijiji vyote vina wawekezaji wakubwa wa parachichi, mahindi, viazi ni watu wanajiweza, hata ukiweka mradi pale kulipia wala siyo tatizo. Kwa hiyo tuwaangalie kwa jicho tofauti, nimelisema hili kwa nguvu sana kwa sababu nina uhakika Wananchi wa Njombe wananitegemea na wanategemea majibu kutoka kwa Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Aweso, tuna mradi mwingine ambao nilipoingia hapa Bungeni ulikuwa mradi chechefu, mradi wa Igongwi. Maji ya mserereko ambayo yanakwenda kwenye Kata Nne, vijiji zaidi ya Kumi. Mradi huu tunaishukuru sana Wizara imeweza kutoa fedha kwa kiasi fulani mpaka hapo ulipofika. Mradi huu umefika hatua za mwisho, mradi huu bado una *lot* moja ambayo naishukuru tena Serikali kwamba imeingizwa kwenye bajeti hii, *lot five* kwa ajili ya kufanya mtawanyiko wa maji kwenye kijiji cha mwisho kabisa katika vijiji

zaidi ya nane. **Vijiji hivyo ni Kitulila, Kona, *Denseland*, Madobole, Luponde, Njomlole, Majengo, Uwemba na Ikisa.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso bado tuna tatizo, nina uhakika kwamba mradi huu unapata fedha kutoka kwenye Mfuko wa Maji. Mfuko wa Maji kwa mwaka jana tunaambiwa kwamba ulipokea karibu bilioni 105, na ilikuwa ni kati ya mwezi Aprili mwaka huu ulikua ni asilimia 60. Kwa hiyo, ni wazi miradi ni mingi sana na mahitaji ni makubwa na Mfuko wa Maji hauwezi ku-*cover* miradi yote. Ndiyo maana umesema kwenye hotuba yako na mimi naungana mkono na wewe kwamba ni lazima tutoe vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapanga vipi vipaumbele, umetuambia utapanga vipaumbele kukamilisha miradi ambayo imefikia hatua za mwisho ili wananchi waanze kupata maji. Nami napenda kusema mradi wa Igongwi umefikia hatua za mwisho kabisa, naomba sana kwamba mradi huu upewe kipaumbele katika kupewa fedha hizi za mwisho ili wananchi wa Njombe wa vijijini, vile vijiji vingine ambavyo vyenyewe viko vijijini kabisa, waweze na wenyewe kuanza kupata maji haraka iwezekanvyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha kwamba Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais, akiwa kwenye kampeni alisimamishwa na wananchi wa vijiji hivi walikusanyika na walimwomba sana vitu viwili, kimojawapo ilikuwa barabara hicho kimeshatekelezwa mkandarasi yuko *site,* pili ilikua ni kukamilisha mradi wa Igongwi. Kwa hiyo, ni matumaini yangu ukiongezea na nguvu na ahadi ya Rais mwenyewe kwenye mradi huu, tutaukamilisha kwa hizi hatua chache za mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kabisa, tumshukuru sana Mkandarasi ambaye alisimamia mradi huu, mradi huu

ulikuwa chechefu, tuliutoa ulikuwa mradi wa 2017 ulikuwa umekufa kabisa, 2020/2021 tumeuanza upya. Niendelee kusema kwamba Mkandarasi aliyesimamia mradi huu baada ya kuufufua amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yako na Kamati wamesema kwa kweli tutoe motisha kwa wafanyakazi na makandarasi ambao wanafanya kazi vizuri. Kutoa pongezi ni moja ya motisha nzuri sana, tusiogope kusema kama mkandarasi ametufanyia kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi huyu ana madai bado, ninaomba sana mkandarasi aliyefanya kazi nzuri kwa kujitoa kizalendo kama huyu *Jobea General Construction* kwa kweli tumfikirie tumkamilishie malipo yake maana yake ni miezi sita toka ame-*raise certificate* yake na kazi karibu ameimaliza, naishukuru sana Kampuni hii ya Jobea kwa kazi nzuri sana iliyotufanyia Wananjombe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus Mwanyika. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Kamonga, tutamalizia na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa upendo mkubwa kwa wananchi wa Jimbo la Ludewa na

Watanzania wote, kazi zake tunaziona. Sambamba na hilo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Dada yangu Naibu Waziri wake, hongera sana, kazi zenu ni nzuri na zinaonekana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa akifika kiongozi au Mheshimiwa Mbunge akienda kuwatembelea wana kawaida za kuandaa nyimbo zao za utamaduni, kuna nyimbo na ngoma za asili, wanaimba, wanacheza na wanakueleza mambo mazuri ambayo Serikali imefanya kupitia kwako Mbunge na mambo ambayo bado hayajafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilivyokwenda Kijiji cha Kisaula na Kijiji cha Lutala, wananchi walibeba maji machafu kwenye makopo wanacheza ngoma wakawa wanaomba maji, wanaomba sana. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumuomba sana Mheshimiwa Waziri. Ninakushukuru ulimtuma Naibu Waziri alikwenda kule akawaahidi wale wananchi wa Lutala kwamba ule mradi wa Iwena ambapo Serikali ilifanya kazi nzuri sana, mradi wa bilioni moja na milioni mia mbili, kuna matenki mawili ambapo maji yanamwagika, Mheshimiwa Naibu Waziri aliwaahidi wananchi wa Lutala kwamba ule mradi utakuwa *extended* kwenda kuwahudumia wale wananchi wa Lutala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru sana Serikali kwa dhamira hii njema kuwakomboa wale wananchi, kwa kweli wapo kwenye changamoto kubwa sana, ule mradi unaweza pia ukahudumia na pale Kisaula, ni muhimu sana. Kwa sababu Jimbo la Ludewa lina tarafa tano, kuna hii Tarafa ya Masasi kidogo ina changamoto na inahitaji uangalizi wa karibu na msaada. Nilipanga kusema mengi lakini nashukuru Mheshimiwa Waziri nimekaa nae ameniahidi atakuja Ludewa kwa ajili ya kusaini mkataba wa mradi wa maji Ludewa Mjini wenye thamani ya bilioni saba. Kwa hiyo, naamini nitapata muda zaidi wa kuongea naye pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishukuru sana Serikali kwa miradi mingi ya maji Ludewa. Tulipata bilioni 1.5 kwa ajili ya Mradi wa Maji Mavanga, tulipata bilioni moja kwa ajili ya mradi wa maji Mavala, tulipata bilioni 1.5 kwa ajili ya Mradi wa Kijiji cha Luvuyo, kule ambako na wenzetu wa Njombe wamechukulia maji pale Igongwi, tulipata milioni 900 kwa ajili ya mradi wa Lifua – Manda na miradi mingine mingi sana. Kwa hiyo, nipende kuishukuru sana Serikali. Niombe tu kwamba waendelee kuiangalia Ludewa kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yako Mheshimiwa Waziri kwamba wakandarasi waweze kulipwa fedha naomba ulisimamie sana, maana yake pale Mawengi tulipata mradi wa bilioni mbili, umesinzia kidogo Mkandarasi alikuwa anadai fedha, mradi wa Mavala ulikuwa pia umesinzia kidogo. Kwa hiyo, maelezo yako hayo ya kwamba wale wakandarasi waweze kulipwa naamini yatakwenda kutengeneza furaha kubwa sana kwa wananchi wa Mavala. Hata ziara yako utakapokuja Mheshimiwa Waziri itakuwa yenye baraka sana, utakuta ngoma zile za asili za kioda na mganda zina ujumbe wenye furaha na kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tarafa ya Mwambao, Kata ya Lumbila, Kata ya Kilondo, Kata ya Makonde, na Kata ya Lifuma. Hawa wananchi bado wanategemea maji kwenye asili *(nature),* wanakwenda kuteka Ziwa Nyasa. Ndiyo maana nilileta swali kuomba Wizara ifanye usanifu kuona ni jinsi gani wanaweza wakatumia maji ya Ziwa Nyasa kwa baadhi ya kata kuweza kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba mradi huu unaweza kuwa na gharama kubwa kwa sababu utahitaji *pumping* ya maji kwa kutumia umeme, ndipo yaweze

kuhudumia wananchi. Tusiangalie gharama kwenye kuokoa uhai wa wananchi, kwa sababu anayepewa kazi ya kumpa mwanadamu maji, anapewa kazi ya kulinda uhai wa mwanandamu huyu. Kwa hiyo, naomba wananchi hawa kama wengine ambao tunashukuru, nao ifike siku waweze kutoa shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mamlaka ya bonde la Ziwa Nyasa, naomba sana waweze kufanya utafiti kwenye hili Ziwa kuangalia mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu mwaka huu maji yameongezeka sana kwenye ziwa. Ukiongea na wale wazee wenye umri mkubwa, wanasema hali hiyo ilionekana mwaka 1976. Kwa hiyo, kwa kuwa wataalam wapo, watusaidie waweze kwenda kufanya utafiti tuweze kujua chanzo. Kwa sababu kuna historia, kuna mwaka nchi jirani iliwahi kufunga mto maji yakaleta shida kidogo. Kwa hiyo, ni vizuri tukajua ili tuweze kuwaeleza wananchi chanzo cha maji kujaa kwa kiwango kile: Je, ni mvua tu au kuna sababu nyingine, ili wananchi waweze kuishi kwa amani kando ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niangalie huu mradi sasa wa pale Kipingu. Kijiji cha Kipingu kwenye Mto Ruhuhu kumekuwa na matukio ya wananchi kuliwa sana na mamba. Hivi sasa ninavyoongea, tunauguza mwananchi mmoja, na vifo vingi vimetokea kwa wananchi kukosa maji. Namshukuru Mwenyekiti wangu wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Deo Sanga na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Anthony Mtaka, walifanya ziara pale, waliweza kwenda kuwapa pole wananchi na kuwafariji. Kwa hiyo, waliahidi kwamba watashirikiana nami Mbunge, kuhakikisha wale wananchi wa Kipingu wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea na jirani zetu, Wilaya ya Nyasa, wanaweza wakachukua maji pale, inahitajika kama *roll* kumi tu, wakavusha kwenye daraja la Mto Ruhuhu tukaweza

kuwasaidia wale wananchi wasiende kuteka maji kwenye Mto Ruhuhu. Isitoshe, maji ya Mto Ruhuhu siyo salama sana. Kuna uchimbaji mkubwa wa madini eneo la Amani kule, Ibumi, Nkomang'ombe, Lihugai, wanachimba sana makaa ya mawe na dhahabu. Kwa hiyo, yale maji siyo salama sana. Kwa hiyo, ni vizuri wale wananchi wakatafutiwa chanzo mbadala ili waweze kupata maji ya uhakika ili wajiepushe na magonjwa mbalimbali ambayo yatawagharimu sana uchumi wao. Fedha watakazozipata badala ya kwenda hospitali, basi zitawasaidia kufanya mambo mengine iwapo watapata maji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia lile eneo la Mchuchuma na Liganga ambapo nimetoka kuishukuru sana Serikali kwa kushughulikia suala la fidia ambalo lilikwama, tunatarajia litakuwa na wananchi wengi sana. Pale Amani, Mundindi, namshukuru Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye bajei ameweka mradi. Pale Njelela kulikuwa na tenki lita 100,000 ambalo kuna Padre alituletea, ila tulikosa mtaalam wa ku-*survey* maji na kuyaongoza yakafika kwenye tenki. Nakushukuru umetuletea *Enginee*r mzuri sasa hivi, kwa kweli nakupongeza kijana, wananchi wana matumaini na mategemeo makubwa sana nawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu mradi ambao umeupeleka hapa Njelela na Mundindi, utakwenda kusaidia wawekezaji wale wa Mchuchuma na Liganga. Hata hivyo, mradi uliopelekwa bado ni mdogo, hauwezi kutosheleza idadi ya watu ambao tunawatarajia watakwenda eneo lile la Amani pale Mundindi, na eneo la Njelela. Kwa hiyo, kadhalika na kule kwenye makaa ya mawe, Mchuchuma, Makaa ya mawe yana athari. Ukisoma ripoti za kimazingira. Kwa hiyo, wananchi wanatakiwa wapewe maji mbadala. Kwa hiyo, wale wananchi wa Lifua, Liugahi, Nkomang'ombe, Malamba, nao wanahitaji wapewe maji mbadala na tuweze kuangalia idadi ya watu ambao watakwenda kuishi pale kutokana na uwekezaji

mkubwa ambao Serikali inakwenda kuufanya pale. Halikadharika kule Liugahi iwapo wananchi wale watatumia maji yale ya kwenye mito ambapo makaa ya mawe yanatiririsha maji, ni hatari sana kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja, na nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri, kwani ametutoa mbali. Alipotukuta na sasa kuna mabadiliko makubwa. Kule Ludewa tumepata miradi mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Nilimtaja Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii nyeti. Nawapongeza watani zetu Yanga, kwa jitihada kubwa walizozionesha kwa kuliwakilisha Taifa vizuri. Hongereni sana. Hicho wana Simba ndicho tulichokuwa tunakitaka, msiwe mnadandala dandala tu, pigeni mzigo, boli litembee, mlete ushindi na heshima ya Taifa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo. Maji ni afya, maji ni biashara, maji ni chakula, maji ni dawa, maji ni kila kitu. Nianze na Jiji la Dodoma. Nitambue jitihada zinazoendelea za kwenda kupata maji safi na salama yenye uhakika kwa jiji la Dodoma. Jitihada hizi bado hazileti matumaini kwa wanajiji wa Dodoma kulingana na miradi iliyowekwa ambapo miradi hiyo ni mikubwa na itatekelezwa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, maana yake nini? Wanajiji la Dodoma bado tutaendelea kuteseka na ukosefu wa maji ya uhakika ndani ya jiji hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiji la Dodoma lina mradi unaotarajiwa kuja kumaliza changamoto ya maji Dodoma ni *Farkwa.* Pia tuna mradi wa Ziwa Victoria. Miradi hii yote haiishi leo wala kesho, ni zaidi ya miaka sita. Nikawa najaribu kufikiria, kama miradi hii inatupeleka miaka sita, hiyo ni michache, labda mpaka nane, kumi, jitihada gani za Serikali kwa Wizara yako inayokwenda kuzifanya kwa ajili ya kuhakikisha tunapata maji safi na salama na yenye uhakika kwa kipindi hiki ambacho ninyi mnaendelea na michakato hiyo kwa ajili ya Ziwa Victoria pamoja na *Farkwa*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kuna visima Nzuguni mmechimba. Vile visima mbona navyo vinachukua mchakato wa muda mrefu? Tangu tumekwenda kutembelea mwaka 2022 mpaka leo kuko kimya. Tunaomba hiyo miradi ikamilike mpunguze hiyo *jam* kwenye Kata ya Nzuguni, Kata ya Ipagala na Kata ya Kisasa ili yale maji yaliyokuwa yanatoka Mzakwe kuja kwenye hizi kata yaweze kugawanyika yaende kwenye maeneo mengine. Wizara toeni fedha, mpeni Mkandarasi asambaze maji kwenye vile visima ili tupunguze hiyo adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mchakato wa Ziwa Victoria, upembuzi wa awali umekamilka, Farkwa, halikadharika, hivi ni nini kinachosuasua mpaka leo? Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja utawaambia wana Dodoma changamoto ambayo bado ipo inayosababisha kutokuendelea na miradi hii miwili ni nini? Nitaomba uje uwaambie wanajiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, miji 28, Waheshimiwa Wabunge wamesema; Chemba Mkandarasi ameripoti, amefika, lakini Mheshimiwa Waziri Mkandarasi huyu karipoti. Jimbo la Chemba lina vijiji 114, kata

26, na vitongoji 436. Jimbo hili kati ya vijiji 114 lina vijiji 47 tu vyenye maji. Vingine vilivyobaki havina maji. Tunatarajia na tunaendelea kutarajia na kuiomba Serikali kubadilisha mtazamo wa maji ya *Farkwa* kutokuja Chemba, kwa sababu mtakuwa hamtutendei haki. Mradi huu wa miji 28 unakwenda kutekelezwa Chemba na viunga vyake. Ina maana tutatekeleza kwenye vijiji visivyozidi vitano. Kwa hiyo, jumlisha 47, tutakuwa na vijiji 52. Angalia huo upungufu wa maji kwa Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatamani na tunawaomba sana, mradi wa *Farkwa,* maji tupate na sisi wana Chemba, ndiyo suluhisho letu, badala ya kutuambia, mnatoa maji *Farkwa,* Wilaya ya Chemba ambako ndiko maji yanakozalishwa, mje myapitishe yaende Bahi, yaje Chamwino, yaje Dodoma Mjini, Chemba tubaki tunatazama tunapiga picha. Hatutakubali hicho kitu mkifanya kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kuondokana na changamoto ya maji kwenye Wilaya ya Chemba, ulitupatia mabwawa matatu; mabwawa mawili yamekamilika. Tuna suala la bwawa la Kiboka, Mkandarasi alileta *certificate* tangu mwaka 2022 mwezi wa Kumi na Moja, hamjampa *advance payment.* Tunaomba huyu Mkandarasi apewe *advance payment* aweze kwenda *site* aanze mradi ule ili nasi tuondokane na hiyo adha ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitambue jitihada kubwa za mamlaka zetu za maji zinazofanya huko kwenye Mikoa yetu na kwenye Wilaya zetu. Katika jitihada hizo zote mamlaka za maji wanazozifanya, bado wana changamoto kubwa ya ukusanyaji wa madeni kwa watumiaji wa maji. Kwenye hili Waziri nitakuomba, Mamlaka zako naomba uzisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana naomba nizitaje chache kuhusiana na madeni haya. Naomba nianze na mamlaka *RUWASA,* imeshindwa kukusanya Shilingi milioni 119, ziko huko, hawajakusanya wao; *DUWASA* Shilingi bilioni 207; *SUWASA* Shilingi milioni 532; *KUWASA,* Shilingi bilioni 1.7; *MUWASA* Shilingi bilioni nne; *DUWASA* Shilingi bilioni 6.7; *MWAUWASA* Shilingi bilioni 6.9 na *DAWASA* Shilingi bilioni 11. Hizo chache! Jumla kwa haya madeni yote ukijumlisha ni Shilingi bilioni 31.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii laiti ingekusanywa vizuri, ingetusaidia kuwasaidia na wenzetu wengine wa vijijini kuhakikisha nao tunawaboreshea mazingira bora ya upatikanaji wa maji safi na salama ya kunywa. Wanafanya kazi kubwa, tunaitambua, lakini tunaomba uwasimamie waongeze jitihada ya ukusanyaji wa madeni kwa watumiaji maji kwenye maeneo yao waliyosambaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, tasisi za Serikali zinazodaiwa na mamlaka ya maji pia tuziombe zilipe madeni yao zimalize ili taasisi hizi ama mamlaka zetu hizi, ziweze kujiendesha na ziendelee kutoa huduma za maji kwa watumiaji wengine wa maji ambao mpaka sasa bado hawajapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la majitaka kwa Jiji la Dodoma na majiji mengine. Bado tuna changamoto ya majitaka katika nchi yetu na hususan Jiji la Dodoma. Niliona jana Mheshimiwa Waziri ukisaini mikataba kwa ajili ya mchakato sasa wa kwenda kuhakikisha tunaanza miundombinu ya uondoaji wa majitaka ndani ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *speed* ni ndogo, kutoka asilimia 20 mpaka kufikia asilimia 40, Mheshimiwa Waziri tunaomba mpambane. Hizi fedha ambazo leo *DUWASA* wameshindwa

kukusanya Shilingi bilioni sita, na pia kuna upotevu wa maji yanapotea huko barabarani kutokana na miundombinu mibovu; hizi fedha wangekusanya wangeweza kusaidia pia kwenye suala la uwekezaji kwenye miundombinu ya majitaka na hatimaye Jiji hili likaendelea kuwa safi na watu tukaepukana na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *speed* wanayokwenda nayo ya kwenye suala zima la majitaka tunaomba waiongeze, ni eneo ambalo wamelisahau sana. Kwa hiyo, tunawaomba sasa twendeni kwenye suala zima la uwekezaji wa majitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo nilitamani kulisemea ni suala zima la upandishaji wa *bill* za maji. Kumekuwa na utaratibu wa mamlaka zetu kwamba wanakwenda, wanaona gharama za uendeshaji zimekuwa kubwa na kuamua kupandisha bili za maji. Wamekuwa wakitumia mfumo wa kutuma ujumbe kwenye simu za wateja ili kwenda kushiriki kwenye vikao vya kupandisha maji, lakini taarifa zile, na huu ni mkanganyiko wa hizi taasisi; anayetaka kupandisha bili ya maji, tuseme ni *DUWASA*, lakini kibali anatakiwa apewe na *EWURA*, Wizara ya Nishati. Sasa huyu anayetakiwa kupewa kibali ili aweze kupandisha gharama ya bili za maji, yeye ndiye anayealika wajumbe ama wadau wa watumiaji maji kwenye huo mkutano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja. Mwezi uliopita, mimi binafsi na baadhi ya Wabunge tulipata *message*.

**MBUNGE FULANI:** Mmh!

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Saa 7.00 mchana ndiyo tunatumiwa *message* za kwenda kwenye kikao kesho, lakini ukiangalia hata hizo jumbe zenyewe namna zilivyotumwa, siyo

rafiki sana. Nikawaza kwamba aidha, kuna mbinu inayochezwa baina ya *EWURA* pamoja na *DUWASA* ili watumiaji wa maji wasiende wengi ili wao wapitishe kile wanachokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji, suala la kupata maoni kwa ajili ya kupandishwa bili za maji, wasiwe wanaalika mkutano wa hadhara wa kuja kukaa JK pale, waende chini kwa watumiaji wetu wa maji kule walikopeleka mita. Tuwaitishe mikutano; tuna taasisi zetu, tuna mifumo ya kitawala. Tuna Mwenyekiti wa Mtaa, Mwenyekiti wa Kijiji, tuna watendaji wako kule, wawape taarifa, waweke kipaza sauti, wawatangazie wadau wa maji, ili waende wakatoe maoni yao kuhusiana na sula zima la kupandisha bili za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitolea mfano Dodoma kwa sababu ndilo eneo ambalo nina uzoefu nalo. Dodoma leo tunapandishiwa maji, lakini kutokana na hali halisi tuliyonayo ya mgao wa maji, kwa mwezi tunapata maji siku nane. Siku nane ndizo tunazopata maji, sasa unataka unipandishie bili tena, kwa hiyo, unajikuta unaanza kuwaza, kama maji siyapati, kwa nini unataka kupandisha bili? Kwa hiyo, kwenye hili, nawaomba sana Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Nishati, angalieni namna bora na msiwe mnaona tu, wakati mwingine Mheshimiwa Aweso, haya madeni mamlaka zikusanye, ziache kukimbilia tu kwenda kupandisha bili, kuwaongezea wananchi mzigo. Wakusanye madeni yao, waboreshe mabomba yao ili upotevu wa maji usiwepo, maji yapatikane vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri, ili kuondokana na hizo gharama za madeni, tulikuomba hapa *pre-paid meter*. Lete *pre-paid meter*. Mmefunga kwenye baadhi ya taasisi, tunaomba na Watanzania wengine tupeni. Zipe mamlaka ziagize *pre-paid meter* wafungiwe watu. Moja utapunguza hata watumishi ndani ya Wizara, kwa sababu

umeme leo tunalipa ndiyo tunatumia, kwa nini maji tusilipe ndiyo tutumie? Tutaondokana na migogoro, na kusuguana na kunyoosheana vidole kusikokuwa na tija. Utaondokana na malalamiko ya ubambikizaji wa bili, utaondokana na malalamiko ya kila aina. Tutafutie *pre-paid meter* zitazoenda kutuletea ukombozi katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ndani ya Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Nakutakila kila la heri Mheshimiwa Aweso katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na watendaji wake wote, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Kunti Majala.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuwapongeza sana kwa kuwajibika vizuri tokea asubuhi na michango yenu ambayo ninaamini kabisa ina dhamira njema ya kuboresha sekta hii ya maji ambalo ni jambo muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia nawapongeza kwa kuwa na shukurani. Mnajua watu mara nyingi tunapokuwa tunashukuru kwa kile kidogo tunachokipata, basi na Mwenyezi Mungu hutia baraka. *(Makofi)*

Naamini kabisa Mheshimiwa Aweso na Mheshimiwa Mayprisca hapa walikuwa makini sana kusikiliza zile changamoto ambazo mmezizungumza, hasa zile zinatokana na miji inayokua haraka liwemo Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya nchi yetu sasa hivi. Basi nami naamini, na Watanzania tuwe na matumaini sana, kama ambavyo mmempa pongezi, hii yote inatokana na kauli mbiu ya kumtua mama ndoo

kichwani, ambayo aliitoa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akiwa Makamu wa Rais. Kwa kweli hii ndiyo inachangia utekelezaji mzuri, kwa kuwa dhamira yake ilikuwa njema kwa nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamini, ndiyo maana Mwenyezi Mungu akajalia na Wizara ikapata watu wazuri, na watendaji ambao wote wametajwa hapa, na ambao hawakutajwa, niendelee kuwapongeza na wao, basi Mwenyezi Mungu awajalie waweze kufanya hii kazi iweze kutekelezeka na baadaye kuwa na manufaa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawatakia kila la heri, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.19 Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 11 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*